**7 MEI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 7 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na: -

**WAZIRI WA FEDHA:**

Hati ya Uhamisho wa Bajeti baina ya Mafungu Na.1 kwa Mwaka 2022/2023 *[Statement of Reallocation Between Votes – Reallocation Statement No.1 of 2022/2023];*

Hati ya Uhamisho wa Bajeti Ndani ya Mafungu Na. 2 kwa Mwaka 2022/2023 *[Statement of Reallocation Within Votes - Reallocation Statement No.2 of 2022/2023];*

Hati ya Uhamisho wa Bajeti baina ya Mafungu Na.1 kwa Mwaka 2023/2024 kufikia 31 Desemba, 2023 *[Statement of Reallocation Between Votes – Reallocation Statement No.1 of 2023/2024 As at 31st December, 2023];*

Hati ya Uhamisho wa Bajeti Ndani ya Mafungu Na. 2 kwa Mwaka 2023/2024 kufikia 31 Desemba, 2023 *[Statement of Reallocation Within Votes - Reallocation Statement No.2 of 2023/2024 as at 31st December, 2023]*.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Mwamtumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 257

### Kuwaendeleza Watoto Wenye Ulemavu

**MHE. MWAMTUMU DAU HAJI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuwaendeleza Watoto wenye Ulemavu wanaofaulu kwenda Sekondari lakini wanatoka kwenye mazingira magumu?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobas Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwamtumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Sera ya Elimu Bila Ada imewezesha wanafunzi kupata elimu bila malipo kwa watoto wote wakiwemo watoto wenye ulemavu wanaotoka katika mazingira hatarishi iliyoanza kutumika mwaka 2016 mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa watoto wenye ulemavu wanaofaulu kwenda sekondari na wanaotokea katika mazingira hatarishi, wanaendelezwa kwa kupata huduma ya elimu kwa kuzingatia masuala yafutayo: -

(i) Kuwabaini watoto wenye ulemavu wanaotoka katika mazingira magumu na hatarishi kwa kutumia Maafisa Ustawi wa Jamii, Afisa Elimu na Wataalamu wa Afya kwa ngazi za Mkoa na Halmshauri, na;

(ii) Kutenga kifungu cha kusaidia watoto wenye ulemavu wanaotoka katika mazingira hatarishi kupitia halmashauri na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuhudumia katika masuala ya fedha ya kujikimu, vifaa saidizi, vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na bima ya afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwamtumu Dau Haji, swali la nyongeza.

**MHE. MWAMTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake zuri alilolitoa sasa hivi, na kwa kweli halina mjadala. Napenda kumwuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watoto hawana mahitaji muhimu kwa ajili yao, wanategemea kutoka kwa wazazi, je, Serikali haioni umuhimu wa kuwatengea fungu lao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwamtumu Dau Haji kama alivyouliza kwamba, kwa kuwa watoto hawa wanakuwa tegemezi, Serikali hatuoni umuhimu wa kuwatengea fungu lao?

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba watoto hawa wanakuwa tegemezi na wazazi wanapata shida sana kuwalea watoto hawa ambao wana changamoto ya ulemavu. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imeweka mpango mzuri wa kuanza kwanza kutengeneza mwongozo wa kutambua watoto hawa wenye ulemavu mapema na umepelekwa kwenye halmashauri zote nchini ili kuhakikisha zinawatambua kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhakikisha katika mwaka wa fedha Halmashauri wanatenga fedha maalum kwa ajili ya kuwasaidia watoto hao. Tatu, ni mpango uliopo wa Serikali kuhakikisha kwamba familia au kaya maskini zinazoratibiwa kwenye *program* ya *TASAF* inatambua pia pamoja na watoto hawa wenye ulemavu ili kaya zile ziweze kusaidiwa na kuingizwa kwenye mpango wa *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, nne, pia upo utaratibu wa wadau wa maendeleo ambao tumekuwa tukisaidiana nao, na tunawashukuru sana *UNICEF, ADI International* na *UNESCO,* kwa ushirikiano wao mzuri na Serikali katika kuhakikisha tunatoa huduma hizi kwa watu wenye ulemavu. Sambamba na hilo pia tumekuwa na ushirikiano mzuri…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge tayari ameelewa majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Watoto wenye ulemavu ni wengi sana hapa nchini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwatambua huko waliko, vijijini, wilayani na mikoani ili waweze kupatiwa huduma ambazo wanastahili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, Profesa amesema watoto wenye ulemavu ni wengi sana. Kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi, niongezee tu kwamba, Serikali ina takwimu za kisensa kwamba walemavu sio wengi kwa kiwango hicho. Tunazo takwimu ambazo zinatusaidia kuweza kuanza kuwatambua, pia kupata muda wa kuweza kuwasikiliza na kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, moja ya huduma ambazo tunazitoa ni pamoja na hizo nilizosema za kutenga bajeti kwenye halmashauri zetu; pili, kutengeneza mfumo mzuri na uratibu kupitia Wizara ya Afya na Wizara ya Maendeleo ya Jamii kutengeneza utaratibu wa kuhakikisha huduma zao za kibinadamu zinazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali tumechukua hatua nyingine hata kwenye haki yao ya elimu. Tunazo shule maalum ambazo zinafundisha, zipo katika Mikoa ya Njombe, Singida na maeneo mengine, ikiwa ni pamoja na kutengeneza utaratibu.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa

mabweni kwenye shule ili kuweza kusaidia watu wenye ulemavu na kutengeneza miundombinu rafiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli katika Sekta ya Watu Wenye Ulemavu tumefanya vizuri na kwa hatua kubwa sana, hata kwa wale watu wenye ulemavu kwa ujumla tumeendelea kutoa fedha za kuwasaidia. Kwa mfano, zile asilimia mbili kwenye halmashauri, tumeendelea pia kuhakikisha kwamba wanapata fedha wakati wote. Ndiyo maana unaona kwamba sasa hivi hata ombaomba wamepungua. Ni kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani hoja ilikuwa kwamba, kwa mfano sasa hivi ukiulizwa tunao watoto wenye ulemavu wangapi? Kwa sababu kama hatuna hizo takwimu za wangapi tulionao, ndiyo hoja yake. Kuna watoto wanazaliwa wenye ulemavu wanafichwa ndani, kuna watoto hawaendi shule kwa sababu hawana vitimwendo, kuna watoto hawaendi shule kwa sababu wazazi hawana uwezo wa kuwabeba, yaani vitu kama hivyo.

Kwa hiyo, nadhani hoja yake ni kwamba Serikali lazima iwe na utaratibu wa kuwatambua kwamba nyumba ile hatujamwona huyu mtoto, mbona alizaliwa kipindi fulani, lakini hajaenda shule mpaka leo? Yaani awe anafuatiliwa kwa sura hiyo. Ndiyo ilikuwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge. Ila kwa maana ya juhudi ambazo Serikali inazifanya, juhudi ni kubwa sana, lakini bado wapo watoto ambao hawatambuliwi na kwa hiyo hawapati huduma.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuliliona hilo kama Serikali na tayari tumechukuwa hatua. Hatua mojawapo ndiyo hiyo niliyosema ya kutengeneza mapema mwongozo wa utambuzi wa watoto wenye ulemavu ambao umetoka mwaka 2023 na tumeshaanza kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili ni sensa ya watu na makazi iliyofanyika. Tuna tafsiri zile takwimu ambazo tayari tunazo. Tatu, tayari maafisa ustawi wa jamii katika halmashauri zote tumehakikisha kwamba wanafanya kazi ya kwenda kuanzia ngazi

ya vitongoji, vijiji na mtaa ili tuweze kupata takwimu kwa ujumla. Wale ambao tayari tumeshawabaini hata kupitia mpango wa *TASAF* tumeshaanza kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunasubiri tuweze kupata zile takwimu za sensa kwa tafsiri ya wataalamu wa sensa ili tuendelee na huduma, lakini kwa wale ambao tumeshawatambua kama wapo ambao mnadhani hawajaweza kuhudumiwa na Serikali, nipewe majina yao ili tuweze kuwahudumia, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Sylvia Francil Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 258

**Kuitengea *TARURA* fedha za dharura**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kutenga fungu la fedha za dharura kwa *TARURA* kwa ajili ya kukarabati miundombinu iliyoathiriwa na mvua?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINABU A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tathmini ya uharibifu wa miundombinu ya barabara za wilaya imefanyika kuanzia mwezi Juni, 2023 hadi mwezi Aprili, 2024 ambapo jumla ya shilingi bilioni 301.72 zinahitajika. Aidha, uharibifu huo umetokea kwenye barabara zenye urefu wa kilometa 1,742.19, makalavati 4,260, madaraja

319, mifereji ya kuondoa maji barabarani urefu wa mita 108,833, na maeneo yanayohitaji kuimarishwa kwa kuwekwa changarawe kilometa 664.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* ilitenga shilingi bilioni 21.4 katika mwaka wa fedha 2023/2024, na imetenga shilingi bilioni 21.4 katika mwaka wa fedha 2024/2025. Hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni 81.4 zimepokelewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya tathmini na kutenga fedha za dharura kwa ajili ya kukarabati miundombinu iliyoathiriwa na mvua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, katika Halmashauri ya *Sumbawanga DC,* barabara ya Chombe – Kiandaigonda – Kahoze, kilometa 15 haipitiki kabisa na wananchi wanahangaika. Pamoja na kutenga fedha, je, Serikali ina kauli gani kuhusu barabara hii mahususi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Daraja la Ilembo linalounganisha Ilembo na Makao Makuu ya Kata ya Mpui limekatika na mawasiliano hakuna, mazao hayasafirishwi na wananchi hawawezi kupita. Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na kupeleka fedha hii ili daraja hilo lijengwe, kwa sababu imeombwa shilingi bilioni 1.3 na mpaka sasa haijaenda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINABU A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na barabara hii ya Chombe nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara nyingi zimeharibika kutokana na mvua na zimesababisha hitaji kubwa la fedha nje ya bajeti, lakini kwa upekee kabisa Mheshimiwa Rais, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan ameongeza bajeti ya dharura kutoka bajeti ya kawaida ya shilingi bilioni 21.4 hadi shilingi bilioni 131. Yote hiyo ni kwa ajili ya kurekebisha miundombinu ambayo imeharibika. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa ongezeko la bajeti ya dharura kutoka shilingi bilioni 21 mpaka shilingi bilioni 131 barabara hii itajengwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili linalohusiana na daraja la Ilembo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha kwamba mawasiliano hayakatiki. Kwa hiyo, yale maeneo yote ambayo mawasiliano yamekatika, Serikali inaweka kipaumbele ili kuhakikisha inarudisha mawasialiano hayo. Aidha, kwa ongezeko la bajeti ya dharura ambayo imekuja, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba daraja hili litajengwa haraka iwezekanavyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza, kwa kifupi, moja kwa moja kwenye swali.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mafuriko makubwa yamelikumba Jimbo la Arumeru Magharibi na kuharibu miundombinu ya barabara na madaraja, je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kurejesha miundombinu ya barabara hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINABU A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pindi mvua zitakaposimama, tutaanza kuona wakandarasi wanaingia kazini kwa ajili ya kurekebisha barabara hizi, kwa sababu fedha ya dharura imeongezwa na madhara ya mvua yamejulikana, na tayari mpaka mwezi wa Nne, 2024 tathmini ya uhitaji wa shilingi bilioni 301.72 kwa ajili ya kurekebisha barabara hizi ambazo zimepata madhara ya mvua imeshafanyika. Kwa hiyo,

nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ipo kazini; na kwa kuzingatia umuhimu wa barabara aliyoitaja, baada tu ya msimu huu wa mvua wakandarasi wataanza kuingia kazini kwa ajili ya kurekebisha barabara hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu yako. Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu Mbunge wa Singida Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 259

**Kukamilisha Ujenzi wa Maboma ya Zahanati – Jimbo la Singida Magharibi**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Zahanati za Mayalia, Mpetu, Kinyampembe, Mlandala, Kangeri, Nsonga Ndogo na Masweya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Zahanati za Nsonga Ndogo na Mlandala zilipokea shilingi milioni 100 katika mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo ujenzi umekamilika na zahanati zimeanza kutoa huduma mwishoni mwa mwaka 2023. Aidha, zahanati za Kinyampembe na Mpetu zilipokea shilingi milioni 100 katika mwaka wa fedha 2021/2022 na ujenzi wa zahanati hizo upo hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati za Mayalia, Masweya, Mayaha na Kahugeri, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Elibariki Kingu, swali la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikari, kwa kweli nakiri kwamba zahanati hizi wakati nauliza swali zilikuwa hazijapata fedha, lakini hadi leo zimeshajengwa na baadhi zimeshaanza kufanya kazi, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua, ni lini sasa Serikali itakwenda kukamilisha ahadi ya ujenzi wa Kituo cha Afya kilichoko Kata ya Minyuge ambacho kimsingi kitaweza kuhudumia Kata ya Makilawa, Kata jirani ya Ihanja pamoja na Kata ya Mtunduru kulingana na jiografia ngumu waliyonayo wananchi wangu latika kata hiyo niliyoitaja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ikiwa Serikali ilitoa ahadi ya kujenga kituo cha afya katika Kata hiyo ya Nayuge na ambayo itahudumia takribani kata tatu au nne ambazo Mheshimiwa Mbunge umezitaja.

Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia tu kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeshaweka mkakati wa kuandaa fedha kwa ajili ya kwenda kutekeleza ahadi zote za Serikali kuhakikisha wananchi wanapata huduma. Kwa hiyo, tutahakikisha tunatoa kipaumbele katika kata hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 260

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Lyamgungwe Kalenga**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Lyamgungwe katika Jimbo la Kalenga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa itatenga shilingi milioni100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Lyamgungwe. Aidha, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa kituo hicho cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Wananchi wamekuwa wakijitolea sana kujenga maboma mbalimbali yakiwemo ya vituo vya afya. Maswali yangu: Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inatenga fedha sambamba na wananchi kwa ajili ya kujenga majengo ya watumishi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kituo cha Afya Kata ya Ukumbi Jimbo la Kilolo kimejengwa kwa nguvu ya wananchi na kinahitaji kama shilingi milioni 200 ili kiweze kukamilika. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inakamilisha kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilishaweka mkakati wa kujenga vituo vya huduma za afya, na pia ilishaweka mpango madhubuti kuhakikisha tunajenga nyumba za watumishi kwa awamu ili watumishi wakae karibu na vituo hivyo waweze kuwahudumia wananchi wetu saa 24 na siku saba kwa wiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kukuhakikishia tu kwamba tumeshaanza utekelezaji. Kuna vituo vya afya hospitali za halmashauri, zahanati ambazo zinajengewa nyumba za

watumishi na zoezi hili ni endelevu. Tutahakikisha tunaendelea kujenga nyumba na pia tutatoa kipaumbele katika hicho kituo cha afya ambacho Mheshimiwa Mbunge umekitaja.

Mheshimiwa Spika, pili, nawapongeza sana wananchi wa Jimbo la Kilolo kwa kuchangia nguvu zao kuanza ujenzi wa kituo cha afya. Namwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilolo walete taarifa ya mahitaji ya fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo hicho cha afya ili tujiridhishe na pia tuweze kuona namna gani fedha inapatikana kwa ajili ya kwenda kukamilisha kituo hicho cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwongozo unasema kwamba eneo likiwa lina zaidi ya wakazi 10,000, linatakiwa liwe na kituo cha afya, napenda kufahamu, je, ni lini Serikali itaweka utaratibu wa kujenga kituo cha afya kwenye Kata ya Bakoba iliyopo Jimbo la Bukoba Mjini lenye wakazi zaidi ya 16,000?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kata hiyo ya Bakoba ambayo Mheshimiwa Mbunge Neema ameisema, ni moja ya kata ambazo tayari Serikali ishaainisha kwamba ni Kata za Kimkakati kwa ajili ya kutafuta fedha na kwenda kujenga vituo vya afya. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaifanyia kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba, aweze kuleta tathmini ya mahitaji ya ujenzi wa kituo hicho cha afya, lakini atuambie sehemu ya mapato ya ndani ya halmashauri ambayo wanakwenda kutenga kwa ajili ya kuanza ujenzi huo wakati Serikali ikitafuta fedha kwa ajili ya kuwaunga mkono kukamilisha kituo hicho, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, Mbunge wa Sengerema, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

Na. 261

**Kumalizia Ujenzi wa Zahanati 12 – Sengerema**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA K.n.y. MHE. HAMIS M. TABASAM** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamalizia ujenzi wa zahanati 12 zilizojengwa kwa nguvu za wananchi katika Halmashauri ya Sengerema?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2022/2023, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 89.9 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 1,798 ya zahanati kote nchini. Katika kipindi hicho, Halmashauri ya Sengerema ilipelekewa shilingi milioni 350 kwa ajili ya ujenzi wa maboma saba ya zahanati ambayo yamekamilika na zahanati hizo zinatoa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga shilingi bilioni 18.8 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 376 ya zahanati, ambapo Halmashauri ya Sengerema imepelekewa shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati za Nyasigu na Tabaruaka. Ukamilishaji wa zahanati nyingine utaendelea kufanyika kwa awamu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa ikipeleka pesa ikiwa imechelewa, na

nguvu za wananchi mara nyingi wanakata tamaa kwa kazi kubwa inayofanywa, je, Serikali inatuhakikishiaje kwamba pale ambapo jamii inakuwa imeshatimiza wajibu wake kwa kufanya maendeleo kama wanavyopanga wenyewe, watapeleka hela kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na haya maboma yaliyosemwa, lakini kuna vituo vya afya vya Serikali ambavyo tayari vimeanzishwa, lakini miundombinu yake haijakamilika. Je, navyo viko katika mpango wa ukamilishaji wa maeneo yote ambao Mheshimiwa Waziri amesema?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuanza kwa kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kimsingi Serikali haipeleki fedha za kukamilisha maboma kwa kuchelewa. Changamoto ambayo tumeiona na tulishapeleka maelekezo kupitia Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi, ni kwamba ujenzi wa maboma lazima uratibiwe.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na utaratibu wa ujenzi wa maboma kiholela. Kila mmoja anaamua leo anaanza kujenga boma kabla taarifa hazijafika ngazi ya Mkurugenzi, hazikafika ngazi ya Katibu Tawala Mkoa, wala Ofisi ya Rais, TAMISEMI haijapata taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kutumia nafasi hii kusisitiza Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakarugenzi kuratibu ujenzi wa maboma ili Serikali ipate taarifa mapema na iweze kutenga fedha mapema badala ya kujenga kila siku kiholela na mwisho wa siku majengo yale yanakaa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali, maboma yote ambayo yamekamilika, kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2021/2022 – 2022/2023, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametenga zaidi ya shilingi bilioni 90 kwa ajili ya ujenzi wa maboma zaidi ya 1,788, lakini mwaka huu wa fedha tunaoongeza, zaidi ya shilingi bilioni 19 zimetengwa kwa ajili

ya maboma. Kwa hiyo, nawahakikishia kwamba tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na vituo vya afya ambavyo vimejengwa na vina majengo pungufu ya yale yanayohitajika, vipo vituo ambavyo havina wodi za wanaume, wanawake, watoto na majengo mengine. Serikali imeendelea kukamilisha kwa awamu na namhakikishia kwamba tutaweka mpango huo na ni endelevu kuhakikisha kwamba maboma hayo yanakamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, sasa aulize swali lake.

Na. 262

**Kukomesha Ukataji Holela wa Miti Nchini**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kukomesha ukataji holela wa miti na uchomaji moto wa misitu nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kisera, kimkakati na utekelezaji wa miradi ili kukabiliana na changamoto hizi. Mikakati hiyo ni pamoja na Mpango Kabambe wa Uhifadhi wa Mazingira wa 2022 – 2032 ambao umebainisha hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umma

kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ikiwemo misitu na kutambua fursa zinazopatikana kutokana na utunzaji wa rasilimali za misitu. Hivi sasa Serikali imekuja na Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 – 2034 ambao kwa kiasi kikubwa utapunguza matumizi ya nishati itokanayo na misitu.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kuendeleza na kuimarisha doria zinazofanywa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)* ili kulinda misitu kutokana na mioto na uvunaji holela, kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi na jamii katika usimamizi endelevu wa misitu; na kuandaa Sheria na Miongozo ya Uvunaji na Usafirishaji wa Mazao ya Misitu katika halmashauri zetu nchini, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ili taarifa zetu zikae vizuri, moto una wingi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, samahani…

**SPIKA:** Wingi wa moto ni mioto! Ili Kiswahili chetu kikae vizuri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, moto ni moto tu.

**SPIKA:** Moto ni moto.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Basi hapo uliposoma "mioto," pasomeke moto.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, sawa.

**SPIKA:** Haya, sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa *TFS* imeshindwa kabisa kudhibiti uchomaji moto wa misitu yetu kila inapofika kiangazi, je, Serikali ina mipango gani zaidi wa kudhibiti watu wanaochoma misitu kwa makusudi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa majibu ya msingi ya Wizara, wanamesema Serikali inaandaa Sheria na Miongozo, ni lini Sheria hiyo italetwa Bungeni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumebaini moja ya miongoni mwa sababu za kuchomwa kwa misitu mingi hapa Tanzania, ni kutokana na shughuli nyingi sana za kibinadamu zikiwemo za kilimo na shughuli nyingine na makazi. Zipo hatua mbalimbali ambazo Serikali tumeanza kuzichukua kwa ajili ya kudhibiti vitendo hivyo vya uchomaji misitu na vingine kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, moja, tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waelewe kwamba shughuli za kibinadamu ndizo zinazoharibu mazingira. Pia ziko hatua mbalimbali za kinidhamu ambazo tumeanza kuzichukua kupitia Sheria hii ya Misitu Na. 4 ya Mwaka 2002, na pia tumekuwa tunafanya doria mbalimbali kwenye misitu hii. Hapa nataka kutoa maelekezo na vile vile kutoa wito kwa Kamati zote za Ulinzi na Usalama kwenye Vijiji, Kata, na Wilaya, moja ya miongoni mwa kazi kubwa watusaidie ni kulinda misitu hii.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumeanza mchakato wa kufanya marekebisho ya sheria hii, lakini namwomba nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, viko vikao ambavyo vimeanza kuifanyia mapitio sheria hii, itakapokamilika, tutaileta hapa kama alivyoomba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, sasa aulize swali lake.

Na. 263

**Kusambaza Umeme Vijiji Vyote – Nkenge**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itasambaza umeme katika Vijiji vyote vya Jimbo la Nkenge?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nkenge lina jumla ya vijiji 77 ambapo kati ya hivyo, vijiji 74 vimeshapatiwa umeme kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)*. Kwa sasa mkandarasi anaendelea na kazi ya ujenzi wa njia za kusambaza umeme katika vijiji vitatu vilivyosalia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri katika vijiji vyote ndani ya Jimbo la Nkenge, na ni kweli vijiji vitatu mkandarasi anaendelea kufunga umeme katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kuna mradi wa vitongoji 15 ambavyo vinaendelea katika taratibu kuwekewa umeme vikiongozwa na Kitongoji cha Nyungwe na vingine. Sasa tumekuwa tukiambiwa kwamba, tuko katika hatua za manunuzi, je, ni lini sasa mradi huo wa vitongoji 15 ndani ya Jimbo la Nkenge utaanza kutekelezwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, baada ya vitongoji 15, bado vitongoji zaidi ya 180 ambavyo hatujajua hatima ya umeme katika vitongoji hivyo. Je, ni lini na vitongoji hivyo vilivyobaki ndani ya Wilaya ya Misenyi vitafungiwa umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuhusiana na vitongoji 15, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tupo katika hatua za mwisho za manunuzi, na mpaka kufikia mwisho wa mwezi huu, tutakuwa tayari tumeshapiga hatua ya kuelekea kwenye utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vitongoji ambavyo vipo katika Jimbo la Nkenge, jimbo hili lina vitongoji 358 ambapo mpaka sasa vitongoji 188 vina umeme. Ni vitongoji 170 vilivyobakia. Vitongoji 15 tayari vipo kwenye mradi wa vitongoji 15, vitongoji 11 kuna mradi wa ujazilizi unaendelea na vitongoji vingine vilivyobakia, vitapata miradi ya umeme kupitia mradi wa vitongoji 20,000 ambao unaenda kuanza kuanzia mwaka ujao wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 264

**Fedha Zilizotumika kama Kifuta Jasho Kutokana na Tembo**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, kwa mwaka 2017 – 2022 ni kiasi gani cha fedha kimelipwa kama kifuta jasho kwa uharibifu wa mazao na watu kuuliwa na Tembo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kufuatia madhara yanayosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini, Wizara ya Maliasili na Utalii imelipa jumla ya shilingi 11,085,850,400 katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017/2018 hadi Machi, 2024.

Mheshimiwa Spika, sambamba na malipo hayo, jitihada mbalimbali za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu zinaendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kujenga vituo vya Askari kwenye makazi ya wananchi ili kuwasogeza askari karibu na maeneo yenye changamoto; kujenga vizimba vya kuzuia mamba wasidhuru wananchi wanapotumia maji ya mito au maziwa, kuandaa mfumo wa kielektroniki ili kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa na utunzaji wa taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu na kuweka namba maalum za simu kwenye vituo vya kanda za kiutendaji na taasisi za uhifadhi kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kutoa taarifa za matukio ya wanyamapori bila malipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hebu tusomee, ni kiasi gani ambacho Wizara imeshalipa? Kiasi tu, hicho cha shilingi bilioni 11, tusomee hicho kiasi ili kiingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, shilingi 11,085,850,400.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Swali langu ni kwamba, ukiangalia kwa miaka saba, uharibifu mkubwa mashamba ya wananchi, wakulima ambao wameharibiwa mazao yao wamelipwa tu shilingi bilioni hizi tu 11 katika hiyo miaka saba. Serikali haioni kwamba inamfukarisha mkulima ambaye kwa eka moja angepata kwa mfano magunia 30 ya mpunga ambayo ni takribani shilingi 3,000,000, lakini analipwa shilingi 100,000 tu, je, Serikali haioni kwamba badala ya kumsaidia mkulima, inamfanya awe maskini zaidi?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inachukua hatua gani ku-*address* hii *problem*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, malipo haya yanafanyika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo. Tumeshaona kwamba Kanuni hizi sasa zimepitwa na wakati, na tayari Wizara imezifanyia mapitio na sasa tuko kwenye mashauriano na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili viwango vipya viridhiwe, tuanze kufanya shughuli hiyo ya kuwalipa wananchi kwa viwango vya sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni ulazima wa kulipa kifutajasho kwa wakati kwa sababu wananchi wengi wanapokuwa wamepata shida hiyo ya tembo, huwa wanakuwa katika njaa kali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi sana kuhakikisha inalipa kwa wakati mara tu baada ya kupata taarifa hizo kutoka kwenye halmashauri, na mchakato wa tathmini kufanyika ili kujua gharama halisi na baada ya hapo tunaweza kulipa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali kuhusiana na wanyamapori. Kwa sasa hivi Jimbo la Same Magharibi, wananchi waliopata madhara ya wanyamapori kwenye mashamba yao wanalipwa fidia lakini wanalipwa shilingi 25,000 kwa ekari. Wakati huo huo, majina mengi sana hayapo katika wale ambao wamepata athari ya mashamba yao. Je, ni lini Serikali itarekebisha upungufu huo ili wananchi waweze kupata haki yao stahiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi. Tayari tumeshaona kwamba, viwango vinavyotumika sasa vimepitwa na wakati, tumevifanyia mapitio, tuko kwenye majadiliano ya mwisho na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili wenzetu wakisharidhia tuweze kufanya malipo kwa viwango vipya. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati tunakamilisha jambo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 265

**Kuwaongezea Pensheni Wastaafu**
**Wanaolipwa na Hazina**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawaongezea pensheni wastaafu wanaolipwa shilingi 100,000 kwa mwezi na Hazina?

**SPIKA:** Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeunda Kamati ya Kukusanya na Kuchambua Maoni na Mapendekezo ya Viwango vya Nyongeza ya Pensheni ili kuwezesha maandalizi ya Rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu nyongeza ya pensheni kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina. Kazi ya uchambuzi wa maoni pamoja na

mapendekezo ya wadau inatarajiwa kukamilika kabla ya tarehe 30 Juni, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kumekuwa na malalamiko ya *formular* ya kikokotoo cha pensheni kwa wastaafu. Ni nini mkakati wa Serikali wa kufanya mapitio ya *formular* hiyo ili iweze kuwasaidia wastaafu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Nini mpango wa Serikali wa kuwapa mafunzo wastaafu wanaolipwa pensheni na Hazina kabla hawajastaafu ili iweze kuwasaidia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maswali mazuri ya Mheshimiwa Mbunge. Kuhusiana na suala la *formular,* kama nilivyosema Kamati imeundwa na ni Kamati pana inayohusisha sekta mbalimbali. Pia Wizara inayosimamia masuala ya utumishi na yenyewe inaendelea na zoezi kubwa ambalo linahusisha suala hilo la pensheni kwa upana wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo. Tumepokea hoja hiyo. Tumekuwa na utaratibu huo, lakini tutaendelea kuboresha kadiri ya Mbunge alivyoshauri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 266

**Hitaji la Mawasiliano Iyovi**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafunga minara ya mawasiliano katika eneo la Iyovi kwenye Barabara ya Morogoro – Iringa?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imeshafanya tathmini na kubaini uwepo wa changamoto za mawasiliano katika eneo la Iyovi. Hivyo basi, hatua za utekelezaji zitaendelea ili kuhakikisha eneo hili linapata huduma ya mawasiliano ya uhakika kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, Rungwe, Kisiba, Masoko, Suma, Matwebe, Masukuru, Swaya, Mbarali, Ipwani, Mawindi, Itemboleo, Mapogoro, Utengule, Mwatenga, Chunya, Upendo, Kambikatoto, Sangambi, na Ifumbo: Je, ni lini Serikali itapeleka minara kwa ajili ya mawasiliano kwenye Kata hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Je, ni lini Serikali itapeleka minara ya mawasiliano kwenye Barabara ya Iyovi ambayo ni barabara muhimu sana, ambayo wananchi wote wa Nyanda za Juu Kusini wanapita pale? Sina sababu ya kutaja Mikoa. Pia hata magari ya nchi za nje kama Malawi, Zambia, *South Africa*, Burundi na Rwanda yanapita pale. Ukiharibikiwa na gari pale, mawasiliano ni shida sana. Ni lini Serikali itapeleka mawasiliano pale kwa maana ya minara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suma Fyandomo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo aliyoyataja kwa Mkoa wa Mbeya kwa maana ya Rungwe, Mbarali na Chunya, baadhi ya maeneo haya aliyoyataja yapo katika programu ya minara yetu 758 na kazi hii tayari imeishaanza. Kwa hiyo, maeneo haya pia, tutaendelea kuyafikia kadiri ya tunavyopata fedha, lakini ni lazima ndani ya miezi 24 ya mkataba wa minara hii 758 iweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile maeneo haya ya Iyovi aliyouliza Mheshimiwa Mbunge, pia tunaendelea kuyafanyia kazi. Japo kwa Wizara kipaumbele ni kule ambako tayari wananchi wapo kama maeneo haya aliyoyataja ya Mbarali, Rungwe na Chunya tuweze kuyafikia kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maeneo haya ya barabara kuu ambayo magari ya nchi jirani yanapita pamoja na wafanyabiashara, ni muhimu kuwa na mawasiliano. Kote tunatoa kipaumbele na tutahakikisha kadiri tunavyopata fedha ni lazima mawasiliano kote yaweze kufika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kijiji cha Uliwa, Kata ya Uliwa, Halmashauri ya Mji wa Njombe, tumeahidiwa muda mrefu sana hapa ndani kwamba, tutapata mnara. Ni lini kijiji hiki kitapewa mnara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Mwanyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kijiji hiki alichokitaja Mheshimiwa Mbunge, tayari wataalamu wetu wameweza kufika na kufanya

tathmini, lakini tunarajia kadiri tunavyopata fedha mnara huu pia utakwenda kujengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Je, ni lini Serikali itakamilisha Ujenzi wa Minara 15 ya Mawasiliano katika Wilaya ya Kilwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Ndulane, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kipaumbele chetu kabisa kuhakikisha tunaikamilisha hii minara 15 kwa sababu lengo ni kuona kwamba mawasiliano yanahimarika katika maeneo haya yote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, toka Serikali iahidi ujenzi wa minara sita kwenye Jimbo la Msalala, ni kituo kimoja tu cha Ntoba ndiyo kimekamilika. Sasa ni lini Serikali itaenda kukamilisha minara mitano ambayo imebaki? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza kwa ufuatiliaji. Katika hii minara sita mmoja umekamilika. Tambua safari ni hatua. Kwa hiyo, hata hii minara mitano tunakuja kuitekeleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 267

**Soko la Uhakika la Zao la Mahindi**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kutafuta Soko la uhakika la Zao la Mahindi ili kuepusha Wakulima kupata hasara?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuwatafutia wakulima wa zao la mahindi masoko ya uhakika. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuwaunganisha wakulima na wasindikaji wa mahindi kwa ajili ya kuzalisha unga na chakula cha mifugo;

(ii) Kuiwezesha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko *(CPB)* pamoja na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* kununua nafaka kwa wakulima kwa bei shindani kwa lengo la kuimarisha mjengeko wa bei;

(iii) Kutumia Balozi za Tanzania nje ya nchi kwa kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, *Tan Trade* na taasisi nyingine za kimataifa kusaidia upatikanaji wa fursa za masoko katika nchi mbalimbali; na.

(iv) Serikali kuendelea kutumia mifumo ya kielektroniki kama vile *TMX* ambayo itasaidia kutoa taarifa za upatikanaji wa masoko ya mazao husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Clement Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Katika Jimbo la Kwela wakulima wa zao la mahindi wanategemea sana Soko la

*NFRA,* lakini kuna vituo viwili katika Mji wa Laela na Mto Wisa: Je, Serikali haioni katika msimu ujao kuna haja ya kutumia maghala, hasa katika Vijiji vya Kaengesa, Nyangarua, Kaoze na pale Kisa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Waziri wa Kilimo alipofanya ziara Jimbo la Kwela, aliahidi ujenzi wa ghala pale Kijiji cha Kilyamatundu, Kata ya Kipeta, ambalo litakuwa ndiyo *center* ya soko la zao la mpunga katika Bonde lote la Ziwa Rukwa. Je, ahadi hii Serikali imefikia wapi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, katika maeneo ambayo ametushauri, hususan maeneo ya Kaengesa kwamba Serikali tutumie maghala, tuko tayari na tumeishauri Wakala wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* waweze kufanya hivyo katika msimu unaokuja. Kwa hiyo, ninaamini katika mpango wetu litatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Waziri kujenga ghala katika Kata ya Kipeta kule Kilyamatundu iko pale pale na iko katika mpango, kwa sababu tunajua umuhimu wa lile bonde na mchango wake katika uzalishaji mkubwa wa mpunga. Kwa hiyo, namwondoa shaka Mheshimiwa Mbunge, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nini mkakati wa Serikali wa kuinua bei ya soko la mahindi ambayo kwa sasa kwa mfano, Mbozi gunia la mahindi linauzwa shilingi 25,000 mpaka shilingi 30,000? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Moja ni kwamba, kama nilivyojibu katika swali la msingi, kikubwa ni katika mwaka huu unaokuja, Serikali imejipanga kuongeza wigo wa kununua mahindi kutoka tani 300,000 mpaka kufikia tani

700,000 katika mwaka wa fedha 2024/2025. Hilo ndiyo lengo la Serikali. Ninaamini kwa mkakati huu sasa tutaongeza walau bei kuwa inayoridhisha kwa wakulima wote nchini, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 268

**Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Korosho – Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Ghala la kuhifadhia Korosho Tunduru ambapo ujenzi wake umesimama tangu mwaka 2015?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania ilianzisha mradi wa kujenga ghala kwa ajili ya kuhifadhi korosho katika Wilaya ya Tunduru, Mkoani Ruvuma, lenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 za korosho ghafi. Ujenzi huo umegharamiwa na fedha za Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho ambao chanzo chake kikuu kilikuwa ni kodi ya usafirishaji wa korosho ghafi nje ya nchi *(Export Levy)*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya kisera, mapato ya *export levy* yalielekezwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na hivyo, Mfuko wa Korosho kukosa fedha na kusababisha ujenzi wa ghala hilo kusimama ukiwa katika hatua za msingi.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea na mradi huu, Serikali ilipitia upya gharama za mradi na tayari shilingi bilioni 2.6 zimetolewa kwa Bodi ya Korosho ili kuendelea na ujenzi. Aidha, Serikali imetenga fedha katika bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa ajili ya uendelezaji wa maghala ikiwa ni pamoja na ghala la Tunduru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imetoa shilingi bilioni 2.6 kwa Bodi ya Korosho na ule ujenzi bado haujaanza, naomba majibu ya uhakika, ni lini Bodi ya Korosho wataanza kuendeleza ujenzi ule?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani unahitaji sana maghala makuu pamoja na maghala kutoka kwenye vijiji, Serikali ina mpango gani wa kujenga maghala kwenye vijiji ili kuhifadhi korosho hizo ambazo zinaenda kwenye maghala makuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge na ninamhakikishia tu kwamba, Waziri ameshaielekeza Bodi ya Korosho kuanza ujenzi huo mara moja. Kwa hiyo, tutakachofanya, hata mimi mara baada ya Bunge nitakwenda kwa ajili ya kuangalia hatua ambayo watakuwa wamefikia kwa sababu, wanatakiwa waanze sasa kabla ya kufunga mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa maghala, tunaendelea kufanya hivyo na katika bajeti kuu tumetenga fedha kwa ajili ya ujenzi ili kusaidia zao la korosho. Kwa hiyo, jambo hilo lipo katika mipango ya Serikali, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 269

**Kudhibiti Matukio ya Unyanyasaji kwa Wanawake na Watoto**

**MHE. TAUHIDA C. GALLOS** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti matukio ya unyanyasaji na ukatili wa kingono dhidi ya Wanawake na Watoto nchini?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto uliosababisha kuanzisha Kamati 18,186 za Ulinzi na Usalama wa Wanawake na Watoto zinazotoa elimu na taarifa ya masuala ya ukatili wa kijinsia. Aidha, Serikali imeunda madawati 2,405 ya Ulinzi wa Mtoto katika Shule za Msingi 1,765 na Sekondari 640, Madawati ya Kijinsia katika Vyuo Vikuu 296, madawati 115 katika maeneo ya sokoni pamoja na madawati 420 katika Vituo vya Polisi yanayoshughulikia kesi za ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, juhudi hizi zimewezesha kupungua kwa vitendo vya ukatili wa kimwili kutoka 40% mwaka 2015 hadi 27% mwaka 2022 na ukatili wa kingono kutoka asiliia 17 mwaka 2015 hadi 12% mwaka 2022. Aidha, Serikali itaendelea na kampeni mbalimbali za ulinzi na usalama wa wanawake na watoto ili kumaliza kabisa tatizo la unyanyasaji wa ukatili wa kingono dhidi ya wanawake na watoto, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, swali la nyongeza.

**MHE. TAUHIDA C. GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, vitendo hivi vya

unyanyasaji kwa wanawake bado vipo na vimeshika kasi. Je, Serikali inachukua hatua gani mahsusi kuweza kupunguza vitendo vya ukatili kwa wanawake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Kila tunapoamka asubuhi vitendo vya unyanyasaji wa kingono kwa watoto vimeshika kasi. Je, Serikali ina mipango gani mahususi kuweza kutoa elimu ya kutosha kwa watoto kuweza kujikinga na suala hili? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge, yeye mwenyewe kwa jitihada zake za kuwainua wanawake kiuchumi. Wizara imechukua hatua ya kuwajengea uwezo wanawake na kuwawezesha kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha katika fursa zilizopo katika jamii zetu. Lengo ni kupunguza uwezekano wa kuathiriwa na ukatili.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swali lake la pili, Serikali imechukua hatua zinazowezesha watoto kupata elimu ya kujitambua, kujieleza na kutoa taarifa zinazohusu ukatili wa kingono, kuanzisha Bunge la Watoto, Mabaraza ya Watoto na Madawati ya Ulinzi na Usalama wa Watoto katika Shule za Msingi na Sekondari. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, sasa aulize swali lake.

*(Hapa kuna Mbunge ambaye hakutajwa jina alipita mbele ya Mzungumzaji kinyume na Kanuni ya 73(c) za Bunge Toleo la Februari, 2023)*

**SPIKA:** Mheshimiwa unayepita mbele ya anayezungumza tafadhali tafuta kiti uketi. Mheshimiwa Eric Shigongo, uliza swali lako.

Na. 270

**Ujenzi Wa Barabara ya Sengerema – Nyehunge**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Sengerema – Nyehunge utaanza?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Sengerema – Nyehunge yenye urefu wa kilometa 54.4 ulisainiwa tarehe 23 Aprili, 2023. Baada ya kusainiwa kwa mkataba mkandarasi hupatiwa muda wa miezi mitatu, kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi *(mobilization)* ambapo hutakiwa kuleta mitambo, vifaa vya ujenzi pamoja na wataalam muhimu wa kusimamia kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Mkandarasi ameshindwa kuleta mitambo na wataalam kwa ajili ya kuanza kazi. Serikali imeamua kuvunja mkataba huo na mnamo tarehe 17 Aprili, 2024 *TANROADS* walipeleka maombi kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya kupewa idhini ya kuvunja mkataba huu na kazi itangazwe upya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric James Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa wananchi wa Vijiji vya Iseni, Uchiri, Bukokwa - Kalebezo hadi Nyehunge, wapo kwenye mateso makubwa sana hivi sasa, barabara hii haikupangiwa kabisa fedha za matengenezo; na kwa kuwa mkandarasi huyu amethibitisha hana uwezo na hakuna mashaka ali-*forge documents* zake wakati anaomba *tender,* Serikali inasita

vipi kuweka mkandarasi aliyeshinda wa pili kuendelea na kazi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa barabara hiyo inasomeka Sengerema – Nyehunge na sehemu ya Kahunda ila itakayotekelezwa ni Barabara ya Sengerema – Nyehunge peke yake. Je, Sehemu ya Kahunda ambayo ni kilometa 32 itatekelezwa kwenye bajeti ya mwaka huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tathmini ilifanyika kuhusu mkandarasi huyu, lakini ameshindwa kutimiza yale masharti ya kimkataba na ndiyo maana Serikali ikaamua kuvunja huo mkataba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kumchukua mkandarasi wa pili; tunaongozwa na sheria za kimkataba, lakini kama bado kutakuwa na *deed validity* kwa maana kwamba, yule aliye-*bid* wa pili kama itaonekana muda bado unaruhusu na anaweza akachukuliwa, akafanyiwa majadiliano na ikaonekana inawezekana, basi itakuwa ni hivyo. Kama muda utakuwa umepita, basi tutatangaza upya hiyo tenda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya kuanzia Nyehunge kwenda Kahunda, naomba nijiridhishe kama kwenye mpango huu wa bajeti tumepanga kwa ajili ya kuendeleza, kwa sababu bajeti bado hatujaisoma, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, sasa aulize swali lake.

Na. 271

**Eneo Lililochukuliwa katika Kijiji cha Kasesya – Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani juu ya eneo lililochukuliwa bila fidia na halijaendelezwa Kijiji cha Kasesya mpakani mwa Tanzania na Zambia?

**SPIKA:** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Jerry William Silaa, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mwaka 1996 Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ilipanga ardhi katika eneo la Mpango lililopo Kijiji cha Kasesya *(Kasesya Trading Center*). Upangaji huo ulizalisha jumla ya viwanja 52 vya matumizi mbalimbali. Aidha, mpango huu uliidhinishwa kupitia Mchoro wa Mpango Miji Na. 80/01/495 tarehe 26 Aprili, 2001 na umilikishwaji wa viwanja tajwa ulifanyika kupitia michoro ya mipango miji kabla ya upimaji kukamilika. Taratibu za kupanga eneo hilo zilifanyika katika kipindi ambacho fidia ya ardhi ilikuwa hailipwi isipokuwa kwa mwendelezo uliopo.

Mheshimiwa Spika, viwanja Na. 5 mpaka 32 katika eneo la *Kisesya Trading Center* yenye jumla ya mita za mraba 19,127 lilimilikishwa kwa Taasisi ya *Tanzania Chambers of Commerce Industry and Agriculture (TCCIA)* kwa barua ya toleo Na. LDSDC178/3 ya tarehe 10 Desemba, 2002 kwa matumizi mchanganyiko.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi uliofanyika uwandani Mwezi Aprili, 2024 umebaini uwepo wa machinjio na maduka ya nyama katika sehemu ndogo ya eneo hilo yanayomilikiwa na *TCCIA* na kuacha sehemu kubwa ya ardhi ikiwa haijaendelezwa. Kufuatia hali hiyo, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi wa Kijiji cha Kasesya kutaka kurejeshewa ardhi yao ili waweze kuitumia

kwa shughuli za kiuchumi, kwa kuwa sehemu kubwa ya ardhi hiyo haijaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, nimemwelekeza na tayari ameshaanza kuchukua hatua Kamishna wa Ardhi Msaidizi, kushirikiana na mamlaka nyingine katika Mkoa wa Rukwa kufuatilia kwa kina masuala yanayolalamikiwa na wananchi na kuchukua hatua stahiki za kisheria. Aidha, Wizara yangu imeshaelekeza kwa nchi nzima Makamishna wa Ardhi Wasaidizi kuchukua hatua kwa wamiliki wote wa ardhi watakaobainika kukiuka masharti ya uendelezaji. Natoa rai kwa wananchi wa Kijiji cha Kasesya kuwa na subira wakati Serikali ikiendelea kutafuta ufumbuzi wa malalamiko yao. Shukrani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ila kwanza ili kuweka rekodi sawa ni vizuri nikaeleza majibu ambayo Mheshimiwa Waziri amesoma na ambayo nimeletewa mimi, kuna utofauti kubwa sana kiasi kwamba hata katika kujenga msingi wa maswali ya nyongeza kidogo amenipeleka ambako siko. Ni vizuri tuweke kwenye rekodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja …

**SPIKA:** Ngoja. Mheshimiwa Waziri amesoma majibu ambayo wewe huna!

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, niliyoletewa mimi na ambayo amesoma Mheshimiwa Waziri kuna utofauti mkubwa sana. Katika hali ya kawaida kwa majibu ya msingi anayosoma natakiwa nami niwe nayo ili niweze kujenga msingi wa maswali ya nyongeza.

**SPIKA:** Sasa hapa unanipa wakati mgumu. Nisaidie ya kwako. Msaidizi, hebu nichukulie kwa Mheshimiwa Mbunge tuone anayo majibu gani? Kachukue kishikwambi cha Mbunge nione ana majibu gani? Fanya haraka kidogo, la sivyo inabidi niliahirishe swali. *(Makofi)*

*(Hapa Mhudumu wa Bunge alikwenda kuchukua Kishikwambi cha Mbunge na kumpelekea Spika)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majibu aliyonayo Mheshimiwa Mbunge, ndiyo niliyonayo hapa mbele. Sasa Mheshimiwa Waziri hebu nione ya kwako uliyoyasoma. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa Mhudumu wa Bunge alikwenda kuchukua majibu ya swali namba 271 kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kumpelekea Spika)*

**SPIKA:** Sawa, sasa nimejiridhisha kuna ongezeko la maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaweka kwenye majibu yake. Kwa maana hiyo, sehemu kama mbili hivi Mheshimiwa Mbunge atakuwa hana haya majibu. Kwa hiyo, inawezekana akauliza swali la nyongeza kumbe tayari Mheshimiwa Waziri amesoma kwenye jibu lake.

Kwa hiyo, swali la Mheshimiwa Kandege ili aweze kujiandaa vizuri na maswali yake ya nyongeza tutalipeleka kesho ili akabidhiwe majibu mapya, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hilo lilikuwa liwe ndiyo swali letu la mwisho, lakini sasa swali la 15 tutalipeleka kesho ili Mheshimiwa Mbunge aweze kupata majibu ambayo Serikali inampa kwa swali lake naye aweze kuuliza maswali ya nyongeza kama atakuwa nayo.

Nawasubiri mnaozungumza, mkimaliza nitaendelea, kwa maana mwalimu naye huwa anachoka kuongea saa nyingine. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa tunarudia kila siku jambo moja hilo hilo. Kwa hiyo, nikisimama, mkiwa mnaongea nitanyamaza ili mmalize kwanza halafu nitazungumza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo hapa mbele na tutaanza na tangazo la wageni walioko hapa Bungeni, asubuhi hii.

Tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika na hawa ni wageni wangu, lakini ni viongozi wa Chama cha Bao Tanzania, yupo Ndugu Monday Likwepa, ambaye ni Rais, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Magreth Method Mapunda ni Katibu Mkuu, yupo Ndugu Msafiri Abdallah Himba ni Mjumbe na yupo Ndugu Jenipha Njabir ni Katibu Hamasa, ahsante sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, tutaanza na Dkt. Carolyne Nombo ambaye ni Katibu Mkuu, yupo pia Profesa James Mdoe - Naibu Katibu Mkuu na yupo pia Dkt. Franklin Rwezimula - Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Yupo Profesa Makenya Maboko - Mwenyekiti wa Kamati ya Maboresho ya Mitaala na yupo Profesa Joseph Semboje - Mwenyekiti Kamati ya Mapitio ya Sera. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Fadhili Maganya - Mwenyekiti Chama Cha Mapinduzi, Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Dogo Idd Mabrouk - Makamu Mwenyekiti Jumuiya ya Wazazi Chama Cha Mapinduzi, Taifa na yupo Ndugu Alli Issa Alli - Naibu Katibu Mkuu CCM Jumuiya ya Wazazi Taifa. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Nurdin Babu - Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Patrick Boisafi - Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Mkoa wa Kilimanjaro na yupo Bi. Mercy Mollel - Katibu wa Chama Cha Mapinduzi, Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Raymond Mangwala ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Rombo. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Selemani Mfinanga, ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa kutoka Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Adam Simba - Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Ivan Moshi - Mwenyekiti Umoja wa Vijana Chama Cha Mapinduzi, Mkoa wa Kilimajaro. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Mary Sulle, Katibu wa CCM Wilaya ya Rombo. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Ndugu Mahamoud Karia - Mjumbe wa Kamati ya Siasa, Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Lyabwene Mtahabwa - Kamishna wa Elimu. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ni Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, wote wasimame kwa pamoja na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambao pia ni wa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Waziri wa Katiba na Sheria na hawa ni Wanawake na Samia kutoka Chamwino, Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Halafu hapa Jijini Dodoma, Dodoma siyo jiji ni hili peke yake, kule kwingine ni kawaida tu. Kule kwingine ni Mkoa?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya sawa. Kwa hiyo, jamani ni Mkoani Dodoma, maana nisije nikaipa hadhi Chamwino kuwa jiji, wakati siyo.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Nashon Bidyanguze ambaye ni mpiga kura wake kutoka Uvinza. *(Makofi)*

Wapo wageni 100 wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David ambao ni Makatibu Wenezi wa Matawi kutoka Same Magharibi, Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Haya ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na tunao wageni 12 ambao ni Viongozi wa Idara ya Udhibiti Ubora wa Shule kutoka Wilaya ya Bahi, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 88 na walimu saba wa Shule ya Awali na Msingi ya *Peter Vigne* kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndiyo wageni tulionao hapa Bungeni. Ninalo tangazo linguine, tangazo hili ni la Wafanyakazi Bora wa Ofisi ya Bunge waliotangazwa kwa mwaka 2024.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba Siku ya Jumatano tarehe 01 Mei, 2024 ilikuwa ni Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Kitaifa ambapo yalifanyika Jijini Arusha na Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye aliwakilishwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango.

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa sherehe hizo huwa wanatambuliwa wafanyakazi bora na kupongezwa. Leo nimewaleta ndani ya Bunge, Wafanyakazi Bora wa Ofisi ya Bunge ambao wamekaa Jukwaa la Spika ili tuwatambue na kuwapongeza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wa kwanza kabisa ni Ndugu Joakim Kindole ambaye ni Mtunza Kumbukumbu Msaidizi Daraja la Pili na huyu ndiye Mfanyakazi Bora wa Ofisi ya Bunge kwa ujumla. Naomba asimame. *(Makofi)*

Hongera sana. Huyu alipata nafasi pia ya kupewa zawadi siku ile ya tarehe 01 Mei na Mheshimiwa Makamu wa Rais.

Tunakupongeza sana na tunakushukuru kwa utumishi mzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wengine sasa ambao wamepata nafasi hii ya kuwa wafanyakazi bora, kutokana na vitengo ambavyo wanafanyia kazi na kwa utaratibu wetu hapa, *TUGHE* ndio wametuletea hawa kwamba ni washindi.

Wa kwanza ni Ndugu Said Mohamed ambaye ni Dereva Mwandamizi, Ofisi Binafsi ya Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huyo ni dereva wangu lakini siyo kwamba amepewa kwa sababu ananiendesha mimi, ahsante sana Ndugu Said *(Makofi/Kicheko)*

Yupo pia Ndugu Proscovia Rutaharatwa ambaye pia ni Mwandishi Mwendesha Ofisi Mkuu Daraja la I, Ofisi Binafsi ya Naibu Spika. Tunakupongeza sana na ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Anna Bukos ambaye ni Mwandishi Mwendesha Ofisi Mwandamizi, Ofisi Binafsi ya Katibu wa Bunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Lilybeth Mrema ambaye ni Mwandishi Mwendesha Ofisi Mkuu Daraja la I, Idara ya Huduma za Sheria, ahsante sana. *(Makofi)*

Mwingine ni Ndugu Veronica Komba - Afisa Sheria Daraja la II, Idara ya Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Mwingine ni Ndugu Mkuta Masoli - Katibu Msaidizi wa Bunge Daraja la I, Idara ya Kamati za Bunge. *(Makofi)*

Ndugu Avelini Kiwango ambaye ni Dereva Mwandamizi Idara ya Bajeti.

*(Hapa Ndugu Avelini Kiwago hakusimama)*

**SPIKA:** Hajasikia? Avelini Kiwango - Dereva Mwandamizi, Idara ya Bajeti, ahsante sana. *(Makofi)*

Ndugu Abdallah Hancha - Mkurugenzi Mwandamizi Msaidizi, Huduma ya Maktaba, ahsante sana. *(Makofi)*

*CPA* Michael Simkanga - Mhasibu Mwandamizi, Kitengo cha Fedha na Uhasibu. *(Makofi)*

Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutambua mchango mkubwa wa Mhasibu Mwandamizi. *(Makofi)*

Ndugu Kokuwaisa Gondo - Msaidizi wa Ofisi Mwandamizi, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Ndugu Tatu Kwayu - Afisa Ugavi Daraja la II - Kitengo cha Ununuzi na Ugavi. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Halima Laizer - Afisa Habari Daraja la II - Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Sarah Chanai - Mwandishi Mwendesha Ofisi Mwandamizi, Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Matilda Mosha - Afisa TEHAMA Mwandamizi, Kitengo cha TEHAMA, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Peter Magati - Katibu Msaidizi wa Bunge Mkuu II na Msaidizi wa *Sergeant-At-Arms* hapa Bungeni Kitengo cha Ulinzi na Usalama, ahsante sana. *(Makofi)*

Mwingine ni Ndugu Suleiman Miraji - Dereva Mwandamizi Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar. Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nyote natumia fursa hii kuwapongeza sana wenzetu ambao wametambuliwa kama wafanyakazi bora kwa mwaka huu wa 2024 na tunawatakia utendaji mwema wa shughuli zinazoendelea ili mwendelee kushikilia hizo nafasi ambazo wenzenu wamewaamini kwamba ninyi ndio mmeonesha jambo la tofauti. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri na Waheshimiwa Wabunge wote wanawashukuru sana. *(Makofi)*

Pia tunamshukuru sana Katibu wa Bunge kwa uongozi mzuri ambao umesababisha hawa wenzetu kuweza kutambuliwa na kutoa nafasi ya wao kuonekana wakifanya kazi nzuri. Kwa hiyo, ninampongeza sana pia Katibu wa Bunge kwa niaba yenu ninyi nyote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, liko tangazo lingine kutoka kwa kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo tarehe 7 Mei, 2024 kutakuwa na semina kuhusu mita za malipo kabla *(pre-paid water meters)*, pamoja na ufafanuzi wa matumizi ya mitambo ya uchimbaji wa visima na mabwawa itakayotolewa na Wizara ya Maji. Semina hii itafanyika mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo la mwisho ni kwamba leo wengi mlikuwa mmesimama hapa kuomba maswali ya nyongeza, lakini muda wetu ulikuwa finyu, kwa hiyo, watu waliyopewa nafasi ya kuuliza maswali ni wale wenye maswali pungufu ya sita. Maana huwa napenda kusema hivyo kwa sababu kuna watu huwa wanawaza Spika akikaa pale huwa hanioni. Huwa nakuona lakini kwa sababu umeshaonwa na Wenyeviti na Naibu Spika, basi mimi inabidi niwaone wengine pia.

Kwa hiyo, huwa napenda kusema ili watu mmjue kwamba tunajaribu kutenda haki. Tunayo orodha hapa ya kila mtu ameshauliza mara ngapi, kwa hiyo, leo wamepewa wale ambao wana pungufu ya maswali ya nyongeza sita.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namwita sasa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda, aje awasilishe hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba hotuba yangu yote iliyowekwa Mezani iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge ili nisome muhtasari wa hotuba yenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 46, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Fungu 18, Tume ya Taifa, *UNESCO*, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Fungu 46 na Fungu 18 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema, kutuwezesha kukutana leo kujadili utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Taifa *UNESCO*, kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais

wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Bunge lako Tukufu, Ndugu, jamaa na Watanzania wote; kwa kuondokewa na kiongozi wetu mpendwa Hayati Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika tutaendelea kumuenzi kwa mchango wake mkubwa katika mageuzi ya kisiasa, kiuchumi, kielimu na hususan kwa kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote kwa kuondokewa na Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakumbukwa kwa uchapakazi na umahiri wake katika usimamizi wa kazi za Serikali, ikiwemo uanzishwaji wa shule za sekondari za Kata zilizoongeza fursa ya elimu ya sekondari nchini.

Mheshimiwa Spika, naungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Ahmed Yahya Abudulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani, Zanzibar.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge mnazungumza kwa sauti sana, Waziri anashindwa kusikika. Kwa hiyo, tuzungmze kwa sauti ya chini. Najua mnaongea mambo ya muhimu sana.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani Zanzibar ambaye pia alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha salamu zangu za pole kwa kutoa pole kwa Watanzania wote waliopoteza ndugu na jamaa na kupoteza au kuharibikiwa na mali kutokana na

athari za mvua kubwa zinazoendelea nchini. Mwenyezi Mungu awape Marehemu pumziko la milele, Amina. Aidha, tunamwomba Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji majeruhi wote ili waweze kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu ya uongozi ulio mahiri na wenye weledi mkubwa. Katika kipindi cha miaka mitatu, Mheshimiwa Rais ametuongoza katika kupata mafanikio makubwa nchini ikiwemo mageuzi katika mfumo wa elimu na mafunzo yanayolenga kuandaa nguvukazi yenye maarifa, stadi na mtazamo chanya katika kuleta maendeleo endelevu ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo yake yaliyotusaidia katika kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na kufanya marekebisho kwenye mitaala ili kutoa elimu na ujuzi kulingana na mazingira ya nchi na soko la ajira. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini mimi pamoja na Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, kuongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao mahiri katika kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani, mwanamke wa tatu kushika nafasi hiyo duniani na wa kwanza kutoka Afrika. Vilevile nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimwia

Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii pia kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, Mbunge wa Madaba; na Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kwa umakini wao katika kuliongoza Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Deogratius John Ndejembi – Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu; Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa namna ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima; na Wajumbe wote wa Kamati. Aidha, naomba niwashukuru kwa kupokea, kuchambua na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka 2023/2024 na kuishauri vyema Wizara kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua na kuthamini sana mchango wa Kamati katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inachangia katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2021/2022 – 2025/2026 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020, kwa kuandaa rasilimali watu wenye ujuzi, maarifa na stadi zitakazowezesha kujenga uchumi shindani wa viwanda na kuendelea kustawisha maisha ya kila Mtanzania, kutokomeza umaskini na kuhakikisha kuwa Taifa linafikia uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia wananchi wa Jimbo la Rombo kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu, hasa mke wangu Beatrice kwa kuendelea kuwa karibu yangu na kunitia moyo na kuniwezesha kufanya kazi kwa juhudi na ari kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Fungu 46 na Fungu 18 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi 1,675,753,327,000 kwa ajili ya Fungu 46, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo shilingi 537,880,762,000 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 1,137,872,565,000 zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia Tume ya Taifa *UNESCO* Fungu 18, Wizara iliidhinishiwa kiasi cha shilingi 2,733,888,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo yanajumuisha shilingi 1,124,980,000 za Mishahara na shilingi 1,608,908,000/= za Matumizi Mengineyo.

Mhesimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya shilingi 679,362,572,548.64 ambapo kiasi cha shilingi 11,660,665,000 kilipangwa kukusanywa na idara na vitengo na shilingi 667,701,877,548.64 zilipangwa kukusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya maduhuli hayo ni kutokana na ada, malipo ya ushauri elekezi, huduma za udhibiti ubora wa shule na utoaji wa huduma mbalimbali. Hadi kufikia Aprili 15, 2024, Wizara imekusanya shilingi 397,598,746,452.42 sawa na 59% ya makadirio ambapo shilingi 11,072,869,332.29 zilikusanywa na idara na vitengo na shilingi 386,525,877,130.13 zimekusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya shilingi 537,880,762,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, matumizi ya Mishahara ni shilingi 500,957,569,000 na Matumizi Mengineyo ni shilingi 36,923,193,000.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia April, 15, 2024, Wizara imepokea jumla ya shilingi 405,900,247,712.40 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kupitia Fungu 46 sawa na 75% ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa. Aidha, kupitia Tume ya *UNESCO* Fungu 18, Wizara imepokea jumla ya shilingi 1,906,916,317.62 sawa na 70% ya fedha za matumizi ya kawaida ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,137,872,565,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani ni shilingi 979,083,678,000 na fedha za nje ni shilingi 158,788,887,000.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo, hadi kufikia Aprili 15, 2024, Wizara imepokea jumla ya shilingi 988,598,227,608.28 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, sawa na 89% ya bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliekeleza viapaumbele vitano ambavyo ni: -

(1) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo kwa Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu na kuanza utekelezaji wake kwa lengo la kuimarisha ujuzi kwa wahitimu;

(2) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali (ufundi na mafunzo ya ufundi stadi) kwa sekondari na vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

(3) Kuwezesha ongezeko la fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya msingi, sekondari na ualimu;

(4) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na

(5) Kuimarisha uwezo wa nchi katika tafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na kuandaa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023. Vilevile tumefanya mabadiliko makubwa na kuboresha mitaala ya elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu ya sekondari pamoja na mafunzo ya ualimu. Utekelezaji wa mitaala mipya umeanza kwa awamu kuanzia Januari, 2024.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuhakikisha mitaala inatekelezwa kwa ufanisi, Serikali imetoa Waraka wa Elimu Na. 5 wa mwaka 2023 wenye kutoa Mwongozo wa Utekelezaji wa Mitaala iliyoboreshwa ili kurahisisha utekelezaji wake. Uboreshaji wa sera na mitaala utaimarisha utoaji wa elimu na kuwezesha wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo, kupata elimu bora zaidi kitaaluma na pia yenye ujuzi na maarifa na kuendana na mipango ya nchi na mahitaji ya kitaaluma na ajira.

Mheshimiwa Spika, ili mitaala iliyoboreshwa iweze kutekelezwa ipasavyo, Serikali imewajengea uwezo walimu na wasimamizi kuhusu utekelezaji wa mitaala kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, imetoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa kwa wawezeshaji 11,521 wa Kitaifa ambao ni Walimu Weledi wa Darasa la Awali, Maafisa Elimu Kata, Wadhibiti Ubora wa Shule na Walimu Weledi kutoka taasisi mama zinazomiliki shule zisizo za Serikali, wakuza mitaala na wakufunzi.

Mheshimiwa Spika, pili, imewajengea uwezo viongozi wa elimu 569 wakiwemo Maafisa Elimu wa Mikoa, Maafisa Elimu Msingi, Maafisa Elimu Taaluma, Maafisa Elimu wa Elimu Maalumu

na Wadhibiti Ubora wa Shule kuhusu usimamizi na utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, imetoa mafunzo kwa walimu 182,297, sawa na 81% ya walimu wa awali na msingi kuhusu mitaala iliyoboreshwa wakiwemo walimu 155,476 wa shule za sekondari za Serikali, walimu 26,301 wa shule zisizo za Serikali na walimu 920 wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu, waliofundishwa kuhusu mitaala iliyoboreshwa na utoaji wa elimu jumuishi.

Mheshimiwa Spika, nne, imetoa mafunzo kuhusu maudhui ya ufundishaji wa somo la *english* na sayansi kwa walimu wa shule za msingi 70,717 ambapo shule za Serikali ni walimu 69,872 na shule zisizo za Serikali ni walimu 845.

Mheshimiwa Spika, tano, imetoa mafunzo ya walimu 346, walimu wa shule za sekondari 147 na zisizoza Serikali 199. Kwa Kidato cha Kwanza Mkondo wa Amali katika shule 96 ambazo zimeidhinishwa kutoa mafunzo ya Elimu ya Amali ambazo ni shule 28 za Serikali na shule 68 zisizo za Serikali ambazo zimeteuliwa rasmi kuanza kutekeleza Mtaala wa Amali kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, sita, imetoa mafunzo kwa walimu 428 wanaofundisha masomo ya historia ya Tanzania na maadili, *english*, elimu ya biashara na hisabati katika shule 96 za sekondari zilizoteuliwa kutekeleza mtaala wa kidato cha kwanza mkondo wa amali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, imechapa na kusambaza nakala 9,818,251 za mihtasari, vitabu vya Kiada na Kiongozi cha Mwalimu kwa mchanganuo ufuatao: -

(1) Nakala 509,582 za mihtasari na mitaala iliyoboreshwa ya elimu ya awali, msingi na sekondari;

(2) Nakala 8,074,326 za vitabu vya Kiada vya kimacho kwa darasa la awali, darasa la kwanza na darasa la tatu;

(3) Nakala 43,785 za vitabu vya maandishi yaliyokuzwa kwa darasa la awali, darasa la kwanza na darasa la tatu.

(4) Nakala 600,990 za vitabu vya *braille*;

(5) Nakala 1,183,568 za Viongozi vya Mwalimu; na

(6) Nakala za vitabu 6,900 vya Masomo ya Amali kwa Kidato cha Kwanza katika shule 99 ambazo zimeanza rasmi kutoa elimu kwa mkondo wa awali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa miongozo mbalimbali ili kuwezesha utekelezaji wa sera na mitaala. Miongozo hiyo ni Mwongozo wa Shule ya Nyumbani, Mwongozo wa Ziara ya Nyumbani, Mwongozo wa Ubainishaji na Upimaji wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu, Mwongozo wa Uanzishwaji na Uendeshaji wa Elimu pamoja na Mwongozo wa Utoaji wa Huduma za Kielimu, Maalumu kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalumu ili kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, wanafunzi 429 wenye kiwango cha juu cha mahitaji maalumu na changamoto ya afya, wanafundishwa masomo mbalimbali na kupata huduma ya utengamao na uchechemuzi wakiwa nyumbani.

Mheshimiwa Spika, mwisho, mwongozo wa utoaji wa elimu ya kujitegemea katika shule za awali, msingi na sekondari kwa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha miundombinu kwa ajili ya kuboresha mafunzo ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, Serikali imetekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, imebainisha shule 96 za sekondari. Kati ya hizo 28 za Serikali, na 68 binafsi ambazo zimeanza kutekeleza mitaala ya Mkondo wa Amali kwa mwaka 2024. Imekamilisha ujenzi wa vyuo 29 vya Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi. Kati ya hivyo, 25 ni vya Wilaya na vinne ni vya kiwango cha Mkoa.

Mheshimiwa Spika, pili, vyuo 25 vya *VETA* vya Wilaya vimeanza kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Aidha, Serikali imetoa vifaa vya kufundishia, mitambo na kompyuta 20 kwa kila chuo kwa lengo la kuimarisha mafunzo

Mheshimiwa Spika, tatu, imeanza ujenzi wa vyuo 64 vya *VETA* vya wilaya kikiwemo Chuo cha *VETA* Chamwino ambapo ujenzi wa Chuo hicho umekamilika kufikia 83%. Kadhalika Serikali imejenga Chuo cha *VETA* cha kiwango cha mkoa katika Mkoa wa *VETA* na ujenzi unaendelea. Ujenzi huo umejumuisha majengo 18 kwa kila chuo cha wilaya na majengo 25 kwa chuo cha mkoa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inaendelea na ujenzi wa karakana nne kwa ajili ya fani ya umeme, ufundi bomba, ujenzi na ufundi magari katika Chuo cha *VETA* cha Kihonda, ambapo ujenzi umefikia 25%. Aidha, imekamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya Chuo cha Ufundi Dodoma chenye uwezo wa kudahili wanafunzi 3,000.

Mheshimiwa Spika, nne, imekamilisha ujenzi wa *hostel* ya wanafunzi wa kike yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 436 katika Chuo cha Ufundi Arusha, ujenzi wa madarasa 10 yenye uwezo wa kuwahudumia wanafunzi 1,800 katika Chuo cha Kumbukumbu ya *Mwalimu Nyerere Campus* ya Pemba ambapo ujenzi umefikia 85% pamoja na *hostel* mbili zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 768 kila mmoja katika *Campus* ya Karume Zanzibar ambapo ujenzi umefikia 49%.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza fursa za mafunzo ya amali kupitia vyuo vya amali kwa kutekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, imeongeza udahili katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi *(Technical Education and Training Colleges)* kutoka wanafunzi 171,581 kwa mwaka 2022/2023 hadi wanafunzi 235,404 kwa mwaka 2023/2024. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa idadi ya vyuo vya elimu ya ufundi kutoka vyuo 465 vilivyokuwepo mwaka 2022/2023 hadi vyuo 474 kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, pia, imeongeza uandikishaji wa wanachuo katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi *(Vocational Education and Training Colleges)* kutoka wanafunzi 380,748 mwaka 2022/2023 hadi wanafunzi 454,935 kwa mwaka 2023/2024. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa vyuo vya mafunzo ya ufundi kutoka 687 kwa mwaka 2022/2023 hadi kufikia vyuo 880 kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi na mashirika mbalimbali katika utoaji wa mafunzo kwa vitendo kwa vyuo vya ufundi stadi kwa kutekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, imeendelea kushirikiana na taasisi na mashirika 22 kutoka sekta rasmi na kutoa fursa ya masomo kwa vitendo kwa wanafunzi 1,128 na walimu 23 kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wa mafunzo ya amali wanapata ujuzi na umahiri utakaowawezesha kujiajiri na kuajiriwa. Pia, imeanza utekelezaji wa programu ya *Integrated Training for Entrepreneurship Promotion* katika kanda saba ambapo jumla ya wanufaika 2,101 sawa na 105% ya lengo walipatiwa mafunzo katika fani za ushonaji, kilimo, uvuvi, mama lishe, mapishi na ufugaji kupitia *VETA*.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeendelea kuimarisha mafunzo kwa vitendo kupitia utaratibu wa uanagenzi kwa wanafunzi wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kuwajengea uwezo walimu 16 na walezi 19 kuhusu utekelezaji wa mafunzo ya uanagenzi pacha.

Mheshimiwa Spika, aidha, imetoa mafunzo kwa wanafunzi 376 ambapo programu za mafunzo za uanagenzi 195 na programu ya kukuza ajira na ujuzi kwa vijana 181 katika fani za umeme wa viwandani na nishati ya jua, ufundi vipuli, ufundi majokofu na utayarishaji wa vyakula.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetekeleza yafuatayo: -

(a) Imewezesha ujenzi wa shule mpya za sekondari ngazi ya kata 228 na shule 26 za Sayansi za wasichana za bweni za mikoa. Vilevile imewezesha ujenzi wa shule mpya za msingi 302 nchi nzima.

(b) Imewezesha ujenzi wa madarasa 4,140, maabara 18, mabweni 119, matundu ya vyoo 21,237 na nyumba za walimu 285 zenye uwezo wa kuchukua watumishi 452 katika shule za msingi na sekondari.

(c) Imewezesha ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa 869, maabara ya Sayansi 132 na matundu ya vyoo 1,650 katika shule mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza fursa za elimu kwa kutoa ithibati kwa shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kutekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, imesajili jumla ya shule 1,073 zilizoomba usajili na kukidhi vigezo na pili imetoa vibali vya kuanzisha shule 251 mpya zilizokidhi vigezo kati ya shule 315 zilizoomba. Kati ya shule hizo, shule za awali pekee ni 31, awali na msingi 180 na sekondari zipo 40.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kutekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, imefanya tathmini ya jumla ya asasi 7,418 zikiwemo asasi za Serikali 6,011 na zisizo za Serikali 1,407. Katika tathmini hiyo asasi zilizobainika kuwa na upungufu zilipewa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

Mheshimiwa Spika, pili, imefanya ufuatiliaji wa ushauri uliotolewa wakati wa tathmini ya jumla katika shule za msingi 1,750, za sekondari 382 na chuo cha ualimu kimoja. Ufuatiliaji ulibaini mabadiliko chanya ya vyombo vya ubora baada ya

kufanyia kazi maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika tathmini ya jumla.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha fursa ya elimu ya ualimu kwa kusajili jumla ya wanachuo 23,531 ambapo katika vyuo vya ualimu vya Serikali, wanachuo ni 23,162 na vyuo visivyo vya Serikali ni wanachuo 169. Vilevile imeendelea na ujenzi mpya wa Chuo cha Ualimu Sumbawanga, Mahonda, Dakawa na Ngorongoro ambapo ujenzi wa vyuo hivyo umefikia 95%.

Mheshimiwa Spika, umahiri wa walimu na wakufunzi ni nyenzo muhimu katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji. Ili kufikia azma hiyo Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(a) Imetoa mafunzo kwa walimu wa elimu ya awali 4,000 kuhusu ujuzi wa kufaragua dhana za kufundishia na kujifunzia zinazotokana na rasilimali zinazopatikana katika maeneo yao.

(b) Imetoa mafunzo kwa walezi na waangalizi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum 148 kuhusu namna ya kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na stadi za maisha ikiwemo ufugaji wa kuku na uanzishaji wa bustani ili waweze kujikimu.

(c) Imetoa mafunzo kwa walimu 80 wa shule za msingi na sekondari wasioona kuhusu namna ya kutumia vifaa vya kidijiti kama vile *computer* katika kufundishia na kujifunzia.

(d) Imetoa mafunzo ya ubainishaji wa watoto wenye mahitaji maalum kwa washiriki 114 wakiwemo Maafisa Elimu wa Wilaya na Mikoa, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Wauguzi, Maafisa Taaluma wa Mikoa, Walimu wa Elimu Maalum na Maafisa Elimu Maalum Wilaya katika mikoa mitano ambayo ni Tabora, Kigoma, Katavi, Kagera na Rukwa iliyokuwa chini ya wastani wa 50% ya uandikishaji wa watoto wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha upatikanaji wa vitabu kwa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi na sekondari ili kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kukuza ujuzi wa uandishi, kuhamasisha tabia ya usomaji na kuongeza machapisho katika maktaba zetu kwa kutekeleza yafuatayo: -

(a) Imefanya maadhimisho ya wiki ya usomaji vitabu mkoani Mwanza, ikiwa na kauli mbiu "Wasomaji na Wachapishaji Tukutane Maktaba." Lengo ni kuhamasisha jamii kuwa na utamaduni wa kusoma vitabu.

(b) Imeratibu mashindano ya uandishi wa insha kwa wanafunzi 442 wa shule za sekondari ambapo washindi watano wamepatikana kwa ajili ya kushiriki mashindano ya ngazi ya kikanda. Lengo la mashindano haya ni kukuza stadi na ujuzi wa uandishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini.

(c) Imeratibu utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi unaozingatia ubunifu uliofanyika tarehe 13 Aprili, 2024 ambapo Mgeni Rasmi katika hafla hiyo alikuwa ni Prof. Abdulrazak Gurnah ambaye ni mshindi wa tuzo ya *Nobel* katika Fasihi kwa mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi unaozingatia ubunifu imehusisha mashindano ya uandishi wa riwaya, mashairi na hadithi za watoto ambapo jumla ya miswada 208 ilipokelewa, ambapo washindi 10 kutoka katika kila nyanja walitunukiwa cheti kila mmoja. Katika mashindano hayo, mshindi wa kwanza alipata ngao pamoja na fedha taslimu wakati mshindi wa pili na wa tatu alipata zawadi ya fedha taslimu.

Mheshimiwa Spika, lengo la tuzo hiyo ni kuhamasisha uandishi utakaosaidia kuongeza idadi ya vitabu vilivyoandikwa na Watanzania na kutumika katika shule zetu badala ya kutegemea vitabu vilivyoandikwa nje ya nchi tu. Imeendelea kuimarisha fursa

za huduma ya maktaba nchini kwa kuendelea na ujenzi wa maktaba ya kumbukumbu ya John Pombe Magufuli, Chato.

Mheshimiwa Spika, vilevile imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wakutubi 70 wa maktaba kuhusu huduma za maktaba na matumizi ya Mfumo wa Malipo ya Serikali. Aidha, imepokea nakala za vitabu 62,777 kutoka katika taasisi mbalimbali za kielimu na kuzisambaza katika maktaba zetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha fursa na ubora wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na kuondoa vikwazo katika ufundishaji na ujifunzaji, Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(a) Imekamilisha kiunzi cha kitaifa cha kuwezesha shule zinakuwa jumuishi zaidi *(National Framework for Enabling School to become more Inclusive)*. Kiunzi hicho kimebainisha vigezo vya shule kuwa jumuishi na namna ya kufikia vigezo hivyo.

(b) Imesambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vifaa saidizi kwa ajili ya wanafunzi, wakufunzi, walimu na walimu tarajali wenye mahitaji maalum katika shule za msingi 732, vitengo 565 na shule jumuishi za sekondari 72.

(c) Imewezesha zoezi la upimaji kwa wanafunzi 935 viziwi na kubaini wanafunzi 281 wenye usikivu hafifu ambao walipatiwa *hearing aids*, wanafunzi 300 wenye maambukizi walishauriwa kwenda hospitali na wanafunzi 354 viziwi kabisa walipewa *tablet* zenye kamusi ya lugha ya alama.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la upimaji na tathmini ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu, Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(a) Imeendesha upimaji wa kitaifa wa darasa la nne wa mwaka 2023 kwa wanafunzi 1,545,530 ambao ni sawa na 91.25% ya wanafunzi waliosajiliwa. Katika upimaji huo, 83.34% ya wanafunzi walifaulu.

(b) Imeendesha mtihani wa kumaliza elimu ya msingi wa mwaka 2023 kwa watahiniwa 1,356,292 ambayo ni sawa na 97.07% ya waliosajiliwa. Katika mtihani huo, wanafunzi 1,920,960 sawa na 80.52% walifaulu mtihani wao.

(c) Imeendesha mtihani wa kidato cha nne kwa mwaka 2023 kwa watahiniwa 529,596 ambayo ni sawa na 97.47% kati ya wale waliosajiliwa. Katika mtihani huo, wanafunzi 471,427 sawa na 89.36% walifaulu.

(d) Imeendesha mtihani wa maarifa kwa wanafunzi 3,630 kati ya watahiniwa 10,953 waliosajiliwa na kufanya mtihani ambapo watahiniwa 4,339 sawa na 49.12% walifaulu.

(e) Imesajili watahiniwa 104,172 kwa ajili ya mtihani wa kidato cha sita ambao umeanza kufanyika tarehe 6 Mei, 2024 yaani jana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha elimu inayotolewa katika vyuo vinavyotoa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi kwa kutekeleza yafuatayo: -

(a) Imesajili wanafunzi 22,131 wakiwemo wasichana 2,794 kwa elimu ya sekondari kwa njia mbadala katika vituo vya elimu ya watu wazima. Vilevile imetoa mafunzo ya kisomo kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa watu wazima 6,238 katika mikoa 26.

(b) Imekamilisha moduli 11 za hatua ya kwanza na ya pili kwa ajili ya vituo 151 vya elimu ya sekondari kwa njia mbadala ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika vituo hivyo na imeongeza idadi ya vituo vya elimu ya sekondari kwa njia mbadala kutoka 168 hadi kufikia 190 kwa lengo la kuongeza fursa kwa wanafunzi waliokosa elimu kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha fursa za upatikanaji wa elimu ya juu kupitia utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo: -

(a) Imetoa mkopo kwa wanafunzi 229,652 yenye jumla ya shilingi 786,724,730,000;

(b) Imetoa ufadhili kwa wanafunzi 1,220 kupitia *Samia Scholarship*; na

(c) Imetoa mkopo kwa wanafunzi 2,299 wa ngazi ya stashahada yenye jumla ya shilingi 6,114,790,500 na mwisho imekusanya jumla ya shilingi 132,731,358,063.47 sawa na 55% ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 241kutokana na mikopo iliyoiva.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ithibati na udhibiti wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu na taasisi ya elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo: -

(a) Imeratibu maombi 144,755 ya wanafunzi walioomba kujiunga na elimu ya juu kwa ngazi ya shahada ya kwanza katika vyuo vikuu nchini kwa mwaka wa masomo 2023/2024. Kati ya maombi hayo, waombaji 133,617 sawa na 92% wamedahiliwa katika vyuo mbalimbali hapa nchini;

(b) Imefanya tathmini na kutoa ithibati ya mitaala 65 kati ya mitaala 289 iliyopokelewa kwa mchanganuo ufuatao: Ngazi ya astashahada tatu, stashahada tatu, shahada 20, stashahada ya uzamili mbili, uzamili 34 na uzamivu mitatu; na

(c) Imetathmini na kutambua tuzo 2,076 sawa na 83% ya tuzo 2,515 zilizowasilishwa kutoka vyuo vya elimu ya juu vya nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu na kuongeza fursa katika vyuo vikuu na taasisi za sayansi na teknolojia kwa kutekeleza yafuatayo: -

(a) Imeendelea kuratibu taratibu za ujenzi wa miundombinu katika *campus* 14 za vyuo vikuu ambapo ujenzi katika Chuo Kikuu cha Ardhi umefikia 48%, Chuo Kikuu cha

Sayansi na Teknolojia Mbeya *Campus* Kuu 35%, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya *Campus* ya Rukwa 45% na Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere *Campus* Kuu 15%. Aidha, zoezi la kupata wakandarasi katika *campus* zilizobakia linaendelea; na

(b) Inaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika vyuo vikuu ikiwemo kumbi za mihadhara, *hostel* za wanafunzi, madarasa na maabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na taasisi za Sayansi na Teknolojia kuwawezesha jumla ya wanafunzi 3,107 kuhudhuria mafunzo ya vitendo kwenye viwanda, kampuni na taasisi mbalimbali nchini. Vilevile imetoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 1,966 wa *cluster* ya pili na ya tatu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

Mheshimiwa Spika, pili, kuwajengea uwezo wahadhiri na watumishi waliopo katika taasisi za elimu ya juu, Serikali imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa wanataaluma 396 kutoka vyuo vya elimu ya juu wakiwemo wanafunzi 27 kutoka vyuo binafsi. Vilevile imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 24, yaani shahada tisa, astashahada 14 na stashahada moja. Aidha, imewezesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 1,557.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na nchi za nje na vyuo vikuu kwa kutekeleza yafuatayo: -

(a) Imeratibu ufadhili wa wanafunzi 23 wanaosoma nchini China kupitia programu ya *China Scholarship Council*. Vilevile imeendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi watano kutoka China wanaosoma lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

(b) Imefadhili wanafunzi 193 katika programu mbalimbali kupitia Jumuia ya Madola ya Uingereza tisa, kupitia

*Chevening UK* 17, Hungary 23, Urusi 90, Mauritius mbili na China 52.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeendelea kuimarisha tafiti kwa lengo la kutumika katika kutatua changamoto mbalimbali za jamii na kuchangia katika maendeleo ya nchi kwa kutekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, imeendelea kuratibu miradi 106 ya utafiti na ubunifu kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH)* ikiwemo miradi 34 ya utafiti na miradi 72 ya ubunifu katika vyuo vikuu, taasisi za maendeleo pamoja na vyuo vya kati vya ufundi ambapo miradi saba imekamilika na kufungwa. Utekelezaji wa miradi hiyo umewezesha upatikanaji wa bidhaa, teknolojia na kampuni changa. Kwa mfano, kampuni nne zimezalishwa na kusajiliwa kutoka katika miradi hiyo ya ubunifu na kuajiri vijana 27.

Mheshimiwa Spika, pili, imefanya tafiti 638 kupitia taasisi za elimu ya juu katika maeneo ya elimu, afya, mazingira, uongozi, viwanda, TEHAMA, usafirishaji, kilimo, ubunifu, kuzalisha bidhaa mbalimbali na kutumia taka zilizozalishwa katika mazingira ya nyumbani, tiba za wanyama, biashara, haki za binadamu, watu wenye mahitaji maalum, matumizi bora ya ardhi, usanifu na ujenzi kwa gharama nafuu wa majengo mapya, njia mbadala ya uvunaji wa maji ya mvua na imeendelea kusimamia miradi ya tafiti 169 katika maeneo yafuatayo: -

(a) Utatuzi wa migogoro ya ardhi;

(b) Matumizi bora ya ardhi;

(c) Usanifu na ujenzi wa majengo mapya kwa gharama nafuu;

(d) Njia mbadala ya uvunaji wa maji ya mvua ili kuongeza huduma ya maji katika majiji;

(e) Ubunifu na matumizi ya maeneo ya wazi katika kuzuia mafuriko;

(f) Kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia taka zilizozalishwa katika mazingira ya nyumbani; na

(g) Uzalishaji wa chakula kwa kutumia *scheme* ndogo ndogo za maji katika vijiji vilivyo karibu na mto.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi pamoja na kuhamasisha ushiriki wa jamii katika sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii kwa kutekeleza yafuatayo: -

(a) Imeandaa andiko la mradi la kuanzisha kituo cha kitaifa cha teknolojia *(National Technology Park)* na kuandaa dira ya miaka 15 ya mahitaji ya teknolojia nchini *(National Technology Roadmap)*.

(b) Imeboresha vyuo vya maendeleo ya wananchi 12 ili vitumike katika kuchagiza uibuaji na uendelezaji wabunifu na teknolojia.

(c) Imeandaa andiko la mradi, kuanzisha vituo vinne vya umahiri wa utafiti na ubunifu katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela. Aidha, vituo hivyo vitajikita katika teknolojia zinazoibukia *(emerging technology)*, bidhaa na maarifa asili *(natural products and indigenous knowledge)*, sayansi na teknolojia anga *(space science and technology),* chanjo na teknolojia za kubaini magonjwa ya binadamu na wanyama *(vaccine and diagnostic for human and animal diseases)* na teknolojia za kufundishia na kujifunzia *(education technology)*.

(d) Imetoa tuzo za watafiti kwa washindi 47 waliochapisha matokeo ya tafiti katika majarida yenye hadhi ya juu ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Juu imetoa machapisho 1,519 kati ya machapisho 1,806 yaliyolengwa

katika majarida mbalimbali ya kitaaluma kwenye ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa lengo la kuongeza maarifa katika jamii kuhusu utatuzi wa changamoto mbalimbali na kuvitangaza vyuo. Vilevile imefadhili wanataaluma 173 ili kufikia hatua ya kuchapisha machapisho katika majarida mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu Serikali imetekeleza yafuatayo: -

(a) Imeandaa mkakati wa kitaifa wa matumizi ya TEHAMA na teknolojia nyingine za kufundishia na kujifunzia kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufundishaji.

(b) Imeendelea kusimamia bunifu mbalimbali zilizobuniwa kupitia watumishi na wanafunzi ili ziweze kufikia hatua ya kuuzika sokoni. Bunifu hizo ni uundaji wa mita za malipo kabla ya matumizi, programu ya Bishamba na programu ya Leo Leo Gulio.

(c) Imewezesha Taasisi iitwayo *Ujuzi Net* kutengeneza programu ya simu kwa ajili ya kutafuta taarifa za teknolojia. Programu hiyo itaziwezesha taasisi za umma na binafsi kukusanya taarifa kuhusu teknolojia zinazopatikana katika sekta mbalimbali. Programu hii imeundwa mahususi ili kunasa taarifa katika umwagiliaji wa kilimo, taarifa za teknolojia ya afya na mitambo ya kilimo kulingana na mahitaji yaliyopokelewa.

(d) Mheshimiwa Spika, mwisho, imewezesha ubiasharishwaji wa bunifu nne ambazo ni, ushonaji, ubunifu wa mavazi, mashine za kuongeza madini joto kwenye chumvi na mashine za kufungasha bidhaa mbalimbali katika Kanda ya Dar es Salaam kupitia *VETA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha udhibiti na ukuzaji wa matumizi ya salama ya teknolojia ya nyuklia kwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Imesajili vituo vipya 43 vya miozi ayonishi *(ionizing radiation)* na kufanikisha jumla ya vituo vya mionzi

1,386, vilivyosajiliwa na vituo vipya 42, vya mionzi isiyo ayonishi *(non-ionizing radiation)* na kufikisha jumla ya vituo vya mionzi isiyo ayonishi 409, vilivyosajiliwa. Aidha, imesajili vituo vipya 36, vya mionzi na kufikia jumla ya vyanzo vya mionzi vilivyosajiliwa 1,647;

(ii) Imetoa leseni 633 za kulimiki na kutumia vyanzo vya mionzi, uingizaji nchini wa vyanzo vya miezi 95, utoaji nje ya nchi wa vyanzo vya mionzi 13 na usafirishaji wa vyanzo vya mionzi 47 ndani nchi;

(iii) Imepima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 1,980, wanaofanya kazi katika vyanzo vya mionzi katika vituo 429;

(iv) Imepima sampuli 37,717, ya vyakula na mbolea. Kati ya sampuli hizo 9,062 ziliingia nchini, sampuli 27,774 zilisafirishwa nje ya nchi na sampuli 695 zilikuwa za mbolea na tumbaku na bidhaa nyingine;

(v) Imeanzisha Ofisi kwenye Bandari ya Fumba Unguja kwa ajili ya usimamizi wa usalama na udhibiti wa vyanzo vya mionzi ayonishi *(ionizing radiation)* na mionzi isiyo ayonishi *(non-ionizing radiation)* kwa ajili ya ulinzi wa umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele vitano vyenye lengo la kuongeza ubora wa elimu kwa kuwezesha vijana wa Kitanzania kupata maarifa, ujuzi, kujiamini, kujiajiri na kuajirika. Vilevile vipaumbele vyenye kujielekeza katika kutengeneza tafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu katika agenda ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo: -

(i) Kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria na kuandaa miongozo ya utoaji wa elimu na mafunzo nchini;

(ii) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (amali na amali sanifu);

(iii) Kuongeza fursa na uimarishaji ubora wa elimu ya msingi, sekondari na ualimu;

(iv) Kuongeza fursa na uimarishaji ubora wa elimu ya juu; na

(v) Mwisho, kuendeleza tafiti matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 na mitaala kwa ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu.

Mheshimiwa Spika, aidha, itaendelea na uandaaji wa zana za utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo Toleo la 2023, ambazo ni miongozo, mfumo wa kitaifa wa tuzo na sifa linganifu *(Tanzania Qualification Framework),* sheria na kanuni, mfumo wa mtaala wa kitaifa na mfumo wa tathmini ya kitaifa katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari, ualimu, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu kwa lengo la kuwezesha ufanisi katika utekelezaji wa sera.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na maboresho ya mitaala ya elimu ya amali sanifu na elimu ya juu ili kuwezesha nchi kuandaa rasilimali watu yenye ujuzi na maarifa. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo: -

(i) Itafanya mapitio ya mitaala 171, kuandaa mitaala mipya 18, kuanzisha programu za vipaumbele 145 pamoja na matumizi ya mbinu bunifu za ufundishaji katika elimu ya juu. Aidha, itawezesha ziara za kimkakati kwa wafanyakazi wa sekta ya elimu katika nchi zenye uzoefu wa uandaaji wa rasilimali yenye maarifa na ujuzi mwenye kuchangia katika ukuaji wa kati wa Uchumi;

(ii) Itasasisha *(update)* na kuandaa mtaala mpya katika taasisi 17 za elimu ya juu;

(iii) Itahakiki mitaala 230 ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Lengo ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi mipango ya nchi, soko la ajira la kitaifa na kimataifa na kuwawezesha wahitimu kujiajiri na kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu maboresho ya elimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 kwa watendaji wa ngazi zote za elimu na mafunzo wakiwemo walimu wa shule za msingi, walimu wa shule za sekondari, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, wakufunzi wa vyuo vya ufundi, wakufunzi wa vyuo vya *VETA*, wakufunzi wa vyuo vya maendeleo ya wananchi, Maafisa Elimu Msingi, Maafisa Elimu Sekondari, Wasimamizi wa Elimu Ngazi ya Mkoa, Maafisa Elimu Kata, wadhibiti Ubora wa shule na wanataaluma kutoka Taasisi za Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na mapitio ya Sheria ya Elimu Sura 353 ili iendane na Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 Toleo la 2023. Vilevile itafanya mapitio ya sheria na miundo ya taasisi mbalimbali ikiwemo *COSTECH, TLSB, NECTA, VETA, TCU, NACTVET, TIE, TEWW* na *TEA* ili ziendane na maboresho ya sera na sheria na makubaliano mbalimbali ya kikanda na kimataifa. Vilevile itafanya maboresho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo kwa lengo la kuongeza ufanisi wake ikiwemo kurahisisha ufunguaji wa mashauri na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhuisha miongozo mbalimbali ya utoaji elimu na mafunzo nchini ili kuendana na maboresho ya mitaala ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 Toleo la 2023 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, itakamilisha mwongozo wa kuwatambua na kuwaendeleza wanafunzi wenye vipawa na vipaji na itaandaa mwongozo wa elimu jumuishi wa ufundishaji na matumizi ya

teknolojia kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufundishaji na matumizi ya teknolojia katika elimu na mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaongeza wigo wa ukusanyaji, uchakataji na utoaji wa takwimu za elimu kwa kuunganisha mifumo yote ya takwimu za elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, elimu ya juu pamoja na mifumo ya upimaji na tathmini. Maboresho hayo yatahusisha kujumuisha taarifa za shule binafsi zisizotumia mitaala ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo yatawezesha Wizara kuwa na taarifa za kila mwanafunzi, fani na programu zinazotolewa nchini na kuandaa Kitabu cha Taifa cha Takwimu Muhimu za Elimu *(Basic Education Statistics in Tanzania),* ambacho kitakuwa na taarifa za kuanzia elimu ya awali hadi elimu ya juu. Kazi ya maboresho hayo imeshaanza na inafanywa na wataalamu wa ndani kutoka vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaanzisha jukwaa shirikishi la utafiti la wadau wa elimu ambalo litatambua na kuratibu tafiti za kielimu zinazofanyika hapa nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa, maamuzi ya kimageuzi na maendeleo katika katika sekta yanazingatia taarifa, takwimu na tafiti sahihi zenye maslahi kwa sekta na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha tunaimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika agenda ya maendeleo Serikali itaendelea na Mapitio ya Sera ya Sayansi na Teknolojia ya Mwaka 1996, kwa lengo la kuandaa sera inayoakisi hali ya sasa na baadaye ya maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na sekondari za amali ili kuongeza fursa za mafunzo kwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Itawezesha ujenzi wa shule mpya za sekondari za amali za ufundi, na kati ya hizo shule 26 zitaanza kupokea wanafunzi kuanzia Januari, 2025. Ninaomba nirudie tena, itawezesha ujenzi wa shule mpya za sekondari za

amali, uhandisi 100, na kati ya hizo shule 26 zitaanza kupokea wanafunzi kuanzia Januari, 2025. Aidha ujenzi wa shule za amali utapewa kipaumbele katika maeneo ambayo hayana vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi *(VETA);*

(ii) Itaendelea na ujenzi wa vyuo 65 vya mafunzo ya ufundi stadi. Kati ya vyuo hivyo 64 ni vya wilaya na kimoja na cha ngazi ya mkoa ambacho kinajengwa Songwe. Vilevile imeongeza vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo 29 ambavyo vimeshakamilika ujenzi wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza fursa za mafunzo ya amali (elimu ya ufundi na mafunzo ya elimu stadi) katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Katika kufikia azma hiyo Serikali itatekeleza yafuatayo: -

(i) Itasajili vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi 150, ambapo vyuo vya elimu ya ufundi ni 100, na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 50; hivyo kuwa na jumla ya vyuo 504 vya elimu ya ufundi na vyuo vya 885 vya mafunzo ya ufundi stadi. Usajili wa taasisi hizo utawezesha kuongeza fursa na kutoa mafunzo kwa kuzingatia viwango na ubora;

(ii) Itadahili wanafunzi 263,718 kwa elimu ya ufundi mafunzo ya ufundi stadi, ambapo wanafunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi ni 190,518, wanafunzi wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 73,200, sawa na ongezeko la 23% ikilinganishwa na udahili wa mwaka 2023/2024;

(iii) Itatoa mkopo kwa wanafunzi wa stashahada takribani 10,000 katika fani za kipaumbele zenye uhaba wa wataalamu nchini ikiwemo fani za sayansi na ufundi; na

(iv) Itadahili wanafunzi 2,089 katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro ili kuongeza idadi ya walimu wanaofundisha vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na Vyuo vya Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu, Serikali itatekeleza yafuatayo: -

(i) Itawezesha ujenzi wa shule za sekondari za kata 226, nyumba za walimu 184 na ujenzi wa sekondari na ununuzi wa vifaa vya maabara;

(ii) Itawezesha ujenzi wa madarasa 2018, mabweni 114 kwa shule za sekondari na nyumba za walimu 658 na matundu ya vyoo 2,846, maabara 10 na vituo vya walimu *(Teachers Resources Centers)* 300, kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji; na

(iii) Itaweka nishati safi ya kupikia ili kuendelea kuhifadhi na kuimarisha mazingira katika vyuo vya ualimu 11.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha udhibiti ubora wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na vyuo vya maendeleo ya wananchi, Serikali itatekeleza yafuatayo: -

(i) Itafanya tathmini ya jumla ya asasi 6,620;

(ii) Itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa lengo la kubaini ubora katika uandikishaji, ufundishaji na ujifunzaji, usimamizi na uongozi na kutoa ushauri kwa walimu wa masomo katika taasisi 1010;

(iii) Itaendelea na ujenzi wa ofisi ya udhibiti ubora wa shule katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele na ukarabati wa ofisi nne za udhibiti ubora katika Halmashauri za Mpwawa, Chato, Mpanda na Halmashauri ya Mji wa Ifakara; na

(iv) Itanunua samani na vitendea kazi katika ofisi 210 za udhibiti ubora wa shule na itanunua magari matatu kwa ajili ya shughuli za udhibiti ubora wa shule katika Halmashauri ya Mlele, Tunduma na Serengeti.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari kwa lengo la kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi na hivyo kuboresha ufundishaji na ujifunzaji na kuchochea tabia na utamaduni wa kujisomea kwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Itachapa na kusambaza nakala za vitabu 2,000,000 vya masomo ya sayansi kwa kidato cha kwanza hadi cha nne; na

(ii) Itachapa na kusambaza vitabu vya kiada katika maandishi yaliyokuzwa na *braille* kwa darasa la pili na la nne, Sekondari kidato cha kwanza na cha sita na viongozi vya mwalimu kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa watoto wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali itaendelea kukuza ujuzi wa uandishi na kuhamasisha tabia ya usomaji na kuimarisha matumizi ya maktaba katika ngazi zote za elimu kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Itaandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Huduma za Maktaba nchini. Vilevile itaendelea kununua vitabu kwa ajili ya maktaba za mkoa na kuendeleza maktaba 15 za jamii;

(ii) Itaendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu yenye lengo la kuhamasisha uandishi na usomaji wa vitabu, kutunza historia na utamaduni wa Mtanzania na kuinua sekta ya uchapaji hapa nchini. Tuzo hizo zitatolewa kwa waandishi mahiri katika nyanja kama riwaya, hadithi fupi ma mashairi.

(iii) Itagharamia uchapaji na kununua na kusambaza kwa taasisi za elimu na maktaba vitabu vya washindi wa tuzo hiyo ya Mwalimu Nyerere.

(iv) Itaendelea kuratibu na kukuza stadi za ujuzi wa uandishi wa insha kwa walimu wa elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu nchini katika nyanja za ujenzi wa Taifa, mageuzi ya kimaendeleo ustahimilivu na maridhiano. Tutaandaa shindano maalumu la uandishi wa insha kwa wanafunzi ili kuchochea uelewa na fikra tunduizi kuhusu Falsafa ya *4Rs* ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(v) Vilevile Serikali itaendelea kuratibu shindano la uandishi wa insha kwa nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kwa wanafunzi 2,000 kwa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, Serikali itanunua vifaa vya maabara kwa ajili ya shule za sekondari 1,322 na vyuo 13 vya ualimu pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo 35 vya ualimu. Vilevile, itanunua vifaa vya kujifunzia na kemikali kwa ajili ya kufundishia na masomo ya sayansi kwa wanafunzi wa elimu kwa njia mbadala kwa hatua ya kwanza na ya pili.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaimarisha utoaji wa elimu jumuishi kwa wanafunzi na walimu wenye mahitaji maalumu kwa lengo la kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimuundo ili kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutekeleza yafutayo: -

(i) Itafanya tathmini ya awali ya kubaini hali ya usaidizi uliopo na unaohitajika kwa wanafunzi 1,000 walimu 200 wenye mahitaji maalumu kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalamu.

(ii) Itajenga uelewa kwa jamii na wadau wa elimu kuhusu elimu jumuishi kwa lengo la kuhamasisha uandishikishaji wanafunzi mwenye mahitaji maalumu;

(iii) Itawajengea uwezo maafisa 368 wa elimu maalumu msingi na sekondari kuhusu ubainishaji wa awali wa watoto wenye ulemavu, kwa lengo la kurahisisha zoezi la upimaji kwa kiwango kinachohitajika; na

(iv) Itanunua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vifaa saidizi kwa wakufunzi 105, walimu 103 na walimu tarajali 188 wenye mahitaji maalumu ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha kuimarisha huduma ya utoaji na upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wenye sifa na uhitaji, Serikali itatekeleza yafuatayo: -

(i) Itaongeza fursa za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka wanafunzi 223,201 hadi kufikia 252,245;

(ii) Itatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 40, wenye ufaulu wa juu kwenye masomo ya sayansi hususan wanafunzi wa kike waliohitimu mitihani ya Taifa ya kidato cha sita na shahada ya awali kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(iii) Itaendelea kutoa *Samia Scholarship* kwa wanafunzi waliofanya vizuri zaidi katika masomo ya sayansi;

(iv) Itaendelea kukusanya madeni ya mikopo yaliyoiva ya kiasi cha shilingi bilioni 198 kutoka sekta ya umma na kuimarisha makusanyo kutoka sekta binafsi na isiyo rasmi; na

(v) Itaanza kutoa ufadhili kwa ajili ya shahada za juu ikiwemo eneo la fani na mionzi na nyuklia.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya taasisi za elimu za juu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Itajenga miundombinu katika taasisi za elimu za juu kupitia Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Juu kwa ajili ya Mabadiliko ya Kiuchumi *(HEET)* kama ifuatavyo: Kumbi 27 za mihadhara, ofisi 302, vyumba 90 vya madarasa na vyumba 17 vya semina.

Mheshimiwa Spika, miundombinu hiyo itajengwa katika Kampasi 15 za vyuo vikuu katika mikoa ifuatayo: Kwanza, tunajenga upande wa Zanzibar, halafu tutaenda katika Mkoa wa Kagera, Lindi, Kigoma, Mwanza, Katavi, Tanga, Rukwa, Njombe, Shinyanga, Manyara, Ruvuma, Singida na Simiyu; *(Makofi)*

(ii) Vilevile itaendelea na ujenzi wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere na Teknolojia, Kampasi Kuu Butiama, ambapo chuo hicho vilevile kitajenga kampasi yake Mkoani Tabora;

(iii) Itaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika taasisi za elimu za juu, ikiwemo ujenzi wa maabara, madarasa na hosteli.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza idadi ya wanataaluma wenye sifa na kuwajengea uwezo watumishi wasio wanataaluma katika taasisi za elimu za juu ambapo itagharamia mafunzo kwa wanataaluma 308 na watumishi wasio wanataaluma 23 kwa ngazi ya umahiri na shahada ya uzamivu katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaweka mazingira wezeshi kwa kuboresha mifumo ya TEHAMA itakayounganisha taasisi za maendeleo ya tafiti, taasisi ya elimu ya juu na mifumo ya uratibu wa utafiti na ubunifu ili kurahishisha utendaji wa kazi na upatikanaji wa takwimu mbalimbali zinazohusu utafiti, ubunifu na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vilevile itaunganisha mifumo ya takwimu za elimu na mafunzo nchini kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi elimu ya juu ili kuimarisha utoaji na taarifa za elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa tuzo kwa watafiti watakaochapisha tafiti katika majarida yenye hadhi ya juu kimataifa ili kuhamasisha watafiti wa ndani kufanya utafiti na kuchapisha kazi zao katika majarida husika.

Mheshimwia Spika, vilevile Serikali itaanzisha programu itakayowezesha vijana wanaohitimu katika ngazi mbalimbali za

elimu kuendeleza mawazo yao bunifu ili yawe ya kibiashara au kampuni changa kwa ajili ya kujiajiri au kuajiriwa. Aidha, itawawezesha vijana 20 wenye vipaji na wabunifu katika masuala ya uhandisi na teknolojia kupitia programu atamizi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha matumzi ya salama ya mionzi ya nyuklia nchini, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomi itatekeleza yafuatayo:-

(i) Itaendelea kudhibiti matumizi ya mionzi nchini;

(ii) Itapima na kudhibiti viwango vya mionzi kwa wafanyakazi; na

(iii) Itaendelea na upimaji wa sampuli za vyakula, mbolea, tumbaku na bidhaa nyingine kwa ajili ya kuangalia kiwango cha mionzi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utafiti wa tiba za saratani, Serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa kituo cha utafiti wa tiba za saratani *Oncology Research Center* katika Jiji la Arusha ili kuleta tija na ufanisi katika kukabiliana na tatizo la saratani nchini pamoja na kuimarisha utafiti na uchunguzi kwa kutumia teknolojia ya nyuklia.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa *QS* Omari Juma Kipanga, Mbunge na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeza majukumu yangu na kufikia malengo ya Wizara. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu, Profesa Carolyne Ignatius Nombo; Naibu Makatibu Wakuu, Profesa James Mdoe na Dkt. Franklin Rwezimula, kwa kunipa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kutoa shukurani zangu kwa Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi na watumishi wote kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa juhudi na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, walimu, wanafunzi na wadau wote wa

elimu kwa ushirikano wao katika utekelezji wa majukumu yangu. Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa wamiliki na menejimenti za shule, vyuo na taasisi binafsi, ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu na mafunzo nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena, aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa wamiliki na menejimenti, mameneja wa shule, vyuo na taasisi binafsi ambao wameshirikiana na Serikali katika kutoa huduma za elimu na mafunzo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nawashukuru washirika wa maendeleo na wadau wote wa elimu ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa mipango na miradi ya elimu, sayansi na teknolojia. Ninaomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Afrika Kusini, Brazil, Canada, China, Cuba, Ethiopia, Finland, Hungary, India, Israeli, Italia, Japan, Kenya, Korea Kusini, Marekani, Mauritius, Misri, Norway, Sweden, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza Ujerumani, Urusi, Uturuki na Uswisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, natambua mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Napenda pia kushukuru Mashirika ya Kimataifa yaliyochangia kukamilisha miradi ya *program* za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na *Aghakan Foundation Services,* Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Africa, *British Council, Campaign for Female Education, Christian Social Services Commission, Compressive Nuclear Test Burn Treat Organisation, Foreign Commonwealth and Development Office (FCDO), Global Partnership for Education, Human Development Innovation Fund, Enter University Council for East Africa, Atomic Energy Agency, Japan International Cooperation Agency*, Jumuiya ya Madola, *Karibu Tanzania Organisation, Korea International Cooperation Agency, Plan Internation, Swedish Internation Development Agency, Tanzania Education Network, Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMET),* Umoja wa Nchi za Ulaya*, United Nations Development Program, United Nations Education Scientific and Cultural Organisations, United*

*Nations International Children Emergence Funds, United States Agency for International Development (USAIDs)* na *Water Aid.*

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Fungu 46 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,965,330,380,000 kwa mchanganuo ufuatao; shilingi 637,287,706,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara, ambapo shilingi 585,225,310,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 52,062,675,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo; shilingi 1,328,042,672,000 zinaombwa kwa ajili ya mradi wa maendeleo ambapo shilingi 1,032,393,696,000 ni fedha za ndani na shilingi 294,649,005,000 fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO* Fungu 18 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,882,154,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo mshahara ni shilingi 1,319,040,000 na matumizi mengineyo ni shilingi 1,563,114,000.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya Wizara Fungu 46 na Fungu 18 yenye jumla ya shilingi 1,968,218,534,000.

Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara, vilevile na vishkwambi vya Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF F. MKENDA (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika***, Baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa

iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua makadirio ya mapato na matumizi ya FUNGU 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na FUNGU 18 - Tume ya Taifa ya UNESCO, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa mwaka wa fedha 2023/24. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo kujadili utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24 na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Taifa ya UNESCO kwa mwaka wa fedha 2024/25.

3. ***Mheshimiwa Spika****,* ninaomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na kiongozi wetu mpendwa Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika tutaendelea kumuenzi kwa mchango wake mkubwa katika mageuzi ya kisiasa, kiuchumi na kielimu hususan kwa kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu nchini.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile ninaomba kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya uungano wa Tanzania na Watanzania wote kwa kuondokewa na Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakumbukwa kwa uchapakazi na umahiri wake katika usimamizi wa kazi za Serikali ikiwemo uanzishaji wa Shule za Sekondari za Kata zilizoongeza fursa ya elimu ya sekondari nchini.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** pia naomba kuungana na wabunge wenzangu waliotangulia kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa

kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mbeya na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil (Mb) aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani Zanzibar ambaye pia alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kuhitimisha salamu zangu za pole kwa kutoa pole kwa Watanzania wote waliopoteza ndugu na jamaa na kupoteza au kuharibikiwa na mali kutokana na athari za mvua kubwa zinazoendelea nchini. Mwenyezi Mungu awape marehemu pumziko la milele, Amina! Aidha, tunamwomba Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji majeruhi wote ili waweze kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu ya uongozi ulio mahiri na wenye weledi mkubwa. Katika kipindi cha miaka mitatu, Mheshimiwa Rais ametuongoza katika kupata mafanikio makubwa nchini ikiwemo mageuzi katika mfumo wa elimu na mafunzo yanayolenga kuandaa nguvu kazi yenye maarifa, stadi na mtazamo chanya katika kuleta maendeleo endelevu ya Taifa letu. Aidha, natoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo yake yaliyotusaidia katika kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na kufanya marekebisho kwenye mitaala ili kutoa elimu ujuzi kulingana na mazingira ya nchi na soko la ajira.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini mimi pamoja na Mheshimiwa Omary Juma Kipanga (Mb) Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuongoza Wizara hii.

9. ***Mheshimiwa Spika****,* vilevile, ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Dkt.

Doto Mashaka Biteko (Mb) Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao mahiri katika kuliongoza Taifa letu.

10. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kukupongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani; Mwanamke wa tatu kushika nafasi hiyo duniani na wa kwanza kutoka Afrika. Vilevile, ninakupongeza Mheshimiwa Spika pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa. Aidha, natumia nafasi hii kuwapongeza wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama Mbunge wa Madaba na Mheshimiwa Deo Mwanyika Mbunge wa Njombe Mjini kwa umakini wao katika kuliongoza bunge lako Tukufu.

11. ***Mheshimiwa Spika***, ninawapongeza Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mheshimiwa Zainabu Athuman Katimba (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

12. ***Mheshimiwa Spika***, napenda nimshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Makamu Mwenyekiti Musa Ramadhani Simma na wajumbe wote wa Kamati. Aidha, naomba niwashukuru kwa kupokea, kuchambua na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2023/24 na kuishauri vema Wizara kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2024/25. Natambua na kuthamini sana mchango wa Kamati katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inachangia katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano 2021/22 – 2025/26 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 kwa kuandaa rasilimaliwatu yenye ujuzi, maarifa na stadi zitakazowezesha kujenga uchumi shindani wa viwanda na kuendelea kustawisha maisha ya kila Mtanzania, kutokomeza umasikini na kuhakikisha kuwa Taifa linafikia uchumi wa kati.

13. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kuwashukuru pia wananchi wa Jimbo la Rombo kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu hasa mke wangu mpendwa Beatrice kwa kuendelea kuwa karibu yangu na kunitia moyo na kuniwezesha kufanya kazi kwa juhudi na ari kubwa.

14. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya utelekezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25.

## B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24

### TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI

15. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 1,675,753,327,000.00** kwa ajili ya FUNGU 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo **Shilingi 537,880,762,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,137,872,565,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO - FUNGU 18 Wizara iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 2,733,888,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha **Shilingi 1,124,980,000.00** za Mishahara na **Shilingi 1,608,908,000.00** za Matumizi Mengineyo.

### *Ukusanyaji wa Maduhuli*

16. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara kupitia FUNGU 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 679,362,572,548.64** ambapo kiasi cha **Shilingi 11,660,695,000.00** kilipangwa kukusanywa na idara na vitengo na **Shilingi 667,701,877,548.64** zilipangwa kukusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli hayo ni kutokana na ada, malipo ya ushauri elekezi, huduma za Uthibiti Ubora wa Shule na utoaji wa huduma mbalimbali.

17. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili 15, 2024 Wizara imekusanya **Shilingi 397,598,746,452.42** sawa na **asilimia 59** ya makadirio ambapo **Shilingi 11,072,869,322.29** zimekusanywa na idara na

vitengo na **Shilingi 386,525,877,130.13** zimekusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

*Matumizi ya Kawaida*

18. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 537,880,762,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya mishahara ni **Shilingi 500,957,569,000.00** (idara na vitengo **Shilingi 83,200,218,000.00** na Taasisi ni **Shilingi 417,757,351,000.00)** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 36,923,193,000.00** (idara na vitengo ni **Shilingi 26,416,806,658.00** na Taasisi **Shilingi 10,506,386,342.00**).

19. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili 15, 2024, Wizara imepokea Jumla ya **Shilingi 405,900,247,712.40** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46 sawa na **asilimia 75** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO – Fungu 18 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 1,906,916,317.62** sawa na **asilimia 70** ya fedha ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

*Miradi ya Maendeleo*

20. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,137,872,565,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi 979,083,678,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 158,788,887,000.00.**

21. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili 15, 2024, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 988,594,227,608.28** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 87** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 900,697,116,186.31** ni fedha za ndani na **Shilingi 87,897,111,421.97** ni fedha za nje.

**C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA**

22. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/24 Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitekeleza vipaumbele vitano ambavyo ni:

(i) Kukamilisha Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka

2014 na Mitaala ya Elimu na kuanza utekelezaji wake kwa lengo la kuimarisha ujuzi kwa wahitimu;

(ii) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali (ufundi na mafunzo ya ufundi stadi) kwa sekondari na vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

(iii) Kuwezesha Ongezeko la fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya msingi, sekondari na ualimu;

(iv) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na

(v) Kuimarisha uwezo wa nchi katika tafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

**a. *Kuhuisha Sera na Sheria, na Utoaji wa Miongozo ya Elimu na Mafunzo Nchini.***

23. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imekamilisha Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na kuandaa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023. Vilevile, tumefanya mabadiliko makubwa na kuboresha mitaala ya elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu ya sekondari, pamoja na mafunzo ya ualimu. Utekelezaji wa mitaala mipya imeanza kwa awamu kuanzia Januari 2024. Aidha, katika kuhakikisha mitaala inatekelezwa kwa ufanisi, Serikali imetoa Waraka wa Elimu Na. 5 wa mwaka 2023 wenye kutoa mwongozo wa utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa ili kurahisisha utekelezaji wake. Uboreshaji wa sera na mitaala utaimarisha utoaji wa elimu na kuwezesha wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kupata elimu bora zaidi kitaaluma na pia yenye ujuzi na maarifa yenye kuendana na mipango ya nchi na mahitaji ya kitaaluma na ajira.

24. **Mheshimiwa Spika**, ili mitaala iliyoboreshwa iweze kutekelezwa ipasavyo Serikali imewajengea uwezo walimu na wasimamizi kuhusu utekelezaji wa mitaala kama ifuatavyo:

(i) imetoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa kwa wawezeshaji 11,521 kama ifuatavyo: wawezeshaji wa kitaifa 116; walimu weledi wa darasa la awali 5,201; maafisa elimu kata

3,945, wathibiti ubora wa shule 1,669; na walimu weledi kutoka taasisi mama zinazomiliki shule zisizo za Serikali 191, wakuza mitaala 73, wakufunzi 286, maafisa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia 20 na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa 20;

(ii) imewajengea uwezo viongozi wa elimu 569 wakiwemo Maafisa Elimu wa Mikoa 26, Maafisa Elimu Msingi 184, Maafisa Elimu Taaluma 184, Maafisa Elimu 175 wa Elimu Maalum na Wathibiti Ubora wa Shule 184 kuhusu usimamizi na utekelezaji wa mitaala mipya iliyoboreshwa;

(iii) imetoa mafunzo kwa walimu 181,777 sawa na asilimia 81 ya walimu wa awali na msingi kuhusu mtaala ulioboreshwa wakiwemo walimu 155,476 (walimu wa darasa la awali 7,457 na darasa la I – VII walimu 148,019) wa shule za Serikali na 26,301 (awali 6,248 na darasa la I – VII walimu 20,053) wa shule zisizo za Serikali;

(iv) imetoa mafunzo kwa walimu 920 wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum kuhusu mtaala ulioboreshwa na utoaji wa elimu jumuishi;

(v) imetoa mafunzo kuhusu maudhui ya Ufundishaji wa Somo la English na Sayansi kwa walimu wa shule ya msingi 70,717 (shule za Serikali 69,872 na shule zisizo za Serikali 845);

(vi) imetoa mafunzo ya walimu 346 (walimu wa shule za Serikali 147 na zisizo za Serikali 199) wa Kidato cha Kwanza Mkondo wa Amali katika shule 96 (shule za Serikali 28 na zisizo za Serikali 68) ambazo zimeteuliwa kuanza kutekeleza Mtaala wa Amali Mwaka 2024;

(vii) imetoa mafunzo kwa walimu 428 wanaofundisha masomo ya Historia ya Tanzania na Maadili, English, Elimu ya Biashara na Hisabati katika shule 96 za sekondari zilizoteuliwa kutekeleza mtaala kwa kidato cha kwanza Mkondo wa Amali; na

(viii) imechapa na kusambaza nakala 9,818,251 za mihtasari, vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu kwa mchanganuo

ufuatao: nakala 509,582 za mihtasari na mitaala iliyoboreshwa ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari, nakala 8,074,326 za vitabu vya kiada vya kimacho kwa darasa la awali, darasa la I na la III, nakala 43,785 za vitabu vya maandishi yaliyokuzwa kwa darasa la awali, darasa la I na la III, nakala 6,990 za vitabu vya breli, nakala 1,183,568 za kiongozi vya mwalimu na nakala za vitabu 6,900 vya masomo ya amali kwa kidato cha kwanza katika shule 96 (Serikali 28 na zisizo za Serikali 68).

25. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Serikali imetoa miongozo mbalimbali kwa lengo la kurahisisha na kuwezesha utekelezaji wa Sera na Mitaala. Miongozo hiyo ni:

(i) Mwongozo wa Shule ya Nyumbani; Mwongozo wa Ziara ya Nyumbani; Mwongozo wa Ubainishaji na Upimaji wa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum, Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Elimu kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum pamoja na Mwongozo wa Utoaji wa Huduma za Kielimu kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum ili kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi nchini. Aidha, wanafunzi 429 wenye kiwango cha juu cha mahitaji maalum na changamoto ya afya wanafundishwa masomo mbalimbali na kupata huduma ya utengamao na uchechemuzi wakiwa nyumbani;

(ii) Mwongozo wa Usahihishaji wa Insha katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kwa lengo la kuhamasisha ushiriki na kuongeza tija katika mashindano ya uandishi wa insha za SADC na EAC kwa wanafunzi nchini;

(iii) Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Kujitegemea katika Shule za Awali, Msingi na Sekondari Tanzania Bara wenye lengo la kuhakikisha wanafunzi wanaandaliwa katika misingi ya kumudu maisha yao na malengo ya jamii kwa ujumla;

(iv) Mwongozo wa Uandaaji, Uchapaji na Usambazaji wa Vitabu kwa Shule za Msingi na Sekondari (Primary and Secondary – Annualized Material Replenishment Plan) kwa lengo la kuwezesha uchapaji na usambazaji unaozingatia hali halisi ya mahitaji ya vitabu na upatikanaji wa rasilimali fedha;

(v) Mwongozo wa Kubadilishana Walimu na Wanafunzi Kusoma katika Vyuo vya Kikanda vinavyotekeleza Mradi wa Kukuza Ujuzi Afrika Mashariki vilivyopo katika nchi ya Tanzania, Kenya na Ethiopia wenye lengo la kuongeza fursa za elimu na upatikanaji wa maarifa na ujuzi kutoka nchi zilizo katika makubaliano hayo;

(vi) Mwongozo wa Mafunzo ya Uandaaji, Mapitio, Ufundishaji na Tathmini ya Mitaala ya Elimu Inayozingatia Ujuzi (Training Manual on CBET Curricula Development/Review, Delivery and Assessment) wenye lengo la kuhakikisha wanafunzi wanafundishwa stadi na ujuzi utakaowawezesha kumudu mafunzo na maisha kwa ujumla;

(vii) Mwongozo wa Uthibiti Ubora katika Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET Quality Assurance Handbook) kwa ajili ya kuongeza ubora wa mafunzo katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi yaani vyuo vya mafunzo ya amali;

(viii) Mwongozo wa Uandaaji wa Mitaala ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET Curricula Development Manual) ili kuongeza ubora wa mafunzo ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi yaani elimu ya amali; na

(ix) Miongozo mitatu ambayo ni Business Club Guide for Secondary Schools, Mwongozo wa Kuteua Vitabu vya Fasihi kwa Shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu, (Guideline for Selecting Literacy Texts for Secondary Schools and Teacher Education) yenye lengo la kuwezesha wanafunzi kushiriki katika makundi ya kimasomo yenye lengo la kuboresha ushiriki wao katika masomo.

**b. *Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali (Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi) kwa Shule za Sekondari na Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi***

26. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuongeza fursa za mafunzo ya amali kwa shule za sekondari na vyuo vya amali kwa lengo la kuongeza uwezo wa nchi kuandaa wahitimu wenye ujuzi na maarifa ya kazi. Azma hii imetekelezwa kwa; kuimarisha

mazingira ya ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu ya amali, na kuongeza fursa na ubora wa mafunzo ya amali katika taasisi za umma. Utekelezaji huo umewezesha Serikali kupata matokeo yafuatayo:

(i) imeongeza udahili katika vyuo vya elimu ya ufundi (technical education and training colleges) kutoka wanafunzi **171,581** (wanawake 93,684 na wanaume 77,897) mwaka 2022/23 hadi wanafunzi **235,804** (wanawake 114,079 na wanaume 121,725) mwaka 2023/24. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa idadi ya vyuo vya elimu ya ufundi kutoka vyuo **465** (Serikali 180 na visivyo vya Serikali 285) mwaka 2022/23 hadi vyuo **474** (Serikali 180 na visivyo vya Serikali 294) mwaka 2023/24;

(ii) imeongeza uandikishaji wa wanachuo katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi (vocational education and training colleges) kutoka wanafunzi **380,748** (wanawake 155,127 na wanaume 225,621) mwaka 2022/23 hadi wanafunzi **454,937** (wanawake 171,865 na wanaume 283,072) mwaka 2023/24. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi kutoka **687** (Serikali 124 na visivyo vya Serikali 563) mwaka 2022/23 hadi kufikia vyuo **830** (Serikali 125 na visivyo vya Serikali 705) mwaka 2023/24; na

(iii) imedahili wanafunzi 352 (wanawake 128 na wanaume 224) sawa na asilimia 53 ya lengo katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro – MVTTC kwa lengo la kuongeza idadi ya walimu wanaofundisha vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Vilevile, imedahili wanafunzi 107 (wanawake 64 na wanaume 43) wa kozi za muda mfupi na wanafunzi 245 (wanawake 64 na wanaume 181) wa kozi za muda mrefu katika chuo hicho kwa lengo la kuongeza wigo wa upatikanaji wa walimu wa amali.

27. **Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha miundombinu ya taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imebainisha shule 96 za sekondari (shule za Serikali ni 28 na

zisizo za Serikali ni 68) ambazo zimeanza kutekeleza mitaala ya amali mwaka 2024;

(ii) imekamilisha ujenzi wa vyuo 29 vya mafunzo ya ufundi na ufundi stadi kati ya hivyo 25 ni vya wilaya na vinne ni vya kiwango cha mkoa. Vyuo 25 vya VETA vya Wilaya vimeanza kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Aidha, Serikali imetoa vifaa vya kufundishia, mitambo na kompyuta 20 kwa kila chuo kwa lengo la kuimarisha mafunzo kwa vitendo;

(iii) imeanza ujenzi wa vyuo 64 vya VETA vya wilaya kikiwemo Chuo cha VETA Chamwino ambapo ujenzi wa chuo hicho umefikia asilimia 83. Kadhalika Serikali imejenga chuo cha VETA cha kiwango cha Mkoa wa Songwe. Ujenzi huo unajumuisha majengo 18 kwa kila chuo cha wilaya na majengo 25 kwa chuo cha mkoa. Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa karakana nne kwa ajili ya fani ya umeme, ufundi bomba, ujenzi na ufundi magari katika Chuo cha VETA cha Kihonda ambapo ujenzi umefikia asilimia 25;

(iv) imekamilisha ujenzi wa awamu wa kwanza ya Chuo cha Ufundi Dodoma chenye uwezo wa kudahili wanafunzi 3000. Aidha, inaendelea na taratibu za kuwezesha kudahili wanafunzi;

(v) imekarabati vyuo 14 vya maendeleo ya wananchi kwa lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa mafunzo ya amali nchini;

(vi) imekamilisha ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa kike yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 436 katika Chuo cha Ufundi Arusha kwa lengo la kuongeza ushiriki wa mtoto wa kike katika elimu ya ufundi. Vilevile, imekamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa lenye madarasa, ofisi na maabara katika chuo hicho. Aidha, inaendelea na ujenzi wa hosteli mbili, nyumba za watumishi, madarasa, ukumbi wa mihadhara, maabara na karakana tatu, jengo la utawala, canteen na power house katika Chuo cha Ufundi Arusha - Kampasi ya Kikuletwa ambapo ujenzi umefikia asilimia 94;

(vii) inaendelea na ujenzi wa madarasa 10 yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,800 katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – kampasi ya Pemba ambapo ujenzi umefikia asilimia 85. Vilevile, inaendelea na ujenzi wa ukumbi wa mikutano na jengo la utawala ambapo ujenzi umefikia asilimia 10. Aidha, inaendelea na ujenzi wa hosteli mbili zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 768 kila moja katika kampasi ya Karume Zanzibar ambapo ujenzi umefikia asilimia 49;

(viii) inaendelea na ujenzi wa jengo la maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 na ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi umefikia asilimia 96. Vilevile, imekamilisha ujenzi wa uwanja wa mpira wa kikapu na darasa, ofisi, bohari ya zahanati, chumba cha server, mifumo ya maji safi na taka, hosteli, njia za watu wenye mahitaji maalum katika Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere Kampasi Kuu ya Kivukoni; na

(ix) inaendelea na ujenzi wa ofisi tatu za kanda za NACTVET katika Mkoa wa Tabora, Mwanza na Mbeya. Aidha, imekamilisha ujenzi wa ofisi ya kanda ya Kaskazini - Mkoa wa Arusha na ofisi ya Kanda ya Kusini - Mkoa wa Mtwara.

28. **Mheshimiwa Spika**, katika eneo la ithibati na uthibiti wa mafunzo ya amali (ufundi na mafunzo ya ufundi stadi), Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imesajili vyuo 29 katika bodi za masomo zifuatazo: afya na sayansi shirikishi vyuo vinne; biashara, utalii na mipango vyuo nane; Bodi ya Sayansi na Teknolojia Shirikishi vyuo vinne na vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi 13. Aidha, imetoa ithibati kwa vyuo 40 katika bodi za masomo zifuatazo: afya na sayansi shirikishi vyuo 16; biashara, utalii na mipango vyuo 17 na sayansi na teknolojia shirikishi vyuo saba pamoja na programu 12 za ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Lengo ni kudhibiti uanzishwaji na uendeshaji wa mafunzo yasiyozingatia kanuni na taratibu za uanzishwaji wa kozi hizo;

(ii) imeidhinisha uanzishwaji wa programu 40 ili kuendesha programu za ufundi (National Technical Awards - NTA) katika bodi za masomo zifuatazo: afya na sayansi shirikishi vyuo 17; biashara, utalii na mipango vyuo 19 na sayansi na teknolojia shirikishi vyuo vinne;

(iii) imetoa Namba za Uhakiki wa Tuzo (Award Verification Number) 57,158 kwa lengo la kuimarisha uhakiki wa taarifa mbalimbali za wahitimu wa stashahada wanaoendelea na elimu ya juu pamoja na kuviwezesha vyuo kuhakiki udahili unaofanywa na Tume ya Vyuo Vikuu. Vilevile, imefanya ulinganifu wa tuzo 140 ili kuthibiti viwango vya Elimu ya Ufundi nchini;

(iv) imehakiki mitaala 117 kati ya 230 iliyoandaliwa na Vyuo vya Ufundi kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira kwa wahitimu; na

(v) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu katika shule za Amali 96 na Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi 108 kati ya lengo la vyuo 400. Aidha, shule na vyuo vilipewa ushauri wa namna ya kuboresha utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Vyuo ambavyo havikukidhi vigezo vilichukuliwa hatua stahiki ikiwemo kuvisimamisha na/au kuvifutia usajili ili kuvipa nafasi ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika.

29. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakisha wanafunzi wanapata fursa ya mafunzo kwa vitendo katika vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi na mashirika mbalimbali katika utoaji wa mafunzo kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea kushirikiana na taasisi na mashirika 22 kutoka sekta rasmi na kutoa fursa ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 1,128 (wanawake 307 na wanaume 821) na walimu 23 (wanawake 3 na wanaume 20) kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wa mafunzo ya amali wanapata ujuzi na umahiri utakaowawezesha kujiajiri na kuajiriwa. Mashirika na Taasisi zinazoshirikiana na VETA ni: Association of Tanzania Employers

(ATE), Bakhresa Co. Ltd, CUSO - Kigoma, GPSA Kigoma, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, KCB, Kigoma Garage, Kilombero Sugar Co., KUWASA Kigoma, Makandarasi, Mamlaka ya Maji Bashay, Mkwalwani, MZINGA, Prison Wood Work Industry Arusha, TANALEC, TANESCO, TANROADS Kigoma, TARURA, TEMESA, TOYOTA na TPM (1998) Ltd Morogoro;

(ii) imeendelea kubadilishana uzoefu katika masuala ya utawala, menejimenti na mafunzo kati ya VETA na nchi tano ambazo ni Afrika Kusini, China, Ujerumani, Uingereza na Kenya; na

(iii) imeanza utekelezaji wa Programu ya Integrated Training for Entrepreneurship Promotion (INTEP) katika kanda 7 (Dar es Salaam, Mashariki, Kaskazini, Ziwa, Kusini Magharibi, Magharibi na Kati) ambapo jumla ya wanufaika 2,101 (wanaume 618 na wanawake 1,483) sawa na asilimia 105 ya lengo walipatiwa mafunzo katika fani za ushonaji, kilimo, uvuvi, mama lishe, mapishi na ufugaji kupitia VETA.

30. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha mafunzo kwa vitendo kupitia utaratibu wa uanagenzi kwa wanafunzi wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kuwajengea uwezo walimu 16 na walezi 19 kuhusu utekelezaji wa mafunzo ya uanagenzi pacha. Aidha, imetoa mafunzo kwa wanafunzi 376 kupitia programu mbili zinazoratibiwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ambazo ni: Programu ya Mafunzo ya Uanagenzi 195 (wanawake 87 na wanaume 108), na programu ya kukuza ajira na ujuzi kwa vijana 181 katika fani za umeme wa viwandani na nishati ya jua, ufundi vipuri, ufundi majokofu, na utayarishaji wa vyakula.

31. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utendaji kazi wa wakufunzi na watumishi katika Vyuo vya Amali, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa wakufunzi 843 wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kuhusu upimaji na ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri;

(ii) imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 23 (uzamivu 12 na uzamili 11) wa Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Vilevile, imewezesha watumishi wanne kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 55 mafunzo ya muda mrefu katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere;

(iii) imetoa mafunzo kwa wakufunzi 45 kati 150 waliolengwa katika taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa lengo la kuwaongezea uwezo wa ufundishaji wa mitaala inayoendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko la ajira; na

(iv) imetoa mafunzo ya nishati jadidifu (umeme wa nguvu za jua) kwa vijana 200 kutoka mikoa mbalimbali nchini kupitia Chuo cha Ufundi Arusha.

**c. *Kuwezesha Ongezeko la Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu***

32. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa tunakuwa na ongezeko la fursa na ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu, Serikali imeendelea kutoa ithibati kwa shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imesajili jumla ya shule 1,073 zilizoomba usajili na kukidhi vigezo ambapo; shule za awali pekee 42 (zisizo za Serikali), awali na msingi 707 (Serikali 520 na sizizo za Serikali 187), na sekondari 324 (Serikali 298 na zisizo za Serikali 26);

(ii) imetoa vibali vya kuanzisha shule 251 mpya zilizokidhi vigezo kati ya shule 315 zilizoomba. Kati ya shule hizo, shule za awali pekee 31, awali na msingi 180 na sekondari 40;

(iii) imetoa vibali vya kuanzisha huduma ya bweni kwa shule 138 kati ya 167 zilizoomba na kukidhi vigezo. Kati ya shule hizo awali na msingi 94 na sekondari 44;

(iv) imetoa vibali vya kuongeza tahasusi kwa shule 76 za sekondari

kati ya 79 zilizoomba. Aidha, imeongeza mikondo kwa shule 14 za awali na msingi zilizoomba na kukidhi vigezo; na

(v) imetoa uthibitisho kwa wamiliki 247 na mameneja 247 kati ya 326 walioomba. Kati yao, wamiliki wa shule za awali pekee walikuwa 25, awali na msingi 172, sekondari 48 na vyuo 2 vya ualimu.

33. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha ujenzi wa madarasa 4,140 (shule za msingi 4,042 na sekondari 98), maabara 18, mabweni 119, matundu ya vyoo 21,237 (msingi 20,515 na sekondari 722), na nyumba za walimu 285 zenye uwezo wa kuchukua watumishi 456. Ujenzi wa miundombinu hii ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji;

(ii) imewezesha ujenzi wa shule mpya za sekondari ngazi ya kata 228 na shule 26 za Sayansi za wasichana za bweni za mikoa. Vilevile, imewezesha ujenzi wa shule mpya za msingi 302 nchi nzima; na

(iii) imewezesha ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa 869, maabara za sayansi 132 na matundu ya vyoo 1,650 katika shule mbalimbali nchini.

34. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisa tunaongeza matumizi na ujifunzaji wa TEHAMA katika shule zetu, Serikali imeendelea kushirikiana na Shanghai EduTech ya China ambapo ushirikiano huo umewezesha upatikanaji wa Smart Class nne zilizosambazwa kama ifuatavyo: Taasisi ya Elimu Tanzania kwa ajili ya kuendesha mafunzo endelevu kwa walimu kazini kwa njia ya TEHAMA; Shule ya Sekondari Kibaha, Shule ya Sekondari Dkt. Samia – Dodoma, na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

35. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuthibiti ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imefanya tathmini ya jumla ya asasi 7,418 zikiwemo asasi za Serikali 6,011 na zisizo za Serikali 1,407 kwa mchanganuo ufuatao; shule za awali na msingi 5,642 (Serikali 4,633 na zisizo za Serikali 1,009; shule za sekondari 1,730 ambapo za Serikali 1,351 na zisizo za Serikali 379; na vyuo vya ualimu 38 vya Serikali 19 na visivyo vya Serikali 19 pamoja na vyuo nane vya maendeleo ya wananchi). Katika tathmini hiyo asasi zilizobainika kuwa na mapungufu zilipewa ushauri wa kitaalam na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(ii) imefanya tathmini ya ufuatiliaji wa ushauri uliotolewa wakati wa tathmini ya jumla katika asasi 1,750 za shule ya msingi zikiwemo shule za Serikali 1,523 na zisizo za Serikali 227; shule za sekondari ni 382 za Serikali 176 na zisizo za Serikali 106; na chuo cha ualimu kimoja. Ufuatiliaji ulibaini mabadiliko chanya ya viwango vya ubora baada ya kufanyia kazi maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika tathmini ya jumla; na

(iii) imefanya tathmini maalum katika asasi 2,060 (Serikali 1,265 na zisizo za Serikali 795) kwa mchanganuo ufuatao: tathmini ya usajili asasi 1,114 (Serikali 780 na zisizo za Serikali 334) zikiwemo shule za awali na msingi 737 (Serikali 470 na zisizo za serikali 267) shule za sekondari 376 (Serikali 310 na zisizo za Serikali 66) na chuo kimoja cha ualimu kisicho cha Serikali; tathmini ya matukio ya tuhuma asasi 222 (Serikali 125 na zisizo za Serikali 97) zikiwemo shule za awali na msingi 113 (Serikali 61 na zisizo za Serikali 52) na shule za sekondari 109 (Serikali 64 na zisizo za Serikali 45); na tathmini ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mitaala mipya ya elimu ya awali, darasa la I na la III pamoja na elimu ya amali imefanyika katika asasi 724 (Serikali 360 na zisizo za Serikali 364) zikiwemo shule za awali na msingi 628 (Serikali 332 na zisizo za Serikali 296) na shule za sekondari 96 (Serikali 28 na zisizo za Serikali 68).

36. **Mheshimiwa Spika**, vilevile Serikali imeendelea kufuatilia ufundishaji, ujifunzaji na mazingira ya utoaji wa elimu kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kama ifuatavyo:

(i) imefanya ufuatiliaji wa upimaji wa matokeo ya ujifunzaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu katika madarasa ya elimu ya awali, darasa I na II katika Mkoa wa Njombe, Singida,

Arusha, Manyara, Lindi, Mtwara, Iringa, Mwanza, Tabora, Dar es Salaam, Rukwa, Mara, Mbeya na Shinyanga;

(ii) imefanya ufuatiliaji wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) katika mikoa 26 Tanzania Bara na kutoa ushauri wa kuboresha ufundishaji;

(iii) imefanya ufuatiliaji katika shule 240 (msingi 120 na sekondari 120) kwenye mikoa 15 ya Tanzania Bara kwa lengo la kupata taarifa za uboreshaji wa miundombinu ya shule ili kutokomeza maambukizi ya Kifua Kikuu (TB) katika shule za msingi na sekondari nchini;

(iv) imefanya ufuatiliaji kuhusu ufanisi wa njia za ufundishaji na ujifunzaji katika shule 84 zenye madarasa ya elimu ya awali na msingi katika halmashauri 28 za mikoa 14 ambayo ni: Njombe, Shinyanga, Singida, Tabora, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Manyara, Lindi, Morogoro, Rukwa, Mwanza Arusha na Mara;

(v) imefanya ufuatiliaji wa utoaji elimu maalum na jumuishi katika mikoa 20 na shule 100 (msingi 74 na sekondari 26) zinazopokea wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kubaini hali ya ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kutoa ushauri stahiki;

(vi) imefanya ufuatiliaji katika vituo vya kutolea huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Resource centres, Help Desks na miundombinu;

(vii) imetoa mafunzo kazini ya kitaalam ya elimu maalum na jumuishi, ubainishaji, Lugha ya Alama ya Tanzania na huduma zinazohitajika kwa wanafunzi wenye ulemavu kwa walimu 3,383 wakiwemo walimu wa elimu maalum 1,981, wahadhiri na watumishi wasio wahadhiri 2,183 kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - MUST, Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia (NMAIST), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Chuo Kikuu cha Mwl. Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia (MJNUAT) kuhusu elimu maalum na jumuishi; na

(viii) imefanya ufuatiliaji na tathmini katika asasi za elimu zinazopokea wanafunzi wenye mahitaji maalum zikiwemo shule 66 za elimu ya awali, shule 38 za sekondari, vituo 10 vya elimu changamani kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi, na vituo 14 vya mpango wa uwiano kati ya elimu na jamii. Ufuatiliaji ulilenga kutoa ushauri wa kitaalamu wa namna ya kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu pamoja na kuwahimiza kuandaa mipango kazi binafsi.

37. **Mheshimiwa Spika**, umahiri wa walimu na wakufunzi ni nyenzo muhimu katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji. Ili kufikia azma ya kuwa na walimu mahiri, Serikali, imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa walimu wa elimu ya awali 4,000 kuhusu ujuzi wa kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia zinazotokana na rasilimali zinazopatikana katika maeneo yao;

(ii) imetoa mafunzo kwa walezi na waangalizi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum 148 kuhusu namna ya kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na stadi za maisha ikiwemo ufugaji wa kuku na uanzishaji wa bustani ili waweze kujikimu. Vilevile, imetoa mafunzo kwa walimu 80 wa shule za msingi na sekondari wasioona kuhusu namna ya kutumia vifaa vya kidijiti kama vile kompyuta katika kufundishia na kujifunzia;

(iii) imetoa mafunzo kwa walimu 198 wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji;

(iv) imetoa mafunzo ya ubainishaji wa watoto wenye mahitaji maalum kwa washiriki 114 wakiwemo maafisa elimu wa mikoa mitano, maafisa ustawi wa jamii 26, maafisa wauguzi 26, maafisa taaluma wa mikoa mitano, walimu wa elimu maalum 26 na maafisa elimu maalum wilaya 26 katika mikoa mitano ambayo ni Tabora, Kigoma, Katavi, Kagera na Rukwa iliyokuwa na chini ya wastani wa asilimia 50 ya uandikishaji wa watoto wenye mahitaji maalum. Vilevile, imefanya ubainishaji na upimaji katika vituo saba nje ya mfumo rasmi, vituo sita vya mpango wa uwiano kati ya elimu na jamii na vituo vitatu vya

elimu changamani kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi kwa lengo la kubaini changamoto zinazowakabili na kutoa ushauri; na

(v) imewezesha ununuzi wa vifaa vya kompyuta za mezani 573, UPS 573 na projekta 160 kwa ajili ya kuimarisha uendeshaji wa vituo vya walimu (Teachers' Resource Centre - TRC).

38. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuboresha upatikanaji wa vitabu kwa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi na sekondari ili kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imefanya tathmini na kutoa ithibati ya aina 22 za vitabu vya ziada vya mitaala iliyoboreshwa, mitaala inayoendelea vitabu 156 na maudhui 18 ya kielektroniki;

(ii) imefanya tathmini na kutoa ithibati kwa miswada ya vitabu 162 kati ya 203 kutoka kwa wachapaji binafsi;

(iii) imeandaa Moduli 12 za mafunzo kwa darasa la awali, I, na III kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa watekelezaji wa mitaala mpya;

(iv) imeandaa mitaala nane na mihtasari 114 katika ngazi ya elimu ya awali, msingi (darasa I - VI), Sekondari (kidato cha 1 – 4 na kidato cha 5-6) na ualimu (elimu ya awali, msingi, elimu maalum na mafunzo ya ualimu wa karakana);

(v) imekamilisha kutafsiri mihtasari 23 ya elimu ya ualimu na aina 93 za vitabu vya mtaala ulioboreshwa wa darasa la elimu ya awali, darasa la I na III, na kidato cha kwanza mkondo wa amali. Kati ya vitabu hivyo aina 34 ni vya darasa la awali, I na III kwa lugha ya kiingereza kwa ajili ya shule zinazotumia lugha hiyo kufundishia. Vilevile, vitabu aina 19 vya darasa la awali, I na III vimebadilishwa kuwa katika maandishi makubwa kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na aina 19 nyingine katika maandishi ya breli kwa ajili ya wanafunzi wasioona na aina 31 za vitabu vya kiada kwa kidato cha 5 na 6;

(vi) imechapa na kusambaza vitabu vya kiada nakala 2,681,800 vya sekondari vya masomo ya sayansi na hisabati kidato cha 1 -

4; nakala 4,776,461 za vitabu vya darasa la IV - VII; na nakala 4,000,000 za vitabu vya hadithi kwa elimu ya awali, darasa I na II; na

(vii) imechapa na kusambaza nakala 6,060 za vitabu vya breli kwa ajili ya wanafunzi wa awali kwa lengo la kutoa fursa sawa kwa wanafunzi wote.

39. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, vitabu vyote vilivyochapwa na kusambazwa vinapatikana pia katika maktaba mtandao ambapo wanafunzi na walimu wanaweza kuvipata bila gharama yoyote ya kuunganishwa kwa mtandao (Zero - Rating) na hivyo kurahisisha upatikanaji wake.

40. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha tunaongeza hamasa katika uandishi wa vitabu na kuongeza hali ya kupenda kusoma kwa Watanzania, Serikali imeendelea kukuza ujuzi wa uandishi, kuhamasisha tabia ya usomaji na kuongeza machapisho katika maktaba zetu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imefanya maadhimisho ya wiki ya usomaji vitabu mkoani Mwanza ikiwa na kauli mbiu '**Wasomaji na Wachapishaji Tukutane Maktaba'**, lengo ni kuhamasisha jamii kuwa na utamaduni wa kusoma vitabu;

(ii) imeratibu mashindano ya uandishi wa insha kwa wanafunzi 442 wa shule za sekondari ambapo washindi watano walipatikana kwa ajili ya kushiriki mashindano ngazi ya kikanda. Lengo la mashindano hayo ni kukuza stadi na ujuzi wa uandishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini; na

(iii) imeratibu utoaji wa tuzo ya kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi unaozingatia ubunifu uliofanyika tarehe 13 Aprili, 2024 ambapo mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa Prof. Abdulrazak Gurnah ambaye ni mshindi wa tuzo ya Nobel katika fasihi kwa mwaka 2021. Tuzo ya kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi unaozingatia ubunifu imehusisha mashindano ya uandishi wa riwaya, mashairi na hadithi za watoto ambapo jumla ya miswada 208 (riwaya 51, ushairi 97 na hadithi za watoto 60) ilipokelewa ambapo washindi 10 kutoka katika kila nyanja

walitunukiwa cheti kila mmoja. Katika mashindano hayo mshindi wa kwanza alipata ngao pamoja na fedha tasilimu wakati mshindi wa pili na wa tatu walipata zawadi ya fedha tasilimu pekee. Lengo la tuzo hiyo ni kuhamasisha uandishi utakaosaidia kuongeza idadi ya vitabu vilivyoandikwa na Watanzania na kutumika katika shule zetu badala ya kutegemea vitabu vinavyotoka nje ya nchi.

41. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma ya maktaba nchini kwa kuendelea na ujenzi wa maktaba ya Kumbukumbu ya John Pombe Magufuli – Chato na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wakutubi 70 wa maktaba kuhusu huduma za maktaba na matumizi ya mfumo wa malipo ya Serikali. Aidha, imepokea nakala za vitabu 62,777 kutoka katika taasisi mbalimbali za kielimu na kusambaza katika maktaba nchini.

42. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha fursa na ubora wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum na kuondoa vikwazo katika ufundishaji na ujifunzaji, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha Kiunzi cha Kitaifa cha Kuwezesha Shule kuwa Jumuishi zaidi (National Framework for Enabling Schools to Become More Inclusive). Kiunzi hicho kimebainisha vigezo vya shule kuwa jumuishi na namna ya kuvifikia vigezo hivyo;

(ii) imesambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vifaa saidizi kwa ajili ya wanafunzi, wakufunzi, walimu na walimu tarajali wenye mahitaji maalum katika shule za msingi 732, vitengo 565 na shule jumuishi za sekondari 72.
Vifaa hivyo ni pamoja na: Hansonet 60, Shimesikio 79, fimbo nyeupe 62, Orbit Reader 107, miwani za jua 52, magongo 29, mashine za breli zinazotumia umeme 17, vitimwendo 120, vioo-kuza vinavyotumia umeme (Electronic Magnifier) 25, kofia 43, karatasi za kuandikia maandishi ya breli box 119 na seika 89 kwa walimu wasioona kwa lengo la kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa elimu maalum. Vilevile, imewezesha utoaji wa bima za afya kwa wanafunzi 480 wenye magonjwa ya kudumu;

(iii) imewezesha zoezi la upimaji kwa wanafunzi 935 viziwi na kubaini

wanafunzi 281 wenye usikivu hafifu ambao walipatiwa hearing aids, wanafunzi 300 wenye maambukizi walishauriwa kwenda hospitali na wanafunzi 354 viziwi kabisa walipewa tablets zenye kamusi ya lugha ya alama. Vilevile, imetoa mafunzo kwa timu ya ubainishaji na upimaji 150 kutoka katika mikoa 5 iliyobainika kuwa na changamoto katika zoezi la ubainishaji na upimaji wanafunzi wenye mahitaji maalum; na

(iv) imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuwabaini na kuwaandikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum kupitia vyombo ya habari, mitandao ya kijamii na maadhimisho ya siku ya watu wenye walemavu duniani, wiki ya viziwi, siku ya fimbo nyeupe kwa wasioona, na siku ya breli na wenye ualbino. maadhimisho hayo yalifanyika katika mikoa mbalimbali.

43. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha fursa ya elimu ya ualimu kwa kusajili jumla ya wanachuo 23,331 (wanawake 11,224 na wanaume 12,107) ambapo katika vyuo vya ualimu vya Serikali wanachuo ni 23,162 na visivyo vya Serikali wanachuo ni 169. Aidha, wanachuo waliodahiliwa mwaka wa kwanza ni 9,701 (vyuo vya ualimu vya Serikali 9,642 na visivyo vya Serikali 59). Vilevile, imeendelea na ujenzi mpya wa Chuo cha ualimu Sumbawanga, Mhonda, Dakawa na Ngorongoro ambapo ujenzi wa vyuo hivyo umefikia asilimia 95. Kukamilika kwa vyuo hivyo kutawezesha upatikanaji wa mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia na kuongeza fursa ya elimu ya ualimu nchini.

44. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha tunaandaa viongozi wa kusimamia sekta ya elimu katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu nchini, Serikali kwa kupitia Wakala wa Maendeleo ya Elimu na Uongozi - ADEM imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo ya muda mrefu kwa walimu 1,903 kati ya walimu 2,147 waliolengwa katika kozi za astashahada, stashahada ya uongozi na usimamizi wa elimu, na uthibiti ubora wa shule katika kampasi ya Bagamoyo, Mbeya na Mwanza;

(ii) imetoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na usimamizi wa elimu pamoja na utawala bora wa shule kwa walimu wakuu

5,602 kati ya 6,500 waliolengwa wa shule za msingi na wawezeshaji 295 kutoka mikoa 26 ya Tanzania Bara. Lengo la mafunzo ni kuwajengea uwezo washiriki katika kuongoza, kusimamia na uendeshaji wa shule;

(iii) imewezesha mafunzo kwa watumishi 37 ambapo watumishi waliohudhuria mafunzo ya muda mrefu ni 6 na mfupi ni 31 kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi; na

(iv) inaendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa moja lenye ofisi 10 na kumbi nne za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa mara moja katika kampasi ya Mbeya ambapo ujenzi umefikia asilimia 75. Kukamilika kwa jengo hilo kutaongeza fursa ya mafunzo ya usimamizi na uthibiti ubora wa elimu kwa walimu, maafisa elimu, wathibiti ubora na wadau mbalimbali wa elimu.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika eneo la upimaji na tathmini ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) wa mwaka 2023 kwa wanafunzi **1,545,330** ambao ni sawa na asilimia **91.25** ya wanafunzi **1,693,444** waliosajiliwa. Katika upimaji huo wanafunzi **1,287,934** (wasichana **681,259** na wavulana **606,675**) sawa na asilimia **83.34** walifaulu;

(ii) imeendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) wa mwaka 2023 kwa watahiniwa **1,356,392** ambao ni sawa na asilimia **97.07** kati ya **1,397,293** waliosajiliwa. Katika mtihani huo wanafunzi **1,092,960** (wasichana **585,040** na wavulana **507,920**) sawa na asilimia **80.58** walifaulu;

(iii) imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) wa mwaka 2023 kwa wanafunzi **695,639** ambao ni sawa na asilimia **91.56** kati ya **759,799** waliosajiliwa. Katika upimaji huo wanafunzi **592,741** (wasichana **314,949** na wavulana **277,792**) sawa na asilimia **85.31** walifaulu;

(iv) imeendesha Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) wa mwaka 2023 kwa watahiniwa **529,596** ambao ni sawa na asilimia

**97.47** kati ya **543,332** waliosajiliwa. Katika mtihani huo wanafunzi **471,427** (wasichana **250,147** na wavulana **221,280**) sawa na asilimia **89.36** walifaulu.

(v) imeendesha Mtihani wa Maarifa (QT) kwa watahiniwa **8,630** kati ya watahiniwa **10,953** waliosajiliwa kufanya mtihani ambapo watahiniwa **4,239** (wanawake **2,423** na wanaume**1,816**) sawa na asilimia **49.12** walifaulu;

(vi) imesajili watahiniwa **104,172** (wasichana **46,934** na wavulana **57,238**) kwa ajili ya Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) na watahiniwa **11,534** (wanawake **5,937** na wanaume **5,597**) wa mtihani wa ualimu. Mitihani hiyo imeanza kufanyika tarehe **6 Mei, 2024**; na

(vii) imechapa na kusambaza vitabu vya taarifa za uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji na mitihani ya kitaifa nakala **429,565** za PIRA-2022 na nakala **556,559** za CIRA- 2022. Lengo la vitabu hivi husaidia walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kufanya mafunzo rekebishi katika ufundishaji na ujifunzaji na kuweka mikakati ya kuboresha.

46. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha elimu inayotolewa katika vituo vinavyotoa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imesajili wanafunzi 22,131 wakiwemo wasichana 2,794 wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala katika vituo vya elimu ya watu wazima. Vilevile, imetoa mafunzo ya kisomo kuimarisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa watu wazima 6,238 katika mikoa 26;

(ii) imekamilisha moduli 11 za hatua ya I na II kwa ajili ya vituo 151 vya elimu ya sekondari kwa njia mbadala ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika vituo hivyo;

(iii) imeongeza idadi ya vituo vya elimu ya sekondari kwa njia mbadala kutoka 168 hadi kufikia 190 kwa lengo la kuongeza fursa kwa wanafunzi waliokosa elimu kwa sababu mbalimbali;

(iv) imeendelea na ujenzi wa vituo vitano (Simiyu, Singida, Njombe, Mbeya na Katavi) kwa wanafunzi wanaosoma nje ya mfumo rasmi ili kuongeza udahili na kuwezesha wanafunzi hao kuendelea na masomo yao bila vikwazo. Vilevile,imekamilisha ukarabati wa vituo sita katika Mkoa wa Dar es Salaam, Morogoro, Ruvuma, Mbeya, Kilimanjaro na Mwanza;

(v) imewezesha wanafunzi wanaosoma elimu ya sekondari kwa njia mbadala katika vituo 168 kufanya Mtihani wa Maarifa - QT kwa watahiniwa 1,699 kati ya watahiniwa 3,513 waliosajiliwa kufanya mtihani ambapo watahiniwa 744 sawa na asilimia 44 walifaulu;

(vi) imewezesha wanafunzi wanaosoma elimu ya sekondari kwa njia mbadala katika vituo 131 kufanya mtihani wa taifa kidato cha nne kwa watahiniwa 794 kati ya watahiniwa 901 waliosajiliwa kufanya mtihani ambapo watahiniwa 550 sawa na asilimia 69 walifaulu;

(vii) imefanya uhamasishaji kwa wadau kwa lengo la kuwafikia wanafunzi walioacha shule ikiwemo wasichana waliokatiza masomo ya elimu ya sekondari kwa sababu mbalimbali ambapo wasichana 3,022 waliandikishwa kwa ajili ya kupata elimu ya sekondari kwa njia mbadala;

(viii) imesambaza vifaa na kemikali kwa masomo ya fizikia, biolojia na kemia katika vituo 190 vinavyoendesha elimu ya sekondari kwa njia mbadala;

(ix) imeanza utekelezaji wa awamu ya pili ya mpango wa elimu changamani kwa vijana walio nje ya shule katika mikoa sita ambayo ni Pwani, Tanga, Manyara, Simiyu, Singida na Shinyanga kwa lengo la kutoa fursa kwa vijana walio nje ya shule kwa kupunguza idadi ya vijana wenye umri kati ya miaka 14+ waliopo mtaani kwa kuwajengea stadi za maisha, ujasiriamali, stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, na ufundi wa awali ili kujiajiri au kuajiriwa; na

(x) imefanya maadhimisho ya juma la elimu ya watu wazima kitaifa 2023 ambapo takribani watu 650 walishiriki maadhimisho

hayo. Lengo la maadhimisho hayo ni kuhamasisha jamii kuhusu elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi.

**d. *Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu***

47. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha ithibati na uthibiti wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu maombi 144,755 ya wanafunzi walioomba kujiunga na elimu ya juu kwa ngazi ya shahada ya kwanza katika vyuo vikuu nchini kwa mwaka wa masomo 2023/24. Kati ya maombi hayo, waombaji 133,617 sawa na asilimia 92.3 wamedahiliwa katika vyuo mbalimbali nchini;

(ii) imefanya tathmini na kutoa ithibati ya mitaala 65 kati ya mitaala 289 iliyopokelewa kwa mchanganuo ufuatao: Ngazi ya astashahada 3, stashahada 3, shahada 20, stashahada ya uzamili 2, uzamili 34 na uzamivu 3;

(iii) imefanya ukaguzi katika vyuo na taasisi zinazotoa elimu ya juu 20 (kawaida 15 na kushtukiza 5) kwa lengo la kuhakiki ubora wa utoaji wa elimu ya juu. Vyuo na taasisi hizo ni: TUMA, UoA, SMMUCo, KCMUCo, MoCU, SUAT- Arusha Centre, MWECAU, NM-AIST, SUZA, SUMAIT, ZU, OUT, DUCE, MU-DCC, KIUT, RUCU, SAUT, MzU na UAUT;

(iv) imetathmini na kutambua tuzo 2,076 sawa na asilimia 83 ya tuzo 2,515 zilizowasilishwa kutoka vyuo vya elimu ya juu vya nje ya nchi. Mchanganuo wa tuzo zilizotolewa ni kama ifuatavyo; cheti 14, stashahada 84, shahada ya juu 11, shahada 1,256, post certificate 13, astashahada 26, uzamili 511 na uzamivu 161;

(v) imefanya ukaguzi kwa wakala saba zinazojishughulisha na kuwapeleka wanafunzi kwenda kusoma katika vyuo vya nje ya nchi kwa lengo la kuhuisha usajili. Ukaguzi umewezesha kusajili asasi na kampuni tano ambazo ni: Universal Career Development Pivot, Goodwill International Educational Consultancy Limited; R10 Overseas Agency and Global Scholarships; YIPT Consultancies; na Universities Abroad Representatives limited;

(vi) imetathmini na kutoa kibali kwa maombi 638 kati ya 761 yaliyowasilishwa kwa ajili ya kwenda kusoma katika vyuo vya elimu ya juu nje ya nchi; na

(vii) imeratibu maonesho ya 18 ya elimu ya juu, sayansi na teknolojia ambapo jumla ya taasisi 89 zilishiriki katika maonesho hayo. Lengo la maonesho hayo ni kutangaza fursa zilizopo katika taasisi za elimu ya juu.

48. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha fursa za upatikanaji wa elimu ya juu kupitia utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mikopo kwa wanafunzi 229,652 (mwaka wa kwanza 83,640 na wanaoendelea 146,012) yenye jumla ya **Shilingi 786,724,730,000.00**;

(ii) imetoa ufadhili kwa wanafunzi 1,220 kati ya 1,200 waliolengwa (wanafunzi wapya 915 na wanaoendelea 305) wenye jumla ya **Shilingi 6,367,169,632.00** kupitia **SAMIA Scholarship**;

(iii) imetoa mikopo kwa wanafunzi 2,299 wa ngazi ya stashahada yenye jumla ya **Shilingi 6,114,790,500.00;**

(iv) imeandaa mwongozo wa utoaji wa mikopo kwa mwaka 2023/2024. mwongozo huo umewezesha kupokea maombi na kutoa mikopo kwa ufanisi;

(v) imekusanya jumla ya **Shilingi 132,731,358,063.47** sawa na asilima 55 ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni **241** kutokana na mikopo iliyoiva;

(vi) imeanzisha kituo maalum cha kupokea simu za wateja (call center) ili kuboresha huduma kwa wateja;

(vii) imeboresha akaunti ya SIPA - Student's Individual Permanent Account kwa lengo la kutunza taarifa za miamala ya wanafunzi wanufaika katika kipindi chote cha masomo na wakati wa kurejesha mkopo; na

(viii) imetoa ufadhili kwa wanafunzi 13 (wanawake 5 na wanaume 8) waliopata ufaulu wa juu katika mtihani wa taifa wa kidato cha sita katika tahasusi za sayansi kupitia chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

49. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na nchi za nje na vyuo vikuu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu ufadhili wa wanafunzi 23 wanaosoma nchini China kwa mwaka 2023/24 kupitia programu ya China Scholarship Council -CSC;

(ii) imeendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi watano wa kutoka China wanaosoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(iii) imefadhili wanafunzi 193 katika programu mbalimbali kupitia Jumuiya ya Madola ya Uingereza 9, Chevening UK 17, Hungary 23, Urusi 90, Mauritius 2 na China 52;

(iv) imeratibu zoezi la kuwapeleka wanafunzi 260 nchini Israeli kwa ajili ya mafunzo ya kilimo na mafunzo elekezi; na

(v) imeingia makubaliano na wadau watano wa nje ya nchi ambao ni Huanggang Polytechnic College, Dongying Vocational Institute, Beijing Institute of Technology, Shandong Vocational College of Science and Technology, Chongqing Water Resources and Electric Engineering College katika nyanja mbalimbali za Teknolojia. Lengo la makubaliano hayo ni kuimarisha ushirikiano na taasisi na mashirika ya maendeleo ya ndani na nje ya nchi yatakayoleta tija kwenye nyanja za ubunifu, utafiti na taaluma kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam.

50. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu na kuongeza fursa katika vyuo vikuu na taasisi za sayansi na teknolojia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na taratibu za ujenzi wa miundombinu katika Kampasi 14 za vyuo vikuu ambapo ujenzi katika Chuo Kikuu Ardhi

umefikia asilimia 48, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kampasi kuu asilimia 35, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kampasi ya Rukwa asilimia 45 na Chuo Kikuu cha Mwl. Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia kampasi kuu asilimia 15. Aidha, zoezi la kupata wakandarasi katika Kampasi zilizobakia linaendelea;

(ii) imekamilisha ujenzi wa jengo la Ardhi Land Building wing "A" linalojumuisha studio nne zitakazokuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 160 kwa wakati mmoja, madarasa mawili yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 100 kila moja, ofisi tano za watumishi 10 katika Chuo Kikuu Ardhi. Vilevile, imekarabati madarasa 17, nyumba za watumishi tano na maabara mbili;

(iii) imeendelea na ujenzi wa majengo mapya manne katika Chuo Kikuu Ardhi Kampasi Kuu yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 6,135 na watumishi 73 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi umefikia asilimia 25. Majengo yanayojengwa ni: maabara ya matumizi anuwai (Multipurpose Laboratory) yenye jumla ya maabara saba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 760 na watumishi 15; jengo la studio lenye jumla ya vyumba 15 lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 780 na watumishi 20; jengo la karakana (Multipurpose workshops building) lenye jumla ya karakana 10 zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 495 na watumishi 20; na jengo la madarasa (multipurpose classrooms) lenye vyumba vya madarasa 28 na lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 4,100 na watumishi 18;

(iv) imeendelea na ujenzi wa maabara kuu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo ujenzi umefika asilimia 45. Vilevile, inaendelea na upanuzi wa hosteli ya Dkt. John Pombe Magufuli ambapo ujenzi umefikia asilimia 98. Aidha, imeendelea na ujenzi wa shule kuu ya Uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo ujenzi umefikia asilimia 85;

(v) imeendelea na ujenzi wa jengo la utawala katika Chuo Kikuu Mzumbe ambapo ujenzi umefikia asilimia 81. Vilevile, imekamilisha ukarabati wa hosteli ya Maria Nyerere kampasi kuu na hosteli ya burito kampasi ya Mbeya na inaendelea na

hatua za mwisho za ukamilishaji wa upanuzi wa zahanati katika Chuo Kikuu Mzumbe;

(vi) imeendelea na ujenzi wa hosteli mbili zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kila moja na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,500 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa ambapo ujenzi wa majengo hayo umefikia asilimia 35. Vilevile, imekamilisha upanuzi wa maabara ya baiolojia katika chuo hicho;

(vii) imeendelea na ujenzi wa awamu ya I ya jengo la taaluma, ukumbi wa mihadhara, Hosteli mbili katika Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam kampasi ya Mwanza ambapo ujenzi umefikia asilimia 70. Vilevile, inaendelea na ujenzi wa awamu ya II ya jengo la leather building ambapo ujenzi umefikia asilimia 35;

(viii) imeendelea na ujenzi wa jengo lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 40 kwa wakati mmoja, ofisi mbili, stoo pamoja na kumbi mbili za karakana katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kampasi ya Mwanza. Vilevile, inaendelea na ujenzi wa majengo mawili yanayojengwa katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Kampasi kuu ya Dar es Salaam. Majengo hayo ni Regional Flagship ICT Centre – RAFIC na hosteli ambapo ujenzi umefikia asilimia 50; na

(ix) imeanza ujenzi wa ofisi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika Jiji la Dodoma ambapo ujenzi umefikia asilimia 10.

51. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha na kuboresha huduma za tume ya nguvu za atomu, Serikali imekamilisha ujenzi wa maabara changamano Arusha, maabara na ofisi Dodoma, maabara ya Mwanza awamu ya II na ujenzi wa ofisi na maabara Zanzibar. Vilevile, inaendelea na ujenzi wa ofisi na maabara Dar es Salaam ambapo ujenzi umefikia asilimia 45.

52. **Mheshimiwa Spika,** Serikali pia imeendelea kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imenunua vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kemikali na vifaa vya maabara za sayansi katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa. Vilevile,imewezesha upatikanaji wa kompyuta 55 na mashine mbili za kuchapisha na kufanya uwiano wa Kompyuta kwa wanafunzi kupungua kutoka 1:21 hadi 1:20 katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa;

(ii) imenunua mashine ya kuchakata mbao na mashine ya kuchakata mazao ya asali kwa ajili ya kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine – kampasi ya Mizengo Pinda; na

(iii) imenunua projekta 31, kirudufu 2, kompyuta mpakato 47, kompyuta 78, printa saba na scanner tano kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kwa lengo la kuimairisha ufundishaji na ujifunzaji.

53. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na taasisi za sayansi na teknolojia kwa kuwawezesha jumla ya wanafunzi 3,107 (wanafunzi 517 kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya na wanafunzi 2,590 kutoka Chuo cha Ufundi Arusha) kuhudhuria mafunzo ya vitendo kwenye viwanda, kampuni na taasisi mbalimbali nchini. Vilevile, imetoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 1,966 wa "cluster" ya pili na ya tatu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

54. **Mheshimiwa Spika,** katika kuwajengea uwezo wahadhiri na watumishi waliopo katika taasisi za elimu ya juu, Serikali imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa wanataaluma 396 (umahiri 189 na uzamivu 207) kutoka vyuo vya elimu ya juu wakiwemo wanataaluma 27 kutoka vyuo binafsi. Vilevile, imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 24 (shahada 9, stashahada 14 na astashahada 1). Aidha, imewezesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 1,557 ili kuimarisha utendaji kazi.

**e. *Kuimarisha Uwezo wa Nchi Katika Tafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa Lengo la Kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda***

55. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano

na taasisi za ndani na nje ya nchi pamoja na kuhamasisha ushiriki wa jamii katika sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa andiko mradi la kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Teknolojia (National Technology Park) kitakachoongeza kasi ya uendelezaji na ubiashirishaji wa ubunifu na teknolojia zinazozalishwa nchini. Vilevile, imeandaa dira ya miaka 15 ya mahitaji ya teknolojia nchini (National Technology Roadmap) itakayowezesha Serikali na wadau wengine kuwekeza katika teknolojia zinazoakisi mahitaji ya muda mrefu;

(ii) imeboresha vyuo vya maendeleo ya wananchi 12 kwa lengo la kutumika katika kuchagiza uibuaji na uendelezaji wa bunifu na teknolojia (Upgrading 12 FDCs into Zonal/Regional Innovation and Technology Support Centers);

(iii) imeanza taratibu za kuanzisha vituo vinne vya umahiri wa utafiti na ubunifu katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela. Vituo hivyo vitajikita katika teknolojia zinazoibukia (Emerging Technologies); bidhaa na maarifa asilia (Natural Products and Indigenous Knowledge); sayansi na teknolojia za anga (Space Science and Technologies); chanjo na teknolojia za kubaini magonjwa ya binadamu na wanyama (Vaccine and Diagnostics for Human and Animal Diseases); na teknolojia za kufundishia na kujifunzia (Educational Technologies);

(iv) imekamilisha tathmini ya kampuni 50 kutoka ndani na nje ya nchi zinazotengeneza teknolojia za kufundishia na kujifunzia ambapo kampuni nane zimebainika kuwa na teknolojia zinazoweza kutumika katika mazingira yetu kufundishia na kujifunzia;

(v) imetoa tuzo za watafiti kwa washindi 47 waliochapisha matokeo ya tafiti katika majarida yenye hadhi ya juu kimataifa tuzo hizo zimeendelea kutoa hamasa kwa watafiti wa ndani kufanya tafiti bora na kuzichapisha na kuchangia katika kutumia tafiti kutatua changamoto za kijamii;

(vi) imeratibu maadhimisho ya kitaifa ya siku ya wanawake na wasichana katika sayansi yaliyofanyika tarehe 11 Februari 2024 yenye lengo la kuhamasisha ushiriki wa wanawake na wasichana katika masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Katika, maadhimisho hayo, zaidi ya wanawake na wasichana 1,500 walishiriki. Maadhimisho hayo yameendelea kuongeza ushiriki wa wanawake na wasichana kujiunga na fani za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati ambapo kwa sasa ushiriki wao ni wastani wa asilimia 39;

(vii) imeshiriki mkutano wa mawaziri wa ubunifu wa mwaka 2023 (Africa Innovation Ministerial Summit 2023) uliofanyika tarehe 30 Novemba hadi 02 Desemba 2023, katika Jiji la Kigali - Rwanda ambapo teknolojia mpya za kufundishia na kujifunzia takribani 15 zinazoweza kuboreshwa na kutumika nchini zilibainishwa; na

(viii) imeratibu ushiriki wa Tanzania katika mkutano mkuu wa 67 wa mamlaka ya kimataifa ya nguvu za atomu uliofanyika Vienna, Austria Septemba, 2023 ambapo katika mkutano huo yalijadiliwa masuala mbalimbali ya matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia ikiwemo matumizi ya Rays of Hope katika matibabu ya kansa na Atoms for Food katika uhifadhi wa mazao ya chakula.

56. **Mheshimiwa Spika,** vilevile Serikali imeendelea kuimarisha tafiti kwa lengo la kutumika kutatua changamoto mbalimbali za jamii na kuchangia katika maendeleo ya nchi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea kuratibu miradi 106 ya utafiti na ubunifu kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia - COSTECH ikiwemo miradi 34 ya utafiti na miradi 72 ya ubunifu katika vyuo vikuu, taasisi za maendeleo pamoja na vyuo vya kati vya ufundi ambapo miradi saba imekamilika na kufungwa. Utekelezaji wa miradi hiyo umewezesha upatikanaji wa bidhaa, teknolojia na kampuni changa. Kwa mfano, kampuni 4 zimezalishwa na kusajiliwa kutoka katika miradi hiyo ya ubunifu na kuajiri vijana 27;

(ii) imeandaa miradi mipya miwili ya tafiti ambayo ni: Geospatial WebInformatics System Development for Managing and

Monitoring Agri- Products in Tanzania na Business Models for Food and Market Wastes Maggot Production, Social Acceptability and Commercialisation in Tanzania kupitia Chuo Kikuu Ardhi ili kutatua changamoto kwa jamii kuhusu masuala ya upatikanaji wa taarifa za masoko ya mazao yenye kukuza uchumi wa wakulima wadogowadogo pamoja na kuzalisha bidhaa ikiwemo chakula cha kuku kutoka katika taka ngumu na hivyo kuongeza fursa za kujiajiri;

(iii) imefanya tafiti saba ambapo tafiti tano katika eneo la usalama wa mionzi, TEHAMA moja na nishati moja kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa taarifa mpya ya udhibiti wa madhara ya mionzi, uboreshaji wa mifumo ya udhibiti pamoja na kujua mahitaji ya teknolojia ya nyuklia kwenye uzalishaji wa umeme;

(iv) imeboresha Mwongozo wa Kitaifa wa Kupima Umahiri wa Watafiti wa Kisayansi (National Framework for Scientific Research Competence - NFSR). Mwongozo huo utatumika kutathmini na kukadiria kiwango (rating) cha umahiri wa watafiti wa kisayansi;

(v) imeendelea kutoa fedha kulingana na Mwongozo wa Kitaifa wa Ruzuku wa Utafiti na Ubunifu kwa miradi 16 ya ubunifu, miradi saba ya utafiti na miradi miwili kwa vituo vya utafiti;

(vi) imeendelea kusimamia jumla ya miradi 174 inayoendelea (ubunifu 133, utafiti 30 na miundombinu 11) ambayo inafadhiliwa kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE). Aidha, imefanya ufuatiliaji wa miradi ya utafiti na ubunifu 60 iliyopo Mkoa wa Lindi, Mtwara, Njombe, Mbeya, Rukwa, Arusha, Kilimanjaro, Kigoma, Tabora, Dodoma, Geita, Kagera, Mwanza, Musoma, Simiyu, Shinyanga, Morogoro, Pwani, Zanzibar na Dar es Salaam. Lengo la ufuatiliaji huo ni kuimarisha utekelezaji wa miradi hiyo;

(vii) imetoa mafunzo kwa watafiti kuhusu kuchapisha utafiti katika majarida yenye hadhi ya kimataifa ambapo jumla ya makala 33 za utafiti zilichapishwa katika Jarida la Sayansi, Teknolojia, na Ubunifu la Afrika Mashariki - EAJSTI;

(viii) imefanya tafiti 638 kupitia taasisi za elimu ya juu katika maeneo ya elimu, afya, mawasiliano, mazingira, uongozi, viwanda, TEHAMA, usafirishaji, kilimo, ubunifu na matumizi ya maeneo ya wazi katika kuzuia mafuriko, kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia taka zinazozalishwa katika mazingira ya nyumbani, tiba za wanyama, biashara, tiba, haki za binadamu, maliasili, watu wenye mahitaji maalum, matumizi bora ya ardhi, usanifu na ujenzi wa gharama nafuu wa majengo mapya, njia mbadala za uvunaji wa maji ya mvua; na

(ix) imeendelea kusimamia miradi ya tafiti 199 katika maeneo yafuatayo: utatuzi wa migogoro ya ardhi, matumizi bora ya ardhi, usanifu na ujenzi wa gharama nafuu za majengo mapya, njia mbadala za uvunaji wa maji ya mvua ili kuongeza huduma ya maji katika Majiji, ubunifu na matumizi ya maeneo ya wazi katika kuzuia mafuriko, kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia taka zinazozalishwa katika mazingira ya nyumbani na uzalishaji wa chakula kwa kutumia skimu ndogo ndogo za maji katika vijiji vilivyokaribu na mito.

57. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia taasisi za elimu ya juu imetoa machapisho 1,519 kati ya machapisho 1,806 yaliyolengwa katika majarida mbalimbali ya kitaaluma kwenye ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa lengo la kuongeza maarifa katika jamii kuhusu utatuzi wa changamoto mbalimbali na kuvitangaza vyuo. Vilevile, imefadhili wanataaluma 173 ili kufikia hatua ya kuchapisha machapisho katika majarida mbalimbali.

58. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu Serikali, imetekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa mkakati wa kitaifa wa matumizi ya TEHAMA na teknolojia nyingine za kufundishia na kujifunzia kwa lengo kuongeza ufanisi katika ufundishaji;

(ii) imetoa mafunzo ya utumiaji wa mifumo mitatu ya TEHAMA ambayo ni Students Course Evaluation Management Information System (CEMIS), Postgraduate Admission Management Information System (PAMIS) na Consultancy Management Information System (CoMIS) kwa lengo la kuboresha utendaji kazi

katika Chuo Kikuu Ardhi;

(iii) imewezesha taasisi iitwayo **UjuziNet** kutengeneza programu ya simu kwa ajili ya kutafuta taarifa za teknolojia. Programu hiyo itaziwezesha taasisi za umma na binafsi kukusanya taarifa kuhusu teknolojia zinazopatikana katika sekta mbalimbali. Programu hii imeundwa mahsusi ili kunasa taarifa katika umwagiliaji wa kilimo, taarifa za teknolojia ya afya, na mitambo ya kilimo, kulingana na mahitaji yaliyopokelewa;

(iv) imewezesha ubiasharishwaji wa bunifu nne (ushonaji, ubunifu wa mavazi, mashine za kuongeza madini joto kwenye chumvi na mashine ya kufungasha bidhaa mbalimbali (packaging machine) katika kanda ya Dar es Salaam kupitia VETA;

(v) imeendelea kusimamia bunifu mbalimbali zilizobuniwa kupitia watumishi na wanafunzi ili ziweze kufika hatua ya kuuzika sokoni, bunifu hizo ni uundaji wa mita za malipo kabla ya matumizi; programu ya Bi - Shamba na Programu ya Leo Leo Gulio; na

(vi) imesajili wabunifu 14 katika kanzi data ya wabunifu ya Tume ya Sayansi na Teknolojia - COSTECH. Kati ya wabunifu waliosajiliwa 10 walihitaji usaidizi wa fedha na wabunifu wanne waliunganishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania – TCRA.

59. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia taasisi za elimu ya juu imeendelea kuimarisha huduma za jamii na kutatua changamoto mbalimbali, kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa ushauri wa kitaalamu katika usanifu na usimamizi wa ujenzi wa ghorofa tatu wa jengo la ofisi za Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba - TMDA Dodoma; usanifu na usimamizi wa ujenzi wa uwanja wa mashujaa (National Heroes Stadium) katika mji wa Serikali Dodoma; usanifu na usimamizi wa ukarabati wa majengo ya biashara, nyumba ya uwekezaji, maisha house, NIC Kisutu, NIC Morogoro na Kihonda apartments, usanifu na usimamizi wa ujenzi wa karakana za TEMESA katika mji wa Dodoma na Geita kupitia VETA;

(ii) imetoa huduma za ushauri wa kitaalam 96 katika maeneo yafuatayo: TEHAMA, biashara, uongozi, sayansi, jamii, mazingira, kilimo, ufugaji, chakula, mazingira, usanifu na usimamizi na ushirika kwa lengo la kutatua changamoto za kijamii;

(iii) imetoa ushauri kwa wadau mbalimbali ikiwemo huduma za ugani kwa washiriki wapatao 65,210 wakiwemo wakulima, wafugaji, maafisa ugani, watafiti katika nyanja ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na uimara wa udongo; na

(iv) imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika eneo la usanifu na usimamizi wa ukarabati wa maabara za sayansi, maktaba na maabara ya TEHAMA katika vyuo saba vya Ualimu na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Dakawa, Mhonda, na Sumbawanga, ujenzi wa vyuo vinne vya VETA vya Mkoa wa Geita, Ludewa - Njombe, Rukwa na Morogoro. Vilevile, imetoa ushauri wa usanifu, tathmini na usimamizi wa ukarabati wa vyuo 31 vya maendeleo ya wananchi.

60. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha udhibiti na kukuza matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imesajili vituo vipya 43 vya mionzi ayonishi (Ionizing Radiation Facilities) na kufikisha jumla ya vituo vya mionzi 1,386 vilivyosajiliwa na vituo vipya 42 vya mionzi isiyoayonishi (Non-Ionizing Radiation Facilities) na kufikisha jumla ya vituo vya mionzi isiyoayonishi 409 vilivyosajiliwa. Aidha, imesajili vyanzo vipya 36 vya mionzi na kufikia jumla ya vyanzo vya mionzi 1,647 vilivyosajiliwa;

(ii) imetoa leseni 633 za kumiliki na kutumia vyanzo vya mionzi, uingizaji nchini wa vyanzo vya mionzi 95, utoaji nje ya nchi wa vyanzo vya mionzi 13 na usafirishaji wa vyanzo vya mionzi ndani ya nchi 47;

(iii) imetoa vyeti vya usajili 86 kati ya 100 sawa na asilimia 86 kwa wenye sifa za kufunga mitambo, matengenezo, uendeshaji wa vifaa vya mionzi;

(iv) imekagua vituo 401 kati ya lengo la vituo 450 vinavyotumia vyanzo vya mionzi. Vilevile, imekagua shehena za vyakula 19,435 kati ya shehena 15,000 zilizopangwa kufikiwa kuhusiana na mnyororo wa chakula katika sehemu za mipaka ya kuingia na kutoka kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa mionzi ya bidhaa zinazosafirishwa na kudhibiti usafirishaji haramu wa vyanzo vya mionzi;

(v) imepima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 1,980 wanaofanya kazi katika vyanzo vya mionzi katika vituo 429. Aidha, viwango vya mfiduo vilivyopokelewa katika miezi mitatu mfululizo vilianzia 0.1 hadi 3.2 millisievert (mSv), ambavyo viko ndani ya ukomo unaokubalika wa udhibiti;

(vi) imepima sampuli 37,717 za vyakula na mbolea, kati ya sampuli hizo 9,062 ziliingia nchini, sampuli 27,774 zilisafirishwa nje ya nchi na sampuli 695 zilikuwa za mbolea na tumbaku na bidhaa nyingine. Upimaji ulibaini kuwa sampuli hizo hazikuwa na madhara yoyote yatokanayo na mionzi;

(vii) imefanya matengenezo ya Vifaa 74 ya vyombo vya nyuklia kutoka Albizia 1, Dangote 1, ofisi ya Rais 1, Namanga 1, kiwanja cha ndege Mwanza 1, na Uganda Atomic Energy Council 1, Hospitali ya Bugando 4, ORCI 2, Good Samaritan Ifakara 1, mgodi wa Bulyankulu 1, Chrysos Corporation Limited 1, TAEC (KIA 3, Namanga 2, Tarakea 2, Manyovu 1, Kigoma 3,Mtwara 3 Tanga 3, Kabwe 2, Tunduma 3, TAEC SSDL 2, Mtwara 3, Dodoma 2, Sirari 2, Holili 2), Azhar Construction Co Ltd 1, Konkola Zambia 2, Tanzania Steel Pipe Ltd 1;

(viii) imeanzisha ofisi katika bandari ya fumba Unguja kwa ajili ya usimamizi wa usalama na udhibiti wa vyanzo vya mionzi ayonishi (ionizing radiation) na mionzi siyoayonishi (non ionizing) kwa ajili ya ulinzi wa umma;

(ix) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 10 ya utafiti wa kitaifa inayofadhiliwa na International Atomic Energy Agency - IAEA ambayo inatekelezwa katika Sekta ya maji, afya, kilimo na mifugo; na

(x) imeandaa mwongozo wa usalama na utunzaji, usafirishaji na uhifadhi wa urani pamoja na mwongozo wa usalama wa usanifu wa kituo cha kuhifadhi vifaa vya mionzi.

## D. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)

61. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO, imesimamia, imeratibu, imefuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikataba 10 ambayo imeridhiwa Kimataifa kama ifuatavyo:

(i) mkataba wa kulinda nyara za kiutamaduni katika kipindi cha majanga ya kivita;

(ii) kulinda tamaduni zisizoshikika; (iii)

(iii) ulinzi wa urithi wa asili na kiutamaduni;

(iv) kukataza, kuzuia uingizwaji, usafirishaji na umiliki haramu wa nyara za urithi wa kiutamaduni;

(v) ulinzi na ukuzaji wa vielelezo vya tamaduni anuai;

(vi) makubaliano ya uingizwaji wa elimu, malighafi za sayansi na utamaduni;

(vii) kupinga ubaguzi katika elimu;

(viii) utambuzi wa mafunzo, vyeti na vigezo vingine vya kitaaluma katika ngazi za juu za elimu katika ukanda wa nchi za Afrika;

(ix) kupinga matumizi ya dawa za kuongeza nguvu na mbinu haramu katika michezo; na

(x) mkataba wa ardhi oevu muhimu ya kimataifa kama ya makazi ya dubu maji.

62. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali kupitia tume ya taifa ya UNESCO imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu nchini, lengo namba nne (SDG 4) kuhusu elimu bora na usawa inayotoa fursa ya kujiendeleza kwa wote. Aidha, imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa lengo namba tano (SDG 5) kuhusu usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana;

(ii) imewajengea uelewa Wadau kwa kutoa mafunzo kuhusu umuhimu wa Tanzania kuridhia mkataba wa 2001 wa Urithi wa Chini ya Bahari (Underwater Heritage) uliokuwa na lengo la kulinda urithi wa kiutamaduni hususan kumbukizi za binadamu zenye sifa ya kiutamaduni, kihistoria na kiikolojia;

(iii) imehamasisha matumizi ya mitandao ya UNESCO (ASPNet, UNEVOC, UNITWIN) kwa wanafunzi kuanzia elimu ya awali hadi elimu ya juu kwa lengo la kubadilishana taarifa za kitaaluma, kuongeza maarifa na utendaji katika maeneo ya umahiri. Aidha, mpaka sasa taasisi 10 zimejiunga na mtandao wa ASPnet na taasisi nne na vyuo vikuu viwili vimejiunga na mtandao wa UNITWIN/UNESCO Chairs; na

(iv) imefuatilia na kutathmini maeneo mapya ya urithi yaliyopendekezwa na wadau nchini yanayotambuliwa na UNESCO kuwa maeneo ya urithi wa dunia kwa lengo la kuongeza vivutio vya utalii. Aidha, mpaka sasa maeneo ya Tendaguru katika Mkoa wa Lindi na Jozan Chwakabay Zanzibar yameingizwa katika orodha ya awali ya UNESCO (tentative list) kwa ajili ya uchambuzi wa kina.

## E. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 KWA FUNGU 46

63. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele vitano vyenye lengo la kuongeza ubora wa elimu kwa kuwezesha vijana wa Kitanzania kupata maarifa, ujuzi, kujiamini, kujiajiri na kuajirika. Vilevile, vipaumbele vyenye kujielekeza katika kutegemeza tafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu katika agenda ya maendeleo ya nchi.

64. **Mheshimiwa Spika,** vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/25 ni kama vifuatavyo:

a) kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria na kuandaa miongozo ya utoaji elimu na mafunzo nchini;

b) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (amali na amali sanifu);

c) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya msingi, sekondari na ualimu;

d) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na

e) kuendeleza tafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

**a.** ***Sera, Sheria, Mitaala na Miongozo ya Utoaji Elimu na Mafunzo Nchini***

65. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na mitaala kwa ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu. Aidha, itaendelea na uandaaji wa zana za utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 ambazo ni Miongozo, Mfumo wa Kitaifa wa Tuzo na Sifa Linganifu (Tanzania Qualification Framework – TQF), sheria na kanuni, mfumo wa mtaala wa kitaifa na mfumo wa tathmini wa kitaifa katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari, ualimu, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, na elimu ya juu kwa lengo la kuwezesha ufanisi katika utekelezaji wa sera.

66. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na maboresho ya mitaala ya elimu ya amali sanifu na elimu ya juu ili kuwezesha nchi kuandaa rasilimaliwatu yenye ujuzi na maarifa. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya mapitio ya mitaala 171, kuandaa mitaala mipya 18, kuanzisha programu za vipaumbele 145 pamoja na matumizi ya mbinu bunifu za ufundishaji katika elimu ya juu. Aidha, itawezesha ziara za kimkakati kwa wafanyakazi wa sekta ya elimu katika nchi zenye uzoefu wa uandaaji wa rasilimaliwatu yenye maarifa na ujuzi wenye kuchangia katika ukuaji wa kati wa uchumi;

(ii) itaanzisha vituo vya elimu huria (Open Education Resources - OER) ili kuimarisha majukwaa ya ndani na kuongeza fursa za

upatikanaji wa elimu ya juu;

(iii) itasasisha na kuandaa mtaala mpya katika taasisi 17 za elimu ya juu; na

(iv) itahakiki mitaala 230 ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Lengo ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi mipango ya nchi, soko la ajira la kitaifa na kimataifa na kuwawezesha wahitimu kujiajiri na kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira.

67. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 kwa watendaji wa ngazi zote za elimu na mafunzo wakiwemo walimu wa shule za msingi; walimu wa shule za sekondari; wakufunzi wa vyuo vya ualimu; wakufunzi wa vyuo vya ufundi; wakufunzi wa vyuo vya VETA; wakufunzi wa vyuo vya maendeleo ya wananchi; maafisa elimu msingi, maafisa elimu sekondari, wasimamizi wa elimu ngazi ya mkoa; maafisa elimu kata; wathibiti ubora wa shule na wanataaluma kutoka taasisi za elimu ya juu. Vilevile, itaendelea kutoa mafunzo kazini kwa walimu wa shule za msingi na sekondari kuhusu mitaala iliyoboreshwa.

68. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353 ili iendane na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023. Vilevile, itafanya mapitio ya sharia na miundo ya taasisi mbalimbali ikiwamo; COSTECH, TLSB, NECTA, VETA, TCU, NACTVET, TIE, TEWW na TEA ili ziendane na maboresho ya sera na sheria na makuliano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa. Vilevile, itafanya marekebisho ya sheria ya bodi ya mikopo kwa lengo la kuongeza ufasini wake ikiwamo kurahisisha ufunguaji wa mashauri na utekelezaji wake.

69. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuhuisha miongozo mbalimbali ya utoaji elimu na mafunzo nchini ili kuendana na maboresho ya mitaala na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 kama ifuatavyo:

(i) itaandaa mwongozo wa elimu jumuishi wa ufundishaji na matumizi ya teknolojia kwa lengo la kuongeza ufanisi katika

ufundishaji na matumizi ya teknolojia katika elimu na mafunzo;

(ii) itafanya mapitio ya mwongozo wa uanzishaji na usajili wa shule wa mwaka 2020 ili kuendana na mabadiliko ya sera na mitaala;

(iii) itakamilisha mwongozo wa kuwatambua na kuwaendeleza wanafunzi wenye vipawa na vipaji;

(iv) itaandaa kiunzi, mwongozo na zana kwa ajili ya kuwezesha upimaji wa ujifunzaji kwa wanafunzi wa madarasa ya awali kwa lengo la kubaini ujuzi katika ngazi husika;

(v) itahuisha mwongozo wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(vi) itaandaa mwongozo wa kukabiliana na majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi katika taasisi za elimu yanayoathiri utoaji wa elimu na mafunzo;

(vii) itafanya mapitio ya mwongozo wa huduma ya maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni ili kuimarisha utoaji huduma za maji na usafi wa mazingira katika shule za msingi na sekondari;

(viii) itaandaa mwongozo wa ukarabati wa miundombinu ya shule ili kuwezesha uendelevu wa miundombinu inayojengwa katika shule za msingi na sekondari; na

(ix) itahuisha miongozo ya uanzishaji na usimamizi wa elimu ya watu wazima na programu za elimu nje ya mfumo rasmi.

70. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaongeza wigo wa ukusanyaji, uchakataji na utoaji wa takwimu za elimu kwa kuunganisha mifumo yote ya takwimu za elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, elimu ya juu, pamoja na mifumo ya upimaji na tathmini. Maboresho hayo yatahusisha kujumuisha taarifa za shule binafsi zisizo tumia mitaala ya Taifa. Mabadiliko hayo yatawezesha Wizara kuwa na taarifa za kila mwanafunzi, fani na programu zinazotolewa nchini na kuandaa Kitabu cha Taifa cha Takwimu Muhimu za Elimu (Basic Education Statistics in Tanzania - BEST)

ambacho kitakuwa na taarifa za kuanzia elimu ya awali hadi elimu ya juu. Kazi ya maboresha hayo imeshaanza na inafanywa na wataalamu wa ndani kutoka vyuo vikuu. Vilevile, Serikali itaanzisha jukwaa shirikishi la utafiti la wadau wa elimu ambalo litatambua na kuratibu tafiti za kielimu zinazofanyika nchini. Lengo la utekelezaji wa afua hizi ni kuhakikisha kuwa maamuzi ya kimageuzi na maendeleo katika sekta yanazingatia taarifa, takwimu na tafiti sahihi zenye maslahi kwa sekta na Taifa kwa ujumla.

71. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha tunaimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika agenda ya maendeleo, Serikali itaendelea na mapitio ya Sera ya Sayansi na Teknolojia ya Mwaka 1996 kwa lengo la kuandaa sera inayoakisi hali ya sasa na ya baadaye ya maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Vilevile, itafanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Nyuklia 2013 na Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo 2010 ili kuwezesha kuandaa Sera zenye kuendana na mahitaji ya sasa na ya baadaye.

**b. *Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali (Ufundi na Ufundi Stadi) katika Shule za Sekondari na Vyuo vya Amali***

72. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha tunaongeza fursa za amali nchini, Serikali itaendelea kuboresha na kuongeza miundombinu ya shule za sekondari za amali, vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ujenzi wa shule mpya 100 za sekondari za ufundi, kati ya hizo shule 26 zitaanza kupokea wanafunzi kuanzia Januari 2025. Aidha, ujenzi wa shule za amali utapewa kipaumbele katika maeneo ambayo hayana vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi au shule ya amali ya sekondari;

(ii) itaendelea na ujenzi wa vyuo 65 vya mafunzo ya ufundi stadi, kati ya hivyo 64 ni vya wilaya na kimoja ni cha ngazi ya Mkoa wa Songwe. Vilevile, imeongeza vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo 29 vilivyokamilisha ujenzi. Aidha, itakamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma na kuendelea na ukarabati wa vyuo vitatu pamoja na upanuzi wa vyuo 16;

(iii) itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya nyongeza katika vyuo 10 vya mafunzo ya ufundi stadi (Ndolage-Muleba, Ileje, Newala, Ngorongoro, Gorowa - Babati, Urambo, Kasulu, Mabalanga - Kilindi, Nkasi na Kanadi - Bariadi) ili kuviwezesha vyuo hivyo kufikia viwango vya msingi vya utoaji wa mafunzo;

(iv) itajenga bweni moja lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80 kwa kila chuo katika vyuo 10 vya maendeleo ya wananchi. Aidha, itakarabati karakana nne katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro;

(v) itaendelea na ujenzi wa maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,500 katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(vi) itakamilisha ujenzi na kuweka samani katika bweni la wavulana na bwalo la chakula katika Chuo cha VETA Karagwe. Aidha, itakamilisha ukarabati wa Hoteli ya Mafunzo katika Chuo cha VETA Mwanza na Dodoma;

(vii) itakarabati karakana nne na kuweka samani katika mabweni mawili katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro (MVTTC);

(viii) itaendelea na ujenzi wa karakana nne kwa ajili ya fani ya umeme, ufundi bomba, ufundi magari na ujenzi katika Chuo cha Ufundi na Mafunzo Stadi – Kihonda pamoja na ujenzi wa karakana ya ufundi bomba katika Chuo cha Ufundi na Mafunzo Stadi cha Mkoa wa Mbeya;

(ix) itaendelea na ujenzi wa ofisi ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi - VETA makao makuu pamoja na ofisi ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi - NACTVET ili kusogeza huduma za taasisi hizo katika Mji wa Serikali – Dodoma; na

(x) itaendelea na ujenzi wa hosteli mbili katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Kampasi ya Karume zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 768 kwa kila hosteli. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500, ukumbi wa mihadhara

utakaohudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na itajenga madarasa 12 yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300 kwa kila darasa na ofisi 20 za watumishi katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - kampasi ya Kivukoni. Aidha, itaendelea na ujenzi wa jengo la utawala na madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,800 katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - kampasi ya Pemba.

73. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Serikali itaendelea kuongeza fursa za mafunzo ya amali (elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi) katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itasajili vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi 150 ambapo vyuo vya elimu ya ufundi ni 100 (Technical Education Training Colleges) na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 50 (Vocational Education Training Colleges), hivyo kuwa na jumla ya vyuo 504 vya elimu ya ufundi na vyuo 885 vya mafunzo ya ufundi stadi. Usajili wa taasisi hizo utawezesha kuongeza fursa na kutoa mafunzo kwa kuzingatia viwango na ubora;

(ii) itadahili wanafunzi 263,718 wa elimu ya ufundi na mafunzo na ufundi stadi ambapo wanafunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi ni 190,518 na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 73,200 sawa na ongezeko la asilimia 23 ikilinganishwa na udahili wa mwaka 2023/24. Udahili unalenga kuongeza rasilimaliwatu yenye ujuzi na uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa; na

(iii) itadahili wanafunzi 2,089 katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro - MVTTC ili kuongeza idadi ya walimu wanaofundisha vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na vyuo vya ualimu wa mafunzo ya ufundi.

74. **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia ubora wa mafunzo ya Amali, Serikali itaendelea kuimarisha ithibati na uthibiti katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itatoa ithibati kwa vyuo 70 vya elimu ya ufundi na mafunzo ya

ufundi stadi hivyo kuwa na jumla ya vyuo 320 vilivyopata ithibati ili kuthibiti ubora wa mafunzo yanayotolewa katika vyuo hivyo;

(ii) itaimarisha shughuli za uthibiti ubora wa uendeshaji wa vyuo 835 vya mafunzo ya ufundi stadi na shule za sekondari 96 zinazotoa elimu ya amali; na

(iii) itafanya ufuatiliaji na tathmini katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi 450 (vyuo vya elimu ya ufundi 300 na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 150) kwa lengo la kuhakikisha endapo mafunzo yanatolewa kwa kuzingatia vigezo na miongozo iliyopo.

75. **Mheshimiwa Spika,** katika kuwajengea umahiri walimu wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na vyuo vya maendeleo ya wananchi, serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itatoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi 215 ambapo mafunzo ya muda mrefu ni watumishi 50 na muda mfupi ni 165 kwa watumishi wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na shule za sekondari za elimu ya amali kuhusu mipango ya elimu na ufundishaji unaozingatia ujenzi wa umahiri. Aidha, mafunzo ya muda mrefu yatahusisha watumishi sita katika ngazi ya uzamili, wanne katika ngazi ya uzamivu na watano katika ngazi ya shahada;

(ii) itatoa mafunzo kwa walimu 1,000 wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kuhusu tathmini ya mitaala ya umahiri (CBET) ili kuwawezesha walimu kufundisha na kufanya tathmini ya wanafunzi kwa kuzingatia umahiri; na

(iii) itaanzisha mafunzo ya ualimu katika vyuo vitatu vya VETA (Moshi, Dar es Salaam na Kagera (RVTSC) kwa lengo la kuongeza idadi ya walimu wenye sifa na ujuzi wa kufundisha vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

76. **Mheshimiwa Spika,** katika kugharimia elimu ya amali (elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi) kwa lengo la kupunguza gharama za upatikanaji wake, Serikali itawezesha mafunzo kwa vitendo viwandani (Industrial Practical Training – IPT) kwa wanafunzi 1,724

(Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya 551, Chuo cha Ufundi Arusha 500 na Taasisi ya Tekonolojia Dar es Salaam 673). Vilevile, itaendelea kuwezesha upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi 17,411 (vyuo vya maendeleo ya wananchi wanafunzi 15,000, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam wanafunzi 850, Chuo cha Ufundi Arusha wanafunzi 800 na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya wanafunzi 761). Aidha, itatoa mikopo kwa wanafunzi wa stashahada takribani 10,000 katika fani za kipaumbele na zenye uhaba wa wataalam nchini ikiwamo fani za sayansi na ufundi.

77. **Mheshimiwa Spika;** Serikali itaendelea kuwezesha na kuongeza vifaa vya kufundishia katika vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ununuzi na usimikaji wa vifaa vya mafunzo ya uchomeleaji vyuma katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi (Dar es Salaam, Mtwara, Mwanza, Dodoma na Moshi) ili kuwezesha utoaji wa mafunzo yanayotambulika kimataifa;

(ii) itaweka samani katika vyuo tisa vya mafunzo ya ufundi stadi (Ndolage - Muleba, Ileje, Ngorongoro, Gorowa, Urambo, Kasulu, Mabalanga, Nkasi na Kanadi); na

(iii) itanunua mashine za kisasa kwa ajili ya maabara ya upimaji wa udongo, lami na maji ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa mafunzo kwa vitendo na huduma za ushauri wa kitaalamu katika Chuo cha Ufundi Arusha.

78. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuziwezesha taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kutumia nishati safi ya kupikia kwa lengo la kuhifadhi mazingira na kuimarisha utoaji wa mafunzo kwa kufunga mifumo ya majiko ya gesi katika vyuo 24 vya VETA ambavyo ni; Mpanda, Uvinza, Kishapu, Uyui, Newala, Karatu, Kilindi, Arusha, Ndolage, Igunga, Mabalanga. Vilevile, mifumo hiyo itafungwa katika chuo cha VETA mkoa wa; Mtwara, Kigoma, Iringa, Kagera, Tabora; na chuo cha VETA wilaya ya; Masasi, Ngorongoro, Longido, Monduli, Pangani, Korogwe, Nyasa, na Iringa. Aidha, Serikali itaweka nishati safi ya kupikia katika vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi.

c. ***Kuongeza fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu***

79. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kutoa Ithibati kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itasajili shule za msingi na sekondari takribani 772 ambapo awali pekee 30, awali na msingi 475 (Serikali 313 na zisizo za Serikali 162), sekondari 266 (Serikali 209 na zisizo za Serikali 57), chuo cha ualimu kimoja cha binafsi;

(ii) itafanya tathmini kwa shule 100 zilizopewa usajili wa masharti ili kubaini utekelezaji wa masharti ya usajili; na

(iii) itahakiki shule 200 (msingi 125 na sekondari 75) zilizosajiliwa kwa lengo la kuhuisha usajili.

80. **Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ujenzi wa shule za sekondari za kata 226, nyumba za walimu 184 wa sekondari na ununuzi wa vifaa vya maabara;

(ii) itawezesha ujenzi wa madarasa 2,018 (msingi 1,221 na sekondari 797); mabweni 114 kwa shule za sekondari; nyumba za walimu 658 (msingi 567 na sekondari 81) matundu ya vyoo 2,848 (msingi 1,514 na sekondari 884), maabara 10 na vituo vya walimu (TRCs) 300 kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, itakamilisha ujenzi vyumba vya madarasa 111 katika shule za msingi 37, matundu ya vyoo, maabara, nyumba za walimu na mabweni katika shule za sekondari 50;

(iii) itawezesha utoaji wa elimu ya afya na usafi wa mazingira ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya vyoo na uwekaji wa vifaa vya kunawia mikono katika shule za msingi 360;

(iv) itakarabati nyumba za watumishi wa vyuo vya ualimu 10 na vyuo vya maendeleo ya wananchi 15;

(v) itafanya matengenezo na ukarabati wa nyumba za watumishi 10 pamoja na mifumo ya maji taka katika kituo cha maendeleo DAKAWA; na

(vi) itaweka nishati safi ya kupikia ili kuendelea kuhifadhi na kuimarisha mazingira katika vyuo vya ualimu 11 (Nachingwea, Katoke, Kleruu, Tabora, Dakawa, Patandi, Mpwapwa, Sumbawanga, Mhonda, Kasulu na Monduli). Vilevile, itanunua samani kwa ajili vyuo vya ualimu ambavyo ni; Sumbawanga, Mhonda, Dakawa na Ngorongoro.

81. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uthibiti ubora wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na vyuo vya maendeleo ya wananchi, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya tathmini ya jumla katika takribani asasi 6,620 (shule za awali na msingi 4,965, sekondari 1,525, vyuo vya ualimu 66, vyuo vya maendeleo ya wananchi 14, na vituo 50 vya elimu ya watu wazima na mafunzo nje ya mfumo rasmi). Vilevile, itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa lengo la kubaini ubora katika uandikishaji, ufundishaji na ujifunzaji, usimamizi na uongozi na kutoa ushauri kwa walimu wa masomo katika taasisi 1,010 (awali na msingi 783, sekondari 213, vyuo vya ualimu tisa, na vyuo vya maendeleo ya wananchi vitano);

(ii) itatoa mafunzo kwa wathibiti ubora wa shule kutoka halmashauri 184 ambao watashiriki katika uhakiki wa kiashiria kinachohusu shule za msingi kuwa jumuishi kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika shule jumuishi za msingi. Vilevile, itatoa mafunzo kazini kwa wathibiti ubora wa shule 368 kutoka halmashauri 184 kuhusu utaratibu wa usajili wa walimu wa kigeni;

(iii) itaandaa moduli za mfumo wa taarifa za uthibiti ubora wa shule zitakazojumuishwa kwenye School Information System – SIS ili kuimarisha uthibiti ubora wa shule wa ndani;

(iv) itaendelea na ujenzi wa ofisi ya uthibiti ubora wa shule katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele na ukarabati wa ofisi nne za uthibiti ubora wa shule katika Halmashauri ya Mpwapwa, Chato,

Mpanda, na Halmashauri ya Mji - Ifakara; na

(v) itanunua samani na vitendea kazi katika ofisi 210 (halmashauri 184 na mikoa 26) za uthibiti ubora wa shule na itanunua magari 3 kwa ajili ya shughuli za uthibiti ubora wa shule katika Halmashauri ya Mlele, Tunduma na Serengeti.

82. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaimarisha utoaji wa elimu jumuishi kwa wanafunzi na walimu wenye mahitaji maalum kwa lengo la kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimuundo ili kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itafanya tathmini ya awali ya kubaini hali ya usaidizi uliopo na unaohitajika kwa wanafunzi 1,000 na walimu 200 wenye mahitaji maalum kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalam;

(ii) itajenga uelewa kwa jamii na wadau wa elimu kuhusu elimu jumuishi kwa lengo la kuhamasisha uandikishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vilevile, itatoa semina za uhamasishaji kuhusu haki na wajibu wa watumishi wenye mahitaji maalum kwa watumishi 105 kutoka vyuo 35 vya ualimu. Aidha, itawezesha ushiriki wa watumishi 40 katika maadhimisho ya watu wenye ulemavu;

(iii) itawajengea uwezo maafisa 368 wa elimu maalum msingi na sekondari kuhusu ubainishaji wa awali wa watoto wenye ulemavu kwa lengo la kurahisisha zoezi la upimaji kwa kiwango kinachohitajika; na

(iv) itanunua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vifaa saidizi kwa wakufunzi 105, walimu 103 na walimu tarajali 188 wenye mahitaji maalum ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji.

83. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari kwa lengo la kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi na hivyo kuboresha ufundishaji na ujifunzaji na kuchochea tabia na utamaduni wa kujisomea kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itachapa na kusambaza nakala za vitabu takribani 2,000,000 vya masomo ya hisabati na sayansi kwa kidato cha 1 hadi 4;

(ii) itaandaa vitabu vya kiada kwa darasa la II na IV, sekondari kidato cha 1 na cha 6 na viongozi vya mwalimu;

(iii) itachapa na kusambaza vitabu vya kiada kwa darasa la II na IV, sekondari kidato cha 1 na cha 6 na viongozi vya mwalimu;

(iv) itachapa na kusambaza vitabu vya kiada katika maandishi yaliyokuzwa na breli kwa darasa la II na IV, sekondari kidato cha 1 na cha 6 na Kiongozi cha mwalimu kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa watoto wenyemahitaji maalum;

(v) itaandaa programu za mafunzo endelevu, mashindano, teknolojia ya kidijiti, uchapishaji wa miongozo ya stadi za maisha, mafunzo na usambazaji wa mitaala; na

(vi) itaweka maudhui ya elimu ya sekondari katika mfumo wa kidijiti kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wake.

84. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Serikali itaendelea kukuza ujuzi wa uandishi na kuhamasisha tabia ya usomaji na kuimarisha matumizi ya maktaba katika ngazi zote za elimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaratibu uandaaji wa Sera ya Taifa ya Huduma za Maktaba nchini. Vilevile, itaendelea kununua vitabu kwa ajili ya maktaba za mkoa na kuendeleza maktaba 15 za jamii;

(ii) itaendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu yenye lengo la kuhamasisha uandishi na usomaji wa vitabu, kutunza historia na utamaduni wa Mtanzania na kuinua sekta ya uchapaji nchini. Tuzo hizo

zitatolewa kwa waandishi mahiri wa riwaya, hadithi fupi na ushairi. Aidha, itagharamia uchapaji, kununua na kusambaza katika taasisi za elimu na maktaba vitabu vya washindi wa tuzo hizo. Mafanikio katika azma hii yamelenga kuwezesha sekta ya uchapishaji na uchapaji na kuongeza ari ya kusoma;

(iii) itaendelea kuratibu na kukuza stadi na ujuzi wa uandishi insha kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari nchini katika nyanja za: ujenzi wa taifa, mageuzi ya kimaendeleo, ustahimilivu, na maridhiano. Tutaandaa shindano maalum la uandishi wa insha kwa wanafunzi kuchochea uelewa na fikra tunduizi kuhusu **falsafa ya 4Rs ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.** Vilevile, Serikali itaendelea kuratibu shindano la uandishi wa Insha kwa Nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kwa wanafunzi 2,000 wa shule za sekondari; na

(iv) itakamilisha ujenzi wa maktaba ya kumbukumbu ya John Pombe Magufuli - Chato. Vilevile, itafanya ukarabati wa maktaba katika Mkoa wa Tanga, Mbeya, Musoma na Mtwara.

85. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha wanafunzi wa sekondari na vyuo vya ualimu wanajifunza kwa vitendo, Serikali itanunua vifaa vya maabara kwa ajili ya shule 1,322 na vyuo 13 vya ualimu pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo 35 vya ualimu. Vilevile, itanunua vifaa vya kujifunzia na kemikali kwa ajili ya kufundishia masomo ya sayansi kwa wanafunzi wa elimu kwa njia mbadala kwa hatua ya I na II.

86. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kufanya upimaji na tathimini ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili kwa watahiniwa **1,681,490** na **882,314** mtawalia wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2024;

(ii) itaendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa **1,241,291** wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Septemba, 2024;

(iii) itaendesha Mtihani wa Kidato cha Nne na Mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa **559,646** wanaotarajiwa kufanya mitihani hiyo mwezi Novemba, 2024;

(iv) itaendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa **114,500** wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2025;

(v) itaendesha Mtihani wa Cheti na Stashahada ya Ualimu kwa watahiniwa **8,500** wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2025;

(vi) itaongeza uwezo wa kuchapa mitihani kwa kununua na kusimika mashine ya kisasa ya uchapaji, na itawezesha Baraza la Mitihani kuandaa Kiunzi cha Upimaji cha Taifa; na

(vii) itaandaa Mfumo wa Kieletroniki wa Tathmini ya Ujifunzaji wenye lengo la kurahisisha upimaji wa wanafunzi katika shule za msingi.

87. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mafunzo ya usimamizi wa elimu nchini, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu itatekeleza yafuatayo:

(i) itadahili walimu 2,050 watakaosoma astashahada na stashahada ya uongozi wa elimu, usimamizi na utawala na uthibiti ubora wa shule katika kampasi zote;

(ii) itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 6,702 kuhusu uongozi na usimamizi wa elimu kutoka makundi mbalimbali ya elimu nchini ili kuwajengea uwezo wa kusimamia maendeleo ya shule;

(iii) itafanya tafiti tatu katika maeneo ya uongozi na usimamizi wa elimu kwa lengo la kutatua changamoto zinazojitokeza katika uongozi na usimamizi wa elimu nchini;

(iv) itaanzisha kozi za elimu masafa (E-learning courses) ili kuwafikia viongozi wengi wa elimu nchini na kupunguza gharama za uendeshaji pamoja na kuongeza wigo wa utoaji wa huduma kwa

wateja. Vilevile, itatoa shauri elekezi sita za kitaalamu katika uongozi, usimamizi na utawala na uthibiti ubora wa shule ili kuwajengea uwezo wa kusimamia maendeleo ya shule;

(v) itawezesha watumishi 39 kushiriki mafunzo ambapo muda mrefu ni watumishi 35 (shahada ya uzamivu) na muda mfupi watumishi wanne kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;

(vi) itaendelea na ujenzi wa jengo lenye kumbi tatu za mafunzo katika kampasi ya Bagamoyo lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,400 kwa wakati mmoja na itakarabati majengo ya Wakala ikiwemo nyumba tatu za watumishi ili kuboresha mazingira katika shughuli za utoaji wa mafunzo ya uongozi na usimamizi wa elimu. Vilevile, itajenga ukumbi changamani (multipurpose hall) katika Chuo cha Uongozi ADEM kampasi ya Bagamoyo;

(vii) itakamilisha ujenzi na ununuzi wa samani katika jengo la ghorofa moja lenye kumbi nne za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 564 pamoja na ofisi 10 katika kampasi ya Mbeya ili kuimarisha ufanisi katika shughuli za utoaji wa mafunzo ya uongozi na usimamizi wa elimu; na

(viii) itaendeleza ushirikiano kati ya ADEM na Chuo cha Zhejiang Normal University (ZJNU) kilichopo China ili kuwezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika eneo la uongozi na usimamizi wa elimu nchini.

88. **Mheshimiwa Spika,** katika kutoa fursa kwa wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali, Serikali itaongeza fursa za utoaji wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza udahili wa wanafunzi kutoka 22,131 kwa mwaka 2023/24 hadi 24,891 kwa mwaka 2024/25. Vilevile, itaongeza udahili wa wanafunzi wa astashahada, stashahada na shahada kutoka 4,430 hadi 5,300;

(ii) itajenga vituo vitano vya elimu kwa njia mbadala katika

Mkoa wa Simiyu, Singida, Njombe, Katavi na Mbeya. Vilevile, itajenga ofisi na madarasa katika vituo vya Mkoa wa Kagera, Shinyanga na Singida; na

(iii) itakarabati vituo sita vinavyotoa elimu kwa njia mbadala katika mikoa sita ambayo ni Simiyu, Singida, Njombe, Katavi, Lindi na Mbeya pamoja na kukarabati miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mwanza na Morogoro.

89. **Mheshimiwa Spika,** katika kuwajengea stadi za maisha, ujasiriamali stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu na ufundi wa awali ili vijana wenye umri wa miaka 14 na kuendelea waweze kujiajiri au kuajiriwa, Serikali itaendelea kuongeza fursa za mafunzo kwa vijana 16,000 walio nje ya shule kupitia Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule.

90. **Mheshimiwa Spika,** ili kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika, Serikali itawajengea uwezo maafisa na wataalamu wa kisomo. Vilevile, itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma na kufanya utafiti wa kitaifa kuhusu hali ya kisomo na elimu kwa umma kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa mkakati husika.

91. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuwezesha wanafunzi walio katika mazingira magumu kufanya mtihani wa majaribio (Mock) hatua ya I na II, Mtihani wa Maarifa (QT) kwa wanafunzi wa kike 3,000 na wa kiume 1,000 na mtihani wa kidato cha nne kwa wanafunzi wa kike 3,000 na wa kiume 1,000 katika vituo 151 vya mafunzo ya elimu kwa njia mbadala. Vilevile, itatoa motisha kwa walimu wanaofundisha hatua ya I na II katika vituo hivyo.

92. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya ushauri na unasihi kuhusu haki za mtoto, ukatili wa kijinsia na watoto na namna ya kuunda dawati la jinsia kwa walimu wa shule za msingi na sekondari 4,170 za serikali na zisizo za serikali ili kuwawezesha walimu kutatua changamoto za masuala ya ukatili na kisaikolojia kwa wanafunzi na kupunguza mdondoko. Vilevile, itatoa mafunzo kuhusu malezi kwa washiriki 300 wa Umoja wa Wazazi na Walimu (UWAWA) na kamati/bodi za shule.

93. **Mheshimiwa Spika,** ili kuwajengea umahiri wa ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu wa shule za msingi na sekondari, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itatoa mafunzo kwa walimu 1,500 wa shule za msingi kuhusu utaratibu wa utekelezaji wa Shule Salama (Safe School Package) kwa wanafunzi;

(ii) itawezesha mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 800 wa shule za msingi katika vituo 200 vya walimu;

(iii) itatoa mafunzo kwa walimu 4,500 wa shule za awali kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wa darasa la awali;

(iv) itatoa mafunzo kwa walimu 3,000 wa masomo ya sayansi na hisabati kwa lengo la kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari inayotolewa nchini;

(v) itatoa mafunzo kwa wawezeshaji 20 wa vyuo vya ualimu kuhusu matumizi ya mwongozo wa malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu;

(vi) itatoa mafunzo kwa walimu 400 wa shule za msingi kuhusu matumizi ya mfumo wa tathmini katika ngazi ya shule. Vilevile, itatoa mafunzo kwa walimu 736 wanaofundisha darasa la awali, la I na la II kuhusu kiunzi cha taifa cha tathmini ya ujifunzaji; na

(vii) itatoa mafunzo kwa waratibu wa elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni wa mikoa 26 na halmashauri 184. Vilevile, itasambaza Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (School WASH Guidelines) na Mpango wa Kitaifa wa Kugharimia na kuwekeza katika miundombinu ya huduma ya maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni.

94. **Mheshimiwa Spika,** vilevile Serikali itatoa ufadhili wa masomo katika ngazi ya stashahada ya elimu maalum kwa walimu 200 ili kuongeza idadi ya walimu wenye sifa wa elimu maalum.

95. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaandaa kiunzi cha walimu wa kujitolea

na utarajali katika shule za msingi kitakachotoa mwelekeo wa kukabiliana na changamoto ya upungufu wa walimu. Vilevile, itatoa udhamini kwa walimu tarajali 1,800 watakaosoma kozi ya stashahada ya elimu maalum.

96. **Mheshimiwa Spika,** ili kutoa hamasha kwa watumishi kushiriki michezo mbalimbali, Serikali itawezesha watumishi wa Wizara kushiriki Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) pamoja na kuwawezesha maafisa 20 kusimamia mashindano ya michezo ya UMITASHUMTA, UMISAVUTA, UMISSETA na FEASSSA ngazi ya mkoa na Taifa. Aidha, itajenga miundombinu ya michezo katika vyuo vinavyotoa elimu ya michezo (Butimba na Dakawa) kwa lengo la kuibua, kuendeleza na kuimarisha vipaji vya sanaa na michezo kwa wanachuo wa wanafunzi kwa ujumla.

97. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itawajengea uwezo watumishi 192 wa Wizara ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ikiwemo tathmini za mitaala na mifumo ya TEHAMA.

98. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha utekelezaji wa mipango, miongozo ya ufundishaji na ujifunzaji inatekelezwa kwa ufanisi, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaunganisha mifumo ya takwimu za elimu na mafunzo nchini kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi elimu ya juu ili kuimarisha utoaji wa taarifa za elimu na mafunzo. Vilevile, itawajengea uwezo maafisa wanaohusika na ukusanyaji, uchakataji na utoaji wa taarifa za elimu kwa ngazi zote ili kuongeza ufanisi katika utendaji;

(ii) itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu ya shule salama kwa shule za msingi, kifurushi kilichoboreshwa cha utoaji wa elimu ya awali, uzingatiaji wa mwongozo wa ujenzi, uandikishaji wa elimu ya awali, mafunzo ya utawala bora na Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) katika mikoa 26;

(iii) itafanya ufuatiliaji na tathmini katika vituo 151 vinavyotoa Elimu kwa njia mbadala katika mikoa 26;

(iv) itafanya ufuatiliaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia

vilivyotolewa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule 1,200 na vyuo vya ualimu 16;

(v) itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa waraka na mwongozo wa kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatiza masomo kutokana na sababu mbalimbali katika elimu ya msingi na sekondari; na

(vi) itafanya tathmini ya kuzitambua stadi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

99. **Mheshimiwa Spika,** Serikali pia itaendelea kuimarisha ufuatiliaji na tathmini kwa kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kidijiti. Vilevile, itafanya ufuatiliaji na tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu wa Mwaka 2021/22–2025/26 ili kubaini mafanikio na changamoto katika utekelezaji na kuwezesha kusasisha mpango huo.

**d.** ***Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu***

100. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kutoa ithibati na uthibiti wa ubora wa elimu katika ngazi ya elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kuratibu udahili wa wanafunzi 145,800 wa mwaka wa kwanza wanaotarajiwa kujiunga na programu mbalimbali za masomo katika vyuo vya elimu ya juu;

(ii) itasajili na kukagua asasi 25 zinazoratibu wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuzitambua na kuzisajili zitakazokidhi vigezo au kuhuisha usajili kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania;

(iii) itakagua na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya vyuo vikuu 25 kwa lengo la kuhakiki ubora wake;

(iv) itafanya tathmini ya maombi ya utambuzi wa tuzo 5,000 za wahitimu zilizotolewa katika vyuo vikuu vya nje na kuzitambua zitakazokidhi vigezo; na

(v) itafanya tathmini ya maombi ya wanafunzi 2,000 wanaotarajiwa kuomba udahili katika vyuo vikuu nje ya nchi

kwa lengo la kuwapatia uhakika kwamba vyuo wanavyotaka kujiunga vina ithibati za mamlaka husika.

101. **Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha na kuimarisha huduma ya utoaji na upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wenye sifa na uhitaji, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza fursa za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka 223,201 hadi 252,245;

(ii) itatoa mikopo kwa wanafunzi 84,500 wa mwaka wa kwanza ambapo shahada ya kwanza 80,000, shahada za juu 2,000, wanaosoma nje ya nchi 500 na **SAMIA** Skolashipu 2,000;

(iii) itatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 40 wenye ufaulu wa juu kwenye masomo ya Sayansi hususan wanafunzi wa kike waliohitimu Mtihani wa Taifa ya Kidato cha Sita na shahada ya awali kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(iv) itaendelea kukusanya madeni ya mikopo iliyoiva ya kiasi cha **Shilingi Bilioni 198** kutoka sekta ya umma na kuimarisha makusanyo kutoka sekta binafsi na isiyo rasmi. Aidha, itatafuta wanufaika wapya **40,000** wenye marejesho ya mikopo iliyoiva ikijumuisha wanufaika wapya **5,000** wenye mikopo chechefu kutoka sekta binafsi na isiyo rasmi;

(v) itaanza kutoa ufadhili kwa ajili ya shahada za juu ikiwemo eneo la fani ya mionzi na nyuklia;

(vi) itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu bidhaa, huduma na mikakati ya Bodi ya Mikopo kupitia kampeni, programu na matangazo katika vyombo vya habari na maonesho ya mbalimbali ili kurahisisha utoaji wa taarifa na kuongeza ufanisi katika utoaji na urejeshaji wa mikopo; na

(vii) itaendelea na ujenzi wa ofisi za Tume ya Vyuo Vikuu katika Jiji la Dodoma.

102. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya taasisi za elimu ya juu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea na ujenzi wa maabara kuu ya kemikali (Central Chemistry Laboratory) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo itatumika kwa ajili ya utafiti na kutoa huduma za kupima sampuli za viwandani. Vilevile, itaendelea na ujenzi awamu ya pili wa jengo la kituo cha wanafunzi na kuweka samani. Aidha, itaendelea na upanuzi wa bweni la Dkt. John Pombe Joseph Magufuli la ghorofa mbili lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,280 kwa wakati mmoja;

(ii) itaendelea na ujenzi wa madarasa mawili katika Shule ya Msingi ya Mazoezi Chang'ombe, maabara za Sayansi nne na darasa moja katika Shule ya Sekondari ya Mazoezi Chang'ombe kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam ili kuongeza ufanisi katika mafunzo kwa vitendo. Aidha, itakarabati mabweni matano na kumbi za mihadhara tatu na miundombinu saba ya TEHAMA;

(iii) itaendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kama ifuatavyo: mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kwa kila bweni, maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,500 kwa wakati moja, jengo la sayansi, jengo la midia anuwai na elimu ya mahitaji maalum, maabara ya fizikia na bweni moja la wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuongeza ufanisi katika mafunzo;

(iv) itaendelea na ujenzi wa ofisi na jengo la taaluma katika Ndaki ya Sayansi ya Jamii na Insia eneo la Kihonda katika Chuo Kikuu cha Sokoine;

(v) itaendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja na ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,868 katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi;

(vi) itajenga miundombinu katika taasisi za elimu ya juu kupitia Mradi

wa Kuendeleza Elimu ya Juu kwa ajili ya Mabadiliko ya Kiuchumi kama ifuatavyo: kumbi 27 za mihadhara; Ofisi 302; vyumba 90 vya madarasa na vyumba 17 vya semina. Miundombinu hiyo itajengwa katika kampasi 15 za vyuo vikuu katika mikoa ifuatayo: UDSM (Kagera, Lindi na Zanzibar); MUHAS (Kigoma); ARU (Sengerema-Mwanza); SUA (Katavi); Mzumbe (Tanga); MUST (Rukwa); UDOM (Njombe); MoCU - (Shinyanga); IAA (Manyara na Ruvuma); TIA (Singida); IFM (Simiyu). Vilevile, itaendelea na ujenzi katika Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia Kampasi Kuu Butiama ambapo chuo hicho kitajenga kampasi yake mkoani Tabora;

(vii) itajenga madarasa nane, kumbi mbili za mihadhara, jengo la TEHAMA na Kituo Atamizi cha Ubunifu (Innovation Incubation Center) na kukarabati barabara eneo la mahafali na kuweka kamera 12 katika kampasi Kuu ya Chuo Kikuu Mzumbe. Vilevile, itakarabati jengo la utawala katika kampasi ya Mbeya;

(viii) itajenga jengo la taaluma na ofisi tano za watumishi katika Mkoa wa Njombe, Pemba, Songwe, Tabora na Tanga kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania;

(ix) itajenga zahanati katika Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius Nyerere;

(x) itajenga majengo mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kama ifuatavyo: Kliniki ya Uporoto (Uporoto Polyclinic) kwa lengo la kuongeza utoaji wa huduma za kitabibu na tafiti katika shule ya meno; jengo la mihadhara; ofisi ya wafanyakazi katika kampasi ya upanga. Aidha, itawezesha ukarabati na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo: maabara ya meno; maabara ya unyevu; maabara ya dawa; maktaba; miundombinu ya mafunzo kwa njia ya kielektroniki; uwanja wa mpira wa miguu wa Upanga; hosteli ya wanafunzi katika kampasi kuu; hosteli za Barabara ya Chole; jengo la Multipurpose Laboratory na mifumo ya umeme;

(xi) itaendelea na ujenzi wa majengo manne mapya katika Chuo Kikuu Ardhi kampasi kuu yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 6,135 na watumishi 73 kwa wakati mmoja ambayo ni: maabara ya matumizi anuwai (multipurpose Laboratory) inayojumuisha maabara saba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 760 na watumishi 15; Jengo la studio lenye vyumba 15 na uwezo wa kuchukua wanafunzi 780 na watumishi 20; Jengo la karakana (multipurpose workshops building) lenye jumla ya karakana 10 na uwezo wa kuchukua wanafunzi 495 na watumishi 20 na jengo la madarasa (multipurpose classrooms) lenye vyumba vya madarasa 28 na uwezo wa kuchukua wanafunzi 4,100 na watumishi 18; na

(xii) itaendelea na ujenzi wa majengo matano mapya katika Chuo cha Ardhi kampasi ya Mwanza yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 2,132 na watumishi 131 kwa wakati mmoja ambayo ni: jengo la madarasa na studio lenye vyumba vya madarasa nane na vyumba vya studio vinne na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,720; jengo la ofisi za watumishi lenye ofisi 52 zenye uwezo wa kuchukua watumishi 131; bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 412; nyumba ya watumishi yenye uwezo wa kuchukua familia nane na jengo la zahanati. Aidha, itaendelea na ukarabati wa madarasa 50, maabara mbili, mabweni matatu, ofisi 25 za watumishi, nyumba tano za watumishi na miundombinu ya TEHAMA.

103. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya ofisi na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika taasisi za elimu ya juu, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itanunua vifaa vya kufundishia pamoja na samani za majengo mapya katika Chuo Kikuu Ardhi;

(ii) itanunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi 57 pamoja na vifaa vya utafiti kwa wanataaluma ili kuimarisha ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vilevile, itanunua vitabu 400 kwa ajili ya maktaba ya chuo na shule za mazoezi kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam;

(iii) itanunua samani na vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na shughuli za uendeshaji ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi; na

(iv) itaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kuongeza kiwango cha upatikanaji wa vifaa na zana bora za kufundishia katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kampasi ya Mizengo Pinda – Katavi.

104. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha mitaala inawawezesha wanafunzi kupata ujuzi na stadi za maisha na kukidhi mahitaji ya soko la ajira, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaunda mabaraza ya tasnia katika vyuo vikuu ambayo yatahusisha watalaam, wajasiriamali na wabobezi katika aina mbalimbali za ujuzi, maarifa na stadi zinazohitajika katika soko la ajira. Vilevile, mabaraza yatashiriki katika kuhakikisha miundombinu inayoaandaliwa inakuwa rafiki kwa watumiaji wote wakiwemo wenye mahitaji maalum;

(ii) itaboresha utendaji wa taasisi rekebu za elimu ya juu ikiwemo NACTVET na TCU kwa kuzijengea mifumo wezeshi na rafiki katika utoaji wa huduma; na

(iii) itafanya tathmini ya programu 300 za masomo mbalimbali katika Vyuo Vikuu nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa programu hizo zinakidhi mahitaji ya wadau na kuzipatia ithibati.

105. **Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na idadi ya wanataaluma wenye sifa, Serikali itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wasio wanataaluma katika taasisi za elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itagharamia mafunzo kwa wanataaluma 308 na watumishi wasio wanataaluma 23 kwa ngazi ya umahiri na shahada ya uzamivu katika fani mbalimbali;

(ii) itawezesha wanataaluma na watendaji wa Wizara makao makuu na taasisi za elimu ya juu 1,664 kuhudhuria mafunzo (mafunzo ya muda mrefu 298 na muda mfupi 1,366) katika maeneo ya; sayansi, teknolojia, uhandisi, hisabati, TEHAMA, matumizi bora ya ardhi, kujikinga na majanga, kutengeneza bidhaa kwa kutumia mabaki ya mazao ya kilimo, kutunza kumbukumbu za biashara ndogondogo, kutunza mazingira, kuunda majukwaa ya kujifunzia mtandaoni na matumizi ya teknolojia, na ukatili wa kijinsia;

(iii) itaandaa na kuratibu mafunzo ya kubadilishana uzoefu kwa viongozi, wahadhiri na maofisa 450 wa vyuo vikuu vya umma na binafsi hapa nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo katika usimamizi na uendeshaji wa taasisi zao;

(iv) itawezesha wanafunzi 100 wenye mahitaji maalum katika taasisi za elimu ya juu kwa kuwapatia fursa katika programu za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati; na

(v) itawezesha ununuzi wa magari matatu ajili ya watumishi wa Chuo Kikuu cha Mwl. Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia.

106. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuboresha na kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji na utoaji wa taarifa kutoka taasisi za elimu ya juu kupitia tume ya vyuo vikuu kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati. Aidha, katika kuongeza ufanisi na matumizi ya TEHAMA ya ufundishaji na ujifunzaji, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza matumizi ya TEHAMA katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kutoka asilimia 25 hadi asilimia 40 ili kuongeza ufanisi katika kufundisha idadi kubwa ya wanafunzi kwa wakati mmoja;

(ii) itaweka mazingira wezeshi kwa kuboresha mifumo ya TEHAMA inayounganisha taasisi za maendeleo ya tafiti, taasisi za elimu ya juu na mifumo ya uratibu wa utafiti na ubunifu ili kurahisisha utendaji wa kazi na upatikanaji wa takwimu mbalimbali zinazohusu utafiti, ubunifu na maendeleo; na

(iii) itaongeza na kuboresha miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika vyuo vikuu vya Serikali ikiwa ni pamoja na kuviwezesha vyuo vikuu na taasisi rekebu upatikanaji wa Bandwith za mtandao za kutosha.

107. **Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha ushirikiano na mataifa mengine na kuongeza fursa za elimu nchini, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itatoa ufadhili kwa wanafunzi watano kutoka China wanaosoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kubiasharisha Lugha ya Kiswahili;

(ii) itatoa ufadhili kwa wanafunzi watano raia wa Oman na wanafunzi watano raia wa Hungaria kusoma katika vyuo vikuu vya hapa nchini kulingana na mikataba; na

(iii) itashiriki katika mikutano ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa (Inter-University Council for East Africa - IUCEA, East African Community - EAC, Southern Africa Development Community - SADC, United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization - UNESCO na Africa Union - AU) ili kuimarisha ushirikiano katika uendelezaji wa elimu ya juu.

108. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakisha elimu na mafunzo nchini yanatolewa kwa kiwango kinachotambulika nchini, Serikali itaimarisha ushirikiano na nchi za China, India na Ujerumani kwa lengo la kuimarisha mafunzo ya amali katika ngazi zote kupitia programu za kupata walimu, kusomesha wakufunzi na wahadhiri na kupata fursa za uanagenzi katika viwanda.

**e. *Kuimarisha Uwezo wa Nchi katika Utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili Kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda***

109. **Mheshimiwa Spika,** ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda, Serikali itaandaa Dira ya Taifa ya Teknolojia inayojumuisha maeneo 12 ambayo ni elimu, lugha, mawasiliano, maliasili, biashara, afya, kilimo, mifugo, uvuvi, haki za binadamu, maendeleo ya watu na TEHAMA. Vilevile, itaandaa mpango wa kuboresha teknolojia za elimu zilizofanyiwa majaribio.

110. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kusimamia maendeleo ya tafiti na kuimarisha matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa lengo la kuchangia maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaendeleza teknolojia na bidhaa zinazozalishwa na wabunifu nchini ili kufikia hatua ya kuingizwa sokoni na kuhamasisha wadau mbalimbali kuendelea kutumia matokeo ya kazi za utafiti;

(ii) itaendelea kuratibu na kuwezesha Mashindano ya Kitaifa ya Teknolojia ya Sayansi na Ubunifu, makongamano na maonesho ili kuibua, kutambua na kuendeleza ubunifu wa watanzania katika nyanja za sayansi, teknolojia na ubunifu;

(iii) itaendelea kukusanya, kuhifadhi na kutangaza matokeo ya utafiti kwa wananchi, watunga sera na watoa maamuzi ili kujenga uelewa na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika kufanya maamuzi yenye tija kwa maendeleo ya Taifa;

(iv) itaendelea kushirikiana na taasisi za kitaifa na kimataifa za utafiti na vituo vya takwimu kwa ajili ya kukusanya na kubadilishana taarifa za utafiti na ubunifu kwa lengo la kutatua changamoto za kijamii, kiuchumi na kuboresha utoaji wa elimu; na

(v) itaanzisha ushirikiano na viwanda vitatu ili kuongeza uwezo wa kuzalisha rasilimali watu katika kada ya afya katika kuendeleza viwanda kupitia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili.

111. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuviwezesha vyuo

vikuu, vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na taasisi za sayansi, teknolojia na ubunifu kufanya utafiti katika maeneo ya elimu, afya, kilimo, mifugo, utawala, nishati, biashara, maliasili na utalii, TEHAMA, ushirika na usafirishaji ili kutatua changamoto za kijamii na kuleta maendeleo. Aidha, itaandaa Kiunzi cha Ithibati ya Tafiti za Maabara na Tafiti nyingine zinazohusu miundombinu ya ubunifu. Vilevile, itawatambua wanasayansi wabobezi na kuandaa kanzidata zitakazoimarisha ukusanyaji wa takwimu za tafiti na kuvutia ugharimiaji.

112. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha taasisi za elimu ya juu na taasisi za kitafiti kuendelea kufanya utafiti wa kimkakati na kuongeza mchango wake katika ajenda ya maendeleo ya Taifa na kuboresha ustawi wa jamii kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaandaa mikakati ya utekelezaji na usambazaji wa matokeo ya utafiti;

(ii) itafanya tafiti 301 katika maeneo ya elimu, sayansi, teknolojia, utawala, ardhi, mazingira, mazao ya kilimo, mifugo, sayansi ya jamii, uongozi, biashara, afya, mifugo, misitu na uvuvi kwa lengo la kuongeza maarifa na kutatua changamoto za jamii;

(iii) itaviwezesha vyuo vikuu kufanya tafiti kwa maendeleo ya uchumi wa nchi na itakamilisha uandaaji wa vipaumbele vya Mpango wa Kitatifa wa Utafiti (National Research Priorities - NRPs);

(iv) itaimarisha makundi ya kitafiti (Research Clusters) na kutoa mafunzo kwa viongozi wa makundi hayo ili kujenga uwezo wa ndani wa kuandaa na kufanya tafiti zenye tija katika kutatua changamoto za afya;

(v) itaandaa machapisho 379 ya tafiti katika maeneo ya elimu, ushirika, afya, usimamizi na uendelezaji ardhi, mazingira, makazi na ujenzi, uongozi; na

(vi) itatoa mafunzo kwa watafiti kuhusu uandaaji na uchapaji wa

majarida ya kisayansi ya ndani (Local Peer Review Scientific Journals) na viunzi vya uthibiti.

113. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaandaa Mpango Kabambe wa Taifa wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Aidha, itafanya utafiti wa kimkakati wa ulinganishaji katika nchi ambazo vyuo vikuu vina uzoefu wa kutumia teknolojia ya kidijiti katika ufundishaji na ujifunzaji na huduma za utawala.

114. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuhamasisha uandishi na utoaji wa tuzo kwa machapisho bora duniani katika majarida ya kitaalam yenye hadhi za kimataifa katika fani za sayansi na afya katika taasisi za elimu ya juu. Aidha, itaendelea kutoa tuzo kwa waandishi mahiri.

115. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuwatambua wabunifu, kuwaendeleza ili wafikie hatua ya kubiasharisha ubunifu wao pamoja na kuendeleza miradi mbalimbali ya ubunifu kwa lengo la kukuza utaalamu asilia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itahamasisha uanzishaji wa vituo vya kuendeleza teknolojia, kongano bunifu na kampuni tanzu katika taasisi za elimu ya juu na utafiti za umma na binafsi nchini kwa lengo la kuendeleza bunifu zinazotokana na tafiti zinazofanyika katika taasisi hizo;

(ii) itaanzisha madawati ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika mikoa 25 na halmashauri 125 kwa lengo la kuimarisha uratibu wa masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu;

(iii) itaendelea kuwezesha jukwaa la mwaka la wadau wa sayansi, teknolojia na ubunifu kwa watanzania wanaoishi au kufanya kazi nje ya nchi (diaspora) ili kuwahamasisha kuchangia katika kukuza sayansi, teknolojia na ubunifu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na

(iv) itaandaa jukwaa la kitaifa la sekta mbalimbali lenye lengo la kujadili na kuratibu mipango ya kuimarisha masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

116. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuadhimisha Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu Mei 2025 kwa lengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu kazi zinazotekezwa na Wizara. Vilevile, itafanya Maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi tarehe 11 Februari 2025.

117. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaanzisha programu (Talent Pool Program) itakayowawezesha vijana wanaohitimu katika ngazi mbalimbali za elimu kuendeleza mawazo ya ubunifu ili yawe biashara au kampuni changa kwa ajili ya kujiajiri au kuajiriwa. Aidha, itawawezesha vijana 20 wenye vipaji na wabunifu katika masuala ya uhandisi na teknolojia kupitia programu atamizi.

118. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuboresha miundombinu katika taasisi za tafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itafanya tathmini ya maabara 10 za utafiti na udhibiti katika taasisi za utafiti na maendeleo ili kubainisha na kuboresha maabara 5 zenye sifa na mahitaji ya kuwa maabara za kitaifa;

(ii) itajenga jengo mtambuka la sayansi, teknolojia na ubunifu katika Jiji la Dodoma na kukarabati jengo la Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia jijini Dar es Salaam;

(iii) itafanya ukarabati mkubwa wa miundombinu ya kufundishia, mitambo, karakana na hosteli katika Taasisi ya Teknolojia - kampasi kuu ya Dar es Salaam;

(iv) itaanza ujenzi wa jengo la ghorofa sita ambalo litatumiwa na kampuni tanzu ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Dar es Salaam pamoja na kituo cha ushauri wa kitaalam ili kuweza kubiasharisha ubunifu pamoja na utoaji wa huduma bora kwa jamii; na

(v) itaendelea na ujenzi wa kituo cha kikanda cha umahiri wa TEHAMA, kituo cha umahiri cha uchakataji ngozi na mabweni ya wanafunzi katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Dar es Salaam kampasi ya Dar es Salaam na Mwanza

119. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuandaa rasilimaliwatu yenye maarifa, stadi, umahiri na uwezo katika kuendeleza tafiti, kuimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaanzisha programu tano mpya za kikanda zenye hadhi ya kimataifa katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam - Kampasi Kuu ya Dar es Salaam na Mwanza. Programu hizo ni Ordinary Diploma in Industrial Automation and robotics; Bachelor of Engineering in Cyber Security; Master of Engineering in Cyber Security; Bachelor of leather processing and allied technologies; na Diploma in leather processing and allied technologies;

(ii) itawaendeleza wahandisi 136 kupitia mkakati wa kuendeleza wataalamu katika utumiaji wa nishati ya umeme kiufanisi (Energy efficiency) kufikia viwango vya kimataifa (Internationally Certified Professionals) ambapo mafunzo hayo yatawezesha Taifa kuwa na wataalamu ambao wanaweza kutekeleza miradi ya kimkatati nchini na ya kimataifa katika fani ya umeme; na

(iii) itaandaa na kurusha satellite itakayoweza kuchakata taarifa kutoka katika anga za juu kwa kushirikiana na International Space Station ISS – Japan. Vilevile, Serikali itaanza kuandaa wataalamu katika maeneo hayo.

120. **Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza maarifa na kutatua changamoto kwa jamii na kuongeza tija katika kazi za kiuchumi, Serikali kupitia taasisi za elimu ya juu itaendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii katika maeneo yafuatayo: matumizi bora ya ardhi; upimaji na tathmini; usanifu majengo na usimamizi wa ujenzi; uimara wa udongo, kokoto na lami; upimaji wa ubora wa maji; biashara; sheria; utawala; uchumi; kilimo; ufugaji; uvuvi; teknolojia kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile vituo atamizi, mashamba darasa, semina pamoja na kuandaa vipindi mbalimbali katika runinga na redio.

121. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha matumizi salama ya mionzi

ya nyuklia nchini, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomu itatekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kudhibiti matumizi ya mionzi nchini kwa kukagua vituo 900 ikiwemo hospitali, vituo vya afya, migodi, viwanja vya ndege, na viwanda na majengo yenye mashine za kupima mionzi ili kuhakikisha uwepo wa mazingira salama kwa wagonjwa, wafanyakazi na umma kwa ujumla;

(ii) itapima na kudhibiti viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,110 wanaofanya kazi katika mazingira ya vyanzo vya mionzi katika hospitali, migodini na viwandani ili kuwalinda dhidi ya madhara yatokanayo na vyanzo vya mionzi sehemu za kazi;

(iii) itaendelea kusimamia kituo cha Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty Organisation - CTBTO cha kupima hewa katika anga kwa lengo la kudhibiti uchafuzi unaotokana na mionzi;

(iv) itaendelea kukusanya na kusafirisha mabaki ya vyanzo vya mionzi yanayotoka katika maeneo ya ujenzi wa barabara, hospitali, viwanda, migodi na taasisi za kitafiti na kuhifadhi katika kituo maalumu cha mabaki ya mionzi (Central Radioactive Waste Management Facility) ili kudhibiti athari za mionzi; na

(v) itaendelea na upimaji wa sampuli 50,000 za vyakula, mbolea, tumbaku na bidhaa nyingine zinazoingia na kutoka nchini kupitia mipaka ya nchi ikiwemo viwanja vya ndege na bandari pamoja na sampuli za maji ya visima, wasambazaji na wamiliki wa viwanda ili kuwalinda wananchi dhidi ya madhara yatokanayo na mionzi.

122. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utafiti wa tiba za saratani, Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa Kituo cha Utafiti cha Tiba za Saratani (Oncology Research Centre) jijini Arusha ili kuleta tija na ufanisi katika kukabiliana na tatizo la saratani nchini pamoja na kuimarisha utafiti na uchunguzi kwa kutumia teknolojia ya nyuklia. Aidha, itaendelea na ujenzi wa maabara za kanda katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mbeya na Mtwara kwa lengo la kusogeza

huduma za udhibiti wa mionzi na teknolojia ya nyuklia kwa wananchi.

## F. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)

123. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO, itaendelea kuratibu, kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kimataifa kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) kuendelea kuiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika vikao na mikutano ya UNESCO kwa lengo la kutetea maslahi ya nchi;

(ii) kuratibu na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kimataifa ya UNESCO ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji; na

(iii) kushirikiana na wadau katika kuhamasisha utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals) katika maeneo ya umahiri ya UNESCO.

## G. SHUKRANI

124. **Mheshimiwa Spika,** ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa QS. Omary Juma Kipanga (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu na kufikia malengo ya Wizara. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Profesa Carolyne Ignatius Nombo, Naibu Makatibu Wakuu, Profesa James Epiphan Mdoe na Dkt. Franklin Jasson Rwezimula kwa kunipa ushirikiano. Vilevile, ninaomba kutoa shukrani zangu kwa kamishna wa elimu, wakurugenzi, wakuu wa taasisi na watumishi wote kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa juhudi na ufanisi.

125. **Mheshimiwa Spika,** pia ninapenda kuwashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, walimu, wanafunzi, na wadau wote wa elimu kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki na mameneja wa shule, vyuo na taasisi binafsi ambao wamekuwa

wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu na mafunzo nchini.

126. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, ninawashukuru washirika wa maendeleo na wadau wote wa elimu ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa mipango na miradi ya elimu, sayansi na teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Afrika Kusini, Brazil, Canada, China, Cuba, Ethiopia, Finland, Hangaria, India, Israel, Italia, Japan, Kenya, Korea ya Kusini, Marekani, Mauritius, Misri, Norway, Sweden, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki, Uswisi. Aidha, natambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

127. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kushukuru Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na: Aga Khan Education Services, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Christian Social Services Commission (CSSC), Comprehensive Nuclear–Test - Ban Treaty Organisation (CTBTO), Deutscher Akademischer Austauschdienst (DAAD), Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO), Global Partnership for Education (GPE), Human Development Innovation Fund (HDIF), Inter University Council for East Africa (IUCEA), International Atomic Energy Agency (IAEA), Japan International Cooperation Agency (JICA), Jumuiya ya Madola, Karibu Tanzania Organization (KTO), Korea International Cooperation Agency (KOICA), Plan International, Swedish International Development Agency (SIDA), Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Umoja wa Nchi za Ulaya, United Nations Development Programme (UNDP), United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO), United Nations International Children's Emergency Fund (UNICEF),United States Agency for International Development (USAID) na Water Aid.

128. **MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25**

129. **Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa

mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,965,330,380,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:

(i) **Shilingi 637,287,706,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo **Shilingi 585,225,031,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 52,062,675,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(ii) **Shilingi 1,328,042,674,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 1,033,393,669,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 294,649,005,000.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

130. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,882,154,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni **Shilingi 1,319,040,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 1,563,114,000.00.**

131. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara (Fungu 46 na Fungu 18) yenye jumla ya **Shilingi 1,968,212,534,000.00.**

132. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

133. **Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara https://www.moe.go.tz

134. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho hilo la hoja ya Wizara yako. Sasa tutamsikia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali ili hatimaye liidhinishe Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, msingi wa Taarifa hii unatokana na masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kifungu cha 6(7)(a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti ya Kanuni niliyoyataja, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 21 Machi, 2023, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka

wa Fedha 2023/2024, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na matokeo yake ni taarifa hii yenye maoni na ushauri.

Mheshimiwa Spika, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya kwanza, inatoa maelezo ya jumla na kuonesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(ii) Sehemu ya pili, inabainisha uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(iii) Sehemu ya tatu inabainisha maoni na ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, ni Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi. Sehemu hii inafafanua matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi. Katika Uchambuzi huo, ufafanuzi unabainishwa kuhusu hali ya uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuhusu uwiano katika Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, itanatoa siku zisizozidi tisa kwa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti. Kanuni hiyo inatambua umuhimu wa kufanya ulinganisho kati ya

utekelezaji wa bajeti unaoripotiwa na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa msingi huo Sehemu hii inaripoti matokeo ya shughuli kuu tano zilizotekelezwa na Kamati kama ifuatavyo: -

(i) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(ii) Hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iii) Hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa maduhuli kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024;

(iv) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; na

(v) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kwa urahisi wa ufuatiliaji na uamuzi wa kibunge, naomba kubainisha matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitengewa jumla ya shilingi 1,137,872,565,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati ilitembelea miradi mitano kati ya miradi yote inayotekelezwa. Pamoja na ziara hiyo, Kamati ilipokea taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ufafanuzi zaidi kuhusu miradi, unaambatishwa pamoja na taarifa hii (Kiambatisho Na. 1).

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaonesha mambo yafuatayo: -

(i) Uwiano wa fedha za Maendeleo kwa Bajeti nzima ya Wizara unalingana na uwiano wa kiasi cha fedha za miradi ya maendeleo kilichopatikana. Kiasi kilichoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo

kilikuwa ni 68% ya bajeti yote na kiasi kilichopatikana kilikuwa ni 68% ya fedha zote zilizopatikana.

(ii) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo unaendana na kipindi cha utekelezaji. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024, fedha zilizopatikana ni 68% ya bajeti ya maendeleo na kipindi cha utekelezaji kilifikia 67%.

(iii) Makadirio ya baadhi ya gharama kwa miradi inayotekelezwa kwa awamu katika kipindi kirefu yanatofautiana na hali halisi. Kwa mfano, mradi Na. 4358 unaohusu kutegemeza Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, ulifanyiwa makadirio mwaka 2021. Mradi huu unaendelea kutekelezwa kwa misingi ya makadirio hayo hadi mwaka 2024. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wa mradi huu, hivyo basi, inasisitiza Wizara kuutazama upya utekelezaji wa mradi ili ulete tija kama ilivyokusidiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inaridhisha; upatikanaji wa fedha kutoka Hazina siyo miongoni mwa changamoto za utekelezaji. Hata hivyo, suala la ufinyu wa bajeti kwa miradi inayopangwa kutekelezwa linahitaji kuangaliwa kwa kina.

Mheshimiwa Spika, hali ya uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati, tarehe 16 Mei, 2023, wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilishauri mambo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, sehemu ya ushauri imefanyiwa kazi na sehemu nyingine utekelezaji wake unaendelea (Kiambatisho Na. 2).

Mheshimiwa Spika, mfano wa ushauri uliofanyiwa kazi unahusu kuandaa mikakati kwa ajili ya ugharamiaji wa elimu na mafunzo ya Amali, ikiwemo kuainisha vipaumbele kwa ajili ya wanafunzi watakaopatiwa mikopo katika vyuo hivi. Maelezo ya

Serikali yalionesha kuwa Serikali imeanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Amali sanifu (Elimu ya Ufundi) kwa kuzingatia fani za kipaumbele hususan zenye uhaba wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji mzuri wa ushauri, upo ushauri ambao unahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalan, ushauri kuhusu Serikali kufanya tathmini ya kina kuhusu utekelezwaji wa sera ya ugatuaji katika sekta ya elimu ili kubaini changamoto na mafanikio yake.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Serikali yalibainisha kwamba, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeendelea kuwa na vikao vya pamoja vya kisekta na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na maelezo yaliyotolewa na Serikali na hivyo, kusisitiza Serikali kuendelea kufanyia kazi ushauri huo.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa maduhuli, Kamati ilichambua ukusanyaji wa Maduhuli chini ya Wizara hii kwa sababu Wizara ililijulisha Bunge kiasi cha maduhuli yaliyolengwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ili kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa jukumu la ukusanyaji wa maduhuli, Kamati ilichambua taarifa iliyoeleza hali ya makusanyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitumia majedwali na grafu ili kubaini hali ya makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo, kwa urahisi wa ulinganisho. Rejea imefanywa katika Kielelezo Na. 01 na Kielelezo Na. 02.

Mheshimiwa Spika, katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Lengo la jumla la makusanyo ya maduhuli kwa Wizara hii ikiwa ni takribani robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji wa bajeti, lilifikiwa kwa 46% tu;

(ii) Uwiano wa lengo la ukusanyaji kati ya idara na vitengo chini ya Wizara na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara unatofautiana na uwiano wa makusanyo halisi kati ya Idara na vitengo vya Wizara na Taasisi zinazosimamiwa

na Wizara. Katika makadirio, Idara na Vitengo vya Wizara zilikuwa na lengo la asilimia mbili na taasisi zilikuwa na lengo la 98% ya jumla ya makusanyo, lakini wakati wa utekelezaji, idara na vitengo zilifikia asilimia tatu ya jumla ya makusanyo na taasisi zilifikia 97% ya jumla ya makusanyo.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huo wa ukusanyaji wa maduhuli unaashiria kutokufikiwa kwa lengo. Aidha, hali hiyo inahitaji kufanyiwa kazi ili kubaini iwapo upangaji wa lengo ulikuwa na changamoto au ni usimamizi wa ukusanyaji unaohitaji kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubaini mwenendo wa makusanyo usioridhisha kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilitaka kujiridhisha na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo. Taarifa za makusanyo zilichambuliwa na kupangwa katika vielelezo viwili: Kielelezo Na. 2:3 na Kielelezo Na. 2:4.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu mfululizo ufikiaji wa lengo la makusanyo ulikuwa ukiongezeka hadi kufikia 63% ya lengo mwaka wa fedha 2021/2022. Kiwango cha kufikia lengo kilianza kupungua mwaka wa fedha 2022/2023 na kufikia kiwango cha chini kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mwenendo huo unaonesha umuhimu wa kutathmini upangaji wa lengo la maduhuli na juhudi za ukusanyaji.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida, baada ya Bunge kuidhinisha matumizi ya kawaida ya Wizara hii, ilibaki kuwa kazi ya Kamati kufuatilia utekelezaji unaofanyika. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati iliendelea kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Aidha, tarehe 20 Machi, 2024, Kamati ilipokea maelezo ya Wizara yaliyofafanua upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Taswira halisi ya mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonekana katika Kielelezo Na. 2:5 na Kielelezo Na. 2:6.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kuwa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umeendana na kipindi cha utekelezaji. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024, kiasi cha fedha zilizopatikana kilifikia 68% ya kiasi kilichoidhinishwa. Hata hivyo, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ulikuwa ni 46% ambayo ni pungufu ya nusu. Hali hii ni ishara ya uwezekano wa matumizi ya kawaida kutokupatikana inavyopaswa.

Mheshimwia Spika, kwa mwenendo huo, utekelezaji wa majukumu ya kawaida utakuwa umeathirika. Kuhusu uwiano wa aina za matumizi, Kamati imebaini kuwa hakuna tofauti ya uwiano ulioidhinishwa na hali ilivyo katika utekelezaji kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 2:6.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilikusudiwa kuwezesha utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara hii. Ili kujiridhisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, Kamati ilipokea na kuchambua maelezo ya Waziri kuhusu majukumu na mipango iliyotekelezwa. Maelezo haya yalihusu majukumu na mipango kwa Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Fungu 18 - Tume ya Taifa ya UNESCO.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa mipango na majukumu uliendana na upatikanaji wa fedha. Kwa ujumla wake, majukumu na mipango kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yanaendelea kutekelezwa vizuri na ufanisi wake unaonekana. Kwa mfano, Wizara ilikuwa na mpango wa kutoa mafunzo kabilishi kuhusu utekelezaji wa mitaala ulioboreshwa. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali iliripoti utekelezaji wa mpango huo. Maelezo ya Waziri yalionesha kuwa Mafunzo Kabilishi yametolewa kwa Wawezeshaji 11,521 wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilidadisi zaidi kuhusu mpango uliowekwa na Wizara ili kuboresha elimu ya msingi na kuongeza fursa na ubora wa mafunzo ya amali, shule za sekondari na elimu ya juu. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa Serikali imeendelea kutekeleza mipango hiyo. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji huo unakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mfano wa changamoto hizo ni uhaba wa walimu, wakufunzi na wahadhiri hususan katika masomo/fani za sayansi, hisabati na mafunzo ya Amali. Vilevile, ipo changamoto kubwa ya mdondoko wa wanafunzi katika elimu ya msingi na Sekondari. Ni maoni ya Kamati kuwa changamoto hizo zinastahili kuwekewa mkakati mahsusi wa kuzitatua.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ulifanyika kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka huo wa fedha husika. Umakini zaidi uliwekwa katika maeneo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli;

(ii) Makadirio ya matumizi kwa ajili ya gharama ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na

(iii) Makadirio ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa maeneo hayo unafanyika kwa kuzingatia majukumu ya msingi ya Wizara hii pamoja na mwelekeo wa jumla wa Taifa letu. Ulinganisho wa aina za matumizi ulifanyika kwa kulinganisha na uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara kupitia Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini yake zinakadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 677,299,142,074. Kamati ilichambua makadirio hayo ili kulisaidia Bunge wakati wa majadiliano. Uchambuzi unaonesha kuwa, makadirio ya maduhuli yamepungua kwa asilimia sifuri nukta tatu ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ingawa bajeti ya matumizi ya Wizara imeongezeka kwa 17%.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha ukusanyaji wa maduhuli hauna dalili ya kufikia lengo.

Kamati inaishauri Wizara iongeze juhudi katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipochambua makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilibaini kuwa makadirio yameongezeka kwa 68%. Matokeo hayo ya uchambuzi yanaonesha kuwa Serikali imeongeza kipaumbele katika miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko hilo, bado bajeti ya elimu ni 14% tu ya Bajeti yote ya Serikali na hivyo kutokufikia lengo la kimataifa la 20% ya bajeti yote ya Serikali. Aidha, pamoja na ongezeko hilo, bado Kamati haijaridhishwa na fedha zilizotengwa katika maeneo yafuatayo: -

(i) Upungufu wa fedha za utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, Toleo la Mwaka 2023 na Mitaala ya Elimu ambapo utasababisha upungufu wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia, upungufu wa walimu wenye ubora na sifa kulingana na mitaala mipya na hata kuathiri uwezo wa wanafunzi kufikia mafanikio ya elimu.

(ii) Upungufu wa fedha za kuchapisha vitabu katika Taasisi ya Elimu Tanzania ambapo kwa sasa uwiano wa vitabu kwa shule za msingi na sekondari ni kitabu kimoja, wanafunzi watano, lakini lengo ni kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu.

(iii) Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu zimepungua ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024 zinaweza kusababisha upungufu wa wanafunzi wengi wenye uhitaji kukosa fursa ya elimu ya juu.

(iv) Bajeti ndogo iliyotengwa kwa ajili ya Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* haitoshelezi mahitaji na hivyo, inaweza kusababisha na kuleta athari ya ukosefu wa vifaa na miundombinu, mafunzo duni, upungufu wa

walimu wenye ujuzi, kupungua kwa uwezo wa utafiti na maendeleo pamoja na kupungua kwa ushindani wa kimataifa.

(v) Baraza la Mitihani la Taifa *(NECTA)* halijatengewa fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 kama ahadi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwezesha Baraza la Taifa la Mitihani *(NECTA)* ya kununua mitambo mitatu ya uchapashaji wa mitihani.

(vi) Kuwepo kwa ukomo mdogo wa fedha za nje na hivyo, kukwamisha shughuli za utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia - Fungu 46, lilikadiria kutumia jumla ya shilingi 1,965,330,380,000. Kati ya fedha hizo shilingi 585,225,031,000 sawa na 31% ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara na taasisi zake; shilingi 52,062,675,000 sawa na 41% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 1,328,042,674,000, sawa na 68% ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ufafanuzi zaidi upo katika kielelezo Na. 2:1 na Na. 2:8.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ni maoni na ushauri wa Kamati. Kutokana na uchambuzi uliofanywa, Kamati inaomba kutoa maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Hata hivyo, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(i) Serikali iweke umakini katika usimamazi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha ili kuwezesha upatikamaji wa thamani halisi na kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati;

(ii) Kamati inasisitiza kuongeza kasi ya utolewaji wa fedha za miradi mbalimbali inayoendana na ujenzi na ukarabati wa vyuo vikuu na kuwepo na usimamizi mzuri wa miradi ili ikamilike kwa wakati na kuweza kutimiza lengo la kuanzishwa kwake.

(iii) Ujenzi wa Vyuo vya *VETA* unaoendelea katika mikoa mbalimbali nchini uzingatie upatikanaji wa maeneo makubwa ambayo yanakidhi ujenzi wa miundombinu ya kisasa na mahitaji ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia sehemu kubwa ni bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambayo ni 60.33% ya Bajeti ya Mendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara hii ili kuboresha na kuimarisha Sekta ya Elimu na kukuza maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)*. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza Sera ya Kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi Nchini. Ujenzi huu ukikamilika utaongeza fursa ya upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi kwa lengo la kuwawezesha wananchi, hususan vijana, kupata ujuzi unaowawezesha kujiajiri au kuajiriwa na hivyo kupunguza tatizo la ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo kwa ufinyu wa bajeti, idadi ndogo ya wakufunzi, upungufu wa vitendea kazi na ukosefu wa zana za kufundishia na kujifunzia. Kamati inasisitiza yafuatayo yafanyike ili kuboresha mpango wa ujenzi wa Vyuo vya *VETA* nchini:-

(i) *VETA* iongezewe bajeti kwa ajili ya uendeshaji wa vyuo vipya 29 vilivyoongezeka ili viweze kutoa mafunzo na kuleta tija iliyokusudiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwezesha Watanzania hususan vijana kupata ujuzi utakaowawezesha kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kujiajiri. Hata hivyo Wizara iweke

mpango madhubuti kwa ajili ya uendeshaji wa vyuo vinavyoendelea kujengwa ambapo vikikamilika taasisi hii itakuwa na jumla ya vyuo 145 kutoka 51 vilivyokuwepo hapo awali.

(ii) Ujenzi wa Vyuo vya *VETA* uende sambamba na kuajiri wakufunzi wa mafunzo ya ufundi kulingana na mahitaji pamoja vitendea kazi husussan karakana za ufundi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na elimu ya kati. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo kwa ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wanaostahili pamoja na Bodi kushindwa kupata marejesho ya mikopo hiyo kwa wanufaika. Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imeongezewa jukumu la kutoa mikopo ya elimu ya kati, Serikali iongeze Bajeti ya Bodi ya Mikopo kwa ajili ya kuongeza idadi ya wanafunzi wa elimu juu na elimu ya kati wanaopaswa kupata mikopo hiyo.

(ii) Kamati inasisitiza kuwa, Serikali iangalie upya vigezo vya utoaji wa mikopo ya elimu ya juu ili kupunguza malalamiko ya kutokuwa na vigezo vya ulinganifu yanayojitokeza mara kwa mara miongoni mwa waombaji na wazazi.

(iii) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iongeze juhudi ya kutoa elimu kwa umma, hususan umuhimu wa ulazima wa wanafunzi waliopata mikopo hiyo kurejesha fedha hizo kama sheria inavyoelekeza.

(iv) Bodi ya Mikopo iangalie namna ya kuweka utaratibu madhubuti wa kurahisisha utoaji wa mikopo na ukusanyaji wa mikopo ndani na nje ya nchi ili mikopo hiyo iweze kukopeshwa kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, katika kuanza utekelezaji wa mitaala mipya ya elimu na kusisitiza mafunzo ya amali, Kamati imebaini kuwepo kwa upungufu wa rasilimali fedha pamoja na miundombinu jambo ambalo linaweza kuathiri madhumuni ya mitaala mipya na ubora wa elimu kwa ujumla wake. Hivyo basi, Kamati ina ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa mitaala mipya pamoja na kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia kama vile kujenga karakana, maabara pamoja na kuhakikisha vifaa vya mafunzo ya amali vinapatikana.

(ii) Serikali iongeze fedha kwa ajili ya vyuo vya ualimu ambavyo vinatoa na kuandaa mafunzo ya ualimu yanayoendana na mitaala mipya.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo wa kuchapisha vitabu kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi ni kwa Wizara ya Fedha kupeleka fedha hizo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao nao wanapeleka fedha hizo katika Taasisi ya Elimu kupitia Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati imebaini kwamba shilingi bilioni 17 zilipokelewa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tangu mwezi Novemba, 2023 zikakaa hadi mwezi Machi, 2024, takribani miezi mitano bila kutumika, jambo ambalo lilisababisha fedha hizo kurudishwa Hazina. Kamati inasikitishwa na hali hii inayoendelea kwani inakwamisha uchapaji na usambazaji wa vitabu shuleni kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa, kwa kuwa jukumu la kuandika, kuchapa na kusambaza vitabu linatekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mamlaka ya Elimu *(TET),* ni vyema fedha za uchapishaji wa vitabu zipelekwe *TET* moja kwa moja kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kuongeza ufanisi katika kufikia lengo lililokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mafunzo ya Ualimu kazini ni sehemu muhimu ya kuboresha stadi za ufundishaji na kuhakikisha walimu wanakidhi mahitaji ya wanafunzi katika mazingira ya kisasa ya elimu kulingana na mitaala mipya; na kwa kuwa, mafunzo haya bado utekelezaji wake siyo wa kuridhisha; hivyo basi, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa mitaala mipya, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha walimu wote wanapaswa siyo tu kufahamu vizuri mitaala hii, lakini pia kujengewa uwezo wa mafunzo ya namna bora ya utekelezaji wa mitaala mipya ili waweze kuboresha ujuzi na kupata mbinu mbalimbali za ufundishaji ambazo zitasaidia kujifunza maarifa mapya. Aidha, mafunzo haya yatolewe kwa walimu wote nchini wa shule za msingi na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za nje kutokana na ukomo mdogo wa fedha ambao unachangia kwa kiasi kikubwa kuchelewesha utekelezaji wa miradi hiyo na hivyo, kusababisha kusuasua kwa baadhi ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa vifungu vya fedha za nje vinavyotekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia vitanuliwe bila kuathiri sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za Serikali ili ziweze kutekeleza miradi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa la mdondoko wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari hususan watoto wa kiume, hali inayosababisha ongezeko kubwa la watoto wa kiume kuwepo mitaani. Kamati imebaini mdondoko huo unasababishwa na watoto wa kiume kutopewa mkazo wa masomo kama ilivyo kwa watoto wa kike. Aidha, sababu nyingine ya ongezeko hilo ni ajira za watoto wadogo kwa baadhi ya wanafunzi kuchagua kuacha shule ili kuweza kusaidia familia zao kutafuta kipato. Hivyo basi, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iweke mkakati madhubiti wa kuhakikisha wanafunzi wote walioandikishwa shule wanahitimu

masomo yao. Aidha, waraka uliotumika kuwarudisha watoto wa kike shuleni utumike pia kuwarudisha watoto wa kiume shuleni. Vilevile, walimu wapewe mafunzo ya kufundisha watoto waliopo kwenye mfumo wa elimu usio rasmi.

(ii) Waraka uliotolewa na Mheshimiwa Rais wa kuwarudisha shuleni watoto wa kike waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali uingizwe kwenye marekebisho ya Sheria ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwa, Sheria iliyopo sasa haina kipengele hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo ya kuanzishwa kwa Vyuo vya Elimu ya Juu nchini ni kutoa elimu ya juu yenye ubora, kukuza tafiti na uvumbuzi, kukuza ujuzi na stadi, kusaidia na kuchochea maendeleo ya kitaifa na kukuza utamaduni na maadili katika jamii.

Mheshimiwa Spika, licha ya kazi nzuri inayofanywa na vyuo hivi, Kamati inaamini kuwa, vyuo vikuu vina wajibu wa kuhakikisha vinatoa mchango wake kwa kuendeleza na kukuza viwango vya elimu na mafunzo nchini ili kupata rasilimali watu yenye weledi, maarifa na ujuzi katika nyanja mbalimbali za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona upo umuhimu wa vyuo vikuu kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia malengo ya uanzishwaji wake ambavyo ni alama katika nchi yetu kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kwamba, Chuo Kikuu cha Dodoma kiendelee na utekelezaji wa malengo yaliyowekwa ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa Ndaki ya Sayansi Asilia na Hisabati na Ndaki ya Sayansi za Ardhi na Uhandisi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Serikali ihakikishe ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali inayoendelea kutekelezwa unakamilika kwa wakati.

Hii iende sambamba na kuboresha miundombinu ya kufundishia, majengo ya utawala na mabweni ya wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru Mheshimiwa Prof. Adolf Faustine Mkenda, Mbunge na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia; na wasaidizi wake, Mheshimiwa Omary Shaban Kipanga, Mbunge na Naibu Waziri; na Mheshimiwa Prof. Carolyne Nombo, Katibu Mkuu wa Wizara hii; pamoja na watendaji wake wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema wakati wote ilipokuwa ikikutana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii ili liijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**7 MEI, 2024**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali ili hatimaye liidhinishe Bajeti ya Wizara hii.

### 1.1 Msingi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Taarifa hii unatokana na masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6 (7)(a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti ya Kanuni niliyoyataja, nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa tarehe 21 Machi, 2023, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na matokeo yake ni Taarifa hii yenye maoni na ushauri.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo:-

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(ii) Sehemu ya Pili inabainisha Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muundo huo, Bunge linaweza kuwa kwenye nafasi nzuri ya kuitumia Taarifa hii wakati wa majadiliano. Mtiririko wa maudhui umewekwa kwa namna rahisi ya rejea na matumizi ya Bunge.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI

### 2.1 Maelezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inafafanua matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi. Katika Uchambuzi huo, ufafanuzi unabainishwa kuhusu hali ya uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hali ya Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuhusu uwiano katika makadirio ya matumizi ya maendeleo na matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

## 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, itanatoa siku zisizozidi tisa kwa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti. Kanuni hiyo inatambua umuhimu wa kufanya ulinganisho kati ya utekelezaji wa bajeti unaoripotiwa na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa msingi huo Sehemu hii inaripoti matokeo ya shughuli kuu Tano (5) zilizotekelezwa na Kamati kama ifuatavyo: -

(i) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(ii) Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iii) Hatua iliyofikiwa katika Ukusanyaji wa Maduhuli kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Februari, 2024;

(iv) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina; na

(v) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa urahisi wa ufuatiliaji na uamuzi wa kibunge, naomba kubainisha matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo:-

### 2.2.1 Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitengewa jumla ya Shilingi 1,137,872,565,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati ilitembelea miradi mitano kati ya miradi yote inayotekelezwa. Pamoja na ziara hiyo, Kamati ilipokea taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Ufafanuzi zaidi kuhusu Miradi unaambatishwa pamoja na Taarifa hii (Kiambatisho Na. 1).

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa hali ya Utekelezaji wa Miradi ya maendeleo unaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Uwiano wa fedha za Maendeleo kwa Bajeti nzima ya Wizara unalingana na uwiano wa kiasi cha fedha za miradi ya maendeleo kilichopatikana. Kiasi kilichoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kilikuwa ni asilimia 68 ya bajeti yote na kiasi kilichopatikana kilikuwa ni asilimia 68 ya fedha zote zilizopatikana.

(ii) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo unaendana na kipindi cha utekelezaji. Hadi kufikia Mwezi Februari 2024, Fedha zilizopatikana ni asilimia 68 ya bajeti ya maendeleo na kipindi cha utekelezaji kilifikia asilima 67.

(iii) Makadirio ya baadhi ya gharama kwa miradi inayotekelezwa kwa awamu katika kipindi kirefu yanatofautiana na hali halisi. Kwa mfano, mradi Na. 4358 unaohusu kutegemeza Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, ulifanyiwa makadirio mwaka 2021. Mradi huu unaendelea kutekelezwa kwa misingi ya makadirio hayo hadi mwaka 2024. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wa mradi huu, hivyo basi, inasisitiza Wizara kuutazama upya utekelezaji wa mradi ili ulete tija kama ilivyokusidiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inaridhisha. Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina si miongoni mwa changamoto za utekelezaji. Hata hivyo, suala la ufinyu wa bajeti kwa miradi inayopangwa kutekelezwa linahitaji kuangaliwa kwa kina.

### 2.2.2 Hali ya Uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 16 Mei, 2023, wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilishauri mambo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa

majukumu ya Wizara hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, sehemu ya ushauri imefanyiwa kazi na sehemu nyingine utekelezaji wake unaendelea (Kiambatisho Na. 2).

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri uliofanyiwa kazi unahusu kuandaa mkakati kwa ajili ya ugharamiaji wa elimu na mafunzo ya amali, ikiwemo kuainisha vipaumbele kwa ajili ya wanafunzi watakaopatiwa mikopo katika vyuo hivi. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa Serikali imeanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa amali sanifu (Elimu ya Ufundi) kwa kuzingatia fani za kipaumbele hususan zenye uhaba wa rasilimaliwatu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na utekelezaji mzuri wa ushauri, upo ushauri ambao utahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalan, ushauri kuhusu Serikali kufanya tathimini ya kina kuhusu utekelezwaji wa sera ya ugatuaji katika sekta ya elimu ili kubaini changamoto na mafanikio yake. Maelezo ya Serikali yalibainisha kwamba, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeendelea kuwa na vikao vya pamoja vya kisekta na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na maelezo yaliyotolewa na Serikali na hivyo, kusisitiza Serikali kuendelea kufanyia kazi ushauri huo.

### 2.2.3 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua ukusanyaji wa Maduhuli chini ya Wizara hii kwa sababu Wizara ililijulisha Bunge kiasi cha maduhuli yaliyolengwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ili kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa jukumu la ukusanyaji wa maduhuli, Kamati ilichambua taarifa iliyoeleza hali ya makusanyo.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitumia Majedwali na Grafu ili kubaini hali ya makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo. Kwa urahisi wa ulinganisho rejea imefanywa kwenye Kielelezo Na. 01 na Kielelezo Na. 02.

**Kielelezo Na. 2:1 Ulinganisho wa Makadirio na Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2022/2023 na 2023/2024**

| MWAKA | CHANZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 2022/2023 | Idara/Vitengo | 8,680,995,000.00 | 6,546,086,027.00 | 75.41 |
| | Taasisi | 633,986,625,483.06 | 331,653,392,514.42 | 52.31 |
| 2023/2024 | Idara/Vitengo | 11,660,695,000.00 | 10,303,067,874.29 | 88.36 |
| | Taasisi | 667,701,877,548.64 | 308,036,472,007.95 | 46.13 |

**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Kielelezo Na. 2:2 Grafu ya ulinganisho wa Makadirio na Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024**




**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

(i) Lengo la jumla la makusanyo ya maduhuli kwa Wizara hii ikiwa ni takriban robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji wa bajeti, lilifikiwa kwa asilimia 46 tu.

(ii) Uwiano wa lengo la Ukusanyaji kati ya idara na vitengo chini ya wizara na taasisi zinazosimamiwa na wizara unatofautiana na uwiano wa makusanyo halisi kati ya idara na vitengo vya wizara na taasisi zinazosimamiwa na wizara. Katika makadirio, Idara na Vitengo vya Wizara zilikuwa na lengo la asilimia 2 na taasisi zilikuwa na lengo la asilimia 98 ya Jumla ya Makusanyo. Lakini wakati wa utekelezaji, Idara na vitengo zilifikia asilimia 3 ya jumla ya makusanyo na taasisi zilifikia asilimia 97 ya jumla ya makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, Mwenendo huo wa ukusanyaji wa maduhuli unaashiria kutokufikiwa kwa lengo. Aidha, hali hiyo inahitaji kufanyiwa kazi ili kubaini iwapo upangaji wa lengo ulikuwa na changamoto au ni usimamizi wa ukusanyaji unaohitaji kuimarishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kubaini mwenendo wa makusanyo usioridhisha kwa mwaka 2023/2024, Kamati ilitaka kujiridhisha na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa kipindi cha miaka mitano (5) mfululizo. Taarifa za makusanyo zilichambuliwa na kupangwa katika vielelezo viwili: Kielelezo Na. 2:3 na Kielelezo Na. 2:4.


**Kielelezo Na. 2:3 Jedwali linaloonesha Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2023/2024**

| MWAKA | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| 2019/2020 | 553,739,899,119.13 | 292,681,843,256.11 | 53 |
| 2020/2021 | 555,651,650,346.52 | 307,254,682,022.00 | 55.3 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2021/2022 | 555,043,008,495.63 | 350,484,167,565.79 | 63 |
| 2022/2023 | 642,667,620,483.06 | 338,199,478,541.42 | 53 |
| 2023/2024 | 679,362,572,548.64 | 318,339,539,882.24 | 47 |

***Chanzo:*** *Taarifa za Kamati 2019/2020 – 2022/2023 na Randama ya Wizara 2023/2024*

**Kielelezo Na. 2:4 Grafu ya Mwenendo wa Ufikiaji wa lengo la Makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi cha mwaka 2019/2020 hadi 2023/2024**




**Chanzo:** Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Taarifa za Kamati Mwaka 2019/2020 hadi 2023/2024 na Randama ya Wizara kwa mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, kwa miaka mitatu (3) mfululizo ufikiaji wa lengo la makusanyo ulikuwa ukiongezeka hadi kufikia asilimia 63 ya lengo mwaka wa fedha 2021/2022. Kiwango cha kufikia lengo kilianza kupungua mwaka wa fedha 2022/2023 na kufikia kiwango cha chini kwa mwaka 2023/24. Mwenendo huo unaonesha umuhimu wa kutathmini upangaji wa lengo la maduhuli na juhudi za ukusanyaji.

### 2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Bunge kuidhinisha matumizi ya kawaida ya Wizara hii, ilibaki kuwa kazi ya Kamati kufuatilia utekelezaji unaofanyika. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Kamati iliendelea kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Aidha, tarehe 20 Machi, 2024, Kamati ilipokea maelezo ya Waziri yaliyofafanua upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Taswira halisi ya mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonekana katika Kielelezo Na.2:5 na Kielelezo Na. 2:6


**Kielelezo Na. 2: 5: Mchanganuo wa Upatikanaji wa Fedha kwa aina mbalimbali za Matumizi**


| AINA YA MATUMIZI | KIASI KILICHOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Mishahara** | 502,082,549,000.00 | 344,377,453,121.48 | 68.6 |
| **Kawaida** | 38,532,101,000.00 | 18,022,611,664.09 | 46.8 |
| **Maendeleo** | 1,137,872,565,000.00 | 775,054,920,713.06 | 68.1 |
| **JUMLA** | **1,678,487,215,000.00** | 1,137,454,985,498.63 | 67.8 |

**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unaonesha kuwa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umeendana na kipindi cha utekelezaji. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2024, kiasi cha fedha zilizopatikana kilifikia asilimia 68 ya kiasi kilichoidhinishwa. Hata hivyo, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ulikuwa ni asilimia 46 ambayo ni pungufu ya nusu. Hali hii ni ishara ya uwezekano wa matumizi ya kawaida kutokupatikana inavyopaswa. Kwa mwenendo huo, utekelezaji wa majukumu ya kawaida utakuwa umeathirika. Kuhusu uwiano wa aina za matumizi, Kamati imebaini kuwa hakuna tofauti ya uwiano ulioidhinishwa na hali ilivyo katika utekelezaji kama inavyoonekana katika Kielelezo Na 2:6

**Kielelezo Na. 2:6: Uwiano wa Aina za Matumizi wakati wa kuidhinisha Bajeti na Uwiano wake kwa upatikanaji wa Fedha**




**Chanzo**: Usanifu wa Kamati kutokana na Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

### 2.2.5 Utekelezaji wa Majukumu na Mipango ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ilikusudiwa kuwezesha utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara hii. Ili kujiridhisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, Kamati ilipokea na kuchambua maelezo ya Waziri kuhusu majukumu na mipango iliyotekelezwa. Maelezo hayo yalihusu Majukumu na Mipango kwa Fungu 46 – Wizara na Fungu 18- Tume ya Taifa ya UNESCO.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa mipango na majukumu uliendana na upatikanaji wa fedha. Kwa ujumla wake, majukumu na mipango kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yanaendelea kutekelezwa vizuri na ufanisi wake unaonekana. Kwa mfano, Wizara ilikuwa imepanga kutoa mafunzo kabilishi kuhusu utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa. Nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Serikali iliripoti utekelezaji wa mpango huo. Maelezo ya Waziri yalionesha kuwa Mafunzo kabilishi yametolewa kwa Wawezeshaji **11,521** wa Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilidadisi zaidi kuhusu mpango uliowekwa na Wizara ili kuboresha elimu ya msingi na kuongeza

fursa na ubora wa mafunzo ya amali, shule za sekondari na elimu ya juu. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa Serikali imeendelea kutekeleza mipango hiyo. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji huo unakabiliwa na changamoto mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa changamoto hizo ni uhaba wa walimu, wakufunzi na wahadhiri hususan katika masomo/fani za sayansi, hisabati na mafunzo ya amali. Vilevile, ipo changamoto kubwa ya mdondoko wa wanafunzi katika elimu ya msingi na Sekondari. Ni maoni ya Kamati kuwa changamoto hizo zinastahili kuwekewa mkakati mahsusi wa kuzitatua.

### 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ulifanyika kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka huo wa fedha. Umakini zaidi uliwekwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya ukusanyaji wa Maduhuli;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya gharama ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na

(iii) Makadirio ya Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa maeneo hayo unafanyika kwa kuzingatia Majukumu ya Msingi ya Wizara hii pamoja na mwelekeo wa Jumla wa Taifa letu. Ulinganisho wa aina za Matumizi ulifanyika kwa kulinganisha na uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

#### 2.3.1 Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara kupitia Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini yake zinakadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya Shilingi 677,299,142,074.83. Kamati ilichambua makadirio hayo ili kulisaidia Bunge wakati wa majadiliano. Uchambuzi unaonesha kuwa, makadirio ya Maduhuli yamepungua kwa asilimia 0.3 ikilinganishwa na lengo la

makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ingawa bajeti ya matumizi ya Wizara imeongezeka kwa asilimia 17. Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha ukusanyaji wa maduhuli hauna dalili ya kufikia lengo. Kamati inaishauri Wizara iongeze juhudi katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

**2.3.2 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipochambua makadirio ya matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ilibaini kuwa Makadirio yameongezeka kwa asilimia 68. Matokeo hayo ya uchambuzi yanaonesha kuwa Serikali imeongeza kipaumbele katika miradi inayotekelezwa na Wizara hii. Pamoja na ongezeko hilo bado bajeti ya Elimu ni asilimia 14 tu ya Bajeti yote ya Serikali na hivyo kutokufikia lengo la Kimataifa la asilimia 20 ya bajeti yote ya Serikali. Aidha pamoja na ongezeko hilo, bado Kamati haikuridhishwa na fedha zilizotengwa katika maeneo yafuatayo:-

i. Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo, 2014 Toleo la Mwaka 2023 na Mitaala ya Elimu ambapo utasababisha upungufu wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia, upungufu wa walimu wenye ubora na sifa kulingana na mitaala mipya na hata kuathiri uwezo wa wanafunzi kufikia mafanikio ya Elimu;

ii. Upungufu wa fedha za kuchapisha vitabu Taasisi ya Elimu Tanzania ambapo kwa sasa uwiano wa vitabu katika shule za awali, msingi kwa mwanafunzi ni 1:5 na mahitaji ni 1:3;

iii. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu *(Higher Education Students Loans - HESLB)* zimepungua ukilinganisha *na mwaka 2023/2024* zinaweza kusababisha upungufu wa wanafunzi wengi wenye uhitaji kukosa fursa za elimu ya juu na wenye uwezo mdogo wa kifedha;

iv. Bajeti ndogo iliyotengwa kwa ajili ya Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) haijoshelezi mahitaji na hivyo inaweza kusababisha na kuleta athari ya

ukosefu wa vifaa na miundombinu, mafunzo duni ya kufundishia na kujifunzia, upungufu wa walimu wenye ujuzi, kupungua kwa uwezo wa utafiti na maendeleo pamoja na kupungua kwa ushindani wa Kimataifa;

v. Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) halijatengewa fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha, 2024/2025 kama ahadi ya Mhe. Rais ya kuwezesha Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) ya kununua mitambo 3 ya uchapashaji mitihani;

vi. Kuwepo kwa ukomo mdogo wa fedha za nje na hivyo kukwamisha shughuli za utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na fedha hizo.

**2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida**


**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (*Fungu 46*) inakadiria kutumia jumla ya Shilingi 1,965,330,380,000. Kati ya Fedha hizo Shilingi 585,225,031,000 sawa na asilimia 31 ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zake, Shilingi 52,062,675,000 sawa na asilimia 41 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 1,328,042,674,000 sawa na asilimia 68 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Kielelezo Na. 2:7: Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa 2023/2024 na Mwaka 2024/2025**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025 | % ONGEZEKO/ PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 500,957,569,000 | 585,225,031,000 | 17 |
| Kawaida | 36,923,193,000 | 52,062,675,000 | 41 |
| Maendeleo | 1,137,872,565,000 | 1,328,042,674,000 | 13 |
| **JUMLA** | **1,675,753,327,000** | **1,965,330,380,000.00** | **17** |

***Chanzo:*** Usanifu wa Kamati kutokana na Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Kielelezo Na. 2:8: Mgawanyo wa Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**




***Chanzo:*** Usanifu wa Kamati kutokana na Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati ina maoni ambayo yanajenga msingi wa ushauri utakaotolewa kama ifuatavyo;-

### 3.2 Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Hata hivyo, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(i) Serikali iweke umakini katika usimamazi wa Miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha ili kuwezesha kupatika kwa thamani halisi ya fedha na kukamilisha haraka na kwa wakati miradi hiyo;

(ii) Kamati inasisitiza kuongeza kasi ya utolewaji wa fedha za miradi mbalimbali inayoendelea ya ujenzi na ukarabati wa Vyuo Vikuu na kuwepo na usimamazi mzuri wa miradi hiyo ili ikamilike kwa wakati na kuweza kutimiza lengo la kuanzishwa kwake; na

(iii) Ujenzi ya Vyuo vya VETA unaoendelea katika Mikoa mbalimbali nchini uzingatie upatikanaji wa maeneo makubwa ambayo yatakidhi ujenzi wa miundombinu ya kisasa na mahitaji ya baadaye.

### 3.3 Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia sehemu kubwa ni bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambayo ni asilimia 60.33 ya bajeti ya mendeleo. Hali hii inakwamisha dhamira ya kuimarisha miundombinu na taratibu za nchi kupata watanzania walioelimika na wanaoendelea kujielimisha na kuongeza tija katika maendeleo ya Taifa. Kamati inaishauri Serikali kuendelea

kuongeza bajeti ya Wizara hii ili kuboresha na kuimarisha Sekta ya Elimu na kukuza maendeleo ya Taifa.

### 3.4 Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza Sera ya kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi nchini. Ujenzi huu ukikamilika utaongeza fursa ya upatikanaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa lengo la kuwawezesha wananchi hususan vijana kupata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri au kuajiriwa na hivyo kupunguza tatizo la ajira nchini. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo kwa ufinyu wa Bajeti, idadi ndogo ya Wakufunzi, upungufu wa vitendea kazi na ukosefu wa zana za kufundishia na kujifunzia. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inasisitiza yafuatayo yafanyike ili kuboresha mpango wa ujenzi wa vyuo hivi:-

(i) VETA iongezewe bajeti kwa ajili ya uendeshaji wa vyuo vipya 29 vilivyoongezeka ili viweze kutoa mafunzo na kuleta tija iliyokusudiwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwezesha Watanzania hususan vijana kupata ujuzi utakaowawezesha kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kujiajiri. Hata hivyo Wizara iweke mpango madhubuti kwa ajili ya uendeshaji wa vyuo vinavyoendela kujengwa ambapo vikikamilika Taasisi hii itakuwa na jumla ya Vyuo 145 kutoka 51 vilivyokuwepo hapo awali;

(ii) Ujenzi wa Vyuo hivi vya VETA uende sambamba na kuajiriwa kwa Wakufunzi wa mafunzo ya ufundi kulingana na mahitaji pamoja vitendea kazi hususani Karakana za Ufundi.

### 3.5 Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na elimu ya kati kwani bajeti na idadi ya wanufaika imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka jambo ambalo ni jema sana. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo kwa ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wanaostahili pamoja na Bodi

kushindwa kupata marejesho ya mikopo hiyo kwa wanufaika. Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa, Bodi ya Mikopo ya Elimu juu imeongezewa jukumu la kutoa mikopo ya Elimu ya kati, Serikali iongeze bajeti ya Bodi ya Mikopo kwa ajili ya kuongeza idadi ya wanafunzi wa Elimu ya Juu na Elimuya Kati wanaopaswa kupata mikopo hiyo;

(ii) Kamati inasisitiza kuwa, Serikali iangalie upya vigezo vya utoaji wa mikopo ya Elimu ya Juu ili kupunguza malalamiko ya kutokuwa na vigezo vya ulinganifu yanayojitokeza mara kwa mara miongoni mwa waombaji na wazazi;

(iii) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iongeze juhudi ya kutoa elimu kwa umma hususan umuhimu na ulazima wa wanafunzi waliopata mikopo hiyo kurejesha fedha hizo kama sheria inavyoelekeza;

(iv) Bodi ya Mikopo iangalie namna ya kuweka utaratibu madhubuti wa kurahisisha utoaji wa mikopo na ukusanyaji wa mikopo ndani na nje ya nchi ili mikopo hiyo iweze kuwakopesha wengine.

### 3.4 Utekelezaji wa MItaala Mipya

**Mheshimiwa Spika**, Katika kuanza utekelezaji wa Mitaala mipya wa Elimu na kusisitiza mafunzo ya Amali, Kamati imebaini uwepo wa upungufu wa rasilimali fedha pamoja na miundombinu jambo ambalo linaweza kuathiri madhumuni ya mitaala mipya na kwamba inaweza kuathiri manufaa ya Elimu waipatayo wanafunzi. Hivyo, basi Kamati inaushauri ufuatao:-

(i) Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa mitaala mipya pamoja na kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia kama vile kujenga Karakana, Maabara pamoja na kuhakikisha vifaa vya mafunzo ya amali vinapatikana;

(ii) Serikali iongeze fedha kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu ambavyo vitatoa na kuandaa mafunzo ya Ualimu yanayoendana na mitaala mipya.

### 3.5 Fedha kwa ajili ya Uchapishaji wa Vitabu

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu uliopo wa kuchapisha vitabu kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi ni kuwa Wizara ya Fedha inapeleka fedha Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambao nao wanapeleka fedha hizo Taasisi ya Elimu Tanzania kupitia Wizara ya Elimu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, Shilingi Bilioni 17 zilizopelekwa TAMISEMI tangu mwezi Novemba, 2023, zilikaa hadi mwezi Machi 2024 takribani miezi 5 bila kutumika. Suala la fedha hizo kukaa kwa muda mrefu TAMISEMI na kutokutumika kama ilivyokusudiwa limesabibisha fedha kurejeshwa Hazina ingawa Taasisi ya Elimu Tanzania ilikuwa inahitaji fedha hizo kwa ajili ya uchapishaji wa vitabu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitishwa na hali hii inayoendelea kwani inakwamisha azma ya utekelezaji wa mitaala mipya ambayo imeanza kutekelezwa mwaka, 2024 na hivyo kusababisha watoto kukosa vitabu bila sababu za msingi na vile vile kusababisha kuchelewa kwa taratibu za manunuzi, uchapaji na usambazaji wa vitabu shuleni unao athiri ujifunzaji na ufundishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuwa, kwa kuwa jukumu la kuandika, kuchapa, na kusambaza vitabu linatekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), ni vema fedha za uchapishaji wa vitabu zipelekwe TET moja kwa moja kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ili kuongeza ufanisi, kasi na kufikia malengo ya Wizara katika uandaaji na usambazaji wa vitabu shuleni.

### 3.6 Mafunzo ya Walimu Kazini

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa mafunzo ya ualimu kazini ni sehemu muhimu ya kuboresha ustadi wa ufundishaji na kuhakikisha walimu wanakidhi mahitaji ya wanafunzi katika mazingira ya kisasa ya elimu kulingana na mtaala mpya. Na kwa kuwa, mafunzo hayo bado utaekelezaji wake siyo wa kuridhisha. Hivyo basi, ili kuleta

ufanisi katika utekelezaji wa mtaala mpya, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha walimu wote wanapaswa sio tu kuufahamu vizuri Mitaala hii lakini pia kujengewa uwezo wa mafunzo ya namna bora ya utekelezaji wa mitaala mipya ili waweze kuboresha ujuzi na kupata mbinu mbalimbali za ufundishaji ambazo zitasaidia kujifunza maarifa mapya. Aidha, Mafunzo haya yatolewe kwa walimu wote nchini wa Shule za Msingi na Sekondari.

### 3.7 Fedha za Nje zinazotekeleza Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za nje unaotokana na ukomo mdogo wa fedha ambao unachangia kwa kiasi kikubwa kuchelewesha utekelezaji wa miradi hiyo na hivyo kusababisha kusuasua kwa baadhi ya miradi. Kamati inaishauri Serikali kuwa, vifungu vya fedha za nje vinavyotekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia vitanuliwe bila kuathiri Sheria, Kanuni na Taratibu za matumizi ya fedha za Serikali ili zitekeleze miradi iliyokusudiwa.

### 3.8 Mdondoko wa Wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari *(School Droupout)*

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na ongezeko kubwa la mdondoko wa wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari hususani watoto wa kiume, hali inayopelekea ongezeko kubwa la watoto wa kiume kuwepo mtaani. Kamati imebaini mdondoko huo unasababishwa na Watoto wa kiume kutopewa mkazo wa masomo kama ilivyokuwa kwa watoto wa kike. Aidha, sababu nyingine ni ajira za utotoni kwa baadhi ya wanafunzi huchagua kuacha shule ili kusaidia familia zao kwa kufanya kazi au shughuli za kiuchumi na kushindwa kitaaluma. Hivyo basi, Kamati inatoa ushauri ufuatao :-

(i) Serikali iweke mkakati madhubiti wa kuhakikisha wanafunzi wote walioandikishwa shule wanahitimu masomo yao. Aidha, Waraka uliotumika kuwarudisha watoto wa kike shuleni utumike pia kuwarudisha watoto wa kiume shuleni. Vilevile walimu wapewe

mafunzo ya kufundisha watoto waliopo nje ya mfumo rasmi;

(ii) Waraka uliotolewa na Mhe. Rais *(Re-entry)* wa kuwarudisha wanafunzi wa kike waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali uingizwe katika marekebisho ya Sheria ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa kuwa Sheria iliyopo sasa haina kipengele hicho.

### 3.9 Vyuo vya Elimu ya Juu

**Mheshimiwa Spika,** Malengo ya kuanzishwa kwa Vyuo Vikuu nchini ni kutoa elimu ya juu yenye ubora, kukuza tafiti na uvumbuzi, kukuza ujuzi na stadi, kusaidia na kuchochea maendeleo ya kitaifa na kukuza utamaduni na maadili katika jamii. licha ya kazi nzuri inayofanywa na vyuo hivi, Kamati inaamini kuwa, Vyuo Vikuu vina wajibu wa kuhakikisha vinatoa mchango wake kwa kuendeleza na kukuza viwango vya elimu na mafunzo nchini ili kupata rasilimali watu yenye weledi, maarifa na ujuzi katika nyanja mbalimbali kwa maendeleo ya taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona upo umuhimu wa Vyuo Vikuu kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia malengo ya uanzishwaji wake ambavyo ni alama katika nchi yetu kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kwamba, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kiendelee na utekelezaji wa malengo yaliyowekwa ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa Ndaki ya Sayansi Asilia na Hisabati (College of Natural and Mathematic Science) na Ndaki ya Sayansi za Ardhi na Uhandisi (Collage of Earth Science and Engineering) kama ilivyokusudiwa. Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kihakikishe ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali inayoendelea kutekelezwa ikamilike kwa wakati. Hii iende sambamba na kuboresha miundombinu ya kufundishia, utawala na mabweni ya wanafunzi.

### 3.10 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

1. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Musa Ramadhani Sima, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Anastazia James Wambura, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Dr. Thea Ntara, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Ester Edwin Maleko, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Kassim Ali Khamis, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Mwanakhamisi Kassian Said, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Rose Syprian Tweve, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Yahya Ally Hamis, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wasaidizi wake, Mhe. Omary Shaban Kipanga (Mb), Naibu Waziri; na Prof. Carolyne Nombo, Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongonzwa na Katibu wa Bunge *Ndg. Nenelwa J. Mwihambi (ndc),* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema katika

wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili liijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Husna Juma Sekiboko, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO**

07 Mei, 2024

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikiliza Mwenyekiti, sasa tunaendelea na utaratibu wetu ambao ni kusikia maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri na pia, kutazama yale ambayo Kamati yetu ya Bunge imetushauri. Tutaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya. Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu ya Wizara ya Elimu, lilizuka swali la msingi hapa. Nini hasa chanzo cha kushuka kwa kiwango cha elimu Tanzania? Baada ya Majibu ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Spika akauliza, hivi ni kweli chanzo cha kushuka kwa kiwango cha elimu ni lugha ya kufundishia au kuna jambo lingine halisemwi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya mpaka leo swali hilo halijajibiwa. Naomba leo nilijibu swali hili kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najibu swali hili kwa kutumia hoja mbili. Hoja ya kwanza ni kwamba, Kenya na Uganda zinapakana na Tanzania, lakini mazingira na ubora wa elimu wa nchi hizi unatofautiana sana. Kenya na Uganda ni miongoni mwa nchi tano zenye wanafunzi na walimu wenye uwezo mkubwa sana wa kutumia lugha ya Kingereza. Nchi ya kwanza ni Afrika ya Kusini, ya pili ni Nigeria, ya tatu ni Kenya, ya nne ni Ghana, na ya tano ni Uganda. Ndiyo maana shule binafsi za Tanzania zinaajiri walimu wa Kiingereza na sayansi kutoka Kenya na Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili ni nchi tatu zenye elimu bora sana Afrika ni Seychelles ambayo inatumia Kifaransa kama lugha ya kufundishia; Tunisia inayotumia lugha mbili (Kiarabu na Kifaransa) na nchi ya tatu ni Mauritius ambayo inatumia lugha mbili (Kifaransa na Kiingereza), lakini bado zina ubora mkubwa sana wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siri ya mafanikio yao ni nini? Siri ya mafanikio yao ni ubora wa walimu, matumizi sahihi ya vifaa vya kufundishia na vya kisasa; tatu, ni wanafunzi kupata nafasi ya kutumia kwa ufanisi lugha ya kufundishia darasani na nje ya darasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili ambao unashangaza sana ni wanafunzi wa Tanzania wanaokwenda China, Ujerumani pamoja na Urusi wanafunzwa lugha kwa muda wa mwaka mmoja tu na wanakuwa na uwezo wa kuitumia lugha hiyo kwa ufanisi sana. Matokeo yake ni lugha hiyo ambayo wamejifunza kwa mwaka mmoja, wanaitumia kwa masomo ya shahada ya kwanza, masomo ya uzamili na masomo ya uzamivu na wanafanya vizuri sana. Mfano mzuri ni Mheshimiwa Prof. Kabudi, huyu, amesomea Ujerumani kwa lugha ya Kijerumani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini wanafunzi wa Tanzania wanaanza kujifunza Kiingereza kuanzia Shule ya Msingi mpaka Chuo Kikuu, lakini bado uwezo wao wa Kiingereza ni tia maji tia maji, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu ya lile nililolieleza kwanza. Wanafunzi wanapokwenda Urusi, Ujerumani na China, wanatumia lugha ya kufundishia ndani na nje ya darasa kwa ufanisi. Walimu wanaofundisha lugha, wamebobea vizuri sana, wanaijua lugha wanayoitumia katika kufundishia. Pia maabara za lugha zinatumika vizuri, filamu na video zinatumika kwa ufanisi. Haya ni mambo ambayo tunayakosa sana katika Elimu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tutoke hapa tulipo, napendekeza mambo manne. Jambo la kwanza ni Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ianzishe mafunzo ya Shahada ya Diploma ya Juu ya Ufundishaji wa Lugha ya Kiingereza. Zoezi hili liwe la kudumu na katika mafunzo hayo tutumie teknolojia ya kisasa ili tutumie walimu wenye ujuzi kwa ufanisi na kuwafikia Watanzania kila mahali walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, turudishe utamaduni wa zamani. Tuanzishe mashindano ya mijadala, midahalo katika shule za msingi na sekondari ili vijana wetu wapate uwezo mkubwa sana wa kutumia lugha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, vitabu hasa vya Kiingereza na Kiswahili viandikwe na watu wanaozifahamu vizuri lugha hizo. Sisi tuliobahatika kusoma katika miaka ya sabini mwishoni, tumetumia vitabu vya Kiingereza vinaitwa *East African Oxford English*, vimeandikwa kwa lugha fasaha, vina mifano ya kifalsafa vitu ambavyo wanafunzi wanavihitaji sana.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nasema tu, kama kuna uwezekano, tuvitafute vitabu hivyo, vichapishwe kwa wingi, tuvipeleke mashuleni. Vitabu vya Kiswahili, mimi inanishangaza sana kwamba kwa bahati mbaya, haipendezi kutoa mfano, lakini Wakenya wanaandika vitabu vizuri sana vya Kiswahili kuliko Watanzania kwenye lugha. Kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la nne, Wizara ya Elimu izungumze na *British Council* na Ubalozi wa Uingereza tupatiwe walimu wenye

ujuzi, tuwatawanye kwenye vyuo vinavyofundisha ualimu ili walimu wajifunze namna ya kutamka vizuri maneno ya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu na ushauri wa pili. Moja ya tatizo linalotusibu hasa kwenye elimu yetu ya msingi, ni mzigo wa masomo ni mkubwa sana. Haiwezekani mtoto wa shule ya msingi anasomeshwa masomo zaidi ya tisa. Matokeo yake anabeba begi lenye vitabu na madaftari utafikiri anakwenda kwenye mafunzo ya kijeshi. Haikubaliki. Napendekeza hapa kwamba imefika wakati tupunguze idadi ya masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, wanafunzi wa shule za msingi wanahitaji masomo Matano, nitayataja. Kiingereza, Kiswahili, Sayansi, *mathematics* (hisabati) wafundishwe vizuri; na la tano, ni dini na maadili. Kama ni mkristo, ni Dini ya Kikristo na Maadili; kama ni Uislamu, basi Dini ya Uislamu na Maadili. Wanapofika darasa la tano na la sita tuwaongezee somo moja *Programming* ili waendane na mabadiliko ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza masomo kama jiografia, historia na *civics* hakuna haja ya kufundishwa kwenye shule ya msingi, yasubiri mpaka wanafunzi wafike kidato cha kwanza. Kwa nini? Mtaalamu mmoja wa Saikolojia anaitwa Jean Piaget alisema mtoto anapofikia umri wa miaka 13 ambayo ni muda wa kuanza darasa la *Form One,* ndipo anapokuwa na uwezo wa kumudu masomo mengi. Tusimpe masomo mengi anapokuwa shule ya msingi. Ndiyo sababu ya kupendekeza hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa tatu, kwa isivyo bahati sana, uteuzi wa masomo ya ubobezi *(Specialization)* hapa Tanzania tunachelewa sana kuanza. Uchaguzi wa masomo unaanza kidato cha tano na kidato cha sita. Kwa isivyo bahati muhtasari wa masomo ya kidato cha tano na sita ni mpana sana, una mambo mengi. Walimu wanalazimika kufundisha haraka wala hakuna kitu chochote cha kujifunza kwa sababu wanafundisha haraka ili wamalize *syllabus*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri jambo hili halikubaliki. Ushauri wangu ni nini? Ushauri wangu ni kwamba masomo ya ubobezi

yaanze kidato cha nne ili walimu wapate muda wa kutosha wa kufundisha vizuri ili wanafunzi wajifunze vizuri. Weledi wa mwanafunzi yeyote duniani haupimwi kwa kusoma mambo mengi ndugu zangu, unapimwa kwa kusoma mambo machache na kujifunza mambo mengi kwa Kiingereza *study less, learn more*. Huu ndiyo ushauri wangu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nahodha, yale masomo uliyopendekeza kwa shule za msingi (wanafunzi wa shule ya msingi) yafundishwe kwa lugha gani? Aah! Umesikika vizuri. Ukiacha Kiswahili ambacho umekitaja kama somo na Kiingereza kama somo, ili ushauri wako uwe umekamilika yale masomo mengine yafundishwe kwa lugha gani?

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba kwa hali ya sasa ilivyo, mtoto anapofikia darasa la nne, mimi nafikiri ndiyo wakati sahihi ameshaanza kuwa na utulivu kidogo. Sasa hapo anaweza kuanza kuyasoma masomo hayo kwa lugha ya Kiingereza polepole na vizuri. Darasa la kwanza mpaka la tatu tutumie lugha mama ya Kiswahili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, mmesikia uchangiaji kwenye elimu hapa, Kiswahili fasaha na Kiingereza fasaha. Sasa sisi hapa huwa tunaanza wenyewe kuchanganya mambo. Sasa hii ni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na sisi tunamshauri Waziri hapa.

Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, atafuatiwa na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambaye anatamani apitishiwe bajeti ya shilingi trilioni 1.9 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, nianze na pongezi kwa Serikali kwa hatua ambazo imezichukua katika kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata elimu ya vyuo vikuu, na kwa jinsi hiyo kuweka mpango wa kuwapatia mkopo. Nitangulie kusema kwamba mikopo hii kwa wanafunzi wa elimu ya juu pamoja na vile vyuo vya kati imekuwa ni mkombozi mkubwa sana kwa vijana wa Kitanzania ambao kama siyo mpango huo, wengi wetu hata tulioko hapa yawezekana tusingepata hiyo elimu ya juu. Pongezi nyingine kwa Serikali ni kwa jitihada ambazo inaendelea kuzifanya kwa ajili ya kuongeza miundombinu katika vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu asubuhi ya leo itakuwa ni juu ya kuboresha mazingira ya kufundishia pamoja na kujifunza katika vyuo vyetu vikuu. Nasema hivyo kwa sababu katika miaka ya karibuni udahili wa wanafunzi umeongezeka sana katika vyuo vyetu vikuu na ongezeko hilo liko wazi, linatokana na wingi wa wanafunzi wanaohitimu katika elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, utagundua kwamba mara nyingi tunapokutana hapa Bungeni tunaongeza madarasa ya kutosha katika elimu ya sekondari. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba wingi huu wa wanafunzi utapaswa kudhihirika pale katika elimu ya juu. Ongezeko hili kulingana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wanadahiliwa wanafunzi karibia 150,000 kwa mwaka, kuingia katika Vyuo vyetu Vikuu.

Mheshimiwa Spika, sasa hoja yangu hapa ni kwamba ongezeko hili la udahili wa wanafunzi katika elimu ya juu haliendani sambamba na miundombinu iliyopo na kwa jinsi hiyo kuathiri mazingira ya kujifunza na ufundishaji. Mfano, hapa nitatoa mifano kutoka katika vyuo mbalimbali kwa kadiri nilivyoviweka.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wote wa mwaka wa pili na wa tatu katika baadhi ya vyuo vikuu vya umma wote huwa wanalazimika kukaa nje ya *campus* ya Chuo, na ni kwa sababu, mabweni hayo hayatoshi, lakini hata wale wanaobahatika kukaa vyuoni bado chumba kilichopangiwa kukaa wanafunzi wanne wanaweza wakakaa zaidi. Wale wanaokaa nje ya chuo, mfano

katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam watakaa Msewe, Ubungo, wale wa *IFM* watakaa Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, wanajikuta wamekuwa ni wanafunzi ambao wanaanza kuhangaika na changamoto za uraiani. *Boom* likichelewa kutolewa, anaambiwa na yule mpangishaji nyumba kwamba nitakuondolea vitu vyako nje na ilishatokea kwa mwanafunzi mmojawapo. Sasa mazingira kama haya hayamfai mwanafunzi ambaye anapaswa kuweka akili yake katika masomo, lakini anakumbana na changamoto za kupanga nje ya chuo kwa sababu mabweni hayatoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni maabara. Katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam baadhi ya maabara ambazo zamani zilikuwa zinahudumia wanafunzi 20 kwa sasa zinalazimika kuhudumia wanafunzi zaidi ya 200 hadi 300. Mazingira haya hayaleti ubora unaokusudiwa katika kutoa elimu kwa wanafunzi na hasa ile ya maabara au mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna mahali ambapo unakuta mhadhiri mmoja anajikuta ana darasa la wanafunzi 800 hadi 1,000. Uwiano huu wa mhadhiri kwa mwanafunzi ni moja ya kigezo cha mataifa katika kupima ubora wa vyuo vyetu vikuu. Sasa inapotokea mhadhiri mmoja ana darasa la watu 800 anawahudumiaje ili kuwapatia elimu bora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nitangulie kusema kwamba wakati mwingine, kwa mfano ukiangalia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hata miundombinu ya vyoo iliyokuwa inahitaji kuhudumia watu 4,000, lakini sasa hivi kuna watu 20,000 pale na havijaongezeka sana.

Mheshimiwa Spika, pia, nikienda kwa wahadhiri, wakati fulani unakuta wahadhiri wako wanne, watatu, au wawili, wanachangia ofisi moja iliyopaswa kuwa ni ofisi ya mtu mmoja. Tukumbuke katika vyuo vikuu wanakuja wanafunzi wa *Post-Doc* ambao wakati mwingine wanapaswa kwenda kuongea na mwalimu wao. Sasa anafanyaje mawasiliano na mwanafunzi wake iwapo mwalimu huyu ana-*share* ofisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongee jambo lingine ambalo nilitaka nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba wakati mwingine inahitaji kuonekana kwamba mtu anathaminiwa na Serikali yake ambayo ndiyo anayoitumikia. Mfano mmoja ambao nataka niuweke wazi hapa, iliwezekanaje kwa Mheshimiwa Waziri kwamba Afisa Mwandamizi Wizarani au katika Serikali anapewa *perdiem* ya shilingi 250,000 lakini Profesa wa Chuo Kikuu akawekewa *slot* ya shilingi 170,000? Nadhani hii siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, yaani huo msawazo wa kwamba huyu ni Profesa katika chuo kikuu, yeye ndiye Afisa Mwandamizi Chuoni lakini anawekewa *slot* yake kuwa shilingi 170,000 na hiyo ikaonekana inakubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu kama tunatamani kutoa zao bora la wanafunzi wanaotoka vyuoni, Serikali inayo sababu ya kuongeza bajeti ili kuboresha mazingira ya kujifunza na ya kufundishia. Kwa mfano, mafunzo ya vitendo *(practical training)* mara nyingi sana vyuo vimejaribu kupunguza muda wa kwenda katika mafunzo ya vitendo kwa sababu ya bajeti ndogo, yaani unakuta katika mtaala tunapaswa kwenda katika *practical training* kwa wiki nane (miezi miwili), lakini kwa sababu ya bajeti ndogo, tutakaa kule mwezi mmoja peke yake. Halafu baadaye tunasema kwamba wanafunzi sio bora, lakini hawakuwa na muda wa kutosha katika kufanya mafunzo kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine natamani Serikali ingeweka utaratibu ambao ni kama wa lazima fulani hivi kwa taasisi na hata katika miradi, ambapo tunawapeleka wanafunzi wetu kufanya mafunzo ya vitendo. Kwa maana wakati mwingine inaonekana kama ni hisani kupeleka wanafunzi kwa ajili ya mafunzo ya vitendo. Watu wa miradi, watu wa taasisi au kampuni wanaona kama ni hisani kuwapokea wale wanafunzi. Inapaswa isiwe hisani, badala yake iwe ni jambo la lazima, na huko wakae kwa muda wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano dhahiri hapa, ni kwamba tuna miundombinu mingi sana, kama barabara zinazojengwa hapa Tanzania. Je, Wizara ya Elimu inatoa mwongozo gani kuhakikisha

kwamba miradi yote hii inayojengwa na kampuni za nje inahakikisha ina wanafunzi wetu wa kutosha katika ile miradi ili waweze kupata uzoefu wa kutosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunatamani kubadili simulizi *(change of narrative)* lazima tuwekeze katika maabara za kitafiti katika vyuo vyetu vikuu ili tuweze kuja na uvumbuzi, yaani tusi-*predict* taarifa tunazozipata. Tuanze kupata taarifa za uvumbuzi unaotokana na tafiti zinazotoka katika vyuo vyetu, na haiwezekani tukabadili simulizi hii kama hatujawekeza fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, maoni yangu, kuna mwenendo fulani hivi ambao vyuo vikuu vinajitanua kwa kujenga *campus* nyingi nyingi nje ya zile *main campuses.* Kwa hiyo, unakuta yaani tunaendelea kutawanya. Yaani hivi nyuo ambavyo ni vyuo mama, tunasema miundombinu yake haitutoshi bado, lakini bado hivi vyuo vinaendelea kupanua na kutengeneza *campus* nyingine mikoani.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kwamba tunaongeza gharama za utawala badala ya kuandaa wanafunzi ambao ni bora. Kwa nini tusiimarishe *main campus* ili tupate ubora uliokusudiwa badala ya kutawanya rasilimali chache tulizonazo kwa kuendelea kutawanya vyuo kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani tungeanza kuwa na ule mtindo wa kuweka mahali. Mfano, Dodoma ni Chuo Kikuu hiki, kiwe kikubwa kwa kadiri inavyowezekana, tuweke miundombinu yote; wanafunzi watatoka Lindi, Katavi, watakuja Dodoma. Vivyo hivyo na Dar es Salaam, lakini sasa unakuta Dodoma inataka iwe na *campus* Katavi na Kagera. Kwa nini tusingefanya kwamba Arusha kuwe na chuo kinachoonekana ni cha ufundi, kiwe bora kikuzwe watu waende Arusha tujue kwamba pale tunatoa elimu ile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nakushukuru sana kwa nafasi. Naunga mkono hoja nikisema kwamba bajeti hii ipite, lakini, kama ingewezekana, hatuna sababu ya kutumia 60%

kwenye mikopo halafu 40% pekee kwenye miundombinu haitoshi. Wanafunzi wale na wahadhiri waandaliwe miundombinu fulani hivi ambayo itaonesha kwamba wanathaminiwa, lakini pia wanatoa elimu bora iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kabla hatujamsikiliza Mheshimiwa Jasson Rweikiza, kuna wageni ambao wameingia baada ya tangazo la awali la wageni.

Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ana wageni wengine. Kwanza ni wageni ambao ni wadau wa Maendeleo ya Elimu walioalikwa na Profesa, wote wasimame kwa pamoja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Kilimanjaro, wengine walitambulishwa, wengine nadhani wameingia baadaye, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, wapo wafanyabiashara kutoka Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Tiprice Kamando na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, Ndugu Mrindoko, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 15 wa Mheshimiwa Mussa Sima ambao ni Wadhibiti Ubora wa Shule kutoka Dodoma Jiji, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 97 wa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo ambao ni wanafunzi na walimu wa *Mac Britant* kutoka Chamwino, Jijini Dodoma. Jamani Chamwino siyo Jiji, ni kutoka Chamwino Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi na Mheshimiwa Innocent Bilakwate, hawa ni Kwaya ya *The Vine*

kutoka Kanisa la *The New Vine Church* la Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, viongozi 25 ambao ni viongozi wa wanafunzi wanaosoma Shahada ya Kwanza ya Ualimu wa Elimu ya Awali kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, ajiandae.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Wizara hii muhimu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwanza napenda kupongeza sana juhudi zinazofanywa na Serikali kupitia Wizara hii ya Elimu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Adolf Mkenda, Mheshimiwa Naibu Waziri Kipanga, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu wote na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla nasema kwamba kwa kweli kazi ya Wizara ya Elimu ni nzuri na tunaishuhudia wote mahali pote nchini. Hivi karibuni tumeanza mtaala mpya wa elimu kwa nchi nzima kwa ngazi mbalimbali kwa shule za msingi na sekondari na hii ni jambo jema sana. Lengo kubwa ni kuboresha elimu na moja ya matokeo ya mtaala mpya ambayo tutayapata ni kwamba vijana wanapotoka shuleni darasa la saba au kidato cha nne na baadaye mbele huko wanakuwa na elimu fulani ya ujuzi fulani wa ufundi au tunaita amali. Hili ni jambo zuri, anaweza akajiajiri au akaajiriwa mahali ambapo kuna nafasi.

Mheshimiwa Spika, baadaye matokeo mengine ni kwamba vijana wote wa Tanzania watasoma mpaka kidato cha nne. Hili siyo jambo dogo, ni jambo kubwa sana la kujivunia na kuishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa. Itafika wakati wananchi wote wa Tanzania watakuwa ni wasomi, wamesoma mpaka kidato cha nne, wanafahamu vizuri na wana elimu ya kutosha. Kwa hiyo, mimi napongeza sana kwa juhudi hizi ambazo ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia hata maeneo ya kusomea, shule zinazidi kuboreshwa, zinajengwa vizuri, zinaongezwa kwa idadi kubwa, madarasa yanaongezwa. Leo katika majimbo yetu huko tumepatiwa fedha nyingi, tunajenga maboma ya madarasa yaliyokuwa yamekaa miaka mingi bila kukamilishwa, yanakamilishwa; shule zinakuwa na vyoo, wakati hapo nyuma shule hazikuwa na vyoo. Leo vyoo vinajengwa kwa wingi na vinakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kufurahia ni kwamba wananchi wamepumzishwa. Huko nyuma ilikuwa tukijenga darasa au shule wananchi wanachangia, leo kidogo hawachangii wanapata madarasa haya bila mchango mkubwa ambao ni hatua nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, naomba jitihada hizi ziendelee, bado maabara, maboma ya maabara yapo hayajakamilishwa, jitihada zifanyike ziendelee kusimamiwa ili nayo yaweze kupata ukamilifu. Nakushukuru sana kwa nafasi hii, lakini pia niseme kwamba bado tuna kazi kubwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, miaka ya sabini nafikiri kabla kidogo ya 1970 na 1970 mwanzoni pale, Serikali ya Awamu ya kwanza ilianzisha Elimu ya Watu Wazima. Kulikuwepo na ombwe au na uhitaji mkubwa wa watu wengi wa kujua kusoma na kuandika na kuhesabu. Kwa hiyo, Serikali ilianzisha Mpango wa Elimu ya Watu Wazima ili watu waweze kufahamu kusoma, kuandika na kuhesabu kidogo. Leo tuna shida kubwa zaidi ya hiyo, kwani Tanzania au dunia nzima kwa ujumla imeingia kwenye digitali na haturudi nyuma, tunakwenda mbele kidijitali, kila kitu ni dijitali.

Mheshimiwa Spika, ukienda hospitali ile ya kuandika cheti tena imekwisha. Unaanza mapokezi, unamwona aliyekupokea pale anakuandikia jina kwenye kompyuta anakwambia ingia chumba namba mbili. Unaangalia sasa huna karatasi, unaenda kufanya nini? Kumbe jina lipo kwenye kompyuta. Namba mbili ukiingia anakupokea, wewe ndiye Rweikiza, karibu chukua kiti. Hapo ameshakuona, wewe una shida gani, naumwa tumbo, naumwa kichwa na kadhalika, anakuandikia nenda maabara

bila karatasi. Unakwenda kule huelewi unakwenda kufanya nini? Wanakufahamu wameshakuona kwenye mtandao dijitali, hivyo hivyo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, tuna vitambulisho vya *NIDA,* mtu anafikiri *NIDA* ni kitu kidogo. Ile ni digitali kabisa. Kule ndani kuna taarifa za kutosha. Kuna jina lako, ulipozaliwa, tarehe uliyozaliwa, ulipokulia, kazi yako, elimu yako, vipo mle ndani na nchi nyingine mpaka damu yako ni ya aina gani, una *allergy* na madawa gani, vipo mle kwenye vitambulisho. Sasa ile ni dijitali.

Mheshimiwa Spika, kuna benki hapa Tanzania kwa mfano *NBC* muda mrefu hawatumii makaratasi, ni *paperless.* Unasema *account* yangu ni namba fulani, anapigapiga pale anaona mambo yako, anakupa hela au unaweka pesa tunakwenda dijitali. Mambo yemebadilika sana, tunakwenda kwenye *digital*.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye mwananchi anataka kusafiri na basi, siku hizi unaambiwa kata tiketi kwenye simu. Wangapi wanafahamu kwamba kwenye simu unakata tiketi yako ya usafiri huko vijijini na mahali pengine. Hawajui, ni dijitali.

Mheshimiwa Spika, sasa watu wengi hawajui matumizi ya hii huduma, hawaelewi. Tumepata maendeleo, Serikali imegawa vishikwambi kwa walimu, kwa madiwani, hata humu ndani meza ni tupu hakuna karatasi, ni vishikwambi. Wangapi wanafahamu kuvitumia vizuri hivi? Unasikia maelezo, mkongo wa Taifa mtu anashangaa mkongo ni kitu gani? Mkongo ni nini? Mkongo ni pembe ya ndovu? Haelewi mkongo ni nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, juzi nikaona mtu mmoja Dar es Salaam ana kishikwambi amejifunika mvua isimnyeshee, ameweka hivi hapa, hajui kwamba vishikwambi na maji ni vitu tofauti; hajui matumizi ya dijitali. Kwa hiyo, nafikiri Serikali kupitia Wizara ya Elimu iweke madarasa ya Elimu ya Watu Wazima kwa ajili ya elimu ya dijitali, tuongeze hii elimu twende mbele. Bila kufanya hivyo, tutapata shida kubwa sana, tutabaki nyuma na hii haitatusaidia, tutakuwa tumekwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, leo mimi mchango wangu ni huo kwamba Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri mnayoifanya izingatie kwamba tunahitaji dijitali sana kote mijini, vijijini, mashuleni kwenye maofisi, kwenye makampuni, watu wafahamu dijitali vizuri zaidi, mtu aweze kujiongeza na kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie. Nichukue nafasi hii kuwapongeza Wizara ya Elimu kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa sababu ya maslahi ya muda, naomba wapokee pongezi zangu kwa ujumla kwa sababu kuna mambo makubwa sana yamefanyika kwenye sekta ya elimu katika Jimbo letu la Iringa Mjini.

Mheshimiwa Spika, leo naomba niongelee na nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Elimu akiniridhia, aongeze katika vipaumbele vyake haya nitakayoyaongea. Ninataka kuongea kuhusiana na suala la umataifishaji wa elimu hasa elimu ya juu. Umataifishaji wa elimu au *internationalization of high learning education*.

Mheshimiwa Spika, Watanzania ni raia wa Tanzania, lakini pia ni raia wa dunia. Hiyo ni haki yetu ya msingi kuwa raia wa Tanzania, lakini pia ni raia wa dunia. Tunapoongelea umataifishaji wa elimu tunataka kwamba elimu yetu iwe na mwelekeo wa namna ambavyo dunia inakwenda, *whether* ni kiutamaduni katika kutenda kazi kwetu au katika kuweka madhumuni yetu kwenye elimu yetu, lazima tuangalie pia dunia inakwenda namna gani?

Mheshimiwa Spika, kuna faida kubwa ya kufanya umataifishaji wa elimu kwanza. Kwa kuwa sisi siyo kisiwa, tuna haki

ya msingi kupata haki zile za kidunia, lakini kushiriki demokrasia ya dunia pia kushiriki uchumi na kupata faida kutoka kwenye uchumi wa dunia.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwenye elimu ndipo tunapopikwa kuweza kuishi duniani. Sasa namna gani tunapikwa ndivyo ambavyo tutaweza na sisi kupata keki ya dunia au kokosa keki ya dunia. Kiuchumi ni lazima sasa tuwe na mtizamo kwamba elimu yetu ya juu ihakikishe inakuwa ni chanzo kimojawapo cha kuboresha uchumi wetu, kwanza, kwa kuhakikisha kwamba tunakuwa na wanafunzi ambao watakwenda kujifunza nje ya Tanzania, lakini kuwa na wanafunzi watakaotoka nje kuja kujifunza ndani ya Taifa letu. Hapo ndipo ambapo tunaweza tukashiriki kuwa raia wa dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiweka vipaumbele vyetu katika kuwaweka watoto wetu tu wakae katika hali ya kusoma mambo yaliyopo Tanzania na tusiwachangamanishe na dunia, tutakuja kukuta tumebaki kama kisiwa. Ndiyo maana sasa hivi tunabaki kuwa kama wateja wa mambo yanayoendelea duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano, leo hii ukichukua tu kwenye biashara, unakuta kuna vitu vingi sana ambavyo tunaviingiza kutoka nje ambavyo wenyewe tungeweza kuzalisha ndani ya nchi. Wenzetu walifanya uwekezaji mkubwa kwenye elimu yao wakiangalia mazingira yao ya ndani bila kuyasahau mazingira ya nje. Tunapoongelea kimtizamo au kinadharia, unapoongelea kumataifisha elimu ya juu, unaongelea kuboresha miundombinu yetu ya namna vyuo vyetu vinavyotoa elimu.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wa utoaji wa elimu kwenye vyuo vyetu, mitaala yetu tunayotumia kwenye elimu, lakini namna ya ufundishaji na ujifunzaji wa walimu wetu au wanafunzi wetu, je, wanafunzi wetu, tuliwapeleka? Leo hapa tuna changamoto kubwa ya ajira, lakini zipo nchi za wenzetu zina changamoto nyingine. Kwa mfano, changamoto ya kutokuwa na amani na utulivu, lakini zinafika mahali zinatulia.

Mheshimiwa Spika, ingelikuwa ni soko kwetu, la watu wetu hata kwenda kuajiriwa kule, lakini je, watoto wetu wapo tayari kuomba kazi, au wameandaliwa kuomba kazi kwenye nchi nyingine? Hiyo ndiyo tunakuja sasa kwenye umataifishaji wa hiyo elimu. Sasa je, mitaala tunayotoa sisi inaungana na mataifa mengine? Yaani inaweza ikawa ina tija tukienda duniani? Kwa hiyo, mabadiliko ya mtaala ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata ratiba tu, tunataka wanafunzi. Leo tunalalamika humu ndani kwamba hatuna fedha za kigeni, kwenye nchi nyingine elimu ya juu ni *source* kubwa sana ya fedha za kigeni kwenye Taifa. Tuna vyuo vya maana, tuna shule za maana, tuna vyuo vikuu vyenye mazingira mazuri, kwa nini hatuwezi ku-*invite* wanafunzi wengine toka nje wakaja kusoma au tukawa na *exchange program* za walimu wetu na maprofesa wakaenda kwao, na maprofesa wa kwao wakaja kwetu? Tunatumiaje hiyo *advantage? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwa tunaendelea na utamaduni ule ule katika kumataifisha, pia elimu ya juu lazima pia wenzetu waliopo vyuo vikuu - Wahadhiri wabadilishe utamaduni na desturi za kuendesha vile vyuo walivyozoea kwa kawaida. Inatolewa ratiba ya *semester* nzima, lakini mtu hafuati kabisa ratiba ya *semester,* inafika tu siku isiyo na jina, anaamua leo ni *Eid* au *Christmas* wanafunzi wote njooni, nitatoa *test*. Mambo kama hayo ya tamaduni kama hizo ukienda nje ukiwachukua wanafunzi wa nje hawawezi kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini wanafunzi wa nje waje? Wakija hapa kwanza inatupa fursa sisi watoto wetu kujifunza na *culture* nyingine ya nchi nyingine, kuwajengea *confidence* wanapokuwa kwenye *international organization,* hata kwenye *interview* kwa sababu atajifunza kutoka kwa mwenzie namna anavyoji-*express*, namna anavyoongea lugha imenyooka, namna anavyokuwa na *confidence* anavyojieleza, atajifunza kwa sababu yule amesoma naye, na yupo naye darasani, akiitwa na yeye kwenye *interview* ya kimataifa hatakuwa na hofu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye *social* itatusaidia, lakini kuwa na taratibu zile za Kimataifa, yaani hata nidhamu tu ya Kimataifa. Hapa leo fikirieni tulivyo hapa wote, tungekuwa tu tumekulia vijijini kwetu, tumekaa vijijini kwetu na kizuri sana Mwalimu alichokifanya wakati nchi yetu imepata uhuru umataifishaji ulikuwa mkubwa kuliko sasa; aliwatoa maprofesa wengi hapa na kuwapeleka kwenda kusoma nje.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Msambatavangu kuna taarifa. Wapi?

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Kutoka kwa Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan.

**SPIKA:** Aah, Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan.

**TAARIFA**

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nimpe taarifa mchangiaji kwamba nimefuatilia mchango wake kwa karibu sana, amelitumia neno "kumataifisha" kama mara saba hivi, lakini sijui kama ni neno sahihi la Kiswahili, na angetumia labda "kuifanya elimu iwe ya kimataifa." Napata shida kulielewa.*(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Msambatavangu haya, japokuwa ameuliza swali, na kwa sababu tunachangia kuhusu elimu, hilo neno umelitengeneza mwenyewe ama tunalo kwenye Kamusi?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, lugha inakua kwa kutengeneza maneno. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimelitengeneza na nimelifanyaje? Unatohoa *internationalization.* Kwa hiyo, ni umataifishaji na ninaomba wale watu wa Kiswahili walichukue rasmi. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sasa ngoja, kwa sababu neno "kutaifisha" kwenye Kiswahili lina maana tofauti...

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, *internationalization*.

**SPIKA:** Ngoja. Kutaifisha kwenye lugha ya Kiswahili lina maana tofauti, sasa ukiongeza neno nyuma yake ni kama pale mbele linaendelea na ile maana ya mwanzo. Sijui kama umenielewa. Ninayo kamusi hapa, ngoja nikusomee kutaifisha ni nini? Katibu, hebu tunza muda wake.

Haya, natafuta hapa neno kutaifisha ili Mheshimiwa anapotengeneza neno lake twende vizuri. Haya taifisha, "*fanya mali kama vile kampuni, kiwanda shamba zinazomilikiwa na watu binafsi kuwa mali ya umma; taifisha, taifishia, taifishika, taifishwa, taifishiwa, taifishiana.*"

Kwa hiyo, "taifisha," lina maana tofauti kidogo, sasa ukiongeza maneno nyuma na mbele ni kama ule mzizi bado unabaki pale. Kwa hiyo, labda utafute neno lingine ili Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan awe na amani na Kiswahili. *(Kicheko)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, sawa, naomba aondoe tu hofu yake ya akili ataelewa mzizi wa neno ni Taifa.

**SPIKA:** Ngoja. Ninayo kamusi hapa, sasa kwa sababu tunaongozana vizuri, neno "kutaifisha," nawe lile la kwako linaitwa nini Mheshimiwa Msambatavangu?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, wingi wa taifa ni mataifa. Wingi wa mataifa ni mataifa. Mzizi wa neno, ni "taifa," umataifishaji.

**SPIKA:** Sasa taifisha unaliona linasomeka hapo? Kwa hiyo, fupisha neno lako, badala ya kuongeza neno taifisha, labda punguza lile neno fisha kule mbele. Hebu weka neno lako vizuri.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nifanyaje?

**SPIKA:** Ili umalizikie mzizi wako kenye Taifa usiongeze taifisha kwa sababu ile fisha ndiyo inaifanya tupelekwe kwenye maana tofauti.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nifanye umataifa. Halitaleta maana ile?

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Nadhani Mheshimiwa Waziri ameelewa na mtaalamu wetu wa Kiswahili leo hayupo, kwa hiyo, tunapata changamoto kidogo. Mheshimiwa endelea malizia mchango wako. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, nafikiri atakuwa ametuelewa.

Mheshimiwa Spika, kingine nilikuwa naongelea umataifishaji na nimeongelea kwenye jamii faida za kijamii. Pia tunazo faida za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tunapokuwa tumeifanya elimu yetu iwe ya kimataifa kwenye uchumi, ambayo ndiyo *internationalization* inatusaidia sisi kupata wanafunzi wengine na watakaolipa fedha kwenye vyuo vyetu kama ambavyo tuliwapata wanafunzi kutoka Sudan ilipotokea vita, walikuja hapa wakalipa fedha tukapata *foreign currency*. Kwa hiyo, kiuchumi ni kwamba tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, sisi sio kisiwa. Katika uchumi wetu, tukitengeneza mali zetu hapa au tukizalisha vitu vyetu hapa, tunatamani vitumike kimataifa. Kama hatutaweza ku-*associate* na elimu yetu, tukajua kule kwenye mataifa mengine wanahitaji *product* za aina gani, inatuletea shida tukipeleka *product* zetu zinakuwa hazina ubora au zinakataliwa kwa sababu tupo *against* ulimwengu unavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili Wizara ya Elimu lazima ilichukulie kwa uzito wake, nami naomba niwaambie, shirikianeni na sekta binafsi kwenye elimu ya amali, na bila kufanya umataifishaji wa elimu tutakwama, kwa sababu amali, tunataka watoto wajifunze kufanya vitu kwa vitendo na vile vitu wanavyofanya kwa vitendo viendane na wakati.

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Waziri umetuambia watu wamefundishwa mafunzo ya amali, wamepata *yes, well and good.* Aliyewafundisha wale walimu wa kwenda kufundisha mafunzo ya amali amejifunza wapi elimu ya amali? Kwa namna hiyo, Waziri, hatukwepi kuwachukua walimu wetu wa vyuo vikuu na kuwa na *exchange program* na vyuo vya nje wakajifunze nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna hiyo hatukwepi kuwachukua walimu wetu wa vyuo vikuu na kuwa na *exchange programme* na vyuo vya nje, wakajifunze nje. Hata China walipotaka kufanya maendeleo waliamua, hesabu *specific* tujifunze Marekani. Kwa hiyo, lazima watoto wetu wawe na *exchange programme* za wanafunzi na wahadhiri kwenye vyuo ili tulete mabadiliko ya haraka.

Mheshimiwa Spika, wakati Vita ya *Ukraine* inatokea wanafunzi 276 walikuwa *Ukraine,* 96% ya wale wanafunzi kule walipelekwa na mawakala binafsi. Hawa ndio tunasema mshirikiane nao kwa karibu. Wakati inatokea *Covid* China, wanafunzi 4,000 waliokuwa China, wanafunzi karibu 3,600 wote walipelekwa na mawakala binafsi, ni wanafunzi 400 tu ndio walipelekwa na Serikali *approximately*. Sasa ili twende kwa mambo haya kwa haraka kwenye elimu ya amali na umataifishaji na tuweze kuendana na dunia inavyoenda lazima tuhakikishe kwamba tunafanya *internationalization* ya elimu yetu kwa kushirikiana na sekta binafsi. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Kwa sababu uwekezaji kwenye elimu ya amali…

**SPIKA:** Mheshimiwa Msambatavangu, ngoja. Ukiwa unasema taarifa usiketi, usimame ili nikuone.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu kwamba neno analotaka kulitumia ni umataifashaji, umataifashaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo ulipokuwa umeweka /i/ sasa ni /a/, ahsante. Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, napokea kwa sababu mimi ni Daktari na yule ni Profesa, litabaki hivyo umataifashaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ngoja, wewe ni daktari wa nini?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, umataifashaji, *okay*.

**SPIKA:** Mheshimiwa, wewe ni daktari wa nini?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, mimi nitakuletea *documents* zangu uone. Siyo vile ulivyokuwa unasema siku ile wa kisomo na yule, hapana, wa kisomo. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, daktari wa shule.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, daktari wa shule, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee, naomba neno aliloliongea Profesa ndio liingie sasa, ndio liwe lenyewe na Waziri wa Elimu alichukue tulitumie.

Mheshimiwa Spika, inaomba tushirikiane na Sekta Binafsi ili twende *faster* kwenye amali. Mheshimiwa Waziri, mwenyewe amesema, tunamshukuru kwa kutupongeza lakini atusaidie, kwanza hawa mawakala wa nje waje Wizarani, tusiwe chini ya *TCU,* sisi hatuna vyuo au wao hawana vyuo. Tunaomba tuwe sehemu ya Waziri kwenye Wizara awa-*manage* hawa ili awasaidie vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwenye amali pia Mheshimiwa Waziri amesema shule 68 ni binafsi. Kwa maana hiyo ina maana *normally* sekta binafsi inakua haraka kuliko hata sisi. Kwa hiyo, lazima tuwashirikishe sekta binafsi kwamba sasa shule za *private* zinazojengwa ziende kwenye mkondo wa amali. Hawa kwa sababu hela zao hazina *bureaucracy* kwenye maamuzi ya kupanga na kutumia, mtu mmoja anaweza akaamua. Hawa ndiyo wa kwenda kubadilisha hata ule utaratibu wa usajili wa shule, waweke masharti ili tulisaidie Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kumung'unya maneno tuwasaidie wahadhiri wetu na wao, maana yake hapa tena kuna suala la elimu kule kwenye vyuo, wakubali. Kwa sababu moja ya kazi kubwa ya vyuo vikuu ni kuingiza itikadi ya Serikali kwa wananchi. Sisi hapa tuna itikadi ya *BBT*, nchi yetu ina mfumo wa kutaka kwenda labda kwenye kilimo au una mpango wa miaka 50 ya kilimo chetu kitakwenda vipi; ni namna gani chuo cha ardhi kinafundishwa, kinatolewa mifano ya nchi yetu ili nao wajipange kuwaelekeza watoto mwelekeo wa Taifa letu?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kengele ilishagonga Mheshimiwa.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mheshimiwa Charles John Mwijage ajiandae.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Profesa Adolf Mkenda na timu yake yote. Nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati kwa uwasilishaji wa taarifa yetu vizuri na pia niwapongeze Wanakamati wenzangu tumefanya kazi kubwa na kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nataka nianze na rejea ya Hotuba ya Mheshimiwa Rais hapa tarehe 21 Aprili, 2021. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema na aliielekeza Serikali (Wizara ya Elimu) kwamba tunakwenda kufanya mabadiliko makubwa kwenye sekta ya elimu hasa mabadiliko katika Sera ya Elimu ya mwaka 2014 pamoja na mabadiliko ya mtaala ambao elimu inayotolewa iwe ni elimu yenye ujuzi, lakini iwe inaendana na soko la ajira lililopo. Hongera sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba hiyo ya Mheshimiwa Rais, nimeona dhamira ya dhati ya Wizara ya Elimu. Hivi tunavyozungumza wameshafanya mabadiliko na mtaala sasa hivi unafanya kazi, kazi imefanyika vizuri na sisi tumeshirikishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri nitaanza na eneo hili la mkondo wa amali. Pia ameeleza kule moja ya kipaumbele cha pili ni suala la ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Kinachonitia mashaka hapa pamoja na kwamba hili ni jambo zuri, tumeweka *pilot study* ya shule 96, shule 28 ni za Serikali, lakini Mheshimiwa Waziri ametuambia hapa kwamba wana mpango wa kujenga shule za sekondari za ufundi 100, ambapo shule 26 mwakani wataanza kupokea wanafunzi. Hofu yangu hapa ni bajeti, tumeona 60.3% inaenda kwenye mikopo ya elimu ya juu, inayobaki ndiyo tunayoipangia matumizi yote hapa. Ukienda mbali zaidi ni asilimia mbili tu imetengwa kwenye *Technical and Vocational Training*. Sasa kama umeweka asilimia

mbili, tumeweka shule 96 maana yake hatutafikia malengo na bado tuna shule zingine 100, hatutafikia malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ndiyo ilitakiwa itupe picha, ya sasa kweli tunawataka vijana wenye ujuzi? Bajeti hii ilipaswa iweke fedha za kutosha kwenye kitengo hiki cha amali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamefanya *bench marking,* wamezunguka kujifunza kwenye nchi mbalimbali; wameenda katika Nchi za Ethiopia, Kenya, Rwanda, Germany na kwingine kote. Bahati mbaya sisi Wanakamati hatukupata fursa ya kwenda ila tumejifunza kutoka kwenye maandishi yao. Katika kujifunza kwao huko yako mambo mengi wameona, wameona *best practice*, wameona *worse practice*. Sasa nataka nichukue *bench marking* ya historia ya Tanzania, sina sababu ya kwenda nchi nyingine, nchi yetu inajitosheleza.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa hapa na shule za ufundi *(technical schools)* nane. Tulikuwa na *Arusha Technical, Moshi Technical, Mbeya Technical*, Ifunda, Iyunga na nyingine. Hizi shule zote leo hazipo; nyingine zilizoendelea zinazotoa *level* ya *degree* waliamua kujitegemea, ndio maana wanatoa *level* ya *degree*. Sasa tunakwenda kuja na shule 96, tunawezaje kuzi-*manage* wakati bajeti hi ni ndogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuiomba Serikali hapa. Jambo la kwanza hapa tunajua tuna upungufu wa walimu wa taaluma hiyo, tuna upungufu wa vifaa vya kuwezesha kupeleka kwenye hizo shule lakini kuweka *pilot study,* shule nyingi hivi hatutafikia malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa kwanza, tuweke *pilot study* walau kikanda, tuweke shule zetu hizi kikanda, tuanze na kanda halafu baadaye tutakwenda kwenye mikoa kulingana na bajeti yetu. Jambo hili la mtaala ni jambo letu, hatuna sababu ya kukimbizana nalo. Ukiwaangalia kule Ethiopia walivyotuletea wao, walikwama kwa sababu walikwenda kwa *speed* na bajeti yao ilikuwa ni ndogo. Sasa sisi tujifunze kutoka huku tulikotoka,

tutengeneze shule chache ambazo tunaweza kuzi-*manage* ili ziweze kuendelea mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikumbushe eneo jepesi, tuna vyuo hivi tunaita *Focal Development Colleges*, hivi Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vipo chini ya Wizara ya Elimu, tuanzie hapo. Hapo unapozungumza amali tayari tuna shule, tuna vyuo vina kila kitu, vinahitaji tu kuboreshwa. Kama tunataka kwenda huko hatuwezi kuacha hivi Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vikabaki kama vilivyo wakati sisi tumeshaingia kwenye mfumo wa amali. Nataka kuiomba Serikali iende ikaone umuhimu wa kuwekeza hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, mwaka jana nilizungumza sana, nimezungumza kwenye Kamati na nazungumza sasa juu ya eneo la Wadhibiti Ubora wa Elimu. Ithibati ya elimu inasimamiwa na Wadhibiti Ubora wa Elimu. Eneo hili nataka kuipongeza Serikali, wameanzisha muundo mzuri wa madaraka ya watumishi hao, Wadhibiti Ubora wa Elimu. Hili jambo limeanza lakini bado utekelezaji wake haujaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi leo tunavyozungumza, wanapoamua kwenda kufanya kazi yao, anakwenda kumsimamia kule; Afisa Elimu ana *responsibility allowance*, Mkuu wa Shule na Mwalimu Mkuu wote wana *responsibility allowance*, wewe una hela yako unatoa mfukoni unaenda kufanya kazi ya Serikali, jambo hili ni gumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo nataka kuja na ushauri; ushauri wangu tunahitaji hii Idara iwe Taasisi. Kwa nini iwe taasisi? Taasisi ya Vyuo Vikuu inasimamiwa na *TCU,* ni taasisi, kwenye Vyuo vya Elimu ya Kati Taasisi ya *NACTVET* ndio wanasimamia, lakini mpaka hata mitihani wanayo taasisi ya *NECTA*. Kwa nini *level* ya sekondari na shule ya msingi ibaki kuwa Idara? Ndio hoja yangu iko hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimefanya rejea ndogo ya Tume ya Jackson Makweta na yeye wakati anatutoa kule kwenye maarifa na kutupeleka kule kwenye uimara *(competence based),* wakati

anatupeleka huko alikuja na mawazo haya. Nataka niiombe timu ya Wizara ya Elimu iende ikasome ile Tume ya Jackson Makweta vizuri. Ilikotufikisha ilitufikisha vizuri sana na wenyewe walishauri Idara hii ya Udhibiti Ubora iwe taasisi. Ikiwa taasisi hizi changamoto tunazoziona leo hazitakuwepo kwa sababu watakuwa na mamlaka ya kuweza kujisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Afisa Afya akikagua tu zahanati na maeneo mengine, sheria inamlinda na anaweza kufunga hilo eneo, lakini Mdhibiti Ubora anaweza akakagua shule hata akiikuta ina matatizo gani hana sheria hiyo ya kuweza kuichukulia hatua. Nataka eneo hili wakaliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko eneo la mafunzo ya walimu kazini. Eneo hili tumeliacha muda mrefu na inawezekana kwa sababu ya bajeti, lakini tunajua sasa hivi tuna wingi wa wanafunzi na walimu ni wachache hawawezi kutoka kwenda kupata mafunzo kazini nje. Serikali inatakiwa kubadilisha utaratibu tuwe na *learning platform* ya *online,* walimu wasome *online* na wakisoma *online* vyeti vyao wanavyopata vitambuliwe na *NECTA,* vitambuliwe na *NACTVET,* viweze kutambuliwa na *TSC* ili viwasaidie kupanda madaraja, kwa sababu lengo hapa walimu wapate maarifa. Walimu hawawezi kubaki kuwa *dormant* kwa sababu Serikali haina hela, tubadilishe mfumo twende kwenye *e-learning.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kubadilisha huu mfumo, nafahamu wenzetu wa Taasisi ya Elimu Tanzania wameanzisha...

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, ni kengele ya kwanza hiyo?

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, wameanzisha *Learning Management Information System* ambayo wana-*upload material* mle, wana-*upload video* na vitu vyote na walimu wanaweza kusoma. Kwa nini tusitumie hii kuwawezesha walimu kupata maarifa, badala yake sasa hivi tumewagawia walimu vishikwambi, kila mwalimu ana kishikwambi. Changamoto

ninayoiona kule ni *internet,* lakini leo vile vishikwambi ndivyo wanatumia kujaza zile taarifa zao za *PEPMIS* yaani taarifa zao za kuwawezesha kupanda daraja.

Mheshimiwa Spika, tusisahau tumetoka huku tukiwa na *Open Performance Review Appraisal* ime-*fail,* lakini tukaja na *KPI* pia ime-*fail*, leo tunakuja na *PEPMIS*. Kwa nini tunamzungusha huyu mwalimu kwenye suala la kupanda daraja wakati tunafahamu tangu mwalimu anaajiriwa ndani ya miaka miwili akifanya kazi mwaka wa tatu anapanda daraja? Kwa nini tusiende na mfumo huu wa miaka miwili, mwaka wa tatu anapanda daraja pamoja na taarifa hizi ambazo tunaziboresha ili kumwezesha mwalimu huyu awe *competent* katika utumishi wake huu? Nataka kuiomba Serikali ifikirie malengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu sasa hivi tuna upungufu mkubwa sana wa walimu na katika upungufu huu walimu wengi wanamaliza kwenye vyuo. Nataka kuiomba Serikali ije na mfumo mzuri wa kuwawezesha wale wanaomaliza chuo waweze kwenda kufanya kazi. Wakati tunasubiri kuajiri tuwafanye hawa waende kufanya *internship* hata ya miaka miwili akimaliza pale maana yake Serikali inapoajiri anaajariwa akiwa tayari anajitolea yuko *internship. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hii *internship* haiwezi kwenda hivi. Tuwaagize Wakurugenzi watenge bajeti kwa ajili ya kuwapa *incentives* ya hawa ambao wamechagua kwenda kufanya *internship* kwenye hizo shule. Hatutaona kunakuwa na *gap* kubwa la walimu kwenye shule zetu lakini tukiacha kama ilivyo maana yake *gap* la walimu litaendelea kuwa kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, tutamalizia na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba muhimu sana iliyokuwa mbele yetu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwani elimu ndio ufunguo wa maisha.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Sekta hii ya Elimu na nitatolea mfano kwenye maeneo kama mawili hivi kwa uchache tu kuonesha ni jinsi gani Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amekuwa akiongeza bajeti inayotengwa na kuidhinishwa kwa mfululizo wa miaka mitatu. Kwa mfano, mwaka wa fedha 2021/2022 bajeti nzima ya Sekta yote ya Elimu ilikuwa shilingi trilioni 5.5, lakini 2022/2023 ikaongezeka ikawa shilingi trilioni 5.6 na 2023/2024 mwaka huu tuliokuwa nao ni shilingi trilioni 5.9. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Rais wetu kwa kuona haja na tija ya kuongeza bajeti katika Sekta hii ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine tena tunachompongeza Rais wetu, kwa kiasi kikubwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia amepunguza utegemezi wa bajeti ya maendeleo ya elimu kutoka kwa wahisani wa nje. Hivi tunavyozungumza 67% ya bajeti ya maendeleo ya elimu inatoka ndani katika vyanzo vyetu wenyewe, lakini 23% tu ndio kutoka kwa wahisani. Hivyo, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tuwapongeze Mheshimiwa Profesa, Kaka yangu Mheshimiwa Omari Kipanga, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii. Wamekuwa wakifanya kazi nzuri na tunaona mabadiliko na maboresho mbalimbali katika Sekta nzima ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, leo ninaomba kuongea kwa uchache na nitakuwa na masuala mawili tu. Suala la kwanza ni kuhusiana na ukuzaji na uwekezaji katika ubunifu, sayansi na teknolojia.

Ameongea Mheshimiwa Profesa Manya na ameongea Mheshimiwa Rweikiza kwa uchache.

Mheshimiwa Spika, ukisikiliza na kuangalia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri huoni tija ya ukuzaji na uwekezaji wa ubunifu, sayansi na teknolojia. Nalisema hili kwa sababu hii inajidhihirisha katika Hotuba ya Wizara hii. Ni kwa muda wa miaka mitatu mfululizo tumekuwa tukitenga kiasi kidogo sana cha asilimia moja katika masuala mazima ya ubunifu, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kama tunahitaji kufikia uchumi wa viwanda hatuna namna ya kuweka bajeti nzuri katika masuala mazima ya ubunifu, sayansi na teknolojia. Kama tunataka kwenda na kasi ya dunia, sayansi na teknolojia imekuwa ikibadilika kila mwaka, imekuwa ikienda kwa kasi zaidi. Sasa kwa kutenga asilimia moja tutafika tukiwa tumechelewa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 bajeti nzima ya sekta ya elimu ilikuwa shilingi trilioni 5.5 lakini kilichotengwa kwa ajili ya ubunifu, sayansi na teknolojia ni shilingi bilioni 61 ambayo ni sawasawa na 1.1%. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, sekta nzima ilikuwa na shilingi trilioni 5.6, lakini kilichotengwa kwenye masuala ya sayansi na teknolojia ni shilingi bilioni 67 ambayo ni sawa na 1.2%. Kwa mwaka huu tunaoenda nao 2023/2024 sekta nzima ina shilingi trilioni 5.9, lakini tumetenga shilingi bilioni 61 tu ambayo ni sekta moja. Kwa hiyo, imekuwa ikienda ikipungua, lakini pia tumeganda hapo hapo kwenye asilimia moja.

Mheshimiwa Spika, imetolewa mifano hapa na wachangiaji. Tukiangalia nchi za wenzetu jirani katika *aspect* hii ya sayansi na teknolojia wanafanya vizuri sana. Kwa hiyo, nataka niiombe sana Wizara, niiombe Serikali twende tukaongeze bajeti kama kweli tunataka kwenda na kasi ya dunia. Kama kweli tunataka kwenda huko wanakosema kwenye *digital*, kama kweli tunahitaji uchumi wa viwanda, twende tuongeze bajeti ya sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili, ni kuhusiana na suala zima *re-entry*. Tarehe 31 Januari, 2023, nilisimama kwenye Bunge lako Tukufu na kutaka kujua agizo la Mheshimiwa Rais Dkt. Samia la watoto kurejea mashuleni limetekelezwaje. Pia upo mwongozo ambao ulikuwa umetolewa (Mwongozo Na. 2 wa mwaka 2022), ambao unatoa maelekezo ya watoto hawa kurejea shuleni.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri katika lile swali langu alisema kwamba, watoto ambao walisimama kuendelea na masomo kwa ajili ya ujauzito kwa shule za msingi na sekondari, kwa takwimu za mwaka wa fedha 2021/2022 ni takribani watoto 9,011. Hata hivyo, baada ya agizo kuja watoto waliorejea shuleni walikuwa ni 1,692 kati ya watoto 9,011. Kwa hiyo utaona agizo hili halitekelezeki au linatekelezeka kwa kusuasua sana. Kwa hiyo leo tena niiombe wizara ituambie *status* ya watoto hawa ikoje? Kama kuna ongezeko, kama tumesimama au kama tunazidi kuporomoka kwa watoto hawa kurejea shuleni.

Mheshimiwa Spika, pia niliendelea katika maswali yangu ya nyongeza, niliiuliza wizara, kwamba hawaoni haja ya agizo hili la Mheshimiwa Rais Dkt. Samia tukalitungia sheria ili watoto waweze kurudi shuleni? Tunafahamu kwamba hawa watoto wana ndoto, vilevile tunafahamu kwamba si watoto wote ambao walipata ujauzito kwa kujitakia. Tunafahamu pengine watoto hawa wazazi wao walikwishafariki na wanalelewa na familia. Wanaowalea wanawapa vitisho. Kimsingi watoto hawa wanakuwa wanakatiliwa. Kwa hiyo, wana ndoto na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia aliliona hilo na ndiyo maana akatoa hilo agizo.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukuambia ni kwamba, sasa hivi wapo wakuu wa shule ambao wanakataa kuwapokea watoto hawa pindi wanaporejea shuleni. Pia yapo malalamiko ya wazazi wanapowafuata wakuu wa shule ili watoto waweze kurejea shuleni, kwamba wanawaomba fedha ili waweze kuwarudisha watoto wao shuleni. Kwa hiyo tunaomba Serikali ifuatilie kwa karibu. Hata hivyo, wakati umefika, wenzetu wa Zambia wanayo sheria kuhusiana na *re-entry program* na watoto hawa wamekuwa wakijifungua, wakirudi shuleni, wakisoma na wakikamilisha na kutimiza ndoto zao. Kwa hiyo, tunamwomba

Mheshimiwa Waziri atakapokuja aje atuambie kwamba wana mpango gani wa kuja na sheria kwa ajili ya programu hii ya *re-entry* ili hao mabinti wa kike waweze kutimiza ndoto zao?

Mheshimiwa Spika, leo tunaye Rais wa Bunge la Dunia mwanamke, Dkt. Tulia Ackson. Pia, tuna Rais mwanamke Dkt. Samia Suluhu Hassan na viongozi kadha wa kadha. Kwa hiyo, tunaomba suala la viongozi hawa litiliwe mkazo ili waweze kurudi shuleni kama ambavyo agizo linasema.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, tutamalizia na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hii wizara muhimu. Vilevile nipende kukiri kwamba umekaa hapo umeongoza mjadala mzito wenye masilahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na wachangiaji waliotangulia. Mheshimiwa Nahodha, kama jina lako lilivyo umetuongoza vema. Sibadili *Hansard,* lakini kwa sababu Watanzania wote tunazungumza Kiswahili tuanze na Kiingereza halafu tuendelee. Nitambue mchango wa mkuu wa shule na hivyo nataka nianzie hapo.

Mheshimiwa Spika, lengo la Wizara na lengo la Serikali ni kwamba vijana wa Kitanzania wapate maarifa, ujuzi, kujiamini, kujiajiri na kuajiriwa, yaani baada ya kuzungumza yote kuajiriwa ni jambo la mwisho. Ndiyo maana nikasema hili jambo ni mjadala mgumu au mzito. Tunakwenda kubadili dhana au *paradigm shift* ambayo tulikuwa nayo kutoka zile zama za kupata uhuru, ambako watu walielimishwa ili waje waajiriwe na sasa tunakwenda kwenye kuelimisha ili kuajiriwa lije kuwa mengineyo.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza taarifa ya Kamati ambayo Mwenyekiti ni mwanangu na ameunga mkono hoja. Hata hivyo

nilipokuwa namsikiliza kwenye kipengele cha mitaala alikuwa na kigugumizi. Pamoja na mafua aliyonayo, akasema mitaala ina changamoto ya fedha na miundombinu. Ina maana Kamati hii imegundua kwamba hii mitaala; mimi sina matatizo, ni muumini mkubwa wa mitaala mipya kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri na Wizara; ina changamoto ya fedha na miundombinu. Tunaitekeleza, lakini, una lori lako au una gari lako unasafiri kwenda Mbeya kwenye *Marathon* lakini huna *petrol* ndani ya tenki na unasema unakwenda. Sasa unasema huendi mwanangu. Mwanangu Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati *with due respect* wewe umesema hukubaliani na hii safari*; I stand to be corrected.*

Mheshimiwa Spika, suala la pili lililonipa shida ni *pilot study*. Mimi ni mtaalamu wa masoko, nimefanya *pilot study* za bidhaa. Ukifanya *pilot study* za bidhaa isipo-*succeed* unaiua. Sasa tunakuja kufanya *pilot study* kwenye watoto wa watu? Unamchukua mtoto wa mtu kumfanyia *pilot study,* asipofanikiwa? Unamletea mtaala wa amali anakwenda kwa miaka mitano unakuta hauja-*succeed then* unafanyaje? Kwa hiyo hapa nakuja na hoja moja ambayo naishauri Serikali; tuanzishe kitu kinachoitwa *flagship project* (mradi wa kimkakati). Tuhangaike tutenge fedha za kutosha ili huu mtaala utoke moja kwa moja. Tunaweza kuwa hatuna wataalam, twende tuwatafute popote tulipo.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wa rika langu hapa wanakumbuka kwamba tulikuwa na walimu kutoka India (Wahindi) wanatufundisha. Nakumbuka nilikuwa na mwalimu wa fizikia kutoka Urusi, juu ya daraja anasema *under the bridge* kumbe anamaanisha juu ya *bridge*. Sasa twende tukatafute wataalam. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba tuwekeze rasilimali za kutosha. Hatuwezi kufanya majaribio kwa watoto wa watu. Hatuwezi kufanya majaribio katika kitu ambacho ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, nikupe mfano mmoja…

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** …mimi leo nilikuwa nazungumza na mwalimu wangu. Katika wilaya yangu tunahitaji vyumba vya maabara 222...

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Waziri si kawaida sana mwenye hoja kutoa taarifa, lakini naona amesimama huenda ana jambo zito sana. Mheshimiwa Waziri.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mchangiaji. Hakuna *pilot,* mafunzo ya amali si majaribio. Nasema hivyo kwa sababu naogopa mjadala usije ukawa *based* na hoja hiyo, kwamba tunafanya *pilot*. Haya ni mafunzo ya amali, yamekamilika yanafundishwa, si *pilot* na si majaribio. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa imetolewa na mkuu wa shule na baada ya kuzungumza nitakuja kuomba. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo naipokea taarifa kwamba hakuna *pilot*, kuna majaribio. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naelewa hofu ya Mheshimiwa Waziri, kwamba mtaala unaanza na hautakwama. Nimesema ni muumini, lakini pia nikasema twende kwenye mradi wa kimkakati na huko tuweke rasilimali za kutosha. Mheshimiwa Waziri, nadhani tuelewane kwa hivyo, kwamba Mheshimiwa Mbunge amependekeza kwamba tutumie nguvu nyingi na nina imani na mtaala huu. Tutumie fedha nyingi ili haya maneno *pilot study,* kama ninavyoyaelewa, tusiyatumie.

Mheshimiwa Spika, nayaondoa maneno *pilot study*. Sasa itakapokuwa kwamba wale walioanza ni nini hilo sijui neno lake la Kiswahili wala la Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu niendelee…

**SPIKA:** Ngoja. Ili nikuruhusu inabidi kesho Mheshimiwa Waziri aifanye hiyo hoja iwe maalumu kwa ajili ya kutoa ufafanuzi. Kwa sababu kwa namna ulivyoileta kwa kweli ni hoja nzito. Hakuna mtu anataka mtoto wake afanyiwe majaribio. Kwa sura hiyo nadhani ndiyo maana Mheshimiwa Waziri amesimama kwa kuogopa kwamba inaweza ikaleta taharuki kwa watoto ambao wanaelekea kwenye kusoma huo mtaala ambao unazungumziwa. Kwa hivyo, endelea na mchango wako.

Mheshimiwa Waziri, nadhani hoja ya Mheshimiwa Mbunge umeielewa na wewe utapata muda wa kuitolea ufafanuzi vizuri ili wananchi wasije wakafikiri watoto wao wanafanyiwa majaribio kwenye huo mtaala kwa hayo ambayo ameyasema Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, hii mitaala inaanza na nakubali ianze. Hoja yangu haiko kwenye mitaala, nakubaliana nayo. Hoja yangu au changamoto iko katika utekelezaji wa mitaala hii. Nikudokezee kidogo, katika wilaya yangu tuna mahitaji ya vyumba vya maabara 222. Sayansi tunavyo 60 tu. Tunakwenda; tuna mahitaji ya walimu wa sekondari 1,641 lakini tuna 800 tu. Tunakwenda. Kuna shule nyingine, hizo za msingi ambazo sitaki kuzizungumzia. Hoja yangu ni kwamba, tunapoanza tuwe na nguvu ya kusukuma jambo hili. Nakubaliana na msimamo wa Mheshimiwa Waziri, lakini nataka kuiambia Serikali kwamba sisi ni mabingwa wa kutengeneza miradi ya kimkakati *(the Flagship)*. Kama ni mabingwa wa kutengeneza hii miradi tuweke fedha ya kutosha hapa kwa mbinu zote ili watoto wote tuweze kuwatoa katika *paradigm* ya zamani na tuwaweke kwenye *paradigm* mpya kuhusu mitaala hiyo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi mitaala hii haikupaswa kuanza leo, illipaswa kuanza siku nyingi. Kama ni reli iliacha njia siku nyingi.

Sasa ni nini cha kufanya; tunapaswa kuwa *situational*, tunapaswa kwenda na wakati. Leo hii mahitaji ya vijana inaweza kuwa ni kutengeneza simu na kutengeneza vifaa vya kisasa vya kuvulia. Kwa hiyo wale waliopewa dhamana si lazima wawe taasisi, wanaweza kuwa chini ya Wizara lakini wawe *dynamic*, wawe wanaangalia mazingira ya dunia yanavyokwenda ili waweze kusaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa walimu ambao ni watengenezaji wa wanafunzi wetu, niende kwa chuo kikuu. Tutengeneze programu maalumu ambako walimu hasa wa vyuo vikuu wafundishwe kwa wingi kwenye ujuzi. Vilevile walimu wote wa vyuo vikuu wasajiliwe Serikalini. Waende wafanye kazi hata kwenye *private universities,* lakini wawe *highly moderated* na Serikali na Serikali iwape chochote. Iwape mshahara *basic* halafu waende kwenye *private university* wa-*top-up*. Hii itatusaidia kuwa na walimu wakuu kwenye vyuo watakaokuwa na sifa za kuwa walimu ambao wanafundisha vyuo. Unaweza ukamkuta mtu chuo kikuu anakupiga maneno na unayafurahia. Kumbe akienda kukaa mbele na walimu wakubwa wenzake kama akina Profesa Ndakidemi au Profesa Manya akizungumza naye unaona mtu anakimbia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningetaka kulisisitiza ni mshikamano na kusomana kwa Wizara ya Elimu na TAMISEMI. Nashindwa kuona wapi watu wanaachana hapa; huyu wa sera na mtekelezaji. Sera haina maana kama mtekelezaji hataitekeleza kama inavyopaswa kutekelezwa. Kumbe mafanikio ya mitaala hii ni kwamba hizi nyumba zote na kila kitu kinapaswa kiwe kimekwishatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ombi langu linarudi palepale, kwamba tutoe fedha nyingi, tutengeneze mradi maalumu wa kimkakati kusudi tupate fedha nyingi za kutengeneza miundombinu na kuajiri walimu. Pia tuajiri walimu kwa mahitaji na si walimu kwa mkupuo, kwamba mwaka huu tunaajiri 10,000 halafu tunafurahia, hapana. Je, 10,000 au 20,000 ndio tunaowahitaji? Kwa sababu kuna jambo la kuahirisha, unaweza kuahirisha sherehe, lakini huwezi kuahirisha kwenda kwa daktari.

Vilevile watu hatujui madhara ya mtoto kutokusoma akahitimu ni makubwa sana, tutakuja kuyaona.

Mheshimiwa Spika, nikueleze, hakuna kitu kibaya kama mtoto anakuja ametoka shule, wewe uliyesoma zamani kabla ya kompyuta unamwangalia na unaona hakuna kitu. Huwezi kumweleza. Wewe ni Spika au Mbunge amekuja pale unamweleza, mwanangu unataka kufanya nini? Anakwambia nataka kuendesha bodaboda. Unajiuliza kwamba huyu mtoto wa Mheshimiwa Spika naye anaendesha bodaboda? Tunataka tuwape watu ujuzi na kujiamini kama alivyosema mtaalam, Mheshimiwa Msambatavangu. Tunataka watoto wetu tuwasikie Ukraine, tuwasikie Marekani halafu warudi wakati wa *Eid*, *Christmas* na Mwaka mpya ili sisi iwe sehemu ya dunia.

Mheshimiwa Spika, pia niwaeleze, amezungumzia suala la viwanda. Tanzania tuna *location advantage*. Makao makuu ya Afrika yako Tanzania, kwa hiyo tuna fursa na fursa hizi tunapaswa kuzizindua sisi na si watu watoke nje waje kutuambia hii nchi ni ya maziwa na asali. Tunapaswa tutumie vijana wetu na wengine waje kusikia vijana wetu wawe viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini pia nakubaliana na Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Waziri. Hii mitaala nakubaliana nayo na naunga mkono mpango wa Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu waliotangulia kuishukuru Serikali yetu chini ya Rais wetu Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya kuboresha elimu yetu. Nipongeze Wizara ya Elimu kwa mikakati ambayo wamekuja nayo na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, kila nchi ina malengo yake na kila jamii ina malengo yake. Kuna mahali ambapo Tanzania tunataka kufika aidha ndani ya miaka 10, 20 au 50. Hata hivyo, njia ya

kufikia huko ni kuangalia elimu ambayo tunawapa watoto wetu. Sera na mitaala ambayo tunaiweka ina-*determine* sehemu ambayo nchi yetu inataka kufika huko ambako tunakwenda.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naungana na wengine kwa ongezeko hili la 68% kwenye bajeti yetu ya maendeleo. Hata hivyo bado kwenye bajeti nzima ya elimu tuko kwenye 14%, pungufu ya matarajio ya kimataifa ambayo ni 20. Kwa hiyo bado kuna jitihada ambazo tunatakiwa kuwekeza, lakini ni lazima tutambue kwamba hata hapa tulipofika tumepiga hatua na tunapaswa kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, katika 68% hii ya bajeti ya maendeleo 60% inakwenda kwenye mikopo ya elimu ya juu. *Actually,* hatuzungumzii miundombinu na kuendeleza mazingira wezeshi ya kujifunzia na kufundishia. Kama malengo yetu ni kuhakikisha kwamba tunaelekeza nguvu vijijini bila shaka elimu yetu inapaswa kuonyesha kwamba inajiweka ama kuelekezwa huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, suala la Bodi ya Mikopo ambayo inachukua 60% ya bajeti ya maendeleo kujielekeza kwenye elimu ya kati, ni jambo ambalo linahitaji kupongezwa sana. Linahitaji kupongezwa kwa sababu gani; huko kwenye elimu ya kati ndiko kwenye elimu ya ufundi ambayo inachukua watoto wengi wa walalahoi wa nchi yetu ambao wanahitaji na wanastahili mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa tunahangaika na tatizo la ajira kwa vijana wetu na wakati tunahangaika na tatizo la ajira tunaendelea kuzalisha wanafunzi kutoka kwenye vyuo vikuu kwenye kozi ambazo bado wanafunzi wako mtaani hawajapata ajira. Hata hivyo kuna kozi za ufundi, kozi za sekta ya afya na maeneo mengine ambazo zilikosa ufadhili na mikopo kwa watoto wetu, jambo ambalo si tu limeweza kukwaza jitihada za Taifa letu kwenye maendeleo, lakini pia limekwenda kuua vipaji na *talents* za watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wakati tunazungumzia mafundi wazuri mitaani ambao wameweza kututengenezea miundombinu ya mabomba, umeme, magari na vitu vingine,

hawa wote walikosa fursa ya kujiendeleza ama Serikali kuweka mkono wake kupitia mikopo hii ya elimu ya juu. Kwa hiyo, uamuzi wa kupeleka mikopo kwenye elimu ya kati ni jambo ambalo tunapaswa kulipongeza sana.

Mheshimiwa Spika, elimu ni bidhaa kama bidhaa nyingine zozote. Nikiuliza hapa elimu yetu imetuingizia kiasi gani kwenye pato la Taifa, ni ngumu sana kupata *data*. Nikiuliza elimu yetu imetuingizia kiasi gani cha fedha za kigeni, ni ngumu sana kupata takwimu. Hapa naungana na wachangiaji wengine akiwemo dada, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, kwamba kuna umuhimu wa ku-*internationalize* elimu yetu ili kiwe chanzo cha mapato ya elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo pia elimu ni *tool* ya kuonesha Taifa linataka nini kwenye dunia yetu. Ndiyo maana kwenye miaka ya 1960 na 1970 tulikuwa tunakwenda kwenye maendeleo vijijini, tukawekeza huko. Tulikuwa na vituo vya *research* (utafiti) ambavyo vilikuwa vinaieleza dunia ni nini tunachotaka. Ndiyo maana Mwalimu Nyerere alisema kwamba, wakati wenzetu wanakimbilia mwezini sisi kama Taifa tunapaswa kuelekea kijijini. Tulikuwa tunataka tuoneshe mfano duniani kwamba tunawekeza kwa wanawake. Ndiyo maana leo kwa Tanzania Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimezalisha wasomi wa kimataifa ukiwemo wewe mwenyewe ambaye sasa ni Rais wa *IPU,* ni zao la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ni zao la Elimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, si wewe tu, pia tuna Mama Getrude Mongela ambaye ni mwanamke anayefahamika dunia nzima, ni zao la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tuna Mama Asha-Rose Migiro ambaye alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ni zao la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tuna watu wengi kama akina Mama Anna Tibaijuka. Hawa wote wanaweza wakawa *symbol* ya kuonesha Tanzania ina ubora wa elimu kiasi gani na imewekeza kiasi gani. Je, huko mbele tunakokwenda tuna mikakati ya kuzalisha watu ambao ni *notable* katika dunia yetu wa viwango vyenu? Mkakati wetu ni nini? Mtaala ambao tuna *introduce* sasa hivi unakwenda kutupeleka huko?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo elimu pia ni *tool* katika mahusiano ya kimataifa *(internation relations)*. Ndiyo maana mataifa ya wenzetu ambayo yameendelea yanatoa *scholarships* kila siku. Yanachukua *talents* za vijana wetu, wakishaona kwamba wako *smart* na kwamba hawa wanakwenda kulipa huko mbele ya safari wanatoa fedha nyingi kugharamia elimu yao katika mataifa yao na wanauza elimu yao kupitia vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano hapa Tanzania Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hicho hicho kiliweza kuwatoa Rais Yoweri Museveni, Rais wa *Southern Sudan* Dkt. John Garang, Donald Kaberuka, Eriya Kategaya ambaye alikuwa *First Prime Minister* wa Uganda na hata Willy Mutunga; wote hawa ni *product* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Sasa, sasa hivi tuna mikakati gani ya kuzalisha watu ambao ni *notable worldwide* ili tuwaoneshe kwamba Tanzania elimu yetu ni ya viwango vya kimataifa na *alumni* wetu wanaweza wakatoa mchango siyo tu kwa nchi zao lakini pia kwa dunia yetu?

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia suala la vyuo ama elimu ya amali, nakwenda hukohuko. China imeonesha mfano, imebadilisha vyuo vyake vikuu 500 kuwa vyuo vya ufundi. Wakati wenzetu wanabadilisha vyuo vikuu 500 kuwa vya ufundi sisi tunabadilisha vyuo vyetu vya ufundi kuwa vyuo vikuu. Kwa hiyo, kwenye hili kuna jambo ambalo tunapaswa kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya *VETA* ni muhimu sana. tunakwenda kuwa na vyuo 149 vya *VETA*. Je, mfumo wetu wa usimamizi wa elimu yetu bado unaruhusu Wizara ya Elimu kusimamia vyuo hivi kutoka 51 kwenda kuwa 149? Ama tunakwenda kwenye mgongano ambao Mheshimiwa Mwijage amesema, kwamba wapi TAMISEMI na Wizara ya Elimu wanaachana? Ni nani ambaye ni msimamizi wa sera na ni nani mtekelezaji? Je, kuna *mechanism* au *structure* ambayo ndani ya Wizara ya Elimu inakwenda kusimamia vyuo 149 vya *VETA* katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu ni kwamba, kwanza, kuna umuhimu wa Wizara ya Elimu kukaa karibu na Wizara ya TAMISEMI ili kuona kwamba utekelezaji wa vyuo hivi elimu yake inakwenda kujibu changamoto katika halmashauri mbalimbali ambako vyuo hivi vimejengwa

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya halmashauri mbalimbali ambako vyuo hivi vimejengwa yanatofautiana. Kuna wengine ambao wamekaa karibu na maziwa ama Bahari, kwa hiyo elimu ya uvuvi kwa vijana wao ni muhimu. Kuna wengine elimu ya kilimo ni muhimu na wengine elimu ya utalii ni muhimu. Haya tutayapata kama TAMISEMI na Wizara ya Elimu watakaa pamoja kama *partners* na siyo kama *competitors*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza cha leo. Niwashukuru kwa uvumilivu maana baadhi yetu wana dharura, kwa hiyo ilibidi wachangie asubuhi hii. Hata hivyo, Kanuni zetu zinaruhusu; maana watu wanaweza kusema kuwa Mheshimiwa anapenda tufuate Kanuni halafu yeye mwenyewe hafuati. Hata hivyo, Kanuni ya 34 inanipa mamlaka hayo ya kuongeza nusu saa bila kuwahoji. Kwa hiyo niliongeza nusu saa na sasa tumemaliza kabla ya hiyo nusu saa haijakwisha.

Nitaje Waheshimiwa Wabunge ambao tutaendelea nao mchana kwa ajili ya michango mbalimbali ya hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka. Wengine wataendelea kutajwa kadri muda utakavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

*(Saa 7.25 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

**7 MEI, 2024**

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano kwenye Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda. Tutaanza pale tulipoishia, nimwite sasa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, atafuatiwa na Neema Kichiki Lugangira, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuanza leo jioni, pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia fursa hii kujadili haya mambo makubwa katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma tulikuwa na mzee wetu Muadhama Laurean Cardinal Rugambwa. Kati ya mambo makubwa aliyoyasema katika uhai wake alisema watu wapatieni elimu matatizo mengine watasuluhisha au watatafuta suluhu wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo liko mbele yetu ni jambo ambalo linahusu uhai na ustawi wa Taifa letu kubwa. Wakati najiandaa kuchangia nikapitia nyaraka nyingi. kwa ruhusa yako naomba uniruhusu kati ya kitu ambacho nimekumbana nacho, nimekuta baadhi ya Maprofesa wabobezi kati ya watano

mmoja tunaye humu kwenye jengo hili kwenye Ukumbi huu Mheshimiwa Profesa Ndakidemi. Katika tasnia yake kati ya wale watano nimemwona na anastahili maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu waliandaliwa na mazingira ya kuwaandaa yalikuwa ni mazingira mazuri. Hali ikoje sasa? Niwapongeze Viongozi wa Wizara hii ya Elimu wanafanya kazi kubwa sana ya kuwaandaa watoto wetu na kukiandaa kizazi kijacho. Mheshimiwa Waziri, Naibu wake Makatibu Wakuu na nimeangalia ile safu ni safu ya Maprofesa, Madaktari ambao waliandaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya elimu yetu kwa sasa na tunakoipeleka tunayo kazi kubwa ya kufanya, tunayo kazi kubwa ya kutafakari njia sahihi ya kulipeleka hili Taifa mbele. Nilikuwa naangalia taarifa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam peke yake. Hatuwezi kuongelea elimu hatuwezi kuongelea elimu kwa kuangalia majengo, kwa kuangalia miundombinu, tunaongelea elimu kwa kuangalia majengo, miundombinu, lakini pamoja na wafanyakazi kwenye vyuo vyetu vikuu. Asubuhi wamechangia waliotangulia, wameongea mengi kuhusiana na mahusiano baina ya vyuo vikuu, miundombinu tuliyonayo *versus* wafanyakazi wa vyuo vikuu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam peke yake leo kina upungufu wa wafanyakazi zaidi ya 45% hawapo, sasa ukishakuwa na upungufu wa namna hiyo huwezi kuongelea elimu bora kwa watoto wetu na watu walikuwa wanalalamika leo asubuhi na siku zote tumekuwa tukilalamika kwamba elimu inashuka, lakini hatujiulizi na hatutafuti ufumbuzi kwa nini elimu hiyo inashuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia takwimu za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanapaswa kuwa na Maprofesa 161, leo tunavyoongea tuna Maprofesa tisa tu, kuna upungufu wa Maprofesa 152 ambayo ni 94%, sasa tunajenga, tunaelimisha watoto au tunacheza kindakindaki hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo kazi kubwa ya kufanya mbele yetu siyo kujenga majengo, Mheshimiwa Profesa Manya amesema asubuhi kwamba tupunguze ujengaji wa vyuo vikuu tuimarishe hivi vilivyopo kwa kuwa sikubaliani naye kupitia huu mpango na Kagera tumejenga Chuo Kikuu, hongereni sana Mheshimiwa Waziri, lakini lazima twende tukatafute dawa au mwarobaini wa upungufu wa wafanyakazi kwenye vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nita-*deal* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam peke yake. Wanahitajika Maprofesa Washiriki 220, wapo 49, pungufu ni Maprofesa Washiriki 171 ambayo ni 78%, upungufu wa Maprofesa Washiriki, Wahadhiri Waandamizi wanahitajika 430, wapo 182; Wahadhiri 577, wapo 171; na Wakufunzi Wasaidizi 385, wapo 108.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam peke yake, naongelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam idadi ya wafanyakazi inashuka kwa mwaka jana kwa asilimia nane, lakini *enrollment* ya wanafunzi imeongezeka kwa 28%. Unaweza ukaangalia uwiano kati ya kushuka kwa wafanyakazi na kuongezeka kwa wanafunzi; elimu yetu haina afya. Lazima tuna jambo kubwa la kufanya na kutibu tatizo hili. Nilikuwa natafuta kwa nini Wahadhiri wanapungua, lakini tunasajiri wanafunzi wengi, nani anakwenda kuwapatia huduma kwenye vyuo vyetu hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonalo na niishauri Serikali vyuo vyetu vikuu vipeni mamlaka ya kuajiri na kufukuza, viwe *autonomous*. Mchezo wa kuamka asubuhi Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo Kikuu au chuo chochote cha umma anaambiwa huyu mfanyakazi hayupo au analetewa mfanyakazi wakati mwingine wanaowapelekea pale hawana sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali yangu, tunapenda elimu na lazima tuikuze na kuiheshimisha, vyuo vyetu vikuu vya umma Mheshimiwa Waziri…

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** ….alete sheria hapa tuvipe mamlaka kamili ya kuajiri na kufukuza, si mchezo wa kupelekewa kunyang'anywa uishe, kama tunataka kujenga Taifa lenye nguvu, Taifa lenye heshima na Taifa lenye elimu.

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kikoyo kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kumpotezea muda, lakini nataka kumpa taarifa mimi nimefundisha katika vyuo vikuu viwili Mzumbe na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mwajiri wangu yalikuwa ni Mabaraza ya Vyuo Vikuu na hiyo ilikuwa inaniwezesha mimi kusimamiwa kinidhamu na kiutendaji kuanzia kwa Mkuu wa Idara, Mkuu wa Kitivo, *Committee of Deans, Senate* na Baraza lenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Mkurugenzi wa *internationalization* aliyokuwa anaisema jirani yangu hapa. Nilipendekezwa, nilitafutwa na kuthibitishwa na Baraza la Chuo Kikuu, kwa hiyo, uhuru wa kuajiri ndio chuo kikuu chenyewe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Dkt. Kikoyo unaipokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Bashiru ally?

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mwanazuoni mwenye heshima yake na hilo ndio nililokuwa naishauri Serikali turudi huko ili tuweze kujenga nidhamu ya vyuo vikuu vyetu, lakini na wafanyakazi stahiki kwenye vile vyuo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kumalizia, tuviruhusu vyuo vyetu vikuu kutafuta Wahadhiri popote duniani walipo wakatusaidie.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, hata watu ambao wapo nchini nadhani alikuwa Uhuru Kenyatta alisema hawezi kuruhusu akili yake izagae nje huku kama kuna akili yoyote huku tuilete kwenye vyuo vikuu vyetu, tuache ukiritimba, tuwatumie Watanzania popote walipo ili wakatusaidie kuelimisha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana namwita sasa Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota na Mheshimiwa Aloyce Kamamba, ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye Bajeti hii ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nami napenda kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa na kazi kubwa ambayo inaendelea kufanyika katika kuimarisha elimu hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022 mwezi Septemba, Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilisaini makubaliano ya Umoja wa Mataifa kupitia *School Meals Coalition,* ni mpango ambao unalenga kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2030 kila mtoto anayesoma katika shule zetu atakuwa anapata lishe shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kwamba Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ndio ina dhamana kwanza ya kusimamia sera na utekelezaji wake, lakini pia ina dhamana ya kudhibiti Ubora wa Elimu, naamini tutakubaliana kwamba ubora wa elimu si tu majengo, madarasa, walimu, lakini ubora wa elimu ni pamoja na kuandaa ubongo wa yule mwanafunzi aweze

kupokea yale anayopewa. Kwa hiyo, suala la lishe si suala la anasa, ni suala ambalo linapaswa lipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikirejea hilo eneo natambua kwamba usimamizi wa shule zetu katika ngazi za Mikoa, Halmashauri uko chini ya TAMISEMI, lakini nikirejea jukumu la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia la kusimamia utekelezaji wa sera na udhibiti ubora wa elimu napata wasiwasi sana pale ambapo shule zetu za kitaifa hususani zile za bweni ambapo pesa ya kulipia gharama za kulisha wanafunzi huwa zinachelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo kwanza wale wazabuni ambao wanatoa huduma ile ya chakula kwenye zile shule zetu wanaishiwa mitaji, lakini pili, watoto wetu wanashindwa kupata lishe ambayo wanastahili kwa sababu kama bajeti inazidi kupungua ina maana kama ilikuwa inatakiwa wapate tunda, basi hatapata tunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea watoto wetu wa kidato cha sita wapo wanafanya mitihani. Kufanya mitihani ukiwa na njaa, kufanya mitihani ukiwa huna lishe sahihi ni changamoto. Kwa hiyo, nataka kufahamu Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja yake atueleze ni nini anafanya kama mdhibiti wa ubora wa elimu nchini kuhakikisha kwamba wazabuni wanaotoa chakula kwenye shule zetu hawacheleweshewi malipo na nitatoa mfano mdogo kwa haraka haraka. Tukirejea katika Jimbo la Bukoba Mjini kuna shule sita za sekondari za kitaifa Bukoba Sekondari ya wasichana, Ihungo Sekondari ya wavulana, Kahororo Sekondari ya wavulana, Omumwani Sekondari ya wasichana, Rugambwa Sekondari ya wasichana pamoja na Kagemu Sekondari ya wasichana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake shule hizi zinadai takribani milioni 935 ambazo ni gharama ya wazabuni walio-*supply* chakula. Sasa ikiwa shule hizi zinadai kiasi hiki na haya ni madeni ambayo wengine wanadai kwa miaka sita, miaka minne, miaka mitatu, miaka miwili, mwaka mmoja na wengine miezi, ni dhahiri kabisa ubora wa elimu lazima utakuwa kuna mahali

unalegalega kutokana na kwamba watoto wetu hawapati lishe inayostahili pale shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee tena, ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri atueleze yeye kama mdhibiti ubora wa elimu hapa nchini nini anafanya kuhakikisha kwamba watoto wetu hawakosi lishe inayostahili pale shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika eneo la Tahasusi, tumeona kwamba Mtaala Mpya unalenga sayansi na teknolojia, lakini katika Tahasusi hizi mpya kuna takribani Tahasusi mpya 49, lakini katika Tahasusi hizi mpya 49 ni saba tu ambazo zimejikita katika sayansi na teknolojia. Bado napata wasiwasi kuelewa ni kwa namna gani Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inakwenda kutekeleza huu Mtaala Mpya ambao umepaswa kujikita katika sayansi na teknolojia ilihali kati ya Tahasusi mpya 49 ni saba tu ambazo ziko kwenye masomo ya sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi kamili kutoka kwa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake, ni kwa namna gani wanakwenda kutekeleza huu Mtaala Mpya ambao umejikita katika sayansi na teknolojia ilhali ni Tahasusi saba tu kati ya 49 ambazo zimejikita katika sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo watoto ambao watachukua mchepuo wa sayansi katika kidato cha tatu na kidato cha nne watakapoingia kidato cha tano hawatapata Tahasusi nyingi za kuchagua kama wengine wa masomo ya *arts*. Sasa natoa mfano mathalani ametokea mtoto ambaye amechukua mchepuo wa sayansi kidato cha nne akapata *division one,* mtoto huyu akasoma *five* na *six* mchepuo huohuo wa sayansi, kwa bahati mbaya kidato cha sita hajapata zile *grade A, B* na *C,* kwa mantiki hiyo mtoto huyu atashindwa kwenda chuo kikuu, lakini mtoto huyu ambaye tayari amesoma kidato cha tano na cha sita atakapokwenda kusoma diploma atahesabika sawa na yule aliyemaliza kidato cha nne kwa

sababu ule muda aliosoma kidato cha tano na cha sita hauhesabiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili upya kwa sababu tunakwenda kutengeneza vijana ambao watakuwa na msongo wa mawazo. Mtu ameshatumia miaka miwili amesoma kidato cha tano na cha sita, ni kwa bahati mbaya hajafikisha zile *grade* zinazotakiwa iweje sasa akienda kusoma diploma ahesabike kama ile miaka miwili alikuwa anacheza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, saa nyingine tuambiane ukweli mtoto anapofeli haimaanishi kwamba alikuwa anacheza darasani. Tunafahamu shule zetu kuna shule zingine labda walimu hawatoshi au vile vifaa vya kufundishia havitoshi, mtoto huyu akatokea amefeli, sasa kwa nini tumwadhibu mtoto huyu kwamba ile miaka miwili aliyosoma kidato cha tano na cha sita iwe ni kazi bure anaenda kuhesabika kama mtoto wa kidato cha nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri yeye akiwa kama mzazi na sisi wote Wabunge tukiwa kama wazazi tutambue kabisa kitendo hicho kitakweda kuwadhoofisha watoto wetu na kitakwenda kutengeneza vijana ambao wana msongo na mawazo na hata ile hamu na ari ya kusoma na kujiendeleza itafifia. Kwa hiyo, naomba sana hili suala tuliangalie upya kwa sababu ni njia moja ya kunyanyapaa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kuangalia pia hivi sasa kutokana na hizi Tahasusi mpya zipo jitihada za Serikali ambazo ni jitihada za kupongezwa ambayo tunaongeza madarasa kwenye shule zetu hizi za kitaifa pamoja na hizi shule ambazo zina mabweni. Nitatolea mfano pale kwenye Jimbo la Bukoba Mjini, Shule ya Kahororo Sekondari inaongezwa darasa moja ambalo wastani wa darasa moja ni watoto 40, Shule ya Lugambwa Sekondari yanaongezwa madarasa sita ambayo ni wastani wa watoto 240, Shule ya Omumwani wanaongeza madarasa manne ambayo ni wastani wa watoto 160.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati jitihada hizi zinaendelea za kuongeza madarasa bado hatuelewi mpango thabiti wa kuongeza mabweni. Sasa nirudi kwenye ile hoja yangu ya mwanzo Wizara hii ya elimu ikiwa na jukumu la kusimamia na kudhibiti ubora wa elimu ni nini sasa wanakwenda kufanya kuhakikisha ya kwamba Tahasusi hizi mpya pamoja na madarasa mapya ambayo yatajengwa hayatakwenda sasa kusababisha msongamano kwenye mabweni? Kwa sababu msongamano kwenye mabweni nao utafanya watoto wetu washindwe kusoma katika mazingira ambayo yako sahihi. Kwa hiyo, nimuombe sana pia Mheshimiwa Waziri hili nalo aliangalie kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha, kama nilivyosema awali, mtaala mpya unalenga sayansi na teknolojia. Naamini Mheshimiwa Waziri Profesa atakubaliana nami sasa hivi katika vyuo vyetu, siyo Tanzania tu hata huko duniani, kuna suala zima la akili mnemba *(artificial intelligence)*. Siku hizi mwanafunzi anapewa kazi afanye, anaingiza kwenye *artificial intelligence* anapata majibu kila kitu. Sasa je, Serikali inajipanga vipi katika kuhakikisha kwamba, vyuo vyetu vinatumia teknolojia ya kuweza kutambua kama kazi hii imefanywa kwa kutumia akili mnemba ama kweli ni ya mwanafunzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha naiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itenge bajeti ya kukuza stadi za kidijiti kwa walimu wetu katika ngazi zote.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pasipo walimu wetu kuelewa stadi za kidijiti *(digital skills)* hata huu mtaala unaolenga kuimarisha sayansi na teknolojia hautawezekana.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naipongeza sana Wizara hii na naungana na Wabunge wenzangu kusema kuwa, naunga mkono hoja, lakini namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja yake anipe maelezo vizuri yanayoeleweka katika hoja nilizoziwasilisha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa namwita Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, atafuata na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja ambayo iko mezani kwetu. Naanza kwa kumpongeza Waziri wa Wizara hii Profesa Adolf Mkenda kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, Naibu wake Omari Kipanga pamoja na timu ya watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Profesa Carolyne Nombo. Vilevile, kuna Naibu Makatibu Wakuu Franklin Rwezamula na Profesa Mdoe, nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanazozifanya, lakini bila kumsahau mchezaji mahiri kwenye Wizara hii, Kamishna wa Elimu pamoja na wakurugenzi wa taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nitajielekeza kwenye mtaala mpya. Kwanza, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maelekezo yake kwamba mtaala huu sasa uanze kutekelezwa. Naipongeza Wizara kwa kuthubutu kwa sababu, utekelezaji wa mtaala huu umeshaanza, hongereni sana. Walikuwa na maagizo matatu; kwanza ni yafanyike mapitio ya Sera ya Elimu ile ya mwaka 2014, lakini ipitiwe Sheria ya Elimu ile Sura ya 393 ambayo ilikuwa inajulikana kama Sheria ya Elimu, Namba 25 ya mwaka 1978 pamoja na Marekebisho yake ya mwaka 2002, lakini vilevile wakapewa kazi ya kufanya maboresho ya mtaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kazi mbili zimeshakamilika kwa sababu, tumeona sasa sera mpya ambayo ni Sera ya Elimu ya mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023. Vilevile tumeona mwaka huu tunaanza utekelezaji wa mtaala mpya hata kama ni kwa makundi mbalimbali, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa sasa mtaala wetu mpya unaanza kutekelezwa kwa wanafunzi wa darasa la awali, la kwanza, la tatu, kidato cha kwanza na cha tano. Vilevile, kwenye taarifa ya Waziri hapa tumeambiwa kwamba kwenye shule za sekondari utekelezaji umeanza kwa shule 96 ambapo kati ya hizo shule 28 ni za Serikali na 68 ni za binafsi. Sasa mchango wangu ni hapa kwenye utekelezaji wa huu mtaala, tumeanza kwa makundi hayo, lakini bado najiuliza maswali mengi kama kweli utekelezaji huu utatoa matunda ambayo yamekusudiwa kama walivyosema wachangiaji kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mtaala huu unahitaji rasilimali fedha nyingi sana ambazo kwenye kitabu cha Waziri hazionekani. Utekelezaji wa mtaala huu unahitaji rasilimali fedha nyingi sana ambazo kwenye Kitabu cha Waziri hazionekani. Utekelezaji wa mtaala huu unahitaji rasilimali watu na sehemu kubwa ni walimu. Hapa kwenye utekelezaji wa mtaala huu tumeona yale ambayo yamefanyika, kuna mafunzo yamefanywa kwenye ngazi ya kanda, mkoa na wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko yoyote ya kweli ambayo mwalimu atafanya kwa 100% ni yale ambayo mwalimu wa darasani ameshirikishwa. Tunahitaji fedha nyingi kwa ajili ya mafunzo kazini kwa walimu waliopo shuleni sasa hivi. Hapa tumeambiwa kwamba, kuna walimu wawili watatoka kila shule, haiwezekani, ni lazima walimu wote wakae darasani waelekezwe nini cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekondari ambako tunaelekea sasa hivi tunakuwa na pande mbili, tunakuwa na mkondo wa amali na mkondo wa taaluma. Hawa walimu hawafahamu hayo. Sasa tutaingiaje huko bila kuliandaa jeshi ambalo linaweza kupigana? Hawa wanafunzi wa darasa la tatu ambao wameanza kutekeleza huu mtaala mwaka 2027, kwa maneno ya zamani wangekuwa wanahitimu elimu ya msingi, watafika darasa la sita hakutakuwa na mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, tutakuwa na upimaji tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuelewe kwamba, tukiangalia *pass rate* na *transition rate* tulikuwa tuna wanafunzi kadhaa wanaingia

sekondari na wengine wanabaki. Sasa kwa upimaji wetu wengi wataendelea na kiwango kingine, tumejiandaaje? Ni madarasa yaleyale, walimu walewale na ufundishaji uleule, tunatarajia atoke na vyeti viwili, cheti cha amali na taaluma. Je, kwa hali ilivyo sasa hivi kwa bajeti hii ambayo Profesa ameisoma hapa, watoto hawa kweli, watapata ujuzi na maarifa ambayo tunatarajia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa sehemu kubwa ya bajeti ya Wizara hii ni mikopo ya elimu ya juu, Mheshimiwa Profesa pale hana fedha. Kwa hiyo, naomba tunapokwenda kutekeleza mtaala huu, basi lazima tubadilishe mfumo wetu wa ugharamiaji elimu. Tukienda kama kawaida na mwakani fedha nyingi tuta-*budget* kwa ajili ya shughuli za uchaguzi, 2027 haipo mbali, sasa hili kundi ambalo wataingia kwenye upimaji watakwenda wapi? Wataingia huku ili wapate ujuzi gani au maarifa gani ambayo wakirudi mtaani watajiajiri? Kwa hiyo, naiomba Serikali, ni lazima hii tuifanye kama ni *operation* ya kijeshi. Ni lazima tufanye maamuzi magumu, ni lazima tutenge fedha nyingi ili sasa mabadiliko haya tunayoyatarajia yatokee kwenye...

*(Hapa Mbunge hakusikika anachozungumza)*

**MWENYEKITI:** Husikiki, hebu...

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya hivyo, basi tutakimbilia kufanya tathmini ambayo itaonesha kwamba, hatujafanikiwa kumbe hatukupeleka rasilimali za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mtaala huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili ni walimu, ualimu na ugatuaji. Mchangiaji mmoja amezungumza ni lazima tuwe na mipaka halisi kati ya Wizara ya Elimu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Jukumu lao kubwa Wizara ya Elimu ni kusimamia sera na taaluma. Walimu wapo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, lakini ualimu kama *profession,* wanao wao. Hawa walimu wanahitaji mafunzo kazini. Ni kada ambayo sasa hivi inahangaika, yaani mtu anaajiriwa miaka 10 hajakalishwa

kufundishwa mambo mapya, atawezaje kutekeleza huu mtaala mpya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili siyo la Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa bali ni la kwako Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda kuisimamia hii taaluma. Muda fulani nashangaa nikiona tahasusi zinaelekezwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilikuwa wao kwa sababu, wanasimamia sera ndiyo watwambie wanatupeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitarajia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa washughulikie miundombinu na mambo mengine kama hayo ikiwa ni pamoja na utawala. Tunapoingiza taaluma kwa sababu, tahasusi ni sehemu ya mchakato wa mtihani na mtihani ni *process,* unaanza utungaji, usimamizi, usahihishaji, utoaji matokeo na jinsi ya kuwaandaa wale waliofaulu wanaingia ngazi nyingine ya elimu. Hiyo ni kazi ya Wizara ya Elimu, waisimamie. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Chikota. Muda wako umeisha.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekwisha?

**MWENYEKITI:** Hitimisha.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie angalau dakika moja. Mheshimiwa Profesa Mkenda atakapokuja kuhitimisha aniambie amefikia wapi uanzishaji wa *University College* ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni elimu pana na hivyo, ina mambo mengi ambayo yanapaswa kuchangiwa, lakini kwa sababu ya muda nitachangia kadri utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika miaka yake mitatu ya Urais kwetu Kakonko ameweza kutujengea shule sita mpya za sekondari, shule za msingi 16 na Chuo cha *VETA*. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya katika kuhudumia Wizara hii ambayo ni kubwa. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 11(2), inasema; "Elimu ni haki ya kila Mtanzania."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana na hilo Mheshimiwa Rais ameona katika kulitekeleza amepeleka elimu kwa watoto wa kike ambao wamepata ujauzito. Ameona kwamba, ni vizuri warudi shule, tunampongeza sana, lakini katika utekelezaji wake ni vema Wizara ikatambua mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kwamba, huyu mtoto wa kike sasa ana mtoto, anapokwenda shule maana yake anamwacha mtoto nyumbani, anamwachia nani? Huyu mtoto wa kike anapokwenda shule anahitaji maziwa, kwa ajili ya huyu mtoto, maziwa haya anayapata wapi? Kwa hiyo, tunapotekeleza hili ni vema Wizara iangalie kwamba, huyu ambaye tunamrudisha shuleni kusoma ilhali akiwa amepata mtoto, anasomaje? Pia, uchumi wake utakuwaje? Kwa mazingira hayo ni vema Wizara iangalie uwezekano wa kuwawezesha ili wanapokwenda shule

waweze kuwa na uchumi utakaosaidia kuendelea kuhudumia watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika eneo hilo ni huyu mtoto wa kike tunamuita mtoto tu, lakini siyo mtoto tena ni mtu mzima. Ni mtu mzima kwa sababu ana mtoto, kwa maana hiyo anahitajika mwalimu maalumu wa kuweza kumfundisha huyu mtoto. Maana yake ni awe na maarifa, awe na stadi na awe na saikolojia ya kumfundisha mtu mzima huyu ambaye ni binti, lakini ana mtoto. Walimu hao ambao ni maalumu, kwa ajili ya kuwafundisha hawa, tunao? Sasa naiomba Wizara iangalie uwezekano wa kuwapata walimu maalumu wenye maarifa, stadi na saikolojia ya kuweza kuwahudumia watoto hawa wa kike ambao wana watoto shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirudi kwenye Sheria ya Elimu, *section* ya 37(2)(e), inasema kwamba, ikitokea mwanafunzi akiwa nje ya masomo kwa muda wa siku 90 anapaswa kuwa nje ya shule. Sasa kuna huyu mtoto wa kike ana siku zaidi ya 270 yupo shuleni. Huyu mtoto wa kiume yeye sheria bado imemshika mguu na mkono. Siku 90 sheria inamwambia asirudi shule, huyu mwingine kapata ujauzito, siku zaidi ya 270 amerudi shule, hii siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nia ni kuwarudisha watoto wote shule, basi sheria hii sasa iangalie upande wa pili, imwangalie mtoto wa kike, lakini imwangalie na huyu mtoto wa kiume ambaye ana changamoto nyingi na yeye aweze kurudi shule. Mtoto wa kiume ana changamoto nyingi, ndiye yuko mgodini anatafuta fedha kwa ajili ya kulisha familia na yuko kwenye uvuvi, lakini baadaye anahitaji kurudi shule. Ni vema sheria hii iangalie pande zote mbili. Huyu mtoto wa kike kapata ujauzito karudi shule na huyu naye kwa sababu, alikuwa amebanwa na shughuli za kiuchumi, basi na yeye arudishwe shule. Sheria hii iangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la *VETA*. Humu karibu kila wakati kila Mbunge ameomba kupata *VETA* na tunashukuru kwamba, Serikali imeweza kuliangalia hilo. Hapo awali tulikuwa

na *VETA* 51, lakini ndani ya miaka mitatu Mheshimiwa Rais ameweza kukamilisha vyuo 29 na sasa kuna ujenzi wa vyuo vingine 65 na kufikia mwaka kesho tutakuwa na vyuo 145. Hoja inakuja, tunao walimu wa kutosheleza kufundisha vyuo hivi? Tunavyo vifaa vya kufundishia hawa wanafunzi katika vyuo vyetu vya *VETA*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu naomba sana, moja ni walimu waandaliwe, kwa ajili ya wanafunzi wetu katika vyuo vya *VETA,* lakini viangaliwe vifaa ambavyo vitawawezesha hawa vijana wetu ambao wataingia *VETA* waweze kufundishwa inavyostahili. Kama haitoshi, naomba kozi zitakazotolewa katika vyuo hivyo vya *VETA* ziwe kozi zinazokuja kujibu changamoto zinazoikabili jamii yetu. Tusiende kuchukua kozi, eneo ni la uzalishaji katika kilimo na fani mbalimbali, unakuja kuchukua ile kozi ambayo ingefaa labda Mkoa wa kwako Njombe inaletwa Kigoma. Kwa hiyo, zichukuliwe kozi ambazo zitakuja kujibu changamoto katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa wiki nzima iliyopita suala ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa wanaomba katika maeneo yao ni ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari za kata. Hii ni kwa ajili ya kujibu changamoto ambazo zinawakabili vijana wetu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ujenzi wa sekondari maeneo mengi tulikuwa tunatafuta eneo la katikati ili kila kijiji kiweze kufikisha vijana wake bila shida. Kutokana na hili mvua zikinyesha hawa vijana wetu wanahangaika kwa sababu ya mvua, jua likiwaka wanahangaika kwa sababu ya jua, kutokana na hilo vijana wetu hawapati muda wa kutosha kujifunza inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, sasa naishauri Serikali ichukue uamuzi wa ziada kuhakikisha kwamba, kwenye shule zetu za sekondari tunajenga mabweni. Ukijenga mabweni, ni rahisi hawa vijana kusoma pamoja bila shida, lakini kama haitoshi, ni rahisi walimu kuweza kuwafuatilia, ili wasome bila bugudha. Ni rahisi hawa vijana kuishi kwenye maeneo ambayo

tutakuwa na uhakika kwamba, wanaishi maeneo gani ili kutoka kwenye shida ambapo wanalazimika kwenda kuishi kwenye mageto na nyumba nyingine ambazo hatuzifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hilo tutawaepusha vijana wetu wengi kuingia kwenye mitego ya kuvuta bangi na wengine kupata ujauzito katika umri mdogo. Mwenzangu ambaye alipewa jina kwamba ni mwalimu mkuu alizungumzia juu ya wadhibiti ubora. Wadhibiti ubora ndilo jicho la Serikali kwenye upande wa elimu, lakini hawa ambao tunawaita jicho la elimu hawajawezeshwa inavyostahili. Wengine wamepandishwa vyeo lakini mpaka muda huu hawajaweza kupewa stahiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe stahiki zao ambazo wanastahili kuzipata waweze kuzipata ikiwa ni pamoja na kupewa vitendea kazi, ili moja: wapate muda wa kwenda kufuatilia shughuli zinazofanywa na walimu. Pia, nishauri, TAMISEMI kwa sababu wanafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Elimu, zile taarifa ambazo zinatolewa na wadhibiti ubora zifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote kwa yote, Wizara ya Elimu haiwezi ikakamilisha mambo yake yote bila kuajiri walimu. Waziri wa TAMISEMI ameshatoa taarifa hiyo, niombe sasa katika ajira hii yaangaliwe maeneo ya pembezoni ili waweze kupelekewa walimu ambao watajibu kiu ya Mheshimiwa Rais, kiu yako Mheshimiwa Mwenyekiti na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umeshika *mic*, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray ajiandae.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii. Nami niungane na wenzangu

waliotangulia kumpongeza Waziri wa Elimu na Naibu wake, Katibu Mkuu na Naibu wake na wafanyakazi wote wa Wizara ya Elimu. Kwa kweli, nasema wamefanya kazi kubwa kwa kuja na hii Sera ya Elimu ya Mitaala iliyoboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia upande wa *experience* yangu maana nimefanya kazi kwenye Mashirika ya Kimataifa ambayo nimejihusisha sana na mambo ya *skills development* kwa ajili ya ku-*create employment* kwa vijana. Kwa kweli nasema hii elimu ya mkondo wa amali ambayo ndiyo nita-*concentrate on* nimeipenda sana. Nimeipenda sana na najua hii ndiyo itaongoza nchi yetu kutoka kwenye umaskini, vijana wetu wakawa na *skills* zinazoweza ku-*create employment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema hayo, nilipokuwa nikipitia hii *document* ya Waziri, nimekuwa na maswali ambayo nimekosa majibu. Kwa hiyo, labda nikipata majibu hayo, yatanipa amani kwamba tunaenda katika njia bora. Kwanza, nilivyosikia Kamati yenyewe ya Elimu ikisema kwamba kuna uhaba wa fedha na vitendea kazi ikanipa wasiwasi, kwamba kama Kamati yenyewe imeona hivyo, huu mkondo wa amali utafanyaje kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikizungumzia *experience* za sehemu nyingine ambazo nimefanya kazi kwenye *international organizations* mbalimbali, walimu ambao wanatakiwa wafundishe wanafunzi masomo haya ya amali wanatakiwa wenyewe wawe *very competent*, wawe na ujuzi wa hali ya juu sana. Maana tunataka kuwa-*impress* watu kwamba; ile *system* ambayo wanafunzi wamejua kwamba anaenda tu kwenye mkondo wa elimu ya kawaida mpaka *university* angojee elimu, sasa tunataka ku-*change mindset* yao kwamba elimu ya amali ndiyo bora kuliko hii nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unafanyaje hivyo? Nichukue mfano wa China, wenzetu wa China walivyojua kwamba wanataka kuanzisha mkondo wa amali, walihakikisha kwenye zile *priority area* zao wanakuwa na walimu, wanawapeleka nchi za nje. Wakijua kama Marekani ndiyo wanatoa *skill* hii,

wanawapeleka kwa miaka miwili, mitatu. Wakiona wanataka mambo ya magari labda ya Kijerumani wanawapeleka walimu kule, yaani wana *specialization* na kuona *priority* ya nchi yao iko kwenye kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sisi Tanzania tungesema kule Mwanza tuna pamba, tunataka tu-*process* pamba yetu ili tusiuze *raw materials*; mwalimu wa amali anatakiwa ajue ku-*change* ile pamba atengeneze nyuzi atengeneze nguo. Je, sisi tumefika huko? Chai, alizeti, kahawa na madini yetu. Kwa hiyo, unakuta wenzetu India, Japan na China wameendelea maana waliandaa walimu wao wale ambao ndiyo wataenda kufundisha kwa muda mrefu na kwenye *priority areas* zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wameangalia, kwanza; mwalimu lazima apate maslahi mazuri, akae vizuri ili atulie asiweze kufanya kazi kwa papara, atulie. Ile inatoa *impression* kwa wanafunzi kuona kumbe ualimu ni kitu kizuri, kumbe mkondo wa amali ni mzuri zaidi kuliko mikondo mingine. Halafu madarasa yale hayatakiwi yawe yamejaa wanafunzi. Mafunzo ya amali yanatakiwa wanafunzi 20, 30 wakizidi sana 40, ambayo sijui sisi ndiyo itakuwa hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mwalimu akujue mwanafunzi kwamba *skill* hii kweli umeweza kui-*master*? Kama hujaweza, apate muda wa kukufundisha vizuri, kwa vile kinachotakiwa *at the end of the day* ni tija, siyo mwanafunzi ametoka tu and *then what*? Kwa hiyo, inakuwa kwamba darasa lazima liwe *manageable*, dogo, ambalo linafanya mwalimu amjue mwanafunzi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni maabara, karakana zile, lazima ziwe na *equipment* za kutosha. Kwa mfano sasa hivi, ukiangalia vyuo hivyo vya miaka ya 1947 ni tofauti na sasa. Sasa hivi *aspiration* ya wanafunzi wetu ni mambo ambayo yamekwenda kidijiti, sasa tunawarudisha kujifunza mambo ya matofali na kuranda au tunawapeleka kusoma nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo inatakiwa nayo ijulikane ili zile maabara na zile karakana ziwe *equipped* na *modern equipment* na mwanafunzi apate nafasi ya kuzitumia, ku-*practise* ili aweze ku-*master*. Lingine, ku-*change mindset* ya watu wetu. Sijui ni kiasi gani mimi mzazi nikiambiwa mwanao sasa tunataka aende kwenye ufundi nalikubali kuliko labda apite hapa aende *university*. Maana bado *mindset* zetu ni mwanangu amalize na yeye awe na *degree*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayo ndiyo mambo ambayo tunatakiwa tujiulize na kuona tumejiandaaje. Kwa nini tuwe na *crash program*? Tunakimbia wapi? Miaka yote hii tumeharibu elimu ya ufundi zikafungwa zile shule, *I don't know* zilifungwa au zilifanywa nini lakini tuseme basi zikafa. Sasa hivi kwa nini tuanze kama *crash program*? *Me, I would say* inatakiwa tu-*take time* na tuanze kwenye *small scale* ili tuangalie tunakoelekea ni wapi. Hiyo itatupa *roadmap* ya kwamba tunaelekea wapi na tuweze kujiongeza kidogo kidogo *as* tunavyo-*gain experience*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme hivi, *much as* kweli naipenda hii, mimi nilipokuwa nafanya *Danish Embassy* miaka hiyo tulianzisha hii *VETA*. Tulivyoanzisha hizi *VETA* kitu cha kwanza ilikuwa, nafikiri miaka hiyo hata Wizara ya Elimu hakuna ambaye ana umri wangu bado yupo Wizarani pale. Tulivyoanzisha hii *VETA* kitu cha kwanza ilikuwa walimu wafundishwe, wajue na waelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili, wanafunzi walivyopelekwa kwenye masomo yale kuliwekwa fungu pembeni kwamba mwanafunzi akishamaliza yale masomo yake apate vitendea kazi. Apate *equipment* ili akatumie ile *knowledge* yake. Sasa kama hakuna, mwanafunzi amejifunza, amepata hizo *skills*, sasa akirudi nyumbani anafanya nini? Anawezaje kununua *machinery equipment* ili afanye zile kazi? Au bado anaenda kwenye kuajiriwa? Kwenye viwanda vipi ambavyo hatukumwandaa wala hatukuweka hivyo viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba wazo ni zuri sana na nalipenda sana, lakini naona tunafanya kama *crash program*.

Sasa *crash program* na sisi tuki-*crash* kama nchi, niambie. Kwanza, *image* ya wananchi, wazazi, kwamba watoto wamepelekwa, ametoka ujuzi wake ni *half-cooked*, hana mtaji. Maana hatuja-*tie* hapo hii *idea* kwamba wakapewe *equipment* siyo rahisi kwa kila mtu *but at least* ungetegemea tuwe tumefikiria mpaka na *banks* ambazo zitawasaidia hawa wanafunzi wakitoka waweze kununuliwa *machinery equipment* ambapo watafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema, *exposure* ni *very important* kwa walimu wetu. Waelewe, wajifunze na vitu ambavyo kwa kweli vitakuza uchumi wetu *more than business as usual… (Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hitimisha, kengele ya pili.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu kusema kwamba mimi kwa kweli najua wamefanya kazi nzuri sana Wizara, ninachoomba tuanze taratibu tusije tuka-*crash*. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni ambao wapo kwenye ukumbi wetu jioni hii.

Wageni 61 wa Mheshimiwa Rose Busiga pamoja na Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, hawa ni Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) kutoka Wilaya ya Chato, Mkoa wa Geita, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Beatrice Chandika. Hebu tuwaone wako wapi hawa? Naomba msimame. Karibuni sana, ahsante. *(Makofi)*

Tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Mipango, Jijini Dodoma. Karibuni sana, ahsante. *(Makofi)*

Nimwite sasa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Ndege na Mheshimiwa Rehema Juma Migilla ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Elimu. Awali ya yote niwapongeze wanafunzi wa Chuo cha Mipango walioko hapa kwa sababu nilikuwa Rais wao 2010/2011. Kwa hiyo nawapongeza, waendelee kusoma vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Elimu, kimsingi wanafanya kazi nzuri. Wamezungumza Wabunge wengi hapa, nami nilikuwa napapasa, naona maprofesa wote wako Wizara hii. Wote, yaani ile tunaita *software* wote wako huku. Kwa hiyo, tunaamini hii Wizara itaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza upungufu wa elimu katika nchi hii, inawezekana watu wasielewe. Inawezekana tunazungumza tu lakini ukweli ni kwamba nchi yetu imekuwa na matabaka ya elimu. Kuna watu wenye elimu nzuri na kuna watu wenye elimu mbaya. Huku chini, sisi Wabunge, tunachaguliwa na wananchi ambao asilimia kubwa wana watoto wao wanasoma kule chini. Siku hizi hakuna dawati, watoto wengi wanakaa chini. Majengo ya shule za msingi yamezeeka, ni ya muda mrefu, walimu hawapatikani, sasa tunafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa najiuliza, hivi mbona kuna dharura ya mafuriko kwenye mito na kwenye barabara? Kwani hakuna dharura kwenye elimu? Leo nimekuja kivingine, ingawa Wizara hii inafanya kazi, lakini niko kivingine. Nimechukua kati ya shule 125 za Halmashauri ya Bunda, nimechukua *sample* ya shule nane tu na nime-*site* somo la hesabu. Katika somo la hesabu shule inaitwa Makongoro iko jimboni kwangu, watoto waliomaliza *form four* waliopata *B* ni wawili tu, waliopata *C* ni tisa, waliopata *D* ni 12 na waliopata *F* ni 145. Maana yake ni kwamba waliofeli kwenye hilo somo la hesabu ni 86% *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Nyamang'uta waliopata *B* ni sifuri, hatuzungumzi habari ya *A* hapana, *B*, sifuri. Waliopata *C* ni watatu, waliopata *D* ni tisa na waliopata *F* wapo 74, sawa na 86% waliofeli somo la hesabu. Shule ya Salama, waliopata *B* ni sifuri, waliopata *C* nane, waliopata *D* ni saba na waliopata *F* ni 116, wana 88%. Shule ya Hunyari, waliopata *B* ni sifuri, waliopata *C* ni wawili, waliopata *D* ni watano na waliopata *F* ni 111, waliofeli ni saw ana 94%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Chamuriho, waliopata *B* ni sifuri, waliopata *C* ni watatu, waliopata *D* ni watatu na waliopata *F* ni 116, wana 95%. Shule ya Msingi Mikomarilo aliyepata *B* ni mmoja, waliopata *C* ni wanne, waliopata *D* ni wanne na waliopata *F* ni 68, sawa na 88%. Shule ya Mihingo aliyepata *B* ni mmoja, *C* ni mmoja, *D* ni mmoja, waliofeli 58 kati ya wanafunzi 61; maana yake waliofeli ni 95%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Esperanto ya nane, aliyepata *B* mmoja, waliopata *C* watano, waliopata *D* saba, waliofeli ni 104, sawa na 88%. Sasa, jumla hizo shule nane zina wanafunzi 876, waliofeli 788, hiyo ni 90% na walioshinda ni 10%. Hayo ni kuanzia *grade B*, *C* na *D*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hali ndiyo hii, kwa nini hatutoki hapa? Kwa nini tunapeleka watoto shule wanaenda kukaa? Kwa hiyo nchi yetu sasa hivi ina watu wanaoenda kusoma, hawa ni wa *private sector* na wengine; na kuna watu wanaenda kuhudhuria shule, basi ndiyo tumetokea hapo. Kuna watu tunapeleka kuhudhuria shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki mbili zilizopita nimekutana na mwanafunzi mmoja aliyefeli *form four (o-level)*, aliyekwenda akamaliza mtihani, akajiunga na JKT, akachukuliwa polisi, akasoma polisi, akashinda mafunzo yote, akaajiriwa kazini, akashindwa kulipwa mshahara; hajapata cheti, kwa sababu inaonekana alipata sifuri na hapewi cheti. Sasa huwa najiuliza kama *form four* matokeo ndiyo haya na vyeti havitoki na amekaa miaka minne, ukiongeza miaka saba ya *primary*, halafu hatuwapi

cheti kwa nini? Tuwape hivyo hivyo, kama ni *F* zote tuwape, kuna kitu gani sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi nani alaumiwe kati ya mzazi au shule au sisi Serikali? Nimekupa mtoto wangu shule mimi sijasoma, umfundishe, anapata F zote humpi cheti, polisi wanamchukua wanasema hawezi kulipwa mshahara kwa sababu hana cheti cha *form four*, tunafanyaje? Kwa hiyo, Profesa Mkenda hii kazi ni ya kwake. Bahati nzuri ana wataalam wote, Naibu Waziri wake mtaalam, Makatibu wake wataalam, viongozi wake wataalam, watafute namna ya kujitoa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *option* ya kwanza; hoja siyo kuwapeleka watu wafundishe halafu ndiyo tuajiri, hapana. Hoja ni kwamba sasa tutangaze nafasi ya masomo ya sayansi, *biology*, *physics*, *chemistry* na *mathematics*. Hata huo msingi, tutangaze nafasi hizo tuwaite wanafunzi wenye vipaji ambao wanaelewa masomo hayo tuwape mafunzo ya miezi sita au mwaka mmoja halafu tuwapeleke shuleni. Hilo litakuwa linasaidia sana. Hilo ni jambo la dharura, tutangaze watoto wapo wanaoweza kufundisha, tuwapeleke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tuwe na sheria sasa ambayo zamani ilikuwepo ya *internship* kwamba, kila anayehitimu *certificate*, Stashahada na Shahada, wanaomaliza eneo hilo waende wakafundishe mwaka mmoja kabla hawajapewa kazi, iwe ni sheria maalumu. Kwa namna hiyo basi, tutapata wanafunzi wengi watakaoenda kufundisha huko na tukaokoa wanafunzi wetu, kwa hiyo, itakuwa hoja nzuri sana kwenye jambo hili la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere; namshukuru Mheshimiwa Rais ametoa hela nyingi kidogo za kusaidia kile chuo, lakini tangu 2014 hiki chuo kimekaa muda mrefu sana. Tulitaka chuo kikijengwa, matawi yake yaende Bunda, Serengeti, Tarime na Rorya. Bahati nzuri kuna hospitali ya Kongwa imejengwa pale, tunataka tawi la Chuo cha Afya liende pale Hospitali ya Kongwa ili tupate elimu ya afya kwa maana tawi

la wapi? la Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, nafikiri kwamba hiki chuo nako twende tukafanye hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo ya wanafunzi, leo nikisema wanipe nafasi ya kuamua, mikopo ya wanafunzi, nitakachokifanya ni kupata wanafunzi wenye sifa za kupewa mikopo, lakini wote nawalipia karo, wote nitawalipia karo. Nitakwenda kupunguza habari ya matumizi, hiki kitu kinaitwa *boom*, mimi nimekaa chuoni, nimeona wanafunzi wanaopewa *boom* ni matatizo! Wanafunzi wote wanaopata *boom* wana matatizo makubwa, hawasomi, wana nidhamu mbaya, wanalewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitakachokifanya ni kuwalipia wanafunzi wote wenye sifa za kupata mikopo, tunawalipia wote wapate mkopo kwa maana ya karo, tunawalipia karo, tukimaliza tunapunguza matumizi ya hapa, ikiwezekana, hata kama mtu hawezi kupewa matumizi, mzazi wake hawezi kushindwa kumsaidia. Watoto wengi wanapata shida ya kupata mkopo, wanahangaika hawana karo, kinachowasumbua ni karo siyo *boom*, ni karo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tufanye maamuzi ya kutosha tulipe karo kwa wanafunzi wenye sifa, halafu wengine wale wote tuwape hela kidogo, kama hawezi kusaidiwa na mzazi wake, anajisaidia mwenyewe anavyojua lakini asome, mbona wengine walikuwa wanasoma bila karo. Kwa hiyo, nafikiri kwamba tufanye hivyo, ili jambo ambalo tunalizungumza liende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, ukienda shule za msingi, wanadai *printer*, wanadai kompyuta. Ukienda sekondari, wanadai, Waheshimiwa Wabunge tuko hapa tunadaiwa kompyuta. Kwa nini Serikali isiamue, ikaamua shule za msingi zote tukawapa ile sijui inaitwa *canon* ambayo ina-*print* na kutoa *photocopy*, shilingi 2,500,000. Kwa nini tusiamue shule za msingi zote tukawapa, tukatafuta andiko tukawapa wote, tukawapa na kompyuta moja, kwa nini tusifanye hivyo? Kuna haja gani, kuna hii

shilingi 235,000,000 tunayotoa kwa ajili ya elimu bure, tuiangalie vizuri inakaaje, inamsaidia nani kwenye jengo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hela tunatoa za karo, siyo kwamba elimu ni bure, hapana! Hela zile zilikuwa zinalipwa na wazazi, sasa wanalipa Serikali, hela zipo, tuangalie hizi hela zina faida gani kwenye maeneo haya? Tuwalipie hawa watu tuwape kompyuta na tuwape hiyo *printer* ili waweze kufanya kazi kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Mkenda na watu wote waliokuwa kwenye Wizara ya Elimu, nimeshawaomba sana *VETA*. Nimesikia mnajenga shule za ufundi, sijui shule gani, nimesikia Waheshimiwa Wabunge wengine wanasema kwamba shule hizi zimekuwa nyingi, tuweke tumalize zilizopo, hapana! Watanzania wako wengi sana, maeneo yameongezeka, maeneo ni mengi, wajenge hizo shule, kitu cha msingi watuletee na walimu kwenye hizo shule. Kwa hiyo naomba sana, kwenye kipande watakachokitoa hiyo keki, Jimbo la Bunda Vijijini waliweke ili liweze kufaidika na hiyo keki ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniphace Getere. Namwita sasa Mheshimiwa Regina Ndege, atafuatiwa na Mheshimiwa Rehema Migilla na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi ajiandae.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii Bajeti ya Wizara ya Elimu jioni ya leo. Kwanza naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, ameamua kuleta mabadiliko katika jamii yetu, ameweza kuleta mabadiliko kwa kuamua kwamba, ili Taifa lako liwe endelevu, ni lazima wananchi wako wapate elimu. Hilo Mheshimiwa Rais ameonyesha kwa vitendo kwa kufuta ada kutoka elimu ya awali mpaka kidato cha sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, Mheshimiwa Rais aliona ni nafuu kuwapunguzia gharama wananchi wake, amekwenda kujenga madarasa katika shule zetu za sekondari pamoja na msingi. Leo hii, wanafunzi ikifika Januari, wote wanaenda shuleni bila kuwabughudhi wanachi. Hivyo, Mheshimiwa Rais ana dhamira ya dhati ya kuleta mabadiliko ya kweli katika jamii hii ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara ya Elimu kwa kuleta mabadiliko ya mtaala. Mabadiliko haya ya mtaala ilikuwa ni kilio cha muda mrefu kwa wananchi wa Tanzania. Tumekuwa tukiongea mara wa mara hapa Bungeni, hatimaye leo limeenda kutimia. Wizara hii naipongeza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake, wamefanya kazi kubwa sana, mabadiliko haya ya mtaala yameshirikisha makundi tofauti tofauti, kila kundi limeweza kutoa maoni na hatimaye tunaendelea kutoa maoni ili kuendelea kuboresha huu mtaala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoboresha mtaala, bado naona Wizara hii ina mzigo mkubwa, mabadiliko ya mtaala ili twende pamoja, lazima kuna vitu Serikali iende kuwekeza katika mambo mbalimbali. Moja, mtaala huu umeanza kutekelezwa lakini bado tuna mapungufu makubwa ikiwemo vifaa vya kujifunzia. Mfano, leo ni mwezi Mei tunazungumza, lakini shule zetu nyingi vitabu vya kiada bado havijafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi bado wanatumia vile vitabu vya zamani katika kujifunzia. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara, inapoenda kuleta mabadiliko, kwa mfano mwakani tunapokwenda kuanza mwaka wa masomo, lazima Wizara ijiridhishe kwanza kwamba vitabu vya kiada vimeandaliwa mwaka mmoja kabla ya mwaka wa masomo. Badala ya kwenda kuanza mwaka wa masomo vitabu havionekani, wanafunzi wanaendelea kusoma kwa kutumia vitabu vya zamani. Hivyo, hatutaenda sambamba na mabadiliko ya mtaala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mheshimiwa Waziri hapa ameeleza kwamba mafunzo yanatolewa. Nasema tu

kwamba, mafunzo haya yanayotolewa ni kwa kundi dogo sana hasa Walimu. Leo mafunzo yanatolewa kwa Walimu Wakuu, Walimu wa Taaluma, ni walimu watatu kwa shule moja. Sasa, kuna Walimu hasa wanaofundisha yale masomo bado hawajapata haya mafunzo. Kuna walimu wanaofundisha darasa la tatu, hawajapata haya mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mabadiliko yataenda kwa kasi? Naomba sasa Wizara iangalie kwamba, kuna haja ya kutoa mafunzo kwa Walimu wote, ikiwezekana walimu watoe kwa *session*, mafunzo yatolewe kwa *session* kwamba walimu kundi hili wanapewa mafunzo kwa wakati huu mpaka walimu wote wawe wamefanikiwa kupata yale mafunzo ili tuweze kwenda pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia iangalie, tunaenda kwenye mabadiliko haya ya mtaala mpya, je, tumejipangaje? Leo tuna darasa la tatu, tuna darasa la nne, darasa la tatu wanakwenda kumaliza wakiwa darasa la sita, lakini darasa la nne wanakwenda kumaliza wakiwa darasa la saba. Hili kundi linakwenda kukutana *form one* wote kwa pamoja. Je, Serikali imejipangaje na huu mzigo? Madarasa ya kutosha yapo? Tuna Walimu wa kwenda kuwafundisha hawa wakifika *form one* kwa pamoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kutakuwa na mgawanyiko kwamba wengine wataenda kwenye elimu ya amali, lakini bado kuna wale watakaobaki kwenye elimu ya kawaida. Je, walimu wetu wanatosheleza? Madarasa yetu yanatosheleza kuwa-*accommodate* hawa wanafunzi tulionao? Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo Wizara inatakiwa iendelee kuumiza vichwa kwa ajili ya kuona kwamba mabadiliko haya yasibaki kwenye maneno, mabadiliko haya yaende kwenye vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, bado mabadiliko ya mtaala yaende sambamba na maslahi ya Walimu. Tukibaki kwenye mabadiliko ya mtaala bila kuangalia maslahi ya Walimu, tutakuwa hatuendi mbali. Walimu ndiyo watendaji wakubwa,

ndiyo wanaoenda kufundisha, ndiyo wanaokwenda kutekeleza huo mtaala, tusipowaangalia Walimu kwa kuangalia maslahi yao ikiwemo madaraja na posho zile za kujikimu kwenye mazingira magumu, bado tutakwenda kufeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu, ukichukua matokeo leo ya shule za msingi, mfano, shule za msingi za vijijini pamoja na shule za msingi za mjini tofauti utaiona ni kubwa sana. Hii ni kwa sababu shule zetu za msingi za vijijini, kwanza mazingira yao bado ni magumu, ukirudi, hata Walimu hawapo kule shuleni, tofauti na shule za mjini. Leo shule za msingi kuna shule zina Walimu watano, lakini wana darasa la kwanza mpaka la saba, halafu eti unataka ile shule ya msingi ifanane na shule ya mjini, ni kitu ambacho hakiwezekani! Kwa hiyo, tusipoangalia, huu mtaala utabaki mtaala wa mjini na siyo wa vjijini. Kwa hiyo naomba sana, Wizara ya Elimu na Wizara ya TAMISEMI washirikiane katika kuhakikisha shule za vijijini zinapata walimu wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, mazingira ya vijijini pamoja na ugumu wake, Walimu wengi wakipangwa katika shule hizo, wanakwenda kuripoti na mwisho wa siku wale walimu wanaondoka kwa sababu ya ugumu wa maisha hivyo, Wizara ione namna ya kuwamotisha walimu wa vijijini, tuwapatie posho ya mazingira magumu, wale walimu wakipatiwa posho ya mazingira magumu, ataona utofauti wake na walimu wa mjini walau yeye wa kijijini anapata posho ya mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, hata shule zetu za mjini, kuna Walimu wanapangwa kwenye shule moja labda ni walimu wa *history*, wanakuwa walimu wengi mfano walimu saba wanakuwa kwenye shule moja. Hawa walimu saba wanagawana vipindi kwa maana kwamba wanapewa *topics*, lakini kuna mwalimu anafundisha *Physics*, akafundisha *form one* mpaka *form four* yeye peke yake. Huyo mwalimu hawezi kujiona kama yuko sawa na mwenzake kwa sababu mishahara wanalingana. Basi naomba sana wizara iandae motisha walau wapate zile

*teaching allowance* ili mwalimu yule apate moyo wa kuendelea kufanya kazi na kuona hii kazi bado ni kazi nzuri kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wangu wa Manyara, nashukuru Serikali ilileta Chuo cha Walimu cha Mamire. Chuo hicho kilianzishwa mwaka 2014. Wakati chuo hicho kinaanzishwa, kilichukua walimu kutoka shule za msingi na sekondari, walimu saba wameenda katika shule hiyo, lakini mpaka leo ninapozungumza, Walimu wale tayari wameshachukuliwa na Wizara ya Elimu, wako chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Walimu wale hawajapewa stahiki zao kama vile kubadilishiwa muundo wa utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, waliangalie hili, wale walimu wapewe stahiki zao, muundo wao wa utumishi ubadilike kutoka kwenye Ualimu na kwenda kwenye Ukufunzi ili walau wapate moyo wa kuendelea kufanya kazi, badala ya kubaki na daraja lile lile la mwanzo walilokuwa nalo, Walimu wale wanakata tamaa na kujiona kwamba wamefika sehemu ambayo siyo sehemu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la utafiti katika vyuo vikuu. Ukiangalia katika vyuo vikuu, Wahadhiri wetu wengi wa vyuo vikuu, wamekuwa wakifanya utafiti kwa gharama zao, lakini baada ya kuweka machapisho, ndiyo Serikali inakuja kuwapa motisha. Naomba Serikali iandae bajeti kwa ajili ya kuwatazama Wahadhiri wengi wa vyuo vikuu ili waweze kufanya utafiti, wawezeshwe kwa kutengewa bajeti ili wakafanye utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya utafiti, tutaona matatizo mengi yamepungua kwa sababu wataalam wetu watakuwa wanajishugulisha na utafiti. Wapo wataalam wazuri lakini wanashindwa kufanya utafiti kwa sababu tu hawana Fungu. Kwa hiyo, naomba Bajeti ya Wizara ya Elimu, iangalie namna ya kuwawezesha hawa Wahadhiri ili waweze kufanya hiyo kazi ya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala hili la uhamisho kwa upande wa wanafunzi hasa naongelea suala la shule za *private*.

Mfano, mwanafunzi anapokuwa *form one* mpaka *form two*, akishafanya ule mtihani wa *form two*, sasa ikitokea yule mwanafunzi, mimi mzazi nimempeleka mtoto wangu shule za *private*, lakini amefika *form two* anakwenda *form three*, nimeshindwa kuendelea kumsomesha katika shule za *private*. Kinachotokea ni nini, unapoenda kuomba uhamisho kumtoa pale kwenda shule za Serikali, uhamisho haukubaliwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali haioni kama inamyima yule mtoto fursa ya kwenda kuendelea na masomo wakati huo ikijua kwamba mzazi wake amefilisika au yule mfadhili wake hana uwezo tena wa kuendelea kumsaidia yule mtoto. Kwa hiyo, jambo hili liangaliwe kwa jicho la pekee kwa sababu litaendelea kuleta matabaka kwamba mtoto ambaye anasoma shule za *private*, aonekane kundi ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linawezekana kwa sababu lilishawahi kutokea wakati wa kuomba mikopo ya elimu ya juu, wanafunzi waliosoma *private* walikuwa wanatengwa na wale waliosoma shule za kawaida wanatengwa, lakini limerekebishika. Hili linawezekana kwamba mtoto anapoomba sasa uhamisho kwenda shule za sekondari za kawaida za Serikali, aruhusiwe kwa sababu kwanza ni Mtanzania, lakini Serikali ya CCM imetoa elimu bila ada. Kwa hiyo mtoto huyu apewe nafasi ili aweze kuendelea na masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia kipindi hiki kifupi, miaka hii ya karibuni, kwamba msimu wa mvua wanafunzi wengi wamekuwa wakipata shida sana hasa shule zetu ambazo zinatumia *school bus*. Hata watoto wanaotembea kwa miguu, kipindi hiki uliona kwamba watoto wengi walipoteza Maisha, lakini na wengine walipata majeraha. Naomba, Wizara ifikirie namna ya kuangalia upya mihula yetu, kwa sababu gani, sioni kama kuna ulazima, *otherwise* tuambizane kuna ulazima kwamba mihula iwe mwezi Juni na Desemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama siyo lazima, Serikali ione namna ya kubadilisha mihula yetu ili walau msimu wa mvua, kama mwaka huu ilivyotokea, basi watoto wawe likizo na kipindi

ambacho siyo cha mvua basi watoto waendelee na masomo. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, ajiandae.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kushukuru nami kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu kwa jioni ya leo. Pia nianze kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara ya Elimu, Katibu Mkuu Dada yangu Profesa Nombo na viongozi wote ambao wako kwenye Wizara ya Elimu. Kiukweli mnafanya kazi vizuri, tunaona mabadiliko makubwa sana kwenye hii Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kuna mabadiliko hasa na mafanikio. Kuna uongezekaji wa bajeti kwenye Wizara ya Elimu mpaka tumefikia shilingi trilioni 5.9, siyo kidogo, pia tumeona hata utegemezi wa wizara kutegemea hela za wafadhili kwenye miradi ya mendeleo, kiukweli tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea suala la elimu, ni dhana pana sana, suala la elimu haliwezi kukamilika kama hakuna vitu kadhaa. Kwanza kama hakuna Walimu, hakuna elimu, kama hakuna wanafunzi, hakuna elimu. Kama hakuna vifaa vya kujifunzia, hakuna elimu. Pia miundombinu mingine ndiyo suala zima la elimu linapokuwa limekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutakwenda kuanza utekelezaji wa mitaala mipya ambapo tumeona mwaka huu 2024 tumeanza utekelezaji wa mtaala mpya kwa kuanza na elimu ya awali, darasa la kwanza, darasa la tatu, *form one* na hivi Juni au Julai tutaanza kidato cha tano. Hili ni wazo zuri sana, ni wazo jema sana lakini naona kama tumewahi sana japo tumethubutu ila

tumewahi sana. Kwa nini, nasema hivyo, nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Elimu.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Shangazi.

**TAARIFA**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa Taarifa mzungumzaji anayeendelea kuchangia bila kuathiri mchango wake, usahihi wa bajeti ambayo wanaomba ni shilingi trilioni 1.9 na siyo shilingi trilioni tano kama ambavyo ametamka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema Migilla, umeipokea Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Shangazi?

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimeona kama hili suala tumelianza, lakini pasipokuwa na maandalizi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Nikianza kwenye suala la vitabu, kwa mujibu wa sera zinavyotaka na uboreshaji wa mitaala, mwanafunzi kitabu kimoja kinatakiwa wasome wanafunzi watatu, lakini mpaka sasa *ratio* ya usomaji wa kitabu ni kitabu kimoja wanafunzi watano. Tunaona bado suala la vitabu ni shida. Pia bado hata hao walimu ambao wataenda ku-*implement* huu mtaala, hawajapatiwa mafunzo ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema mchangiaji aliyepita, unakuta shule wanapewa mafunzo walimu watatu, Mwalimu Mkuu, Mwalimu wa Taaluma na mwalimu mwingine.

Hawa wote ukiangalia na majukumu ya kiutawala waliyonayo, siyo wanaoingia darasani, wanaoingia darasani hawapati mafunzo *effectively*, kwa hiyo bado naona kuna shida hapo, lakini bado kuna suala la madarasa pia, madarasa haya bado hayatoshelezi idadi ya wanafunzi wanaotakiwa kusoma, bado mrundikano wa wanafunzi ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, napenda kuishauri Serikali na wizara, kwa sababu tumedhamiria kuingia kwenye huu mtaala mpya, ni lazima tuwe tumejipanga kibajeti ili kuhakikisha sasa haya matarajio ya Watanzania, wazazi kwa ajili ya maendeleo ya watoto wao ya kesho, lazima bajeti iwe ya kutosha. Vitu hivi havitekelezeki ni kwa sababu kuna uhaba wa bajeti. Hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri Mkenda, anapokwenda ku-*windup*, atuambie mipango yake ni ipi ili hili jambo lisiwe kama ni *crash program*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwenye elimu ya amali, idadi ya shule za sekondari, zipo takriban 6,000 lakini kwenye hotuba yake inaonyesha elimu ya amali imeanza kwa shule za sekondari 96. Ndani ya hizo 96, ni shule 28 tu ndiyo za Serikali na shule 68 ni shule za *private*. Kwa hiyo, tunaona kwamba je, hawa ambao sasa hivi wanasoma mfumo wa awali, ambao wako *form one* na hawa wengine ambao shule takribani 5,904 hizo hazisomi mafunzo ya amali na kuna wanafunzi kule waliokuwa wanatamani waende kusoma kwenye mafunzo ya amali. Sasa je, hili kundi kubwa kutoka kwenye hizi shule ambazo hazijaanza haya mafunzo ya amali, mkakati wao ni upi ili kuhakikisha na wenyewe matamanio yao ya kusoma mafunzo ya amali yanatimia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona uwekezaji mkubwa umefanywa na *private*. Shule ziko 6,000 lakini in *short,* sita tu ndiyo zimeanza huu mpango, ina maana hatuko *serious.* Hapa nimwombe Mheshimiwa Waziri kwenye hili kundi kubwa, huko nje wazazi wanajua kabisa watoto wao wameanza mtaala wa mafunzo ya amali na jamii inajua hivyo, lakini kumbe ni shule chache tu ambazo zinakwenda kusoma huu mfumo wa amali na kuna watoto wanatamani kabisa wasome huko. Nimwombe sana

atuambie bajeti au mpango ni upi ili lile kundi kubwa wasiachwe nyuma kwenye huu mfumo wa mafunzo ya amali.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa mzungumzaji hata shule ambazo zimeanza hayo mafunzo ya amali na mtaala mpya, hawajapelekewa vitabu. Vitabu walivyopelekewa ni njia ya *soft copy* na wakaambiwa wazalishe wenyewe ili waweze kufundishia kitu ambacho hakiwezekani. Kuna shule za vijijini: Murongo, Kitwechenkura, Nkwenda na maeneo mengine hawana hata umeme wanawezaje kutoa *copy,* walimu hawajawezeshwa halafu wakaweza ku-*implement* huo mtaala.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema Migilla, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Anatropia unaipokea?

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili kwa sababu ndiyo nilikuwa naelekea huko. Kwa hiyo, nimwombe Waziri Mheshimiwa Mkenda pamoja na nia nzuri sana, kama hatatafuta fedha mahali katika hiki kitu, tutakuwa tuna-*mark time* na tutakuwa tunawadanganya wananchi huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili ambalo nitalichangaia leo, ni kuhusu masuala ya *VETA*. Tumeona kuna harakati kubwa sana ya ujengaji wa *VETA* karibu kila wilaya, ni wazo zuri sana, lakini hii kasi ya ujenzi wa *VETA* ni lazima iende sambamba na walimu wa kutosha. Pia, ni lazima watuwekee hata *course* ambazo zinaendana na soko la ajira. Bado hizo *course* ambazo zinafundishwa huko ni lazima ziangalie mazingira halisi ya wananchi au wanafunzi huko wanapokaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta *course* nyingi za sasa hivi zinazotolewa kwanza nyingi ni *outdated,* hazifanyi kazi. Hata *course* za muda mfupi nazo bado hazina mvuto kwa wanafunzi wetu. Leo hii mtu anayejifunza udereva huko mtaani au ufundi huko mtaani anakuwa na utofauti mkubwa sana na yule ambaye anasoma *VETA,* tena anafundishwa na walimu wenye umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nifahamu, *VETA uniqueness* yao ni ipi mpaka iwavutie hao wanafunzi wetu waende *VETA* na wasijifunze huko kitaa? Kwa sababu unakuta sasa hivi hata madereva wengi hizi *short courses* za udereva wanakwenda kujifunza kule mtaani kwenye *garage* huko, anakuja *VETA* kwa ajili ya kupata cheti tu. Sasa napenda kufahamu; hivi *VETA* kwenye *course* ya udereva wapo kwa ajili tu ya kutoa cheti au vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko *VETA* hata vifaa vya kutosha hakuna. Unakuta mtu anajifunza udereva, anatoka hapa Bunge mpaka anafika Kimbinyiko anaambiwa shuka anapanda mwingine. Kwa hiyo tuweke vitu ambavyo vitakwenda kumpa kweli ujuzi kulingana na kile alichokitarajia siyo huu ujanja ujanja uliopo sasa hivi. *VETA* haivutii lakini bado *VETA* nyingi ambazo tunazijenga kwa sasa, zinakuwa tu ni majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejitahidi *well and good* lakini haya majengo ili yawe na thamani na watu waone hizi jitihada za Serikali ni lazima vianze kazi. Kuna *VETA* zimejengwa huko leo zimeshaweka nyufa, zimeshaweka kila kitu, zinaonekana zimechoka na kuchoka kabla hazijaanza kutumika. Nimwombe ni bora tujenge *VETA* chache ambazo zitakuwa zina vifaa, kila kitu na walimu wa kutosha. Wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali watakuwa wanaenda pale na wapate kile ambacho tunahitaji kuliko kutuwekea *VETA* nyingi ambazo hazifanyi kazi kwa sasa. Hiyo kitu itakuwa haina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye hizi *course* za muda mfupi tuangalie soko la sasa likoje? Sasa hivi kuna uhitaji mfano wa wafanyakazi wa ndani waweke kule, *saloon* na kila kitu. Kila

kitu sasa hivi ni *business* na watu wanataka *course* za muda mfupi wakatengeneze hela huko kwenye soko la ajira. Naomba sana haya mambo yazingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala lingine, nimeona katika bajeti huku; kwenye maelezo ya Waziri tumeona kwenye Kamati kwamba Bajeti ya Elimu ya Juu inachukua 60.3% ya *total budget* ya Wizara ya Elimu. Sasa kama ni 60% peke yake inakwenda kwenye mikopo ya elimu ya juu, asilimia kidogo inayobaki ndiyo inakwenda kufanya shughuli nyingine za kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kusema kwamba wanafunzi wasipate mikopo, lakini napenda kufahamu, hivi kweli kama asilimia zote hizo tutakuwa tunapeleka kwenye mikopo, je, hii Wizara itakuwa ni ya mikopo? Shughuli zingine haziendi kwa sababu tumewekeza hela nyingi huko na tunataka watoto wetu wasome. Je, kuna mpango mkakati gani wa baadaye ili kuhakikisha kwamba hii Bodi ya Mikopo inajiendesha yenyewe ili isiathiri bajeti ya Wizara nzima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo ni aibu eti mashuleni huko hakuna vyoo kwa sababu bajeti kubwa inakwenda kule. Karne ya 21 tunazungumzia matundu ya vyoo? Hapana, nimshauri Mheshimiwa Waziri, hii Bodi ya Mikopo tunaomba sasa kiwe ni chombo ambacho kina fungu lake maalumu, kiwe kina *vote* yake kabisa kisimame chenyewe kama chenyewe. Pia, haya marejesho ya kwenye Bodi ya Mikopo tunaomba yawe ni *revolving,* kwa sababu hata hatujui marejesho yanarejeshwa kiasi gani tangu imeanza kutoa mikopo hatuelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuombe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema, muda wako umeisha…

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani taarifa zilikuwa nyingi, hujanilindia ndugu yangu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba hitimisha…

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kabudi na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango wangu katika hoja ambayo iko mbele ya Bunge lako Tukufu. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda kwa kazi nzuri sana ambayo anaendelea kuifanya katika Wizara hii, pamoja naye Naibu Waziri Mheshimiwa Omari Kipanga, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na kwa ujumla watumishi wote wa Wizara hii hasa kwa kazi hii nzuri sana ya uboreshaji ama uhuishaji wa mitaala ambao wameufanya kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama zipo changamoto basi ndiyo tuko hapa kwa ajili ya kushauri, lakini lazima tuwape shime kwamba wamefanya kazi nzuri na tunaamini kwa kuwa Maprofesa ni watu ambao wanapokea changamoto basi na hizi ambazo tutaziwasilisha, atazipokea na kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nauanzia pale ambapo Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray ameishia kuhusu namna ya kutazama upya mfumo wetu wa elimu kwa maana ya muda wa masomo, lakini pia na nyakati. Ni kweli kwamba mwaka huu tumekuwa na mvua ambazo zimeathiri kiasi kikubwa sana utoaji wa elimu na zimewafanya wazazi wawe katika mihemko ama kuwa katika hofu pindi watoto wanapokuwa wanaenda shuleni hasa kwa kipindi hiki cha mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuone namna ambavyo tunaweza tukatazama kwamba kuna likizo ile fupi ya mwezi wa

Machi kwenda Aprili, tukaipanga upya kwa sababu mvua za masika huwa ni za kila mwaka zinajulikana zinaanza wakati gani. Japokuwa mwaka huu ni mvua za *El Nino* ambazo zilitabiriwa kwamba zitakuwa nyingi lakini kwa kuwa kiasili kipindi hiki cha mwezi Machi kuanzia tarehe 22 kwenda mpaka mwezi Aprili katikati kunakuwa na mvua, basi tuangalie namna ambavyo tunaweza tukaboresha kuwa na kipindi cha likizo ambacho kinaweza kikatuondoa katika hizi hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo mvua za vuli mwezi Desemba huwa hazina athari kwa upande wa taaluma kwa sababu shule zinakuwa zimefungwa. Kwa hiyo ni jambo la kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine sambamba na hilo ni kutazama muda wa masomo na hapa niungane na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwamba kuna umuhimu pia wa kupunguza idadi ya masomo hasa kwa madarasa haya ya mwanzoni. Pia, kupunguza hata vipindi, hawa watoto tunawachosha sana na kwa bahati mbaya sana shule zetu hazina miundombinu hata ya viwanja vya michezo kama ilivyokuwa zamani. Kwa hiyo watoto wanaamka alfajiri saa 11 anafika shuleni saa mbili anaanza masomo. Atakaa huko mpaka saa 11 au saa 12 anarudi hata muda wa kucheza hana kiasi kwamba hata ule ukuaji wa ubongo unakuwa na matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani ni lazima watoto waamke saa 11 alfajiri? Hivi hatuwezi tukatengeneza utaratibu mpya kwamba hawa watoto angalau labda waanze kwenda shuleni kuanzia saa moja, saa mbili ili saa tatu ndiyo masomo yaanze halafu yaende angalau mpaka saa tisa? Hii itasaidia hata katika Miji na Majiji kuondokana na ule muda wa asubuhi ambako kuna foleni kubwa na jioni pia wanawahi kutoka kabla ya zile foleni nyingine. Kwa hiyo watoto wanakuwa wanacheza katika muda ule ambao bado hakujawa na msongamano mkubwa. Hii itasaidia pia kwamba wanapata na muda wa kupumzika jioni wanavyorudi na wanaweza wakashiriki katika masomo mengine hasa ya kidini na kuweza kupata fursa pia ya kujua maeneo mengine hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo sasa nataka nichangie ni eneo la uanzishwaji wa Sera hii ya mwaka 2014. Kwa bahati wakati ule ilikosa bajeti ya kuisukuma na hata mwaka 2023 ni kama tu tumeongeza maeneo machache hasa eneo la mtaala. Sera hii sasa itakumbana na changamoto zifuatazo za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Sheria ya Elimu inayosimamia Elimu ni ya mwaka 1978 na ikafanyiwa mapitio kidogo mwaka 2005. Kwa hiyo bado kuna maeneo ambayo ina matobo, ni lazima ifanyiwe ukarabati wa haraka. Sera mpya inatamka kwamba elimu ya lazima iwe mpaka kidato cha nne, lakini sheria iliyopo inatambua na kutamka kwamba darasa la saba ndiyo elimu ya lazima. Kwa hiyo tayari hapo Sera na Sheria vinakinzana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija upande pili Sera mpya inataka na inatambua kwamba shule iwe na mikondo ya elimu ya taaluma na amali, lakini ukienda kwenye sheria inatambua kwamba mikondo ya elimu ni sayansi na sanaa na siyo taaluma na amali. Maana yake kwa mfano mtu mwenye shule ya binafsi leo akitaka kusajili shule atasajili kwa sheria ipi? Maana Sheria ya zamani inakinzana na Sera iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Sheria ya zamani inatambua lugha ya kufundishia shule za msingi kuwa ni Kiswahili. Sera mpya sasa inatamka kwamba lugha ya kufundishia kwa shule za msingi itakuwa Kiingereza na Kiswahili, kwa hiyo tunaona kwamba tayari kuna mapishano. Sheria ya zamani inatambua kwamba upimaji wa mitihani kwa mujibu wa sheria ni mtihani wa darasa la saba walikuwa wanahitimu, lakini sasa kwa sera mpya inazungumza kwamba darasa la sita atakuwa anapimwa aende kwa sababu atatakiwa aende mpaka kidato cha nne siyo kuhitimu tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hapo utaona kwamba mtihani wa darasa la sita ni sawa na ule wa darasa la nne ni kwamba tu ni wa kupima kuelekea sekondari ambayo sasa ni ya lazima. Kwa hiyo ningeshauri kwamba Sera tumeipata, mkakati wa Sera upo, lakini sasa tutazame eneo zima hilo la sheria na

yenyewe wailete tuifanyie maboresho ili iweze kwenda kutekeleza Sera ambayo tumeipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ningezungumzia kidogo kwenye sekta binafsi ya elimu. Hapa tunataka Wizara itusaidie kujibu maswali kwamba sekta binafsi ya elimu ni biashara ama ni huduma? Maana yake yapo mambo ambayo yanafanyika yanaonekana yapo kibiashara zaidi wakati hawa wanasaidia kutoa huduma katika elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi tunazo shule 6,362 zinazoendeshwa na sekta binafsi ya elimu. Kati yake za awali ziko 2,364; za msingi ziko 2,270; na sekondari 1,728. Shule zote hizi zina wanafunzi zaidi ya 1,020,772 kutoka awali hadi kidato cha sita. Maana yake kwa idadi ya shule hizi ukienda kufuata ule utaratibu kwamba kila wanafunzi 40 ni chumba cha darasa, Serikali ilipaswa kuwa na vyumba 25,500 ku-*accommodate* hawa wanafunzi, lakini kundi lote hili limechukuliwa na Sekta Binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuone kabisa kwamba kuna mzigo ambao kama siyo sekta binafsi ya elimu lingekuwa ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba eneo hili kunakuwa na miundombinu. Kwa hiyo tusiitazame kama biashara, tuitazame kama wasaidizi wa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya walimu kwenye sekta binafsi ni zaidi ya 159,000. Hawa maana yake zisingekuwepo wangekuwa mtaani, lakini leo wameajiriwa na bado kuna ajira nyingine za madereva, ma-*matron, patron* na kadhalika. Kwa hiyo tuitazame kwa jicho la huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna Sheria moja ya Serikali za Mitaa kifungu cha 22(1) ambacho kinaondoa taasisi za elimu ambazo zimesamehewa kulipa tozo zozote kwa mujibu wa Sheria hiyo ya Serikali za Mitaa, lakini bado zipo halmashauri zinaenda kutoza *service levy* kwenye hizi shule za binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unashangaa kwamba TAMISEMI anamiliki shule za msingi hizi ambazo tunaziita za umma. Huyo huyo ndiye halmashauri ambaye anaenda kutoza *service levy* kwenye shule binafsi. Hii sheria haikutaja kwamba zitozwe binafsi ama za Serikali, imetaja tu kwamba wadau wote wa elimu hawatatozwa hiyo. Kwa hiyo kwa nini binafsi wanatozwa? *Of course,* tunajua Serikali hailipi kodi lakini kwa kuwa *service levy* ni ushuru wa huduma na huduma zenyewe ndiyo hizo kujenga matundu ya vyoo, kujenga madarasa na kadhalika na hawa tayari wameisaidia Serikali katika eneo hilo, tukiwatoza hapa ni kuwanyanyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo natamani kuona Wizara inasimamia eneo hili vizuri. Ifike mahali pia ile mamlaka ya elimu inayosimamia elimu ya msingi iwepo ili ile haki ionekane kwamba na TAMISEMI nayo ni mdau katika elimu, siyo kwamba yeye kuna wakati ni *referee,* lakini pia wakati mwingine anacheza, inakuwa kwa kweli haileti usawa. Kwa hiyo hilo ni jambo la msingi sana, tulitazame katika maeneo hayo ili kuhakikisha kwamba Sekta Binafsi ya Elimu tunaichukulia kama ni sehemu ya huduma na siyo sehemu ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa mchango wangu, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi ajiandae.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu rahim kwa ruzuku ya uhai na afya. Pia nikushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuzingatia kwamba elimu ndiyo msingi wa kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujikita katika maeneo mawili la Elimu ya Juu na Maarifa ya Asili *(indigenous knowledge)* na teknolojia ya asili *(indigenous technology)*. Kabla ya kuingia

katika maeneo hayo mawili nami nichukue nafasi hii kupongeza kabisa hatua ya mitaala mipya. Tunazungumzia mitaala mipya tu, mimi kubwa ni kwamba tangu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipochukua maamuzi makubwa ya kuitoa elimu ya lazima kutoka darasa la nne kwenda darasa la saba na kufuta utaratibu wa *primary schools* na *middle schools,* leo tunafanya tena mabadiliko makubwa kuitoa elimu ya lazima kutoka darasa la saba kwenda kidato cha nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndilo kubwa sana na ni lazima tuliseme kwa sauti kubwa. Hizi changamoto zote zilikuja hata wakati wa mabadiliko hayo na wako waliomshutumu Mwalimu kwamba anashusha elimu kwa kufuta *middle school* na kuanzisha elimu ya msingi kwenda mpaka darasa la saba. Kipindi kile cha mpito ndugu zangu hakikuwa chepesi, tuliendelea kuwa na shule za aina mbili; wale walioenda *middle school* na wale ambao hawakwenda *middle school.* Katika shule hiyo hiyo ya msingi akaanzisha darasa la tano, la sita na la saba zikaitwa *extended primary school. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukawa na *extended primary school* na *middle school.* Darasa la saba la *extended primary school* likafanya mtihani pamoja na darasa la saba la *middle school* na darasa la nane la *middle school* na ndiyo ukawa mwisho wa *middle school* na leo neno *extended primary school* tumelisahau. Naamini katika kipindi cha mpito tutakuwa na *extended secondary school* ambazo baadaye hizo *extended secondary school* ndizo zitakuwa *high school* katika kila Kata. Kwa sababu sasa kila shule itakuwa na darasa la kwanza mpaka kidato cha nne na naamini shule za kata za leo ndiyo zitakuwa *high school* za kesho kwenye kila kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko yoyote yana changamoto nyingi. Sisi tumefundishwa kidato cha kwanza na cha pili na walimu wa *grade A* kutoka *middle school.* Siamini kwamba elimu yetu ilifubazwa kwa kufundishwa na walimu waliotoka *middle school* kufundisha *form one* na *two* kwa sababu walimu walikuwa hawatoshi baada ya elimu ya sekondari kuongezwa. Kwa hiyo napendekeza tuendelee na hili.

Changamoto zitakuwepo, lakini ndiyo ziwe chachu ya kuongeza kasi ya mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo nipendekeze tu, somo moja libadilishwe jina lake. Somo la *sports* (michezo) libadilishwe liitwe sayansi ya michezo *(sports science),* kwa sababu wanafunzi hao watasoma *physiology, anatomy, psychology, nutrition,* ili watu wasiseme ni michezo tu. Iwe ni sayansi ya michezo *(sports science)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nije kwenye elimu ya juu. Ni muhimu sasa baada ya mabadiliko makubwa haya ya elimu ya lazima pia tuje na mtazamo mpya katika elimu ya juu. La kwanza, katika elimu ya juu ambalo nalipendekeza ni kuja na utaratibu wa ukuruba wa taaluma. Zipo taaluma leo ambazo zinaonekana hazipo karibu, lakini zipo karibu na wenzetu wameanza kuyafanya hayo. Wenzetu siku hizi hawazungumzii *multidisciplinary* au *interdisciplinary,* wanazungumzia *transdisciplinary* (ukuruba wa taaluma).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana leo ukienda Chuo Kikuu cha Nairobi au Chuo Kikuu cha Makerere, Idara ya Sanaa za Ubunifu *(creative arts),* zipo pamoja na uhandisi na teknolojia. Kwa sababu mwanafunzi wa uhandisi wa nguo *(textile engineering)* atasoma *textile design* na *Textile design* ni somo ambalo ni la *creative arts*. Mwanafunzi leo anayesoma muziki atatumia ala nyingi za kiteknolojia. Ndiyo maana wenzetu sasa wamekwenda kwenye ukuruba wa taaluma na leo unakuta *creative arts* ipo kwenye *college of science and technology*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanze kulifikiria hilo ili watu waone huo ukuruba wa taaluma…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Kabudi, hebu tueleze ukuruba maana yake ni nini? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuruba ni ukaribu wa mambo yasiyofanana lakini yanafanana katika kutajirishana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ndiyo maana anaitwa Profesa, endelea.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, lazima sasa pia tuwekeze katika taaluma na lugha za kiafrika. Tumeanza kuamua kwamba Kiswahili sasa kitakuwa lugha ya Afrika Nzima, maana yake tutakuwa na Kiswahili cha Nigeria, Senegal, Afrika Kusini na kote huko. Lazima baadhi ya vyuo vyetu sasa vitabahali *(specialize)* katika taaluma na lugha za kiafrika. Zianze kufundisha lugha ya Kihausa, Kizulu na Kiwolofu *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1976 mtu anayeitwa Akinwande Oluwole Babatunde Soyinka, ambao wengi tunamfahamu kama Wole Soyinka, ndiye aliyesema kwamba lugha ya Kiswahili itakuwa lugha ya Afrika na watu walimbeza. Leo lugha ya Kiswahili imekuwa ni lugha ya Afrika. Ili tutajirishe Kiswahili katika msamiati wake na katika istilahi yake tuanze kuwa na taasisi za taaluma za Afrika na lugha za kiafrika na baadhi ya vyuo vitabahali *(specialize)* katika eneo hilo. Kwa hiyo, tuwe tuna ukuruba lakini pia tuwe na utabahali katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maarifa ya asili. Hili ni eneo la utajiri mkubwa katika Bara la Afrika na Tanzania, lakini kwa ajali kabisa ni eneo ambalo tumelipuuza na leo tunapoteza maarifa ya asili yetu yote yanakwenda kuhifadhiwa Marekani na Ulaya. Sisi tunayapuuza wao wanakuja kuyachukua. Leo hawaji kuchukua tu mimea dawa, wanakuja kuchukua maarifa hayo. Ndiyo maana leo ukienda sehemu nyingi ambazo zinauzwa dawa za asili, utawakuta vijana wengi kutoka Marekani na Ulaya, ambao kule wanasoma somo la *medical anthropology*. Wanayachukua maarifa hayo na wanakwenda wanayatunza na kuyabadili kuwa mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika vyuo vikuu vyetu tumeng'ang'ania ku-*publish*. Tume-*publish* na tume-*perish*. Wenzetu wame-*patent* na wame-*prosper*. *We have published and perished, they are patenting and prospering from our own local indigenous knowledge. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tubadilike na tubadilike vipi? Nitatoa mifano miwili tu. Sasa hivi Uswisi wanaandaa dawa ya kutibia kifafa na mimea hiyo wameitoa Tanzania. Mmea wa *Cussonia zimmermannii* na sasa wanaandaa hiyo dawa. Chuo Kikuu cha Basel, Chuo Kikuu cha Bern na *Swiss Institute of Tropical Medicine*. Maarifa haya wameyatoa kwa wataalam wa tiba ya asili wa Kinyamwezi. Baada ya hii dawa kutoka madaktari wetu wote watakuwa na fahari ya kuandika dawa hiyo, kwa sababu sasa imetolewa na viwanda vya dawa vya Uswisi, ilhali maarifa hayo na mimea hiyo ya *Cussonia zimmermannii* imetolewa hapa. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Marekani kwa kutumia mmea ambao umetoka kwetu wa *phyllanthus engleri* wanatengeneza dawa ya kutibia saratani. Kwa hiyo, sasa wanachukua mimea dawa na wanachukua maarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tuige mfano wa India. India leo wanakwenda anga za juu, wametua kwa mara ya kwanza katika ncha ya kusini ya…

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu 10 ambazo umenitaja niombe Profesa aendelee nazo. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, unaitwa Katani sijakutaja hapa. *(Kicheko)*

Profesa endelea.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa hiyo, napendekeza katika hili tujifunze kutoka India. India pamoja na mwaka jana kurusha chombo cha Chandrayaan ambacho kimetua katika ncha ya kusini ya mwezi, hao hao India ambao pia wana *Indian Institute of Space Science and Technology*, pia wana *Center for Indian Indigenous Knowledge.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza baadhi ya vyuo vyetu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na vyuo vingine vianzishe taasisi au *centre* ya *indigenous knowledge*. Twende tujifunze India na China. Pia tuanzishe *traditional knowledge digital library,* ambayo inaweza ikahifadhiwa na *COSTECH. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia twende kwenye Ilani cha Chama Cha Mapinduzi. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imehamasisha kuanza mashamba ya mimea dawa na kuanzisha kiwanda kikubwa cha dawa za mimea dawa. Sisi ni mabingwa wa kuanzisha taasisi, lakini hatuzilei. Tulianzisha *Institute of Traditional Medicine,* ikajikita kwenye *research* na ku-*publish,* ime-*perish.* Waliokuja kujifunza kwetu, Chuo Kikuu cha Egerton, leo ndicho chuo kimoja ambacho kinauza mimea dawa mingi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuja watu wa Madagascar, na nilikwenda Madagascar kwa jambo fulani ambalo Watanzania wanalifahamu. Wale wenzetu leo wanauza mimea dawa mingi kutoka chuo kikuu chao kule Madagascar. Maarifa hayo wameyatoa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, *science and technology*. Naomba Taifa sasa liwekeze katika *research and development (R&D)*. Tutenge asilimia fulani ya bajeti ya nchi yetu, iende kwenye *research and development* ili tuweze kufanya sisi wenyewe tafiti zetu ambazo zinaendana na mahitaji yetu. *COSTECH* na taasisi nyingine za utafiti zisaidie katika utafiti. Utafiti huo uwe wa aina

zote. Uwe katika sayansi na teknolojia, pia uwe katika mambo ya jinsia sayansi jamii. Kwa kufanya hivyo tutakuwa na sisi tumerudi tena katika nafasi yetu ya kuongoza katika sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ndiyo ilikuwa na wataalam wakubwa wa maeneo ya sayansi ambayo wakati huo hayakuonekana ni ya msingi, lakini bado Serikali ilitoa fedha ya kuwasomesha. Akina profesa Paul Vita, Hasanali na Dkt. Mohamed Billal katika Nyuklia za *Physics.* Pia Dkt. Ally Mohamed Shein katika eneo la *Metabolism* katika mambo ya tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima sasa Serikali pia iwekeze katika maeneo hayo kwa kuongeza Fedha ya *R&D*. Pia kusomesha watu katika maeneo adimu ambayo hao hawawezi kutupa *scholarship,* lakini sisi wenyewe tuweze kuwapa maarifa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi. Namwita sasa Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo ajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo. Awali ya yote niipongeze Wizara, tumekuwa tukifanya nao kazi vizuri kwa sababu mimi ni Mjumbe kwenye Kamati ya Elimu, Profesa hapo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Wizara imesikia kwamba walimu hawajapata mafunzo. Sisi Wabunge ndio tunaishi na walimu huko kwenye majimbo na mikoa yetu. Katika kutekeleza mtaala huu mpya ama ulioboreshwa, tunaambiwa wamepata

mafunzo walimu 181,000; hiyo ni taarifa ambayo tunayo, lakini kiukweli ukiuliza walimu wengi hawajapata mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ione sasa ni wakati muafaka, yasifanyike kama yale ambayo yalifanyika wakati tunahama kutoka *content based* kwenda *competence based,* ikawa imepita juu juu. Hili jambo ni kubwa na kwa hiyo ni lazima Serikali ione umuhimu wa kulitendea haki, walimu wote katika shule zote wapate mafunzo vizuri ili waweze kufanya kazi vizuri. Sisi tunaishi nao tunawauliza, tunaongea nao wanatuambia kwamba hawajapata mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *issue* ya uchapaji wa vitabu. Waliopewa jukumu hilo ni Taasisi ya Elimu Tanzania. Sisi kama Kamati tunaomba fedha za uchapaji wa vitabu ziende moja kwa moja kwa Taasisi ya Elimu kutoka Hazina, zisipite TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimepita TAMISEMI fedha bilioni 17, zimerudishwa hazina kwa sababu hazijatumika. Tunajua kuwa kuna tatizo kubwa sana la vitabu. Kwa nini fedha mpaka zinafikia kurudishwa maana yake hayo ni matumizi mabaya ya madaraka na rasilimali fedha. Kwa hiyo tunaomba fedha zile ziweze kwenda moja kwa moja Taasisi ya Elimu ili ziweze kufanya kazi ambayo imekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mikopo ya elimu ya juu. Najisikia vibaya, nimepata dharura kidogo samahani.

*(Hapa Mhe. Tunza I. Malapo alisitisha kuzungumza kutokana na changamoto za kiafya)*

**MWENYEKITI:** Pole. Naomba mtunzie dakika zake.

Twende kwa mchangiaji mwingine. Nimwite sasa Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia jioni ya leo. Kwanza,

napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kusimama katika Bunge hili la Bajeti ambapo ni mara yangu ya kwanza katika kipindi hiki cha bajeti.

**MWENYEKITI:** Hebu samahani mchangiaji. Naomba watu wa *first aid* waende pale. *(Makofi)*

Mchangiaji naomba uendelee.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maamuzi yake ya hekima, busara na magumu sana ya kuamua kubadilisha Mtaala wa Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuwa kazi ndogo; ni kazi kubwa na jambo kubwa ambalo linahitaji hekima sana, lakini Mheshimiwa Rais wetu ameweza. Nampongeza sana kiongozi wetu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda niwapongeze viongozi wafuatao: Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Makamu wa Rais, pia viongozi wa Wizara hii yote, Mawaziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu. Kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana. Mchakato wa kuanzisha mtaala mpya haukuwa mdogo. Lilikuwa ni jambo kubwa, limeshirikisha makundi mengi, lakini hatimaye sasa tumeweza kufanikisha mtaala huu mpya kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Profesa Kabudi, jambo hili ni kubwa, tangu tupate uhuru haijawahi kutokea katika nchi yetu. Kwa maana hiyo, kile kitendo cha kuanza kwa jambo hili tumshukuru Mungu na ni la kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuleta maendeleo lazima tukubali mabadiliko. Mabadiliko kuna wakati ni ya lazima. Hatuwezi tukakubali kubadilika kimaendeleo, ni lazima tufanye

mabadiliko ya mambo fulani. Iwe kwa kheri au kwa shari lakini mabadiliko yafanyike ili tuendelee mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mtaala limefanyika, lisingefanyika tusingejua wapi pana mapungufu. Limefanyika sasa na tunaona, walimu kweli wanatuambia kwamba bado elimu ile ya mabadiliko haijawafikia kikamilifu. Haijawafikia kikamiilifu kwa sababu gani? Wameenda kuwezeshwa walimu wachache, walimu wakuu na wao wamekuja kuitoa elimu ile kwa walimu wenzao wa shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mapokeo yanatofautiana. Muda wa elimu ule ulikuwa ni mchache, wengine wamefanya siku moja kabla ya kufunguliwa shule, wengine siku tatu. Kila watu walifanya katika utaratibu wao katika shule yao. Jambo hilo limeleta ugumu katika mapokeo ya walimu. Sasa niombe Serikali iandae mazingira ya kuwapa walimu elimu ya huo mtaala mpya. Niombe, Serikali ina vituo vyake vya walimu *(TRC)*. Zile *TRC* Serikali iziwekee mkazo kwa kuziwekea fungu la fedha ili vituo vile vitumike katika kutoa mafunzo ya walimu kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kwanza vituo vile vinakuwa katika mazingira yale yale kwenye halmashauri zao na kwenye wilaya zetu. Sasa ile inakuwa rahisi kwa walimu kwenda pale kupata mafunzo mafupi mafupi katika vituo vile. Kwa hivi niiombe Serikali itenge fedha na iviboreshe. Kuna halmashauri zingine, kwa mfano sisi Dar es Salaam tunavyo, viko Ubungo, Temeke, Ilala na maeneo yote lakini havina ubora. Hata mashine ya kufotolea karatasi *(photocopier machine)* hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo niiombe Serikali iwekeze katika vituo vile na hasa katika kipindi hiki ambacho tunakwenda kufanya maboresho ya mitaala yetu ili kama kuna mafunzo ya aina yoyote walimu waitwe, wafanyiwe semina ndogo ndogo mambo yaende mbele. Ni lazima tukubali mabadiliko na twende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie tena kwenye upande wa vyuo vikuu. Naipongeza sana Serikali yetu, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 wametoa takribani bilioni 6.9. Wanafunzi wanufaika 73,078, si jambo dogo. Fedha hizi ni nyingi na zinakwenda kwa wanafunzi wetu kwa lengo la kuwafanya wapate elimu. Hata hivyo bado kuna changamoto, mikopo hii vijana wengi haiwatoshelezi. Wapo wanaopata 30%, 20% au 40%. Utakuta haitoshelezi, isipokuwa inaweza wakati mwingine ikatosheleza kwa ada. Tatizo ninaloliona kwenye baadhi ya vyuo wale *dean of students* hawatoi elimu sahihi kwa wale watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utamkuta mtoto yale mafao aliyopata yanamtosha kabisa kulipa ada, lakini hapewi maelekezo, labda andika barua kwa Mkuu wa Chuo na nini, wanaachwa tu, tunasumbuka. Hivi hapa tumepumzika, bado hawajaanza hawa *form five* wanaotoka. Tukija Bunge lingine hapa mtihani hapakaliki hapa ndani. Ukienda kule unaenda mpaka unamfikia Mkuu wa Chuo. Hawa wengine wanafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wale wametoka huko, wengi wametoka mazingira tofauti, hawaelewi wafanye nini, lakini anajiona nimepata mkopo ila hautoshelezi. Sasa, matokeo yake mtu ambaye haelewi, hana mtu wa kumpa mawazo kwamba wewe hii hela inaweza ikakusomesha kwa ada, familia yako ikahangaika kukukimu tu kwa chakula, wanaacha na chuo chenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo nataka niliseme na naiomba Wizara itufanyie tafiti, tumetoa hizi shilingi bilioni 6.9 kwenda kwa wanafunzi. Je, wanafunzi wangapi waliweza kumaliza mwaka wa kwanza? Nataka kujua wanafunzi wangapi wanaweza kuelekea mwaka wa pili. Wanafunzi wa vyuo vikuu wengine wako mitaani, wameshindwa kumudu maisha, wameshindwa kumudu hiyo ada nyingine amekaa. Serikali inampa mkopo huyo huyo lakini hasomi. Sasa, tunafanyaje? Lazima tuangalie kama kweli Serikali imeamua kutaka kuwasaidia hawa vijana, basi tuwafuatilie, zile ni fedha za Serikali. Mheshimiwa Rais wetu anahangaika kuwatafutia hizi

fedha watoto wake wakasome vyuo vikuu lakini tunafika sehemu watoto wanashindwa kumaliza vyuo vikuu na hela ya mikopo inaenda, atarudisha na nini huyu kijana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, naiomba Serikali ikaangalie hawa wanafunzi, wangapi wanakwenda kusoma, wangapi wanamaliza mwaka wa kwanza, wangapi wanamaliza mwaka wa pili na wa tatu pia. Kwa sababu, lengo ni watoto wasome, kama hawasomi tuangalie au tuone namna gani hawa watoto wanashindwa na tuwasaidieje ili waweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu katika kujenga *hostel*, changamoto ya *hostel* kwa wanafunzi wa vyuo vikuu hasa baadhi ya vyuo, ukitoa Mlimani kidogo kuna nafuu lakini vyuo vingine, ukienda *IFM* yale makundi ya watoto wanaoelekea Kigamboni wanajaza ile pantoni nzima. Inaenda huku kivuko kinarudi na wanafunzi lakini wanafunzi wale kuna wengine walianza shule za msingi na miaka mitano, sita, anafika chuo kikuu ana miaka 16; utamkuta mtoto yuko mtaani kile kipindi ambacho wanakuja kusajiliwa kwenye vyuo vikuu mpaka unaona huruma. Unaona huyu mtoto anaweza kupata dhara lolote kwa muda wowote kwa sababu umri wake hautaki, bado alikuwa anahitaji malezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nawaomba wale Wakuu wa Vyuo wanaosema kwamba yule wa mwaka wa kwanza akianza kidogo ana nafasi ya kupata *hostel* ya chuo lakini yule wa mwaka wa pili aende kule mtaani, hapana. Waangalie, waangalie na yule mtoto ana umri gani? Siyo kwamba mwanafunzi yeyote aliyefikia chuo kikuu kwa sasa hivi ni kwamba ni mtu mzima, mwingine bado hajafikia ule umri wa utu uzima. Anakwenda kukumbana na mambo makubwa huko mtaani, anakwenda kukumbana na vijana wahuni, anakumbana na mabaa, yaani anakumbana na vurugu zote za maisha kiasi kwamba yule mtoto Mungu amsaidie asiweze kuingia kwenye mabaya, lakini anaweza kupata ushawishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na uwezo wa Serikali kugharamia ile mikopo, kama mtu hajafikia lile lengo alilokusudiwa ni kazi bure. Naiomba Serikali tena na tena na tena, waweze kuangalia *hostels* za wanafunzi. Kule Kigamboni sisi tumekuwa muda mrefu na lile jipu lilipo la ule Mradi wa Dege. Jamani pale kulikuwa na kijiji, wangewakusanya wanafunzi wote wa vyuo hata Dar es Salaam nzima, wangeweza kujaa pale. Hivi kwa nini mradi ule haukuchukuliwa au haukununuliwa na Wizara ya Elimu, tukatengeneza *hostel* hawa wanafunzi wakawa wanatoka katika vyuo, *IFM*, Mwalimu Nyerere nini ambao wanakosa *hostel*. Tunawaelekeza kwenye eneo moja la uangalizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru jamii inatusaidia, wanawaweka hawa wanafunzi, lakini hata wao wenyewe jamii ile ambayo inawapangisha hawa wanafunzi na wao wanakumbana na changamoto kubwa sana na vijana wetu, ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, Serikali hatuwezi kulikwepa hilo, hawawezi kulikwepa, lazima waangalie jinsi gani tutawasaidia vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine wameelekeza kwamba ndiyo tumejenga sekondari na sekondari zipo lakini bado kwenye hizi sekondari nyingine taaluma inashuka kutokana na miundombinu ya usafiri. Katika Wilaya ya Kinondoni utakuta pale kuna Shule ya Sekondari ya *Mbezi Beach*, iko pale kwa Zena, hakuna hata daladala moja inayopita hapo *Mbezi Beach* kwa Zena, hakuna. Watoto wale wanabebwa kwenye vibajaji, kwenye pikipiki, kwenye lifti, hivi hawa maisha yao na hasa mtoto wa kike yanakuwaje kwa mpango huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Shule za Pemba Mnazi, Mbezi na Makabe, shule zile hazina *hostel* na hata *hostel* zilizopo za shule za pembezoni bado hazitoshelezi, kwa hiyo, tuangalie hata tunapojenga hizi shule, Serikali ishirikiane na mamlaka za usafiri kuhakikisha kwamba angalau daladala inapita. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile eneo la *Mbezi Beach* siyo eneo yaani la kusema mtoto atapata usafiri wa kirahisirahisi na watoto

wale wanatoka Manzese, Ubungo, Mabibo na kwingineko, wanaenda pale, asubuhi utashangaa wanavyofikafika pale shuleni kila mmoja, huyu ana bajaji, huyu sijui bodaboda, huyu mwingine sijui ameomba lifti. Sasa hivyo tunajenga usalama wa watoto wetu au tunabomoa usalama wa watoto wetu? Tuangalie, kama kuna uwezo wa *hostel* zijengwe ili kuboresha elimu na taaluma. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna, basi mamlaka zile zinazohusika zielekeze usafiri kwa wanafunzi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha. Bahati mbaya taarifa haiwezi kutolewa wakati mchangiaji amemaliza.

Nimwite sasa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu na mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Ally Kassinge ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii nyeti ya elimu. Awali ya yote, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Profesa Mkenda pamoja na timu yake yote ambayo inajitokeza pale kwenye ukurasa wake wa kwanza wa Hotuba yake ya Bajeti, pamoja na wengine wote walioko nyuma yao

katika kuhakikisha kwamba Sekta hii muhimu ya Elimu inakwenda vizuri kama ambavyo wanaipeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli lazima tu niseme kwamba wenzetu hawa wameaminiwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu elimu ndiyo kesho ya Taifa letu. Nchi zote ambazo zimeendelea, mojawapo ya mikakati ambayo imewapeleka mbele ni Sekta ya Elimu tu. Ndiyo ambayo ina mchango mkubwa sana katika kuipeleka jamii mbele au kuifanya jamii isiende mbele. Kwa hiyo, nawapongeza kwa jinsi ambavyo wanaifanya kazi hii vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Kamati husika. Mwenyekiti wetu wa Kamati ametusomea taarifa nzuri na ameisoma vizuri sana kiasi ambacho inafanya michango yetu iwe mifupi. Ukurasa wa 97 – 155 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, unazungumzia mwelekeo wa utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Fungu 46 ambapo imeweka vipengele vitano (a) – (e). Vyote ni muhimu lakini nigusie tu kipengele kile cha (e) juu ya suala la utafiti *(research)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nagusia kipengele hiki kwa sababu utafiti ni suala ambalo linahusika moja kwa moja na suala zima la maendeleo endelevu katika sekta zote za uchumi na za jamii katika Taifa lolote lile. Kwa hiyo basi, nishauri kwamba, ni vema Wizara ingeongezewa uwezo mkubwa kabisa kwenye upande wa utafiti ili iweze kuwa na Waratibu wa Tafiti zote nchini. Hii itasaidia pasiwe na urudufishaji ile *reduplication*. Kurudiarudia suala hilo hilo likafanyia *research* mbalimbali labda kutokana na *donors* lakini kukawa na uratibu wa Wizara, itakuwa ni rahisi kwamba sehemu ambayo imeshafanyiwa utafiti isirudiwe tena, tafiti ziende vizuri. Pia, tukifika hapo Wizara kama ya Mipango iweze kuzitumia tafiti hizo katika kupanga mipango ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mafunzo ya Amali ni moja kati ya mambo ambayo yanarudisha matumaini makubwa sana katika nchi yetu. Ni jambo muhimu na siliogopi kwa sababu nilikuwepo zamani sasa nimerudi. Kubwa la kujiuliza tu ni kwamba,

tulikosea wapi mpaka likatuponyoka? Kwa harakaharaka tu nadhani kwamba hatukuwekeza vya kutosha. Kipindi hicho utakuta kuna shule yenye Mchepuo wa Ufundi, kuna ya Kilimo, Kijeshi na kadhalika, lakini nadhani wanafunzi walipoongezeka uwekezaji haukwenda sawasawa na idadi ya watu. Kwa hiyo, ndiyo maana tukafeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri tunaporudi sasa tufikirie umuhimu wa kuwekeza zaidi katika kuandaa walimu wa kutosha na wenye uwezo kama ambavyo baadhi ya watu wamechangia. Pia, kujenga karakana za kutosha zenye vifaa vya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitegemei tena patasi na nyundo ndiyo zitawale katika Shule zetu za Amali. Naamini kwamba tuna vifaa vya kisasa zaidi pamoja na kwamba hata hizo patasi na nyundo hatutaki kuzipoteza kwa sababu bado zinatumika vijijini katika mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia Chuo cha Usafirishaji ambapo awali tulikuwa tunaona kwamba kinafundisha madereva na mambo kama ya *transport management* lakini leo hii wanatoa *Degree* za *Logistics*. Hiyo inaonesha kabisa kwamba, kumbe tuna uwezo wa kuwekeza tukaenda mbali zaidi na tukaendana na kasi iliyoko sasa hivi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia inakwenda kasi sana, mapinduzi ya kidigiti yameifanya dunia hii sasa hivi iwe nyepesi, lakini iwe ngumu kwa wale ambao wataachwa nyuma hasa katika suala hili la akili mnemba *(artificial intelligence)*. Suala hili nadhani tunahitaji kuliundia *task force* ili tusije kubaki nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sisi tunahangaika, leo hii Mbunge unafikiria upate kakompyuta kamoja upeleke kwenye shule au *photocopy machine*, sasa shule za wenzetu zimeenda katika *AI*. Sasa, tukichelewa tukabaki nyuma, kuja kuikamata hiyo treni itakuwa ni vigumu sana kwa sababu ni teknolojia ambayo inapeleka maendeleo kwa kasi sana. Sasa hivi ukienda nchi kama

*Singapore* kuna mahali nilisoma, wanawashawishi hata wazee waliostaafu warudi shuleni wakajifunze *AI* ili wasije wakaachwa nyuma katika Mapinduzi ya *AI* ambayo yataipeleka dunia kwa kasi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani tunahitaji kuwa na *task force* ambayo itahakikisha kwamba tunakwenda na teknolojia hii mpya, nina hakika itaangalia mambo mengi sana. Kwa mfano, sidhani kama mimi ambaye nimesoma Sheria chuo kikuu wakati kitabu cha Megarry *(The Law of Real Property)* kilikuwa kimoja tu pale *special reserve*, una-*skip lunch* ili uwahi kusoma kile kitabu na ukifika pale unakuta alitangulia mtu mkora akasoma akachana zile *pages* akaondoka nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama tuliosoma wakati ule mimi na Mheshimiwa *Attorney General* kwenye mazingira hayo, leo hii muda ule ambao tuliutumia kwa kozi ile, wanafunzi wa leo wanatakiwa watumie muda ule ule wakati ambao *materials* wanazi-*access* kwenye simu na kila mahali. Kwa hiyo, nadhani tunahitaji kuangalia teknolojia inavyokwenda, iturahisishie na pengine itupunguzie hata muda wa kukaa shule. Tupate Maprofesa vijana zaidi, tupate *PhDs* za vijana zaidi kuliko sasa ambapo lazima usafiri safari ndefu ndiyo ufike huko ambako unatakiwa kufika. *(Makofi)*

Mhesimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo ya elimu ya juu limeleta hapa *concern* kidogo kwamba, sehemu kubwa ya bajeti imeenda huko, lakini nadhani hakuna njia kwa sababu uhitaji ni mkubwa na tungependa vijana wetu wote waende shule. Sasa, tufanye nini? Sidhani kama tunahitaji hata kufikiria kupunguza, tunahitaji kufikiria kuongeza bajeti ili kila mwanafunzi apate mkopo, bila kujali huko sekondari alisoma shule ya milioni ngapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la maana ni kuwa na mfumo mzuri wa urejeshaji wa mikopo hii. Kukiwa na mfumo mzuri wa urejeshaji wa mikopo tunaweza kuongeza uwezo ili watoto wengi zaidi wapate. Kwa kweli, hata kama mwanafunzi mzazi wake ana

uwezo wa kumlipia, akifika *level* ya chuo kikuu mwache akope ili aanze kupata *discipline* ya uwajibikaji kuanzia mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, tuongeze bajeti na tukopeshe wanafunzi wote wanaotaka kukopeshwa, lakini mfumo wa urejeshaji wa fedha hizo uangaliwe upya ili fedha ziwe zinarejeshwa angalau 90%. *Defaulters* wawe wachache wachache kwa sababu huwezi ukakwepa vitu kama kifo, ulemavu wa ghafla ghafla na kadhalika, huwezi kukwepa vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la walimu. Rafiki yangu Dkt. Kikoyo amezungumzia zaidi kwenye vyuo vikuu na amezungumza vizuri sana. Lakini shule zetu bado zina upungufu mkubwa sana wa walimu, kiasi ambacho napata mashaka kwamba hata hii mitaala mipya itatekelezwa namna gani. Nichukue tu mfano mdogo sana kwenye Jimbo langu la Mwanga; mahitaji ya walimu wa sayansi ni walimu 283, lakini kwa sasa hivi halisi tuna 199. Kuna upungufu wa walimu 84, ni wengi sana kwa Wilaya ndogo kama ya Mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija sanaa na lugha, mahitaji ni 528 lakini tuna 355, mapungufu ni 173, kwa hiyo, mapungufu haya ni makubwa sana. Maabara, tunahitaji vyumba vya maabara 81 lakini tunavyo 42 tu, kwa hiyo, mapungufu haya yananitia mashaka kwamba, tusipopambana nayo hata jinsi ya kuendesha hii mitaala mipya inaweza itupe tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, wakati tuna uhaba huu mkubwa, bado wapo walimu wengi kuliko hao ambao wamepungua ambao wako mitaani kule kule Mwanga, wanaotoka pale pale Mwanga ambao hawana ajira na wengine wanajitolea. Tungefikiria hili kwamba, wale walimu waajiriwe tu katika maeneo yale yale ili kurahisisha na kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba tuna ajenda yetu ya Utaifa ambayo tungependa watu wachanganyike wa huku waende kule, lakini kwa sasa mambo yameshabadilika. Hata mahali kama Jimboni kwangu Mwanga, hao walimu nafikiri

ni nusu nusu, nusu ni wageni na nusu ndiyo wenyeji wa pale. Kwa hiyo, hata wakiajiriwa pale hakuna tishio kubwa kwamba watu watakuwa wanakaa peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nizungumzie suala la *VETA*. Uamuzi wa Serikali wa kujenga vyuo hivi vya *VETA*, kwa kweli ulikuwa ni uamuzi wa kijasiri sana. Kwa hili namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kushikilia ajenda hii ya kuhakikisha kwamba Vyuo vya *VETA* vinafika kila wilaya, lakini kasi ya ujenzi kwa kweli iko chini. Jimboni kwangu Mwanga Chuo cha *VETA* kilipaswa kiishe mwezi Machi, 2024, imeshindikana, wamepewa *extension* mpaka mwezi Julai, lakini nikiangalia dalili sioni mwezi Julai ile kazi itakamilika, uwezo wa wasimamizi wale ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ningeshauri sana Mheshimiwa Waziri watupie macho usimamizi wa ujenzi wa Vyuo vya *VETA*, vinginevyo nia njema ya Mheshimiwa Rais na kazi kubwa ambayo Wizara imefanya kutawanya hivi vyuo vijengwe kila mahali, inaweza isifanikiwe kwa wakati na ikichelewa basi ndiyo tunaanza kuanguka hivyo kidogo kidogo. Mwezi Julai natarajia kwamba Wanamwanga waone *VETA* yao, lakini nikiangalia dalili zinanitisha, *unless* kama Mheshimiwa Waziri ataingilia kati na umahiri wake ninavyoufahamu kuhakikisha kwamba kazi hii inakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo naunga mkono hoja. Tupitishe bajeti hii viongozi wetu hawa watuletee maendeleo katika Sekta hii muhimu ya Elimu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tadayo. Nimwite sasa Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwigao, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Elimu. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Bajeti ya Wizara hii, kinachonisikitisha hapa ni bajeti naiona ndogo sana, bajeti ya shilingi trilioni 1.9 katika Wizara ya Elimu ambako tunasema

tunakwenda kufufua elimu ambayo tunaona elimu yetu inakwenda kuwa ya chini, halafu tunaweka kiasi kidogo sana cha bajeti kama hapo. Kuna jambo moja ambalo ni kukosekana kwa uwiano katika Bajeti yetu ya Wizara ya TAMISEMI ambayo ni dude kubwa sana, kule elimu iko ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pesa zinazokwenda kwenye elimu ni kubwa sana, ni nyingi, lakini mwenye Wizara yake anapata shilingi trilioni 1.9. Hapa wananipa tabu sana ya kufikiri, najiuliza tunakosea wapi? Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Wizara yake nzima kwa kazi kubwa wanayoifanya. Kwa sababu, maeneo mengi sana ukitaka kufaulu katika elimu lazima uwekeze fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mdau wa elimu zaidi ya miaka 32 sasa hivi, ni kwamba, nimeanza kuwa namiliki shule ya awali mpaka sasa hivi naelekea kwenda katika kuwa na shule ya *advance*. Matatizo mengi sana ambayo nimejifunza kwenye elimu, nimekaa nikawa nafikiri kwamba tunakosea wapi na wapi turekebishe, ni kwamba, nikiangalia maeneo muhimu yote nane yanamilikiwa na Wizara ya Elimu, lakini huyo huyo Wizara ya Elimu kaacha maeneo mengine yanamilikiwa tena na Wizara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Wizara ya Elimu ndiyo watunga sera, ndiyo wenye sera, Sera ya Elimu ya Nchi hii iko chini ya Wizara ya Elimu, Mitaala iko chini ya Wizara ya Elimu, Vyuo vya Ualimu viko chini ya Wizara ya Elimu, walimu wanaandaliwa na Wizara ya Elimu, Baraza la Mitihani liko chini ya Wizara ya Elimu, Idara ya Ukaguzi iko chini ya Wizara ya Elimu, Msajili wa Shule yuko Wizara ya Elimu, Mtungaji wa Vitabu *(Book Management Unit)* wako Wizara ya Elimu, halafu jukumu la elimu anaachiwa mtu mwingine, utamlaumu nani? Nataka Mheshimiwa Waziri aje hapa atueleze kama kote huku wanamiliki wao, hii elimu ni kwa nini wamemwachia mtu mwingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naangalia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tangu naingia kuwa Mbunge hili jambo naliona kabisa na nitaendelea kushauri nikiamini baadaye wataelewa.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni dude kubwa sana, imebeba mambo mengi sana, elimu ya awali - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; elimu ya msingi - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; *o-level* - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; *Advance* - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hao wanafunzi wa chuo kikuu wakitoka huko hawawezi hata kuongea lugha ya Kiingereza wala kuandika barua ya kuomba kazi, halafu watamlaumu nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilizungumza kwamba, *O level* na *Advance* ni lazima Wizara ya Elimu ichukue majukumu yake, huwezi wewe ukatunga mitihani halafu ukampelekea mtu. Nitolee mfano kwangu, Jimbo la Sengerema, lilipata gari la ukaguzi Mwaka 2009, leo lina miaka 15. Ukiangalia bajeti ya ukaguzi tu peke yake, sisi ofisi yetu ya kanda ina gari moja, lakini ndiyo ina kanda nzima, angalia mikoa yote inayoi-*manage*. Haya watawezaje kuja kufaulu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kuboresha elimu yetu ni lazima tuangalie sasa majukumu ya Wizara na Sera zetu tuziangalie sasa, je, tuko sahihi? Akili hii hii iliyoandaa hii mitaala, ikaandaa sijui sera, ikaandaa vyuo, ikaandaa walimu, ikaandaa Baraza la Mitihani, ikaandaa Idara ya Ukaguzi, ikaandaa usajili wa shule, ikaandaa utungaji wa vitabu, sasa akili hiihii ndiyo itumike kurudia kuona kwamba, ni wapi tumekosea tujisahihishe. Huo ndiyo ushauri wangu katika jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kushindwa na bahati nzuri waliopo pale ni Maprofesa, aliyepo kwenye Idara ya Mipango sasa hivi na hata Wizara ya Mipango na yeye ni Profesa; Mheshimiwa Profesa Mkumbo yuko pale, Waziri wa Elimu ni Profesa, kule wamejaa maprofesa na madaktari. Nimekwenda kule *UDOM* kwenye ofisi yao, yaani kila unayemgusa ni Profesa, wanafeli wapi? Mimi ndiyo najiuliza, yaani! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masomo yanayofundishwa kwenye shule zetu za msingi, *o-level* na *advance* ndiko ambako ni lazima uandae, sasa usipoandaa kwenye shule ya msingi vizuri huwezi

kupata huku. Wanafunzi wazuri wote wanaotoka kule wanatoka katika sehemu za ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa mfano mmoja tu, kuna masomo hapa ameyataja Mheshimiwa Nahodha kwamba, tuwe tuna masomo matano, lakini masomo yanayotakiwa yawe saba. Kwa mfano, somo la kwanza labda ni Kiswahili ambalo ndiyo lugha ambayo wanaijua Watanzania. Kule kwenye Kiswahili ni lazima watu wakafundishwe kukijua Kiswahili, lakini huwezi kufundishwa kukijua Kiswahili kama hujui kusoma, kama hujui kuandika. Miandiko ya watoto sasa hivi siyo mizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na madaftari yana mistari wakati huo sisi tunafundishwa na tulikuwa tunapigwa mpaka katika vidole, mtu unaandika. Leo hii, Mungu nisaidie, sijui watu wote watakuwa na *computer,* mtu anachapa, unasema huku anachapa baadaye ana-*print*, je kwenye kuandika itakuwaje? Kwa hiyo, hili liangaliwe ikiwa ni pamoja na Somo la Hisabati, *English,* Sayansi, Historia, Jiografia na somo hili lingine la Maadili. Hili somo la Maadili ni lazima liangaliwe pia, kwa sababu, kule kwenye maadili ndiko kwa muhimu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masomo ya dini sasa hivi kwenye shule zetu hayafundishwi kabisa. Kama tunaweza tukalipa pesa kwenye vyama vya siasa, tunatoa ruzuku, tunashindwaje kuwalipa walimu kama kuna Wachungaji, Mapadri, kule wapo Maimamu sijui, Mashekhe na Walimu wa Madrasa kwenda kufundisha kwenye shule zetu? Kwanza Mwenyezi Mungu atatubariki sana na nchi hii itakuwa na baraka kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi itakuwa na baraka haijawahi kuonekana. Huwezi kumpa mtu elimu halafu akamsahau Mwenyezi Mungu, akashindwa kumjua Mungu wake na pia, huwezi kuwa kiongozi mzuri kama huna hofu ya Mungu, hata wewe Mwenyekiti upo hapo kwa sababu ya hofu ya Mungu. Hofu ya Mungu anaanza kufundishwa mtoto mdogo, kumjua Mungu, ndiyo tunatengeneza maadili katika nchi yetu. Jamani tunakokwenda hali ni mbaya, huwezi kuwajua wazazi, huwezi

kujua chochote kama huwezi kufundishwa hili somo la maadili shuleni. Kwa hiyo, liangaliwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka kuzungumzia suala la walimu. Ni kwamba, tuna vyuo zaidi ya 36 vya ualimu kama sijakosea, tujue kabisa kama ni mwalimu wa *english,* tunajua Serikali imepeleka wataalam Kinampanda au *Butimba TTC,* ndiyo walimu wanaosoma Hesabu, watu waliofaulu *PCM* wanapelekwa Butimba. Tunakwenda kutengeneza walimu tunajua kabisa tunawapeleka *Bunda TTC* kule kwamba, zile ni shule ambazo tunapata Walimu wa Hesabu. Unajua kwamba, kuna shule Kasulu ni Walimu wa Historia, hapo ndiyo tutakapoweza kufaulu kupata walimu, tusipoandaa walimu tutapiga kelele kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu, mwaka jana nilizungumza jambo hili, Mkoa wa Kigoma wanasoma *Oxford*, Mkoa wa Mwanza wanasoma *Mtule and Company*, Mkoa wa Pwani wanasoma sijui *Elimu Supplies*, Mkoa wa Dar es Salaam sijui wanasoma kitabu gani. Kuhusu hili, Wizara ya Elimu ni lazima waliangalie kabisa, ikiwa ni pamoja na suala la maktaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maktaba yetu ya Taifa ina hali mbaya sana na hapa nataka nijue, Profesa ni ndugu yangu, sijui ameshakwenda kuziangalia hizi Maktaba zetu za mikoa na hii ya Taifa iliyopo pale Bibi Titi? Ile Maktaba ina hali mbaya sana, sijui mara ya mwisho imepata bajeti lini Maktaba yetu ya Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia zaidi kwenye Baraza la Mitihani, lakini hatuangalii Maktaba, haiwezekani. Tusipomwandaa mtoto katika shule zetu ili aanze kuyaona mazingira tangu akiwa mtoto mdogo, anakwenda shule ya msingi anajua kuna maktaba, tukijenga tunajenga madarasa tu, tukijenga shule za sekondari tunajenga madarasa, lakini kusema kuna maktaba iko pale, hakuna kitu kama hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapa, naunga mkono hoja. Profesa ana kazi kubwa sana na ndugu yangu ninachotaka

kumwambia ni kwamba, ni lazima aumize sana kichwa, lakini kwa kuwa ana ndugu yake Mheshimiwa Mkumbo, yupo pale, waendelee kufanya kazi kwa Pamoja, nina imani kabisa tutatoboa. Ahsanteni sana, Mungu awajalie sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam. Namwita sasa Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, atafuatiwa na mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Ally Kassinge.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, Hoja ya Wizara ya Elimu. Naanza kwa kusema naunga mkono hoja pamoja na mapendekezo yote ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na suala la jicho la elimu, kwa maana ya udhibiti ubora. Mheshimiwa John Aloyce Kamamba, amesema jicho la Serikali kwenye elimu ni udhibiti ubora. Sasa, ili jicho hili liweze kufanya kazi sawasawa, kufanya kazi kwa utulivu na kufanya kazi kwa ufanisi, tafsiri yake ni wapate vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watengenezewe mazingira bora ya wao kufanya kazi. Maeneo mengi hawa watu wa udhibiti ubora hawana vitendea kazi. Mzungumzaji aliyetoka kuzungumza sasa hivi, Mheshimiwa Tabasam, amesema kule kwao gari sijui ni la tangu mwaka gani huko limenunuliwa mpaka leo, maana yake au tafsiri yake ni bovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine uliohai ni kule kwetu Tunduru, gari la udhibiti ubora lilinunuliwa tangu mwaka 2016, linatengenezwa mara kwa mara, linatumia gharama kubwa kwa ajili ya matengenezo, lakini mbaya zaidi ni gari lile tangu mwaka jana, mwezi wa 11 limesimama kwa ubovu. Maana yake ni kwamba, haliwezi kufanya kazi na kwa tafsiri hiyo ni udhibiti ubora hawana gari la kufanyia kazi na tunasema hili ndiyo jicho la Serikali kwenye elimu, watafanyaje kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tunduru ina eneo kubwa sana na jiografia yake ni mbaya. Wilaya ya Tunduru ina hekta za mraba 18,778, halafu unampa mtu afanye kazi, hana usafiri, anafanyaje kazi? Wilaya ya Tunduru tuna shule za msingi 156, tuna shule za sekondari 31, halafu huyu Mdhibiti Ubora atazitembeleaje hizo shule na hana gari la kutembelea? Namwomba sana Mheshimiwa Waziri kama kuna mpango wa gari, aipe kipaumbele Tunduru, kwa kuwa watu wale wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena yule Mdhibiti Ubora wa Wilaya ya Tunduru anastahili kupewa pongezi. Kama kuna namna yeyote ya kuweza kumpa pongezi yeye pamoja na wadhibiti ubora wenzake, Mheshimiwa Waziri ajaribu kufanya hivyo kwa sababu, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, jiografia ya Tunduru ni mbaya kwenye barabara, lakini pia shule ziko mbali, mbali kweli kweli. Kutoka kwenye Makao Makuu ya Wilaya kwenda kwenye shule nyingine huwa wanatembea mpaka kilometa 120 na hawana usafiri, wanafikaje? Bado wanafanya kazi yao kwa ufanisi, ni lazima wapewe maua yao, wasifiwe na wapongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye udhibiti ubora kuna uhaba wa wadhibiti ubora. Pamoja na wingi wa shule na ukubwa wa eneo lenyewe, lakini wadhibiti ubora wapo sita tu. Tunaomba sana endapo ongezeko la wadhibiti ubora likipatikana, basi Tunduru ipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna suala la mabweni katika shule za sekondari. Kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumepata Shule tatu mpya za Sekondari, Tinginya, Kungu na Majimaji. Pia nyumba za walimu zimejengwa na zimekamilika. Walimu wanaishi kwenye nyumba zao, ni jambo jema sana, lakini ili wanafunzi waweze kupata elimu sawasawa ni lazima kuwe na mazingira bora ya kupata elimu yao. Tunapozungumza mazingira bora maana yake ni miundombinu ya elimu kwa maana ya *hostel* katika zile shule za sekondari, lakini 90% ya shule za sekondari Tunduru hazina *hostel*, nini kinatokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile shule tumesema zijengwe katikati kwa maana ya, kama ni shule ya tarafa basi inajengwa katikati mwa kata zote za tarafa, lakini kama ni shule ya kata inajengwa katikati ya kata. Sasa nini kinachotokea hapo ni kwamba, wanafunzi wanatoka umbali mrefu. Kwa siku moja kutoka nyumbani kwao kuja shuleni na kisha kurudi, kutokana na ule umbali wanashindwa. Tafsiri yake ni wanatafuta mazingira ya kuishi karibu na shule na kwa sababu, shule hazina *hostel* wanafunzi wengine wanalazimika kupangiwa nyumba na wazazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zile nyumba wanazokwenda kupanga ni za mtaani. Unafahamu mazingira ya mtaani, watu hatujafanana akili, yapo mazingira tofauti tofauti sana, tunao walevi, tunao wavuta bangi, tunao watu ambao hawastahili kuishi pamoja na wanafunzi. Sasa unakuta...

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimpe Taarifa mzungumzaji kwa mchango mzuri ambao anaendelea nao. Suala hilo la *hostel* analolizingumzia ndiyo linawakuta wanafunzi wengi sana katika Jimbo la Kibiti wanaotoka maeneo ya *Delta* kuja kusoma Nyamisati na vile vile wanakwenda kusoma pale *Mtanga Delta*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Kungu, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Twaha, je, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili na hili ndilo linasababisha wanafunzi wetu wengi kutotimiza ndoto zao za kupata elimu na wengine wanakatisha masomo yao. Ndiyo maana pia, utakuta kuna wimbi kubwa la wanafunzi kupata mimba wakiwa shuleni kwa sababu

ya mazingira wanayoishi, wangekuwa wanaishi shuleni kwenye *hostel* zao wasingeweza kupata mimba kiurahisi, lakini kule mtaani wanakoishi kwa sababu, wanakutana na wavuta bangi, wanakutana na wavuta unga, wanakutana na walevi, unakuta wanafunzi wengine wanapepesukia kwenye ulevi, wengine wanapepesukia kwenye uvutaji wa bangi. Kwa hiyo, wanashindwa kumaliza elimu zao kwa sababu ya... *(Makofi)*

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Mtemvu.

**TAARIFA**

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa mchango anaoendelea kuchangia Mheshimiwa Kungu, ni mzuri kweli na hasa katika eneo hili la maadili ya watoto wetu. Ndani ya Jimbo la Kibamba kwenye shule nzuri ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameijenga kwa zaidi ya shilingi milioni 400, Shule ya Ukombozi, Kata ya Saranga, ina watoto 1,400 hivi, ikifika saa tano asubuhi, zaidi ya 70% yaani zaidi ya watoto 600 wanakuwa wameshalewa dawa za kulevya na wamelala madarasani. Kwa hiyo, unaweza ukaona hali ilivyo mbaya, siyo tu *hostel,* lakini hata wazazi na jamii ambayo inazunguka shule zetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Kungu, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Issa Mtemvu, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili kwa sababu, huo ndiyo uhalisia. Bila ya shule zetu hizi za sekondari kuwa na *hostel* tunakwenda kupoteza wanafunzi wetu wengi kwelikweli. Kwa hiyo, hili suala la *hostel* lichukuliwe kwa uzito wa aina yake tuhakikishe shule zote za sekondari zinapata *hostel* ili kuweza kuwasaidia wanafunzi hawa kutimiza ndoto zao za kielimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nabaki kwenye suala la elimu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Profesa Adolf

Mkenda. Nimewahi kuona kwenye baadhi ya mikakati yake alikuwa anatarajia ama anataka kupeleka elimu karibu na walengwa, lakini kwenye suala hili la kupeleka elimu karibu kuna suala la elimu ya Kilimo na kule Tunduru tuna tawi la Chuo cha Kilimo kwa maana ya *SUA*. Lile tawi lilifunguliwa mwaka 2018, lakini hadi leo tunavyoongea sijui niite ni nini na wakati mwingine inasababisha kukata tamaa Wanatunduru na hii ndiyo inasababisha hata kuona sisi watu tunaoishi Kusini kwa namna moja ama nyingine jicho la Serikali halitutazami sawasawa. Ni kwa nini nasema hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tawi lile lilianza tangu mwaka 2018, lakini mpaka sasa linafanya kazi kwa mwaka mzima, siku 14 tu. Wanakuja wanafunzi pale kwa vitendo kwa siku 14, lakini halmashauri ilitoa hekari 300, kwa ajili ya kuwapatia watu wa *SUA*, ili kutoa elimu ya kilimo pale, ilitoa majengo ya kutosha kuwapatia watu wa *SUA*, kwa ajili ya kutoa elimu ya kilimo Tunduru, lakini cha ajabu mpaka leo hii chuo kile hakijafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alipotembelea Mkoa wa Ruvuma kwenye ziara yake, alipofika Tunduru alisimamishwa na watu wa Daraja Mbili wakamweleza juu ya uhitaji mkubwa wa Chuo cha Kilimo Tunduru. Aliona maeneo na akatoa tamko kwamba, ifikapo mwaka 2020 chuo kile kiwe kimefunguliwa na wanafunzi wapate elimu ya kilimo pale. Cha ajabu mpaka leo hii hakuna jitihada yoyote inayoonekana kwamba, chuo kile kitafunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisikitika sana sisi watu wa Tunduru, baada ya kuonesha jitihada kwa muda mfupi na jitihada zile zikazimika kama koroboi inayotumia mafuta. Baada ya kuja jitihada zile kuziondosha na kuzipeleka Mkoa mwingine, Mkoa wa Kaskazini na ndipo hapo tunaposema sisi watu wa Kusini tuna nini? Tumekosea wapi? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Naomba uhitimishe mchango wako.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namtaka Mheshimiwa Waziri,atakapokuja ku-*wind up* hapa, atoe neno kutokana na Tawi la Chuo cha Kilimo *(SUA)* Tunduru, ni lini kitafunguliwa kuwa kwa masomo ya muda wote badala ya masomo ya muda ya siku 14?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** … baada ya kusema hayo kama nilivyoanza pale mwanzo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kungu. Nimwite sasa mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Ally Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru nami kwa kunipatia nafasi jioni hii ili niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Elimu. Kabla ya mchango wangu naomba aniruhusu nitoe pole kwa Wanakilwa na Watanzania, ambao mvua zilizoambatana na upepo wa Kimbunga cha *HIDAYA*, Tarehe 4 na 5 zimeacha athari kubwa ya mafuriko katika Wilaya ya Kilwa, lakini pia maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pole sana kwa Wanakilwa wa Somanga, Matandu, Nangurukuru na Masoko kwa uharibifu mkubwa wa miundombinu ya madaraja na barabara. Pia, tunatoa pole kwa Watanzania ambao tangu tarehe 5, wamekwama pale Matandu na pale Somanga wakiwa wanatoka Dar es Salaam kuelekea Mikoa ya Kusini au wanatoka Mikoa ya Kusini kuelekea Dar es Salaam, lakini madhara haya yamewakuta wakiwa pale, tunatoa pole sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatoa pole sana kwa Watanzania wa Kilwa ambao kimbunga hiki kilichosababisha mvua kubwa au kilicholeta mvua kubwa kimeleta madhara na uharibifu mkubwa wa mashamba, makazi na hata kuondokewa na mifugo katika maeneo ya Matandu, Mchakama, Mkondaji, Ruhatwe, Njia Nne, Mitole pamoja na Pande na Malalani. Tunawapa pole sana. Pia, tunatoa pole kwa kaya zipatazo 920 zenye idadi ya watu wapatao 2,042 Wilayani Kilwa, ambao

wamepata madhara haya makubwa, ambao kimsingi wanahitaji mahitaji ya kibinadamu kama vile magodoro, mahema pamoja na vyakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatoa pole sana kwa taasisi ambazo zimeathirika na madhara haya, ikiwemo taasisi za shule pamoja na *health facilities.* Hapa naomba nitaje shule ambazo zimeathirika na maeneo haya Shule ya Sekondari Kilwa, iliyopo pale Masoko, tunatoa pole sana kwa wanafunzi, walimu na jamii inayozunguka pale. Mpaka imelazimika wanafunzi wahamishe kituo cha mtihani wa kidato cha sita, kwenda kupeleka Chuo cha Maendeleo ya Wananchi pale Kilwa ambapo mitihani hiyo inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunatoa pole kwa Shule za Msingi Mchakama, Mkondaji, Ruhatwe pamoja na Ndende, shule hizi hazijapata madhara, lakini kutokana na madhara kuwa makubwa zimegeuka kubwa ni kituo cha kimbilio la wahanga wa mafuriko na hivyo kusitisha huduma za watoto wetu kupata elimu. Tunatoa pole sana kwa wahanga wa maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee wake tunatoa pole kwa Kata ya Kikole, hususani Kijiji cha Ruhatwe, Kikole pamoja na Vitongoji vya Nanyati na Nambunga ambapo watu takribani 300, tangu juzi wameshindwa kupata huduma za kibinadamu kutokana na kuzingirwa na maji. Tunawapa pole sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pole hii, sasa nitumie fursa hii kuishukuru Serikali yangu ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye amesikia kilio chetu. Mara baada ya madhara haya kutokea Mheshimiwa Rais ameagiza Serikali ichukue hatua. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, sisi Wanakilwa na wote tuliopata maafa haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye yeye ndiye anaongoza Ofisi hii inayoshughulikia Kitengo cha Maafa, ametupa ushirikiano wa kutosha sana. Mimi na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu

Mheshimiwa Francis Ndulane, tumemwona mara kadhaa na ametupa ushirikiano wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee wake tutakuwa wachoyo wa shukurani tusipomshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, tumemsumbua vya kutosha tangu juzi na jana. *Weekend* yote tupo naye kwa ajili ya kuona kwamba, wahanga hawa wanapata nafuu. Kwa kweli ametusikiliza vizuri na taarifa niliyonayo sasa hivi Serikali inakwenda kujibu kilio cha wahanga hawa, wanaenda kupata nafuu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, aendelee na utu huo na asituchoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee wake nitoe pongezi na shukurani sana kwa Waziri wa Ujenzi, rafiki yangu Mheshimiwa Innocent Bashungwa, ambaye tangu *weekend* ya tarehe 3, amepiga kambi Kilwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Serikali ipo pamoja na wananchi hawa. Mheshimiwa Bashungwa amekuwa na wahanga pale Njia Nne, amekuwa na wahanga pale Somanga, amekuwa na wahanga Barabara ile ya Kilwa Masoko mpaka Nangurukuru na jana alikuwa pale Kilwa Kivinje. Kwa kweli tunamshukuru sana ameiwakilisha vizuri sana Serikali na kwa sisi Wanakilwa tunasema ahsante sana Mheshimiwa Bashungwa kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutakuwa wachoyo wa shukurani tusipomshukuru Mkuu wetu wa Mkoa, Mheshimiwa Zainabu Telack, amekuwa sambamba na Wanakilwa tangu majanga haya yatokee. Pia sisi Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Lindi na wa Wilaya ya Kilwa tumekuwa naye sambamba kutujuza kwa upekee kila kinachoendelea kule na sisi tumekuwa tukimpa ushirikiano wa jitihada ambazo Serikali imeendelea kuzichukua. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mkuu wetu wa Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunamshukuru Mkuu wetu wa Wilaya Mheshimiwa Nyundo, amefika hivi karibuni, lakini amefika na majanga haya, lakini kama ingekuwa ni kujaribiwa basi

majaribu haya Mheshimiwa Nyundo amefuzu. Sisi Wanakilwa kwa kweli tumepata Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Nyundo, anachapa kazi anawatendea haki Wanakilwa. Mungu ambariki sana na tumekuwa naye sambamba sana katika maafa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pole hizo na shukrani hizo kwa Serikali yangu, pole kwa wananchi wetu, lakini shukrani kwa Serikali yangu. Nina machache sana kwa Wizara ya Elimu, ambayo itakuwa ni moja na mbili yenye maeneo ya (a) na (b). Moja, shule zile ambazo nimezitaja kwa mfano Shule ya Sekondari Kilwa, ambayo imepata madhara makubwa miundombinu imepata uharibifu mkubwa na kwa maana hiyo inahitaji maboresho au ukarabati. Vitabu vyote ambavyo walimu wetu wanavitumia kwa ajili vijana wetu vimesombwa na maji. Tunaomba Wizara ya Elimu, kwenye eneo hili la vitabu ituangalie kwa jicho la kipekee pale Shule ya Sekondari Kilwa iliyopo Mjini Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Shule za Msingi Mchakama, Mkondaji, Ruhatwe na Ndende ambazo ndizo zimegeuka kuwa vituo vya kimbilio la wahanga masomo hayaendelei pale. Tuone jitihada ambazo Wizara ya Elimu, inafanya ili kuona tunaweza kuokoa vipi watoto wetu hawa ambao sasa hivi hawapati huduma ya masomo na vituo hivi vimegeuka kuwa ni kimbilio la wahanga hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, udhibiti ubora wa elimu, kutoka kuitwa wakaguzi wa shule mpaka wadhibiti ubora wa elimu ni hatua ya kuona kwamba, tunaitendea haki hii sekta ya elimu. Nizungumze kwa niaba ya sekta hii ya wadhibiti ubora wa elimu, wana vilio vikubwa viwili tu. Kilio cha kwanza ni kuboreshewa miundombinu na vitendea kazi. Wenzangu wengi wamechangia katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha pili, kutambuliwa kwao kama wakuu wa idara nyingine kwa mujibu wa muundo ili wapate stahiki zao kama walivyokuwa idara nyingine. Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba, mwaka 2014, Wizara ya Elimu ilitoa waraka kwa ajili ya kuwatambua hawa kwa nafasi hizi

za uongozi katika elimu ikiwemo Maafisa Elimu wa Mikoa, Maafisa Elimu wa Wilaya lakini sambamba na hawa Wadhibiti Ubora wa Elimu ngazi ya Wilaya. Waraka ule bado haujatekelezwa mpaka leo. Tunasubiri nini ili kuboresha elimu yetu? Tuiombe sana Wizara ya Elimu iweze kuwakumbuka hawa wadhibiti ubora wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Haki ya Mtoto wa Kike imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge sana na tumeona na tunaipongeza Serikali kwa hatua ambayo imeendelea kuchukua kuhakikisha kwamba mtoto wa kike hakomi masomo anaendelea ili mradi kwamba, kumpatia haki yake. Haki hii ya Mtoto wa Kike nishauri iende sambamba na kutambua Haki ya Mtoto wa Kiume. Ukiangalia watoto wengi ambao leo hii tunawapa majina yasiyopendeza mitaani kama vile chokoraa, wengi wao ni jinsia ya kiume. Hawa ambao nimewaita jina hili lisilowapendeza 'chokoraa' ni wenye umri wa kwenda shule. Serikali inafanyaje kuhakikisha kwamba na watoto hawa wa kiume na wao wanapata haki ya kupata elimu msingi na huko mbele waendelee ili nao waweze kuwa ni wataalam. *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria za nchi yetu katika suala la elimu limekuwa likimlinda mtoto wa kike ambayo ni haki yao stahili, lakini kwa upande wa watoto wa kiume inapotokea, kwa mfano, mtoto wa kiume akampa ujauzito mtoto wa kike, matokeo yake yule mtoto wa kiume analazimika kuacha shule kukimbia kutoka eneo analoishi ili kwenda eneo lingine akahangaike ili kuepuka kifungo. Vinginevyo, anakwenda jela kifungo kirefu sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Toa Taarifa Mheshimiwa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** …sasa hili ni jambo ambalo linafaa kutazamwa…

**MWENYEKITI:** Toa taarifa Mheshimiwa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** …kwa upeo wake ili kutoa haki kwa mtoto wa kiume kama ambavyo mzungumzaji alivyozungumza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kassinge, unapokea hiyo taarifa?

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili. Nimalizie na nihitimishe kwa kuendelea kuishukuru Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi, Chama Tawala inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia. Tunaamini kabisa Serikali sikivu ya Chama Cha Mapinduzi inakwenda kufanyia kazi maoni yetu, lakini kwa upekee sisi wahanga wanaenda kutupatia msaada wa huduma za kibinadamu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Kassinge, kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika karibu mwisho kabisa wa Bunge letu kwa siku ya leo, lakini yamejitokeza mengi kwenye Kikao cha leo cha Bunge la mchana huu. Moja ya mambo ambayo yamejitokeza hapa na kulikuwa na taarifa ilitolewa hapa na Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba na kwa vile ilikuwa taarifa asingeweza kupewa taarifa juu ya taarifa kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Kwa hiyo, kama Kiti hatuwezi tukaliacha hilo lipite hivi hivi. Nadhani ni jambo ambalo linaweza kuleta taharuki katika mazingira ambayo tunaongelea maadili, maana yake inasemekana watoto saa tano asubuhi wamelewa zaidi ya mamia na mamia. Sasa ni jambo kubwa na nadhani Serikali ina wajibu wa kulifuatilia na kuleta taarifa ndani ya Bunge, ukweli wa jambo hili ukoje? Mwakilishi wa Waziri Mkuu kwa maana hiyo *Chief*

*Whip* upo hapa naomba mlichukue hilo na kama una neno la kusema nikupe dakika moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea maelekezo yako na sisi kama Serikali hapa imetushtua kidogo, kama shule moja yenye watoto zaidi ya 1,000 na kitu, halafu inapofika saa tano watoto 600 katika shule hiyo wote wanakuwa wamelala ndani ya madarasa kwa kulewa. Ni taarifa kidogo ambayo imetushtua kama Serikali. Kwa hiyo, tunapokea maelekezo yako, kwa sababu tunafahamu Serikali ya Awamu ya Sita, imejizatiti kwa kiasi kikubwa sana kupambana na matumizi ya dawa za kulevya na nguvu ya pekee imewekwa kwa watoto wadogo na hasa kwenye shule zetu za msingi na shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mifumo ya elimu tuliyonayo nadhani kama kuna upungufu wa kiasi hicho kwamba, mifumo ya kiutawala katika shule zetu wameshindwa kuligundua hilo kwa muda huu wote kiasi kwamba, si bahati. Kwa hiyo, kwa niaba ya Serikali, napokea maelezo ya Kiti na tutafuatilia ili kwanza tuweze kuwaokoa hao watoto kutokana na janga hilo ambalo linawakumba. Pia, tuweze kufuatilia hiyo mifumo yetu ambayo inashindwa kujisimamia katika kutekeleza wajibu wao wa kuwasimamia watoto waweze kuenenda katika maadili mema, lakini wakafanikiwa kupata kile wanachotakiwa kukipata ndani ya shule zetu, kwa maana ya kuwa na elimu halisia. Kwa hiyo, nalipokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, maelekezo ndiyo hayo.

Baada hayo yote yaliyosemwa, naahirisha Bunge mpaka kesho Jumatano tarehe 8 Mei, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.54 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 8 Mei, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*